

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 30 Mei, 2017**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.  
Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO  
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa mwaka wa fedha 2015/2016 *[The Annual Report and Audited Accounts of Arusha International Conference Centre (AICC) for the Financial Year 2015/2016]*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu, tuendeleo.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kama kawaida. Sasa hivi tunaanza na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora). Tutaanza na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo. Sasa aulize swali lake.

Na. 298

**Tatizo la Ajira Nchini**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Ajira kwa sasa ni tatizo hapa nchini hasa kwa walimu wa sanaa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri katika sekta mbalimbali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) mwaka 2015/2016 umebaini kuwepo na ziada ya walimu wa masomo ya sanaa wapatao 7,463 katika shule za sekondari. Kutokana na hali hii Serikali inaendelea na zoezi la kuwagawanya walimu hao (*redeployment*) kwa kuzingatia uwiano na mahitaji halisi ya walimu wa sanaa kwa kila mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kila shule iweze kupata Walimu wa masomo ya sanaa badala ya kuajiri walimu wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 watumishi wa umma 9,721 wameshaajiriwa kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji ya kila mwajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali inatarajia kuajiri Watumishi 52,436 wa sekta mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa pamoja na kuimarisha sekta na maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fredy, swali la nyongeza.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja tu la nyongeza. Taifa lolote duniani ili lisonge mbele linahitaji watu waliosoma kada mbalimbali, iwe ni sanaa, sayansi au biashara.

Je, Serikali ina mpango gani wa ku-*balance* wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi, pamoja na wanafunzi wanaosoma sanaa ili isitokee kama sasa tuna ziada ya wanafunzi wa sanaa zaidi ya 7,463 na inapelekea kutokuwa

na ajira. Serikali ina mpango gani kwa miaka ya hivi karibuni na baadaye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali, imekuwa ikiendelea kuweka mazingira mazuri na kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi. Katika mwaka 2015 mpaka 2016 Serikali ilijikita zaidi katika kuhamasisha Shule za Sekondari kujenga maabara. Katika mwaka 2016/2017 tunasambaza vifaa vya maabara. Hizo zote ni jitihada za kuongeza wanafunzi wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba wanafunzi wanayo hiari ya kuchagua masomo. Kwa hiyo, kama Serikali tunatoa mazingira mazuri. Nangependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuwahamasisha wanafunzi pia kuona kwamba masomo ya sayansi na teknolojia nayo ni muhimu ili waweze kuyachukua kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa hapo utafuata.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Upungufu mkubwa wa lkama na zoezi la uhakiki wa vyeti limepelekea shida kubwa ya watumishi katika maeneo ya afya, elimu, Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata katika Manispaa yetu ya Katavi, kiasi cha kwamba mtumishi mmoja anafanya kazi zaidi ya moja.

Ni lini Serikali itaajiri katika maeneo hayo niliyoyazungumza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunakiri ni kweli kuna upungufu

mkubwa wa watumishi katika baadhi ya maeneo. Niendeleo tu kusisitiza kwamba lengo letu kubwa kama Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunaenda kwa kuzingatia maeneo yenye vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutahakikisha kwamba tunaimarisha maeneo yenye upungufu mkubwa. Nimweleze tu kwamba katika kada alizozitaja zitakuwa ni miongoni mwa kada ambazo pia tutazipa ajira katika mwaka ujao wa fedha. Vilevile labda nimtoe tu hofu kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi; katika mwaka ujao wa fedha tutatoa ajira 52,436 na labda tu niseme kwa mchangano ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Elimu tutatoa ajira 16,516 kwa upande wa Sekta ya Afya 14,102, Kilimo 1,487, Mifugo 1,171, Uvuvi 320, Polisi 2,566, Magereza nafasi 750, Jeshi la Zimamoto 1,177, Uhamiaji nafasi 1,500, hospitali za mashirika ya kidini na hiari kwa kuwa nazo tunatoa ruzuku, nafasi 174 pamoja na nafasi nyinginezo 12,673 ambazo zitahusu Sekta zote na jumla kuu ni 52,436.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe Mheshimiwa Kapufi hofu, ikama zote na mapendekezo kutoka kwa waajiri tumezipokea na tutaangalia katika kuimarisha maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri ulituhidi kwamba unaajiri walimu wa hesabu katika shule zetu, lakini ajira iliyotoka mwezi wa nne kwa upande wa walimu ni walimu wa *biology* na *chemistry*, ulituletea katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimesema katika Bunge hili kwamba, katika shule zangu kumi za Babati Mjini za sekondari hakuna shule yenye mwalimu wa hesabu. Sasa naomba nifahamu ni kwa nini msituambie kwamba

walimu wa hesabu ninyi hamna na hamna mpango wa kutuletea badala ya kutuahidi kila siku kwamba mtatuletea walimu? Watoto wetu hawasomi hesabu. Naomba kauli ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bahati nzuri ninayo orodha ya nafasi 3,081 za walimu wa hesabu na sayansi ambao tumewapangia vituo katika mwezi Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Babati Mjini naweza kuangalia kwa haraka haraka, lakini nitoe tu mfano kwa *Tarime DC*, tumepeleka walimu wa hesabu, *Musoma DC* tumepeleka walimu wa hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tutaliangalia na kama katika Manispaa yake hajapata kabisa, tutaweza kulifanyia kazi ili naye aweze kupata walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumtoa hofu Mheshimiwa Gekul kwamba tulitoa kibali cha walimu wa sayansi na hesabu 4,129 na hizi ni kwa ajira za mwaka 2015. Tayari ukiangalia tumepata tu Walimu 3,081, bado kuna nafasi zaidi ya 1,000 na zaidi katika kibali hicho ambacho tumekitoa, bado hawajajitokeza. Tunashirikiana na Wizara ya Elimu pamoja na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) tuweze kupokea maombi hayo, tumeanza kuyachambua. Watakaopatikana naamini ikitokea na walimu wa hesabu wako katika kundi hilo, basi kwa hakika kabla ya mwaka wa fedha na wewe utakuwa umepata walimu hao wa hesabu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto. Tunamkaribisha Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 299

## **Sheria Zinzowanyima Haki Watoto na Wanawake Nchini**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Sheria nyingi nchini hususan zile zinazohusu haki na stahili za wanawake zimepitwa na wakati na hivyo kuwanyima haki wanazostahili makundi hayo.

(a) Je, ni sheria zipi zinazowanyima haki wanawake na watoto nchini?

(b) Je, ni lini Serikali italeta miswada ili kuboresha au kubadilisha sheria hizo ili ziendane na wakati na kuwapatia haki zao wanawake na watoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Mirathi za Kimila (*Customary Declaration Orders, GN. No. 279* na 436 za mwaka 1963 zimekuwa zikiwanyima haki za urithi na umiliki wa ardhi wanawake na watoto.

Vilevile Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 katika Kifungu cha 13 na 17 vinaruhusu mtoto wa kike kuolewa katika umri mdogo wa miaka 14 au 15 kwa ridhaa ya wazazi au uamuzi wa mahakama. Vifungu hivi humnyima mtoto haki zake za msingi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi tayari yamewasilishwa Wizara ya Sheria na Katiba pamoja na Ofisi

ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Taratibu zote zitakapokamilika muswada utawasilishwa Bungeni.

Aidha, katika jitihada za kukomesha ndoa za utotoni, mwaka 2016 Serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 ili kuzuia watoto wa shule wasiolewe. Kwa mujibu wa Sheria hii Na. 4 ya mwaka 2016 Kifungu cha 60A hairuhusiwi mtu yeyote kuoa au kumpa ujauzito mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari. Kwa kuwa sheria hii inalenga zaidi ulinzi kwa watoto walio mashuleni, bado ipo haja ya kuviondoa kabisa vifungu vinavyoruhusu ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa kama ilivyofanyika kwa nchi nyingine kama vile Bangladesh, Yemen, Kenya na Malawi ili kuondoa mkanganyiko wowote unaoweza kujitokeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inafanya kazi kama timu moja, kwa nini marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 isibadilishwe ili itambue Mahakama ya Kadhi kama chombo cha kuamua hatima ya ndoa za kiislamu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hili la Mahakama ya Kadhi nitaomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu ya kwanza ya swali lake, ufafanuzi ni kwamba Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kile kifungu cha 13 na 14 kwa kiasi kikubwa vinahusu mambo ya nodal, hususan vinaruhusu mtoto mwenye miaka 14 kuolewa kwa sababu mbalimbali ambazo nitazitaja.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sheria ile ilitungwa katika zama ambapo mila na desturi za baadhi ya makabila yaliyopo katika nchi yetu zikizingatiwa. Pia sheria ile ilitungwa kwa kuzingatia pia misingi ya dini mbalimbali ikiwemo dini ya kiislamu ambapo katika imani hiyo inaruhusiwa mtoto kuolewa ama kuoa tu pindi anapobalehe ama anapovunja ungo. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo kama Serikali tunahitaji kuyachukua kwa utaratibu sana kwa sababu yanahusu imani, yanahusu mila na desturi za watu wetu na hivyo lazima ipatikane *consensus* ya kitaifa kabla hatujafanya uamuzi wowote wa mabadiliko ya suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ipo wazi na taratibu kadri tunavyojifunza kwa wenzetu kama nchi ya Kiislam ya Bangladesh, nasi tutaona ni njia ipi muafaka tuweze kupitia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel halafu Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Khatib.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sheria hii imekuwa ikiwazungumzia sana watoto wa kike na tunapozungumzia watoto, wapo watoto wa kike na watoto wa kiume; na watoto wa kiume kwa sasa wanakabiliwa na janga kubwa la ulawiti:-

Je, Serikali inazungumziaje swali hili ili kuhakikisha kwamba inawalinda watoto hawa wa kiume ambao wamekuwa wakipatwa na madhara hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kinyume cha sheria za nchi yetu kwa mtu yeyote yule kumwingilia kinyume cha maumbile mtu mwingine yeyote yule. Makosa haya yanaelezwa kwenye Sheria ya Kanuni za Adhabu, *Chapter 16 of the Law*, nafikiri ni kwenye Kifungu cha 154 na vifungu vinavyofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo makosa haya yamekuwa *criminalized*. Mwaka nafikiri 2012 au 2013 hapa Bungeni tuliongeza ukali wa adhabu ya mtu yeyote yule ambaye atabainika kufanya hivyo. Changamoto inayojitokeza kwa kweli, vitendo vya ulawiti kwa kiasi kikubwa sana vinafanyika kwenye familia. Vinapofanyika kwenye familia, ushahidi unakosekana kwa sababu ndugu wanakuwa hawataki kuripoti vitendo vya namna hii kwa kuhofia ndugu mwingine kwenda kufungwa. Kwa hiyo, wanayamaliza mara nyingi kimya kimya kwenye familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali msimamo wetu uko wazi kwamba adhabu kali ya kifungo kisichopungua miaka 30 itampata mtu yeyote yule ambaye atathibitika bila shaka kwamba amefanya kitendo cha ulawiti kwa mtoto yeyote yule awe wa kiume ama wa kike. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape halafu Mheshimiwa Khatib.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba baadhi ya sheria tulizonazo zinadumaza maendeleo ya wanawake na hasa watoto wa kike na kwa kuwa, tatizo la watoto wa kike wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kukatisha masomo yao kutokana na mifumo ambayo mingine imepaliliwa na Sheria hizi mbovu tulizonazo.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwanusuru hawa watoto ambao sasa wanaendelea kupoteza fursa ya kusoma na kufanikiwa katika masomo yao kutokana na sheria hizi mbovu tulizonazo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie swali lake kwa ufupi. Swali hasa analotaka nijibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape, naomba urudie kuuliza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi ni kwamba tatizo hili la watoto wa kike kutomaliza masomo yao au kukatisha masomo yao kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ni kubwa sana na hasa katika Jimbo la Mtama. Moja ya sababu kubwa ni hizi sheria tulizonazo ambazo zinapallia matendo kama hayo ya watoto hawa kupewa mimba na kukatishwa masomo yao na wengine kuolewa wakiwa bado wanaendelea na masomo na mengine wazazi wanasukuma watoto wao wafanye vibaya ili wafeli waende wakaolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni kwamba Serikali inachukua hatua gani kuwanusuru hawa watoto ambao kwa kweli wanaendelea kupoteza fursa katika maisha yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri umelewa.

**NAIBU WAZIRI AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Vizuri!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Nape kwa swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yetu kama Serikali ni kwamba, kama nchi tulipitisha Sheria hapa Bungeni mwaka jana tu, 2016 na tulifanya mabadiliko kwenye Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, kwenye kile kifungu cha 60(A).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hicho tuliamua kupandisha umri wa mtoto kuolewa mpaka kufikia miaka 21, lakini pia kuzuia mtoto yeyote yule ambaye anasoma *primary school* ama *secondary school* asiolewe kwa mujibu wa sheria na tukaweka adhabu pale. Kwa maana hiyo, suala hili kama Serikali tunalichukulia kwa ukali kama lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa suala hili hauwezi kupigiwa mfano kwa sababu, ni jambo linalohusu maisha ya kizazi cha nchi yetu huko tunakoelekea. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba wazazi wote washiriki kikamilifu katika kuwalea watoto wetu na kuwasomesha ipasavyo kwa mujibu wa sheria; na wa watambue kwamba ni kosa kisheria kumwoza binti ambaye anasoma ama ni kosa kisheria kumpa mimba binti ambaye anasoma. Yule atakayefanya hivyo, awe mzazi, awe ndugu, awe mlezi, atachukuliwa hatua za kisheria kama itathibitika kwamba imekuwa hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika siku za karibuni kumekuwa na harakati nyingi zinazoonesha kutaka kuleta haki na kuondoa ukandamizaji wanawake na watoto, ni jambo jema. Kwa mujibu wa kitabu chetu cha Qurani waislamu, ni kitabu kisicho shaka ndani yake. Kwa sisi waislamu huu mjadala tu wa kukitilia shaka kitabu cha Qurani, pia tunaingia katika makosa. *(Makofi)*

Je, Serikali itakuwa tayari kiasi gani katika marekebisho ambayo yanatakiwa sana kuhakikisha hayaingilii imani yetu na kutuendesha, kutupeleka katika dhambi kubwa ya kukitilia shaka Kitabu cha *Quran* na Sheria zake? Ahsante Sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, majibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kujibu swali hili. Masuala haya ya imani Serikali imeyazingatia sana. Serikali haina dini lakini inaheshimu sana imani za dini. Ndiyo maana tulipotunga Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 zoezi la kuitunga ile sheria lilikuwa shirikishi, watu walishirikishwa wakitoa maoni yao ndiyo ikaja ile sheria. Ndiyo maana hata pamoja na changamoto za wanaharakati kutaka turekebishe ile sheria,

tumesema hapana, lazima tuwashirikishe wananchi kwa upana wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuchukua nafasi hii kuwashauri Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaosikiliza kwamba Serikali haitakaa iingilie mambo ya dini. Hili suala linahitaji muafaka. Hata tulipoleta Sheria ya Kadhi hapa, mwaka juzi, hatukuendelea nayo kwa sababu ni masuala yanahitaji muafaka mpana. Kwa hiyo, wananchi muwe na amani. Hili zoezi litafanyika kwa kuwashirikisha. Hatuwezi tukawalazimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa mustakabali wa elimu, bahati nzuri Waislamu wanatambua umuhimu wa elimu, maana hata Mtume alisema kama inawezekana kuifuata huko chini, akaifuate. Ndiyo maana tulitunga ile Sheria ya Elimu mwaka 2016, tukaweka kulinda wanawake hawa wasiolewe waweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo! Naomba Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, Mbunge wa Malindi sasa aulize swali lake.

Na. 300

### **Faida ya Tanzania Katika Uanachama wa SADC**

**MHE. ALLY SALEH ALLY** aliuliza:-

Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) yenye soko la watu milioni 200 na rasilimali lukuki katika mtawanyika wa nchi 15 wanachama,

zikiwemo fursa kubwa za madini, petroli, gesi, ufundi, elimu na utalii.

(a) Je, Tanzania imefaidikaje na soko hili kwa kipindi cha miaka ya uanachama wake?

(b) Je, ni maeneo gani ya ushirikiano yameonekana zaidi kuwa na maslahi na Tanzania?

(c) Tanzania inapakana na majirani ikiwemo Zambia, Msumbiji, Congo *DRC* na Malawi. Je, tuna miradi au ushirikiano wa kiuchumi na nchi hizo kupitia *SADC*?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inajivunia kuwa moja ya nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) ambapo pamoja na mambo mengine imekuwa ikifaidika sana na fursa za masoko zinazotolewa na nchi 15 wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka 10, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenye nchi za *SADC* yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 301 mwaka 2007 hadi Dola za Kimarekani bilioni 1,017 mwaka 2016. Bidhaa ambazo Tanzania imekuwa ikiuza kwa wingi katika Soko la *SADC* zinajumuisha madini mbalimbali yakiwemo *Tanzanite* na dhahabu, bidhaa za kilimo kama chai, pamba, kahawa, bidhaa za viwandani kama vile vifaa vya *plastic*, sigara, neti za mbu, vipuri vya magari na simenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo Tanzania ina maslahi nayo ni pamoja na maendeleo ya viwanda kwa

lengo la uongezaji wa thamani katika mazao ya kilimo na madini, afya, usafirishaji, nishati, pamoja na ajira katika sekta mbalimbali. Maeneo haya yatachangia katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa kanda kutoka wastani wa 4% kwa sasa hadi 7%. Utaongeza mchango wa sekta ya viwanda katika uongezaji wa thamani ya Pato la Taifa kufikia 30% ifikapo mwaka 2030. Utaongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na teknolojia ya kati na ya juu kutoka kiwango cha sasa ambacho ni chini ya 15% hadi kufikia 30% inapofika mwaka 2030 na kuongeza mchango wa mauzo nje ya bidhaa za viwandani hadi kufikia 50% kutoka wastani wa 20% hivi sasa ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inanufaika pia na miradi ya ushirikiano inayoendelezwa katika nchi za *SADC* hususan miradi inayounganisha nchi jirani, kama vile mpango kabambe wa maendeleo ya miundombinu ya Kanda ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maendeleo ya nishati ya umeme kama vile Mradi wa Zambia – Tanzania – Kenya wenye kilovoti 400 ambayo ni (*400Kv Transmission Line*) unaounganisha kutoka Tunduma, Makambako, Iringa, Singida – Arusha – Namanga, kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Shirika la Maendeleo la Japan; mradi wa vituo vya pamoja vya mipakani kati ya Tanzania na Zambia, Tunduma, Nakonde, mradi wa maendeleo ya maji na uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe; mradi wa kuendelea Kanda ya Mtwara ambao unahusisha nchi za Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia, ujenzi wa Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, ujenzi wa reli na bandari, ujenzi wa vituo vya forodha kati ya Tanzania na Msumbiji, Zambia na Malawi na mradi wa maendeleo ya skimu ya umwagiliaji kwenye Bonde la Mto Ruhuhu, Bwawa la Kikonge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bunge hili limenipa heshima ya kuwa mwakilishi katika Bunge hili la *SADC*, lakini mpaka hivi sasa sifikiri kama *SADC* inaeleweka sana kwenye umma wa Watanzania. Ili kuongeza uhalali wake.

Je, Waziri haoni sasa kuna haja ya kuijulisha *SADC* kwa umma zaidi kuliko ilivyo hivi sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine ni kwamba kwa kuwa fursa zilizopo ni nyingi mno na jana tulijadili sana suala la *economic diplomacy* ambayo siku zote ni *two way* na inataka uwe *very aggressive* katika kuikabili; fursa zilizopo ni nyingi sana.

Je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika mkakati wa Watanzania kunasa fursa zilizoko *SADC* uwe wazi ili Watanzania wengi waweze kuzinasa fursa hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Ally Saleh kwamba wakati umefika wa kunadi fursa zilizoko katika Jumuiya hii ya *SADC*. Na sisi kama Wizara, kama mnavyojua kwamba tumeweka mkakati wa kutangaza na kutoa vipindi tofauti tofauti katika redio, *tv*, *brochures*, lakini pia tutaweka mkakati wa makusudi kwenda sehemu mbali zaidi kwa kuwaita wafanyabiashara na watu wa kawaida ili waweze kujua fursa zilizoko katika *SADC*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu Bilago atafuatiwa na Dkt. Kafumu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Fursa ambazo Tanzania imezipata kupitia *SADC* ni sawa na ambavyo tunapata fursa kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sambamba na mikoa mingine ambayo inazunguka nchi za Afrika Mashariki, Mkoa wa



Kigoma na hususan Wilaya ya Kakonko, hatuna fursa ambazo tunazipata kwa kupakana na Burundi, matokeo yake Warundi wanateswa na kusumbuliwa katika Wilaya ya Kakonko na mwambao wote unaoambaa Wilaya zote za Kigoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kupata maelezo ya Serikali, Burundi siyo sehemu ya Afrika Mashariki? Kama ni hivyo, kwa nini waendeleo kuteswa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho, wiki iliyopita pia alisema kwamba kuna raia wa Burundi kama 300 wamepigwa sana, lakini mimi nimefuatilia suala hilo sijalionga. Kama kuna sababu zozote zinazoonisha kwamba labda Burundi wanawafanyia ndivyo sivyo Watanzania, ningepata tu ushahidi na tutafuatilia, kwa sababu, katika vikao vyetu vya Mabaraza ya Mawaziri yanapotokea mambo ambayo hayaendani na utaratibu wa kisheria, huwa tunakaa na kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mbunge anilettee taarifa hiyo, ili sisi kama Wizara tufuatilie. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa muda sasa nchi za SADC ili kukuza fursa za uwekezaji na soko la pamoja zimeendesha mradi wa ku-*harmonise* au kuwianisha sera na sheria za nchi hizi ili kuweza kuvuna rasilimali hizi, lakini pia soko liwe la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali ya Tanzania imeshirikije kwenye mradi huu mpaka sasa? Tumefikia wapi? Maana bila

ku-*harmonise* sheria zetu, soko hili haliwezi kuwa la pamoja na wala hatuwezi kuvuna rasilimali hizi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Nje, huwa tuna-*co-ordinate* na kuhamasisha Wizara za Kisekta ili zihakikishe kwamba sera au sheria ambazo zinatofautiana na sheria au sera zilizowekwa na jumuiya, ziwe zimekuwa *harmonized* na zoezi hili ni endelevu kwa sababu inategemea na matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *data* zilizokamilika nitampa Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuelewa tulipofikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nashukuru. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 301

### **Wananchi Wanaouawa na Wanyamapori**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Kati ya mwezi Juni – Desemba, 2015 wananchi wapatao sita walishambuliwa na kuuawa na wanyamapori na Shirika la Hifadhi Tanzania (*TANAPA*) halikushiriki mazishi ya watu hawa, wala hakuna fidia yoyote waliyopata ndugu wa marehemu, hali inayoonesha mahusiano mabaya kati ya jamii na Mamlaka ya Hifadhi, zaidi ya hayo wanyama kama tembo, wamesababisha hasara kubwa sana kwa kuharibu mazao katika Tarafa ya Daudi, Kata za Marangwa, Daudi, Bargish na Gehandu.

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa fidia ndugu wa hao watu sita waliouawa na wanyama wakali katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

(b) Je, ni lini Serikali kupitia TANAPA italipa fidia kwa wale wote walioharibiwa mazao shambani mwaka 2014/2015?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaya, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hailipi fidia kwa madhara yanayosababishwa na wanyamapori hatari au waharibifu, badala yake inatoa kifuta jasho au kifuta machozi, kwa mujibu wa kifungu cha 68(1) cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009. Aidha, kifungu cha (3) cha Kanuni za Malipo ya Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2001 kinaainisha masharti na viwango vya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imepokea madai ya wananchi watano waliouawa, wanne walijeruhiwa na 31 walioharibiwa mazao yao katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumzia. Madai hayo yamefanyiwa kazi kwa mujibu wa kanuni na yatalipwa mara fedha zitakapopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niseme kwamba kwanza Serikali haitutendei haki sisi Wabunge. Neno italipa fedha au kifuta machozi pindi hela itakapopatikana haliwafurahishi Watanzania kwa tukio lililotokea la Watanzania kupoteza maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kadhia hii kwa Jimbo la Mbulu Mjini ina changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa Askari Wanyamapori na pia ratiba isiyoonekana ya wenzetu wa TANAPA na jamii zinazopakana na mipaka ya hifadhi na makazi ya watu. Tukio hili la mwaka 2015 lilipoteza maisha ya wananchi saba, siyo watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine niishukuru Serikali kwa sababu, Mheshimiwa Waziri ameleta tu majibu ambayo hajayafanyia kazi kwa sababu, hadi sasa muda mchache uliopita, kama miezi miwili, mitatu, Serikali tayari imetoa fidia kwa wahanga hao wapatao wanne, lakini wale wengine hawakupatiwa hata fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu sasa, kwa kuwa tatizo hili linagusa maisha ya Watanzania, je, ni kiasi gani cha fidia au cha kifuta machozi kinatolewa kwa wale wote waliopoteza maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kwa kuwa tatizo hili linavunja mahusiano kati ya wananchi na wenzetu wa TANAPA ama Serikali, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuandaa ratiba rasmi itakayowaunganisha wadau wa mpakani katika Tarafa yangu ya Daudi ili waweze kujadiliana matukio yanayotokea na hatimaye kudumisha uhusiano kati ya Shirika la TANAPA na wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kama alivyosema tayari Serikali imekwishaanza utaratibu wa kulipa bakaa au madeni ambayo yamekuwepo ya muda mrefu yanahusiana na kifuta jacho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana madeni haya yamekuwa hajalipwa, lakini napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwa ujumla

kwamba Serikali katika awamu hii imeshalipa madeni yaliyokuwa yanafikia kiasi cha shilingi bilioni 2.1 na hata sasa kuwa yamebaki jumla ya shilingi takriban milioni 500 peke yake. Mbulu ni mojawapo kati ya Wilaya ambazo zimelipwa malipo hayo na jumla ya fedha kiasi cha shilingi milioni 7,100,000 zimelipwa kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake mawili ya nyongeza; la kwanza, anazungumzia ni kiasi gani cha fedha kilichobaki kwa ajili ya malipo kwa Halmshauri ya Wilaya ya Mbulu? Katika takwimu nilizonazo, nina takwimu za ujumla wa kiasi chote ambacho fedha zinadaiwa kwa Serikali, lakini mahususi kwa ajili ya Mbulu, ukiacha hiki nilichotaja, kilicholipwa tukionana mchana naweza kumpa taarifa juu ya kifuta jasho na kifuta machozi kilichobaki kwa ajili ya Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili la kuweka ratiba na utaratibu wa kuweza kujadiliana, kuisharisha mahusiano zaidi baina ya TANAPA na wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka hifadhi, hili ni jambo jema na Serikali inalipokea. Tutakwenda kufanya hivyo na tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge ili kuona kwamba tunaimarisha zaidi mahusiano hayo kwa ajili ya uendeleu katika utaratibu mzima wa hifadhi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa kwa vile suala hili lina watu wengi sana ambao wameuliza, yaani wana maswali kila mmoja ana umuhimu wake, kwa hiyo, nitatoa nafasi moja kwa Waziri Kivuli Mheshimiwa Paresso na ya pili nitatoa kwa Mheshimiwa Bashungwa, waliobaki naomba sana mumpelekee Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi zaidi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza.

Kwa kuwa hicho kinachoitwa kifuta jasho au kifuta machozi kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori, imekuwa hailipwi kwa wakati pale ambapo wananchi wakipata

uharibu wa mazao yao hasa katika maeneo ambayo yanapakana na hifadhi:-

Je, ni kwa nini Serikali sasa isifikirie kuanzisha mfuko wa fidia ambao utachangiwa na hizi mamlaka zote kama TANAPA, Ngorongoro ili wananchi wawe wanaweza kutapata fidia yao kwa wakati bila kuchelewesha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna changamoto kubwa sana kuhusiana na malipo ya vifuta jacho na vifuta machozi. Ukweli ambao ni wa kudumu, hakuna namna ambayo tunaweza tukalifanya zoezi hili kwa namna endelevu kwamba madai yote yanahusiana na vifuta jasho na vifuta machozi yakalipwa kwa kile kinachoitwa kwa wakati hata kama tukianzisha mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili namna pekee ya kuweza kuliweka vizuri, namna bora zaidi ni kuzuia zaidi kuweka kinga na kupunguza matukio ambayo yanasabisha ulipaji wa vifuta jasho na vifuta machozi. Ndiyo maana pale awali wakati najibu swali la nyongeza nilisema wazo la kushirikisha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi ni wazo la msingi zaidi. Ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza kufanya uhifadhi kwa namna ambayo tunaweza kupunguza matokeo yanayolazimisha sasa Serikali ilipe vifuta jasho na vifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima twende kwa utaratibu wa kuweka ushirikishi zaidi na kuanza kuangalia kwamba wananchi hawakai kwenye maeneo ambayo ni ya mapito ya wanyama hawakai kwenye maeneo ambayo ni ya mtawanyiko wa wanyama na kufanya shughuli za kilimo na ufugaji kwenye maeneo yale. Pale inapotokea kwamba wanyama wanahama kutoka kwenye maeneo yao, maeneo ambayo siyo yale ya mtawanyiko ya yale ya njia za mpito, basi tutakuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa matukio hayo, lakini pia tutaweka mbinu mbadala za kuweza kuzuia

wanyama kuweza kuleta uharibifu kwenye mazao lakini pia kudhuru wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bachungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Pia katika Wilaya ya Karagwe kuna wahanga ambao wameathirika na wanyama waharibifu hasa tembo na viboko katika kata za Kihanga, Rugu, Nyakasimbi, Nyakabanga, Nyakakika na Bwelanyange, lakini pamoja na kushindwa kuwapa kifuta machozi wananchi hawa, pia vijiji katika hizi kata vinapakana na Pori la Akiba la Kimisi na Burigi na kuna asilimia ambayo inatakiwa kutoka kwenye mapato ya hifadhi kwenda kwenye vijiji ili kuwasaidia katika shughuli za maendeleo. Tumetuma madai katika Wizara kwa muda mrefu, lakini hatujawahi kupata hii fidia ili wananchi hawa nao wafaidike.

Je, ni lini Serikali itatoa kifuta machozi hicho pamoja na yale mapato? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nilisema katika maombi ambayo yamefikia Wizara kwa ajili ya uhakiki, kiwango cha jumla ya fedha takribani shilingi milioni 500 pekee ndicho ambacho kimebaki bila kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kuangalia kwenye orodha ile ya wale ambao wanafanya jumla ya madai yawe shilingi milioni 500 nione kama wananchi wanaolizungumzia ni sehemu ya madai hayo. Kwa hiyo, ikiwa hivyo ndivyo, tumesema fedha hizi zinalipwa ndani ya mwaka wa fedha huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa siyo miongoni mwa wale ambao jumla ya fedha shilingi milioni 500 zinadaiwa,

basi itakuwa wako katika mchakato; wale ambao bado taratibu hazijakamilika kwenye ngazi za Halmashauri na Mikoa, kwa hiyo, tutakwenda kuhimiza tu ifanyike haraka ili madai hayo yaweze kuifikia Wizara yawekwe kwenye orodha halafu tuweke utaratibu wa ratiba ya kuweza kuyalipa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 302

### **Mgogoro wa Kiwanda cha Chai - Lupembe**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-

Mgogoro wa Kiwanda cha Chai Lupembe umewaathiri wakulima wa chai Lupembe na Wilaya nzima ya Njombe kutokana na kukosa soko la zao la chai.

Je, Serikali ipo tayari kujenga kiwanda kingine cha chai kunusuru uchumi wa wakulima wa chai katika Wilaya ya Njombe?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa migogoro inaathiri sana shughuli za uzalishaji viwandani pamoja na kuwaathiri wakulima ambao hukosa soko la malighafi zinazozalishwa. Kiwanda cha Chai Lupembe ambacho kilikumbwa na mgogoro wa muda mrefu uzalishaji ulisimama kwa miaka nane kati ya 2008 na 2015. Katika kipindi hicho na baada ya Serikali kuona wakulima wanakosa soko la majani ya chai, Serikali ilishawishi



Kampuni ya *Mufindi Tea and Coffee Ltd.* kujenga kiwanda cha chai, katika tarafa ya Lupembe, Kijiji cha Ikanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hicho kilijengwa na kuanza usindikaji wa majani ya chai mwaka 2013. Hata hivyo, kufuatia hukumu ya Mahakama iliyompa ushindi mwekezaji wa kampuni ya *Dhow Merchantile East Africa Ltd.*, na *Lupembe Tea Estate Ltd.* dhidi ya Muungano wa Vyama vya Ushirika vya Lupembe, mwezi Januari, 2016 uzalishaji katika kiwanda hicho ulianza na unaendelea. Kwa sasa kuna kesi mahakamani inayoendelea kusikilizwa kufuata rufaa ya MUVYULU dhidi ya ushindi aliopata mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda vya kutosha ili kuchochea kilimo cha zao la chai na usindikaji wa majini ya chai katika Mkoa wa Njombe anakotoka Mheshimiwa Lucia Mlowe ambao una utajiri mkubwa wa zao hilo. Hivyo, Serikali imendelea kuhamasisha uwekezaji katika mkoa huo. Kampuni ya *Unilever* imeanza ujenzi wa kiwanda kipya cha chai. Kiwanda hicho kinatarajia kuanza uzalishaji mwaka 2018 na kitatoa ajira zipatazo 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwekezaji anatarajia kuanzisha mashamba ya chai yenye ukubwa wa Ekari, 1,000. Kati ya hizo ekari 200 zimeshapandwa mbegu za chai. Hivyo wakulima wa zao la chai wa Wilaya ya Njombe watapata fursa ya kuuza mazao katika kiwanda hicho kipya cha *Unilever* kitakapokamilisha ujenzi sambamba na viwanda vya *Lupembe Tea Estate Ltd.* na Ikanga chini ya Kampuni ya *Mufindi Tea and Coffee Ltd.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo yanapolimwa majani ya chai kuwa Serikali inafuatilia kwa makini chanzo cha migogoro katika mashamba hayo na kuitatua na kuipatia suluhu ya kudumu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lucia Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza na nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ilitembelea katika kiwanda hicho na kujionea migogoro katika kiwanda hicho na waliahidi kusaidia kutatua tatizo la migogoro hiyo haraka iwezekanavyo, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

Swali la pili, kwa kuwa moja ya tatizo katika kiwanda kile ni kutokuwa na Bodi yenye uwiano kati ya mwekezaji na MUVYULU, je, Serikali itawasaidiaje wananchi wale kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa bodi ili waweze kupata gawio na kuweza kuwaendeleza wale wakulima? Ahsante.

**MWENYEKITI.** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano, vile vyama vyenu vya MUVYULU vimekwenda mahakamani. Kwa sababu kesi iko mahakamani, suala lako (a) na (b) mimi mikono yangu inakuwa nje, siwezi kuliingilia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Kunchela atafuatiwa na Mheshimiwa Shangazi atafuata.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na changamoto za upungufu wa viwanda katika Mkoa wa Katavi, lakini pia kuna tatizo kubwa linawasumbua wakazi wa Manispaa ya Mpanda.

Je, Serikali iko tayari kufuatilia mashine ya kukooa na kusaga iliyonunuliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ambayo pia iligharimu pesa nyingi mno, mpaka sasa wananchi hawaelewi kwamba mashine hii iko wapi? Sehemu ambayo ilitakiwa kujengwa kwa ajili ya kuiweka ile mashine ili ifanye kazi mpaka sasa lile eneo ni gofu. Wananchi hawaelewi, nini mkakati wa Serikali kusaidia na kuokoa fedha hizi ili wananchi wapate ajira katika Manispaa ya Mpanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali lake ili kuweka msisitizo. Tumeshakubaliana kwamba tutakwenda kwenye Jimbo lako tuweze kuona hilo suala tulishughulikie. Kwa hiyo, hakuna tatizo Katavi na Rukwa, nimeshazungumza, mkoa yote miwili nitakwenda pamoja na ule mwongozo niliowatolea. Kwa hiyo, masuala yenu nitayashughulikia, tutajipanga upya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa msiba uliopo huko Lupembe wa kiwanda kufungwa ni sawa kabisa na msiba ulioko kule Bumbuli Kiwanda cha Mponde sasa ni miaka mitano chai inashindwa kuzalishwa na wananchi hawa wanapata hasara.

Je, Serakali inatoa tamko gani kuhusu msiba huo wa watu wa Bumbuli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya mwisho katika swali nililolijibu nilisema Serikali inafuatilia hizi changamoto au migogoro kwenye viwanda vya chai. Sitaki kusema zaidi, lakini yule aliyelea mgogoro, aliyehusika kwenye mgogoro wa Lupembe ndiyo yule anayehusika na kwenye mgogoro wa Mponde. Sasa sijui kuna nini! Niko chini yangu na juzi nilikuwa Tanga, nimewaeleza kwamba tutalifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa Shangazi kwamba katika Wilaya yake, Halmashauri sasa inakwenda njia ya pili kuanzisha kiwanda. Nimewaelekeza waende *TIRDO* wawaongoze namna ya kutengeneza kiwanda kingine, lakini Serikali inafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, jambo la kusikitisha, anayelalamikiwa Kusini, ndiye anayelalamikiwa Mashariki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, najua maswali ni mengi lakini Mheshimiwa Waziri yupo, mnaweze kumfuata na kupata ufafanuzi.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, ambaye swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

Na. 303

### **Wavuvi Kutekwa na Kuporwa Nyavu-Ziwa Victoria**

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Wavuvi wa Wilaya ya Rorya wanaovua katika Ziwa Victoria wamekuwa wakitekwa, kunyang'anywa nyavu zao pamoja na injini za boti. Aidha, majambazi wanaofanya vitendo hivyo hutumia silaha nzito na inasemekana ni wanajeshi kutoka Uganda.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongea na Serikali ya Uganda ili kukomesha uvamizi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwepo na matukio ya uporaji wa nyavu na injini za wavuvi katika Ziwa

Victoria. Uporaji huu unafanywa na wahalifu ambao bado Jeshi la Polisi halina ushahidi kuwa wanatoka ndani au nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na matukio ya uhalifu ikiwemo uporaji wa nyavu na injini za wavuvi katika Ziwa Victoria, Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina mikakati ya kununua boti zenye uwezo na zenye mwendo kasi mkubwa. Boti hizi zitasaidia askari polisi kufanya doria za mara kwa mara na kufika kwenye matukio haraka. Aidha, Serikali inashirikiana na nchi jirani katika udhibiti wa pamoja kwa matukio ya uhalifu wa majini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto, swali la nyongeza.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, imesema kwamba hawana ushahidi na Serikali ina mkono mrefu, je, ni kwa nini Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake wasiweke mkakati wa *operation* maalum ili kuweze kuwakamata wahalifu hawa ambao wamekuwa wakizorotesha uchumi wa wavuvi? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, kwa kuwa wavuvi wengi Kanda Ziwa wakiwemo wavuvi wa Mkoa wa Mwanza na mikoa ya jirani kama vile Kagera ikiwepo Kata ya Kerebe ambayo iko Bukoba, Ukerewe pamoja na Kalebezo na Kayenze wamekuwa wakiteseka sana na uporaji wa mali zao, hizi bodi pamoja na samaki, suala ambalo limekuwa likizorotesha sana uchumi wa wavuvi, je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi yake ambayo imekuwa ikiahidi kwa takribani miaka kumi sasa ya ununua boti ambazo zinaweza zikafanya doria ili kuwakamata hawa wahalifu ambao wanawapora wavuvi mali zao? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mkakati, mkakati upo

na kuna mahitaji ya *task force* ambayo inahusisha wadau mbalimbali na majukumu yake makubwa ni kukabiliana na uhalifu katika maeneo ya majini. Kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi kwamba mikakati hiyo ikiwemo katika eneo ambalo anazungumzia Mheshimiwa Mbunge ya Ziwa Victoria, tulipeleka hiyo timu na tukaweza kubaini upungufu kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wenyewe ambao umeelekezwa ni kwamba kuna umuhimu wa kuweza kupata boti zaidi zenye uwezo mkubwa zaidi kwa ajili ya kukabiliana na uhalifu huo. Ndiyo maana nikamweleza katika jibu la msingi kwamba Serikali inafanya jitihada kuweza kupata boti hizo za kisasa ili kuweza kudhibiti hali hiyo. Kuhusiana na kwamba wahalifu hawa wanatoka ndani au nje; ndiyo maana nimemwambia kwamba tunashirikiana na nchi jirani ili kuweza kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Msuha.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kuna mambo mengine Serikali haitakiwi hata iyaseme, kwa sababu yanaitia Serikali aibu. Wavuvi wanasema wanawafahamu, ni Waganda. Sasa ni kitu rahisi, kwa nini Serikali isikae na wavuvi, wavuvi wakasaidia kuwa-*identify* hawa watu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi. Mheshimiwa Waziri yupo eh!

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Selasini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi kwamba kuna majambazi kutoka mje ya nchi wanavamia wavuvi huko

ziwani, hata mimi nimepata kuzisikia, lakini baada ya kufanya *verification* kwa kuongea na wavuvi wenyewe, mimi naongea nao wengi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea na wavuvi wenyewe hasa katika visiwa vya huku Mara, kilichothibitika ni kwamba ni Watanzania hawa hawa ambao wanajifanya kwamba ni wageni wanapoenda kwenye visiwa jirani kwa kujifanya wanaongea lugha ambayo kama siyo Kiswahili sawa sawa. Ajenda ya kwamba ni majambazi kutoka sijui nchi za jirani, siyo sahihi. Hawa watu wanafahamika na tumeshatoa taarifa kwa uongozi wa Mkoa wa Mwanza wawatafute kwa sababu *at least identity* zao sasa zinafahamika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Keissy, naomba uulize swali.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Masuala yanayohusu Ziwa Victoria ni yale yale ambayo yanahusu Ziwa Tanganyika. Majambazi wanaingia usiku, hata iwekwe boti ya mwendokasi haiwezekani. Suala lililopo ni mazungumzo kati ya nchi jirani. Majambazi wanaovamia Ziwa Tanganyika hutoka DRC Congo, hakuna la kuficha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama muuliza swali wa swali la kwanza alivyosema ni majambazi kutoka Uganda na Serikali ya Kongo siyo dhibiti, hamna Serikali mama! Ukienda Congo chochote kinachoingia ni halali, iwe gari, iwe injini wakiiba au nyavu ni halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoiomba Serikali ni mazungumzo na Serikali ya DRC Congo kwa ajili ya kuokoa watu wetu. Hata uweke jeshi kila kijiji, haiwezekani. Wanaiba, wanavamia watu wetu usiku wa manane. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye mazungumzo na DRC Congo. Hiyo hamna kingine chochote! Mazungumzo na Uganda ndiyo tutaepuka ujambazi katika maziwa yetu, kukwepa hakuna. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy hilo ni swali au?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye mazungumzo na Serikali za jirani ili kuepusha matatizo ya kuvamia watu wetu. Wameuawa, wanaporwa na Serikali zao siyo dhibiti. DRC Congo hakuna Serikali mwambao wa Ziwa Tanganyika, wanawapora watu na wanawaua watu, hakuna Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, hilo siyo swali. Tunaendelea na Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo sasa aulize swali lake. *(Kicheko)*

Na. 304

### **Nyumba za Polisi**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Jeshi la Polisi lina kazi kubwa ya kulinda usalama wa raia na mali zao, lakini cha kusikitisha ni kwamba askari wanaishi kwenye nyumba duni sana jambo ambalo linashusha hata hadhi zao hasa kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

(a) Je, ni lini askari wetu watatengenezewa nyumba bora nao wajisikie kuwa Serikali yao inawajali?

(b) Katika Makao Makuu ya Polisi pale Ziwani kuna majengo yaliyoachwa na wakoloni, je, kwa nini yasifanyiwe ukarabati mkubwa ili yaweze kutumiwa na askari wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jeshi la Polisi linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa nyumba za kuishi askari. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali ina mpango wa kujenga nyumba 350 za kuishi Askari Polisi Zanzibar. Katika idadi hiyo, nyumba 150 zitajengwa Pemba na nyumba 200 zitajengwa Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kujenga nyumba mpya na siyo kukarabati nyumba za zamani zilizoachwa na wakoloni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri. Vilevile lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Masauni kwa ziara aliyofanya ndani ya Jimbo langu na kupunguza uhalifu, nimpe hongera sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini nyumba hizi zitaanza kujengwa kwa upande wa Unguja?

Swali la pili, kuna vituo vya polisi ambavyo hali yake ni mbaya sana kwa sasa hasa ukiangalia kama kituo cha Ng'ambu pamoja na Mfenesini na vipo vingi ambavyo hali yake ni mbaya sana, je, Serikali ina mkakati gani wa kuvifanyia marekebisho vituo hivyo angalau vilingane na hadhi ya Jeshi la Polisi kwa sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa pongezi zake. Ni kweli Jimboni kwake kuna eneo ambalo lilikuwa ni hatarishi sana kwa usalama wa wananchi na tulifanya ziara pamoja na yeye na tukaweza kuchukua hatua. Napongeza sana Jeshi la Polisi kwa kuweza kudhibiti ile hali.

Sasa hivi nimeambiwa kwamba hali ni shwari na wananchi wanafanya shughuli zao vizuri. Kuhusiana na hizi nyumba kwamba ni lini zitajengwa, ni pale ambapo taratibu za kifedha zitakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine anazungumzia kuhusu vituo vya polisi kwamba vina hali mbaya. Ni kweli tuna matatizo ya vituo vya polisi, siyo tu vina hali mbaya, lakini ni pungufu. Tuna upungufu wa takribani vituo 65 hasa katika Wilaya za Kipolisi nchini. Kwa hiyo, hili vilevile linakwenda sambamba na hali ya kibajeti. Pale ambapo hali ya kibajeti itaruhusu tutajenga vituo vipya katika maeneo ambayo hakuna, lakini vilevile kukarabati vile ambavyo viko katika hali mbaya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Jamani Waheshimiwa muda wetu umekwisha na watu mnaotaka kuuliza hili swali ni wengi, na mimi napenda niwape wote. Nikimpa mmoja nitakuwa nimeonea.

Naomba tuendelee na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara wa Ukonga aulize swali lake.

Na. 305

### **Miradi ya Maji – Ukonga**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Jimbo la Ukonga lina shida kubwa ya maji.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya maji ya Kata za Chanika, Kipunguni na Majohe ili wananchi wa Kata hizo na maeneo ya jirani wapate maji ya uhakika?

(b) Je, ni lini Serikali itachimba bwawa kubwa katika Mnada wa Kimataifa wa Pugu ili ng'ombe wanaouzwa hapo wapate maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kukamilisha miradi ya maji katika Kata za Chanika, Kipunguni na Majohe. Miradi mingi imekamilika na inahudumia wananchi na mingine ipo katika hatua za mwisho za ujenzi. Miradi iliyokamilika ni pamoja na Kipunguni B, Kwa Mkolemba, Chanika Shuleni, Majohe, Nyang'andu na Msongola. Miradi inayoendelea kujengwa ni bomba mbili za Kipunguni B, ambao unatekelezwa na Manispaa ya Ilala. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kuleta maji katika maeneo ya Pugu kutoka katika mradi mkubwa wa visima virefu vilivyopo Mpera katika Wilaya ya Mkuranga. Kazi ya uchimbaji wa visima hivi inaendelea na matarajio ni kukamilisha uchimbaji mwaka huu wa fedha na baada ya hapo Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa mabomba ya kusafirisha maji hayo hadi Pugu na kuyasambaza maeneo yote ya Pugu, Chanika, Ukonga, Gongolamboto, Kinyerezi, Kitunda, Kipawa, Yombo na maeneo ya barabara ya Nyerere kuanzia Pugu hadi TAZARA.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ni mwalimu wa hesabu na *chemistry*, nimesahihisha majibu ya Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri amepata 5% kati ya 100% ya majibu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye ni rafiki yangu sana,

ameandika kimoja tu cha ukweli kwamba mradi huu wa Kipunguni B umekamilika, mengine yote ni ya uongo.

Mheshimiwa Waziri, inaonekana ninaposema Jimbo la Ukonga lina shida ya maji hujui, upo tayari kutafuta taarifa sahihi ya miradi ya maji Jimbo la Ukonga unilettee kabla Bunge hili halijaisha? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, kipengele (b) hukujibu kabisa. Mimi nimeuliza kuchimba bwawa katika Mnada wa Pugu ambao ni Mnada wa Kimataifa, Dar es Salaam, hakuna mnada mwingine tofauti na huu, haukugusa kabisa. Umezungumza habari ya Kipera ambao ni mradi wa tangu mwaka 2016, uliandikwa kwenye Bajeti ya Maji na mwaka huu umeandikwa, haujaanza kutekelezwa. Nimeuliza bwawa la maji, hujajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali la pili, upo tayari sasa nikuitie akina mama wote wa Ukonga pale ambao wanapata shida na hasa pale ambapo wanakwenda kujifungua hakuna maji zahanati kule Yongwe, Chanika, Msongola, Buyuni na Kivule ili uende Ukonga uzungumze nao wakueleze shida ambazo wanazipata wakienda kujifungua, wanaambiwa njoo na maji ambapo ndoo inauzwa shilingi 500? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa amesema kwamba taarifa niliyotoa siyo sahihi na amezungumzia suala la bwawa la Pugu.

Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Serikali imefanya juhudi kubwa sana kupeleka maji katika Jiji la Dar es Salaam na miradi miwili mikubwa imekamilika ambayo inatoa kiwango kikubwa sana cha maji. Mradi wa tatu ambao utahusika na visima vile vya Mpera nao unakamilika mwezi Juni na utakuwa na lita zaidi ya milioni 260. Kazi iliyobaki ni

kuyasambaza na tayari maeneo mengi ikiwemo na Kipunguni tayari mabomba yameshaanza kufika kule ikiwa ni pamoja na kuchimba visima. Siyo maeneo yote lakini tunaendelea. Matarajio yetu baada ya kupata fedha za kusambaza maji, maeneo yote yatapata huduma ya majisafi na salama, hilo nakuhakikishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kama niko tayari kuongea na wananchi? Nimhakikishie kwamba niko tayari, wakati wowote nitakwenda kutoa majibu kwa wananchi bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amezungumzia suala la bwawa, ni kweli Mheshimiwa Mbunge swali hilo nimeliona, lakini wewe kwanza nikwambie umelelewa na CCM. Umechanganya maswali. Swali moja limekwenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji lakini swali lingine lilikuwa ni swali la Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Eneo la Pugu, soko lile linahudumiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali hilo lilitakiwa lielekezwe huko, bahati mbaya lilikua ni namba moja. Kama namba zingekuwa mbili ningelipeleka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu kama ameuliza kama swali la nyongeza, nitajibu kama Serikali. Ni kwamba tayari Wizara husika imechimba kisima kirefu, kisima kile kinatoa lita 1,500 kwa saa na tenki kubwa limejengwa ambalo lina ujazo wa lita 10,000. Kisima hicho hakijaanza kutumika kwa sababu kwa sasa mvua inayonyesha ni nyingi, kwa hiyo, mifugo inapata maji ya mvua. Lakini pia baada ya huu mradi mkubwa wa kutoka Mpera na Kimbiji kukamilika, tenki lililojengwa pale Pugu na Wizara husika litapata maji hayo ili kuhakikisha kwamba mifugo inapata maji na hakutakuwa na wasiwasi wa aina yoyote Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunamalizia swali la mwisho la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafya, sasa aulize swali lake.

Na. 306

### **Mradi wa Maji Kutoka Kiegeani**

**MHE. MBARAKA K. DAU** aliuliza:-

Wananchi wa Kisiwa kidogo cha Jibondo – Wilayani Mafia wamekuwa na shida kubwa ya maji.

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa muda mrefu wa kuvusha maji kutoka Kisiwa Kikuu eneo la Kiegeani kwenda Kisiwani Jibondo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutatua tatizo la maji katika Kisiwa cha Jibondo kwa awamu ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitumia kiasi cha shilingi milioni 80 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa kisima, ujenzi wa nyumba ya pampu na kukiunganisha na umeme kituo cha kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya mradi itaanza mwanzoni mwa mwezi Juni, 2017 na kazi zitakazotekelezwa ni usanifu, uandaaji wa nyaraka za zabuni, kumpata Mkandarasi na ujenzi wa kuunganisha bomba la maji safi chini ya bahari eneo la kutoka Kiegeani kwenda katika Kisiwa cha Jibondo. Ujenzi wa mradi huo utaanza mwaka wa fedha 2017/2018 na utanufaisha wananchi wapatao 3,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau, swali la nyongeza.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri na yenye kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Jibondo kimejengeka kutokana na mawe na miamba mikubwa, huwezi ukachimba kisima pale ukapata maji. Wananchi wa Jibondo wamekuwa kwenye kadhia ya ukosefu wa maji toka dunia hii iumbwe, wanapata maji ya bahari na mara chache maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba usanifu pamoja na ujenzi utanza mwaka ujao wa fedha.

Nilikuwa naomba aliahakikishie Bunge lako, ujenzi huu utanza lini? Kwa sababu usanifu na ujenzi vyote vimewekwa pamoja, utanza lini na utachukua muda gani ili nikitoka hapa niende nikawaambie wananchi wa Jibondo kwamba tarehe fulani maji yataanza kutoka Jibondo? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuingia katika vitabu vya historia na kuwa Waziri wa pili kufanya ziara katika Kisiwa cha Jibondo toka Mzee Malecela alipofanya hivyo miaka ya 1970 akiambatana na mimi Mbunge wa Jimbo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ameuliza ujenzi utanza lini? Kama nilivyosema kwamba usanifu umekamilika na wanakamilisha nyaraka za zabuni, tutatangaza *tender*. Kwenye ule mchakato wa *tender* ndiyo tutapata tarehe kamili kwamba mkandarasi ataanza lini na atakamilisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi ni kwamba kazi hiyo itafanyika katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, Mheshimiwa Mbunge tutahakikisha tunafanya kazi hiyo na tunakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kwamba Kisiwa cha Jibondo kimejaa mawe, ni kweli na ndiyo maana tumechimba kisima eneo lingine la Kiegeani na bomba lile litapita chini ya bahari mpaka liende kwenye Kisiwa cha Jibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeniomba nitembelee pamoja na wewe, Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari. Baada ya kumaliza bajeti hii, basi tutazungumza na tutatengeneza ratiba ili twende mpaka Kisiwa cha Jibondo nikawahakikishie wananchi kwamba wanapata maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Muda wetu wa maswali umeishia hapo. Ningependa niwape wote nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza ili mfurahi, lakini haiwezekani na siwezi kupendelea, mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, naomba tusipeane mitihani. Kwa hiyo, tuvumiliane hivyo hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni hapa ambao wametembelea Bungeni asubuhi hii na wa kwanza wapo Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Wageni 56 wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni viongozi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Ndugu Khatib Kazungu, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mary Mganga, Kamishna wa Bajeti, Ndugu William Mhoja, Kaimu Kamishna wa Sera, Ndugu John Rubuga - Kamishna wa Fedha za Nje, Ndugu Charles Masola - Kamishna wa Udhhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu; Ndugu Maduka Kessy - Kaimu Mtendaji; Ndugu Paul Sangawe - Naibu Katibu Mtendaji; Ndugu Ibrahim Kalengo, Naibu Katibu Mtendaji, Ndugu Happiness Mgallulah, Naibu Katibu Mtendaji na Ndugu



Lowrah Madette, Naibu Katibu Mtendaji. Hawa wameambatana na wageni wengine ambao ni viongozi mbalimbali wa Wizara ya Fedha na Mipango. Karibuni sana wageni wetu watendaji wa Wizara pamoja na wenzao. (Makofi)

Wengine ni wageni 16 kutoka Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali wakiongozwa na Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ni CAG, Profesa Mussa Assad. Karibu sana Profesa Mussa. (Makofi)

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 100 wa Mheshimiwa Angeline Mabula ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango na UDOM kutoka Illemela, Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Ndugu Julius Emily.

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliokuja kutembelea Bungeni hapa leo, tunawakaribisha wote kabisa, mkaribie katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna tangazo kwa Waheshimiwa wote wa imani ya Kikristo, Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katika eneo la wazi la *basement*, aidha, Mtumishi wa Mungu, Mchungaji Anthony Lusekelo atashiriki ibada na Waheshimiwa Wabunge wakiwemo wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Kwaya ya Safina kutoka Kanisa Kuu la Anglikana, Dodoma. Mheshimiwa Mchungaji tunaye, yuko hapa leo kwenye *galleries* zetu. Karibu sana Mchungaji. (Makofi)

Katibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, siyo wa Spika. Haya Mheshimiwa Faida, Mheshimiwa...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Waitara.

**MWENYEKITI:** Eeh, namwangalia huku Mheshimiwa kwanza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mlinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Waitara na yule pale malizia kabisa, haya. Mheshimiwa nani?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mlinga, Mlinga!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga yupo eeh!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Eeh, mimi hapa.

**MWENYEKITI:** Haya, wanatosha jamani. Tunaanza na Mheshimiwa Faida.

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kutokana na swali langu la nyongeza ambalo nimemwuliza Mheshimiwa Waziri. Alivyoniijibu alisema kwamba Mwanasheria Mkuu angetakiwa kunijibu swali langu lile la nyongeza, lakini Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu hakunijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, ili swali lile lijibiwe kiufasaha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwongozo wangu ni kupitia Kanuni ya 68(7) ya jambo lililotokea Bungeni hivi punde. Naongelea hoja ya jana jioni, kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge tunayochangia humu ndani ni *record* ya Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo inaingia kwenye *Hansard* na ni

*record* kwa matumizi binafsi ama kwa matumizi ambayo ni *public*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya michango yetu, tukifuatilia kule ambako inahifadhiwa kama kumbukumbu zetu binafsi ama kwa matumizi yetu, wana-*edit* karibu asilimia 70 na wanaweka mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimechangia hapa Wizara ya Mambo ya Nje na Afrika Mashariki, nikaenda nikaambiwa nijaze fomu, nikajaza fomu kutaka kumbukumbu yangu ya mchango wangu, mchango ambao hata haukuwa na mwongozo, haukuwa na taarifa, haukuwa na utaratibu, nimekwenda, mambo yote yanayohusu mambo ya *Acacia* na diplomasia ya kiuchumi yametolewa, wamenibakizia mahali panaposema tu atakayepinga, mtu yeyote akiongelea uteteaji wa rasilimali ni mwendawazimu. Hicho ndicho kinazungushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yetu humu Bungeni ni kumbukumbu zetu. Hili Bunge limeondolewa kuwa *live*, uhuru wake umeminywa, bado michango yetu ambayo ni halali tukifuatilia *clip* kwa kumbukumbu zetu, mna-*edit!* Sasa ni bora Bunge hili likatoa mwongozo wa kuvunja Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na msipokee maoni yoyote kutoka kwetu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii. Natumia Kanuni ya 68(7) isomwe pamoja na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji anajibu swali langu la msingi, kwanza aliongeza maneno kwamba mimi nimelelewa na Chama cha Mapinduzi, mimi sijalelewa na CCM ila nilikuwa Kiongozi wa CCM. Niliingia Chama cha Mapinduzi nikiwa niko *form six*, kwa hiyo, sikuwa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, siyo kweli kwamba kama ulikuwa kiongozi wa CCM huna haki ya kuuliza maswali humu ndani. Kwa hiyo, alipaswa kujibu swali langu kwa *content* yake na siyo makandokando mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaouomba hapa wa msingi zaidi ni kwamba mimi nimeuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, nilitaka atafute taarifa sahihi za miradi ya maji Ukonga alete kwa sababu asilimia tano peke yake ya ukweli wa swali langu ndiyo ameleta hapa. Alichoeleza ni miradi ambayo itatekelezwa baadaye. Kwa hiyo, swali langu halijajibiwa, nitaomba kupitia Mwongozo wako nipate majibu sahihi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hapa, tangu jana katika Wilaya ya Monduli, Kata za Moita na Nagharami, tembo zaidi ya 40 wamevamia katika mashamba ya wananchi na kuharibu zaidi ya ekari 100 na watu wa wanyamapori walivyojaribu kwenda kuwaondoa wale tembo, walishindwa na waliishiwa risasi na gari ilipata pancha. Mpaka sasa wanyama wale wamezuia watoto wasiende shule na wananchi wameendelea kujifungia katika nyumba zao.

**WABUNGE FULANI:** Duh!

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la dharura na lina hatari sana kwa maisha ya wananchi wetu. Ninaomba mwongozo wako, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wanyama wale wanaondolewa na kusaidia wananchi wale kuondokana na hali ya taharuki ambapo hata watoto walishindwa kwenda shule?

Naomba Mwongozo wako ili Serikali iweze kutoa kauli namna gani *TANAPA* wanashirikiana na wananchi kuondoa wanyama wale katika makazi yao na kuwalipa wananchi fidia stahiki kwa uharibifu uliotokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bunge letu ni Bunge linaloheshimika sana, siyo Tanzania tu...

**MWENYEKITI:** Unasimama kwa Kanuni ipi?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Tanzania tu, ni Afrika pamoja na dunia nzima. Mwongozo wangu ni kwa jambo ambalo limetokea Bungeni mapema leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mmoja wakati akiuliza swali namba 303, swali la nyongeza, alilaumu na alisema kuwa Congo hakuna Serikali. Congo ndiyo soko letu kubwa la bidhaa, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikuwa anaongea na Rais wa Congo ili aweze kuitumia Bandari yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hicho cha kauli, bora kingetokea mtaani, lakini kimetokea ndani ya Bunge letu hili kuwa Congo hakuna Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kauli hii ama ifutwe au Serikali itolee majibu ya kurekebisha au tuwaombe radhi Wakongo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Congo ni mwambao mwa Ziwa Tanganyika, hakuna Serikali, hata yeye mwenyewe akaangalie kule akaone.

**MWENYEKITI:** He, Mheshimiwa Keissy unasimama bila ruhusa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Keissy, unavunja Kanuni, unasimama bila ruhusa, unasema tu! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea Miongozo hapa, naanza na wa Mheshimiwa Faida ambaye ameuliza kuhusu swali la nyongeza ambalo aliambiwa litajibiwa na Mwanasheria Mkuu, lakini anasema kwamba halijajibiwa, nafikiri anakusudia kusema halijajibiwa alivyotaka yeye kwamba apate majibu ambayo amekusudia.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba nitaiomba Serikali kupitia AG iweze kulifafanua vizuri hilo ili tuletewe na wengine wapate faida. Huo ndiyo Mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Faida.

Mheshimiwa Lema anasema michango; *record* za Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba zinafanyiwa marekebisho baadaye wakienda kuomba. Ni kwamba michango ambayo tunaiandika kwa maandishi tunaletewa hapa kwanza kwa ajili ya kuweza kurekebisha, lakini kama ni *clip*, basi hili suala itabidi nilifuatilie kwa sababu sina uhakika nalo kama ni kweli ama siyo kweli, baadaye tutaweza kuleta majibu. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Mheshimiwa Waitara, suala la uwepo wa CCM mimi sielewi, kwa hiyo, siwezi kutolea mwongozo kuhusu uwepo wako CCM huko nyuma. Kuhusu maswali ya nyongeza na miradi ambayo umemwomba Mheshimiwa Waziri aweze kukuletea ufafanuzi, basi nitaomba Serikali kupitia Wizara hiyo ya Maji na Umwagiliaji waweze kutuletea majibu kuhusu miradi hiyo ili twende vizuri tusiharibu mambo.

Mheshimiwa Julius kuhusu wanyamapori, hilo nalo naiomba Serikali iweze kufuatilia kadri iwezekanavyo ili wanafunzi hawa waweze kuendelea. Kuna ufafanuzi wa Serikali, naomba watu wa Maliasili, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ana ufafanuzi hapa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Julius.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote Mheshimiwa Julius pokea pongezi zangu kwamba unafanya jitihada za kufuatilia masuala yanayohusu wananchi wako kwenye Jimbo lako, lakini ingekuwa vizuri ungesema pia kwamba tumezungumza suala hili mimi na wewe dakika kama 15 zilizopita na tumelizungumza hapo nje na nimekupa mwelekeo Serikali itachukua hatua gani. Sasa labda nisisitize tu, pengine pale tulipozungumza uliona kwamba ni vema ukilisema tena ili liweze kupata *coverage* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena ahadi ya Serikali kwamba tayari tumekwishafanya mawasiliano. Tulipokuwa wote nje, nilijaribu kupiga simu ukiwepo, tukakosa kumpata tuliyekuwa tunamtafuta, lakini baadaye nimempata na nimeshatoa maelekezo. Jambo linalokwenda kufanyika sasa hivi ni kwenda kuwafukuza na kuwarudisha kwenye maeneo yao katika hatua ya awali kwanza. Masuala mengine yote yatakayoendana na suala hili yatafuata taratibu za kawaida za Kiserikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante upande wa Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kulipokea hilo, naamini sasa litafanyiwa kazi.

Mwongozo wa mwisho ni wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga kuhusu suala la kwamba Congo hakuna Serikali. *Chief Whip* naona yuko tayari kutoa maelezo hapo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kabisa naomba tu nimwondoe hofu Mheshimiwa Faida Bakar, kwamba Serikali tunafanya kazi kwa umoja ndani ya Bunge hili; na kwa mujibu wa Kanuni, majibu yetu kama Serikali yanaweza yakaanza kujibiwa na Naibu Waziri na

Mwanasheria Mkuu ama Waziri mwingine yeyote anaweza akaongeza majibu.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifanya kazi nzuri, alijibu. Majibu yaliyojibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, akaongeza majibu ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutamwomba tu Mheshimiwa Faida kama anaona kuna eneo halijaeleweka zaidi anaweza akatuletea tena hilo swali na Serikali itakuwa tayari kujibu. Kazi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali leo na Naibu Waziri waliifanya kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe maelezo hapa kwamba sisi kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatambua kabisa nchi ya Congo inayo Serikali ambayo iko madarakani na inaendelea kufanya kazi kama Serikali halali na hatuna taarifa yoyote kama nchi ya Congo haina Serikali kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kiti chako kinao uwezo wa kuona ni namna gani kinaweza kikatamia madaraka ya Kikanuni kuweza kufanya jambo hili lisionekane katika kumbukumbu za taarifa tulizonazo leo Bungeni kwa namna ambayo wewe utakwenda kufuatilia. Kama Serikali, naomba nithibitisha kwamba tunatambua uwepo wa Serikali ya kule kwa wenzetu wa Jamhuri ya Congo. Kwa hiyo, hiyo ilikuwa ni taarifa yetu fupi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa taarifa ya Serikali kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kweli ambayo ameyazungumza, kwa hiyo, kwa mwongozo wangu ni kwamba tunakwenda kulifuatilia hili suala na kama lipo kweli limezungumzwa kwamba Congo haina Serikali, itabidi liondolewe kwenye *Hansard*. Kama kweli ameandika, basi itabidi afute kauli yake hiyo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*



**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane. Tunapitia kwenye *Hansard* tunaangalia, lipo pale linaondolewa na atafuta kauli yake.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza miongozo, Katibu tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Fedha na Mipango**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa tunamkaribisha Waziri wa Fedha na Mipango ili awasilishe Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa muda wa dakika 60. Karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018. Napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulingoza Taifa letu kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu.

Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge)

na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa wanazofanya kwa dhati kumsaidia Rais katika utawala wa nchi yetu na kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya bajeti ya Wizara mbalimbali kwa mwaka 2017/2018 kwa mafanikio makubwa. Aidha, napenda kutambua mchango mkubwa na kumshukuru Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo na Makamu Mwenyekiti, kwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa ili kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondo ambaye pia ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano na msaada anaonipatia katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu unafanikiwa.

Aidha, ninawashukuru Bwana James Dotto, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu, Bibi Dorothy Mwanyika, Bibi Amina Hamis Shaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu, kwa kusimamia vema shughuli za kila siku za kiutendaji za Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; Bwana Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Dkt. Oswald Mashindano, Msajili wa Hazina na Dkt. Albina Chuwa, Mtendaji Mkuu wa

Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kutekeleza majukumu ya kusimamia kwa weledi taasisi nyeti walizokabidhiwa. Taasisi hizi zinatoa mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kutimiza wajibu wao vyema wa kuwatumikia Watanzania. Ninafurahi pia na kumpongeza Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Profesa Mussa Assad, kwa kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba anafichua maovu yote katika bajeti na mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kueleza kwa kifupi majukumu ya Wizara nikianza na kazi muhimu ya kujenga msingi wa uchumi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha jukumu hili, Wizara ilijielekeza katika kuimarisha utulivu wa uchumi, usimamizi bora wa ukusanyaji wa mapato, kupanua wigo wa kodi, kusimamia matumizi ya fedha za umma na kuratibu utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia ikiongozwa na Sera ya Fedha ilijikita katika kuhakikisa kuwa usimamizi wa malengo mapana ya kitaifa ya ukuaji wa uchumi na kudhibiti mfumuko wa bei yanafanyika, lakini vilevile kuhakikisha nakisi ya Bajeti ya Serikali haizidi asilimia 4.5 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 7.0 na ulitokana na ukuaji wa kasi wa Sekta ya Mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 13, Sekta ya Ujenzi kwa asilimia 13, Sekta ya Usafirishaji na Uhifadhi asilimia 11.8, Sekta ya Madini na Uchimbaji Mawe kwa asilimia 11.5. Mchango mkubwa katika pato la Taifa katika mwaka 2016 ulitokana na Sekta ya Ujenzi ambayo ilichangia asilimia 20.2, usafirishaji na uhifadhi asilimia 10.8, biashara ya jumla na rejareja asilimia 9.9, mawasiliano asilimia 8.3 na uzalishaji viwandani asilimia 8.2

Mheshimiwa Mweyekiti, utekelezaji thabiti wa Sera ya Fedha uliwezesha kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani ambapo dola moja ya Kimarekani ilibadilishwa kwa wastani wakati wa shilingi za Kitanzania 2,180 mwezi Juni, 2016 na shilingi 2,220 mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei uliendelea kubaki kati ya asilimia 5.1 mwezi Julai, 2016 na asilimia 6.4 mwezi Machi, 2017 ukiwa ndani ya ukomo wa asilimia 8 uliowekwa chini ya makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki katika viwango vya tarakimu moja katika siku zijazo

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jukumu la msingi la kutekeleza Sera za Fedha na za Kibajeti ambazo zinalenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango imeendelea kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo lakini vilevile Tume ya Mipango iliandaa na kuwasilisha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 katika Mkutano wa Tano wa Bunge la Kumi na Moja mwezi Novemba, 2016.

Aidha, Tume ya mipango ilifanya ufuatiliaji wa miradi 42 ya Sekta ya Umma na binafsi hususan katika Sekta ya Viwanda, Maji, Kilimo, Nishati na Miundombinu katika Mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Tabora, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine ni kuratibu mikakati ya kupunguza umaskini. Katika hili Wizara iliendelea kurtibu jitihada za kupambana na umasikini ikiwemo kuandaa mpango wa Kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini ya hali ya umaskini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo za viashiria vya umasikini nchini, zinaonyesha kuwa kiwango cha umasikini ni asilimia 28.2 ikilinganishwa na asilimia 32 mwaka 2008. Hata

hivyo, kiwango hiki bado ni kikubwa hasa vijijini ambapo kuwango cha umasikini ni takriban asilimia 33.3 na hakikubaliki. Jitihada za Serikali kupambana na umaskini ni pamoja na kuongeza tija na thamani ya mazao na mifugo lakini pia uvuvi na shughuli nyingine za uchumi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za msingi za jamii, viashiria vinaonyesha matokeo mazuri ya kutia moyo ikiwa ni pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja ambavyo vimepungua kutoka vifo 51 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000. Nyumba na makazi zimekuwa bora zaidi lakini pia viwango vya upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia iliendesha mafunzo ambayo yalilenga kueleza juu ya maendeleo endelevu na hali ya umasikini nchini, lakini pia kukuza uelewa wa wataalam waweze kuchambua na kujumuisha malengo hayo katika mipango na bajeti katika mwaka 2017/2018. Maafisa 427 kutoka Halmashauri 185 na Maafisa 52 kutoka Serikali za Mikoa yote nchini walihudhuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ilifanya tathmini ya miradi inayotekelezwa ili kuondoa umasikini na kutunza mazingira katika Wilaya za Bunda, Sengerema, Bukoba, Ikingi, Ileje na Nyasa. Miradi iliyotekelezwa ilihusu ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki, uzalishaji wa nishati mbadala, yaani gesi ya majumbani kwa kutumia samadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine muhimu ilikuwa ni usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hadi mwezi Aprili, 2017 jumla ya makusanyo ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 13,604 sawa na asilimia 76 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 11,644.6 sawa na asilimia 77 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 1,600.8 sawa na asilimia 79 ya lengo la mwaka na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa

shilingi bilioni 398.7 sawa na asilimia 60 ya lengo. Mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia shilingi bilioni 4,715.7 sawa na asilimia 88 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo hayo yanatokana na kuendelea kuwepo kwa changamoto ikiwa ni pamoja na ukwepaji wa kodi, wigo mdogo wa vyanzo vya mapato, udhaifu latika ukusanyaji na elimu ndogo kwa walipa kodi. Wizara imeendelea kusimamia matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu mapendekezo ya wadau mbalimbali ya kuboresha Sera za Bajeti na hususan mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Serikali imepokea kiasi cha shilingi bilioni 2,340.1 sawa na asilimia 65 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, shilingi bilioni 111.4 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, yaani *general budget support* ambayo ni sawa na asilimia 23 ya mwaka. Shilingi bilioni 324.4 ni mifuko ya pamoja ya kisekta sawa na asilimia 87 na shilingi bilioni 1,904.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 69 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kupatikana kwa fedha za washirika wa maendeleo kunatokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kukamilika kwa vigezo na taratibu za kutoa fedha, lakini pia kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa upatikanaji wa mapato ya Serikali umesababisha utoaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kuwa chini ya matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotolewa hadi mwezi Machi, 2017 ni shilingi trilioni 14 matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia 79.2 ya lengo na shilingi trilioni tano ambayo ni sawa na asilimia 42.5 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine alikuwa ni kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Wizara ilitoa muongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti wa mwaka 2017/2018 ilichapisha vitabu vya makisio ya bajeti ya Serikali katika juzuu zote (moja mpaka nne) na kuviwasilisha Bungeni, Wizara pia ilifanyia marekebisho na kuchapisha vitabu vya makisio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 juzuu zote kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia iliandaa Waraka wa Hazina Na. 1 wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017, Mwongozo wa Mafunzo ya Sheria ya Bajeti na iliendesha mafunzo ya mfumo wa matumizi ya muda wa kati (*Medium Term Expenditure Framework*). Kadhalika, Wizara iliendesha mafunzo mbalimbali juu ya uboreshaji wa mifumo ya uandaaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha na kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Tulifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma katika Halmashauri 73, Baraza la Mitihani la Taifa, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) na matumizi ya fedha za chakula cha wanafunzi wa bweni na fedha za uendeshaji wa shule katika Mikoa 11. Pia Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za kutangaza utalii katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine ilikuwa ni kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Umma. Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali alifanya uhakiki wa madeni ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 yakiwemo madeni ya Walimu, alifanya uhakiki wa wastaafu wanaolipwa *pension* na Wizara na matokeo ya mradi wa huduma ya afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa malipo, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa malipo ya kuunganisha mfumo wa malipo wa *Tanzania Inter-bank Settlement System (TISS)* na Mamlaka za Serikali za Mitaa

46, lakini pia mfumo wa malipo wa *Electronic Fund Transfer* umeunganishwa katika malipo ya mishahara ya watumishi kwa Wizara za Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wizara imeendelea kuthamini mafunzo kwa watumishi 77 wa kada ya Uhasibu, Ugavi na *Computer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Deni la Taifa, Wizara imeendelea kusimamia deni la Taifa ili kuhakikisha inakopa mikopo yenye masharti nafuu ambayo hutumika kwenye miradi ya maendeleo. Serikali inapitia viwango vya deni la Taifa kila robo mwaka na kwa mwaka mzima ili kuhakikisha kuwa deni linaendelea kubaki himilivu. Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanya pia ukaguzi wa deni hilo na Serikali itazingatia ushauri utakaotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,218.1 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani ambalo hadi kufikia Aprili, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 912.87 sawa na asilimia 84 zilitumika. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 617.1 kwa ajili ya kulipia riba ya deni la nje na hadi Aprili, 2017 shilingi bilioni 456.57 sawa na asilimia 74 zilitumika kulipia deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 Serikali ilitarajia kukopa kutoka soko la ndani kiasi cha shilingi bilioni 3,777 kwa ajili ya kulipia mtaji (*roll over*) wadeni la ndani na hadi kufikia Aprili, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 3,963.17 kilikopwa kutoka soko la ndani kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la ndani sawa na asilimia 104 ya lengo. Serikali ilitenga shilingi bilioni 999.3 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje ambapo hadi kufikia Aprili, 2017 shilingi bilioni 811 sawa na asilimia 81 zilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa mifumo ya taarifa za kifedha, Wizara iliendelea na uandaaji wa mishahara na usambazaji wa nyaraka za taarifa za mishahara ya watumishi wa umma.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inandelea na kazi ya kuboresha mfumo wa kutolea taarifa ya za kulipia mishahara kwa njia ya kielektroniki ambao uko kwenye hatua ya usimikaji na utumiaji. Mwezi Aprili, 2017 Wizara tatu zimeanza kulipa mishahara kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuanzia mwezi Julai, 2017 Wizara, Mikoa, Halmashauri zilizobaki zitaanza rasmi kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa mali za Serikali, Wizara imeendelea kufanya uhakiki wa mali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali na imefanya uhakiki maalum wa mali za watu binafsi zilizochini ya uangalizi wa Serikali katika Vituo vya Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam. Wizara imekamilisha uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali katika mafungu 16. Wizara inaendelea pia na zoezi la kuondosha mali chakavu katika Wizara, Taasisi, Wakala, Mikoa na Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo jumla ya shilingi bilioni 8.42 zimekusanywa kutokana na mauzo ya mali hizo. Pia shilingi milioni 91.7 zimekusanywa ikiwa ni fidia kutoka kwa Kampuni za Bima kutokana na ajali zilizosababisha uharibifu wa magari ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ununuzi ya Umma, Serikali kupitia Wizara yangu imefanya mapitio ya Kanuni za Ununzi wa Umma na kanuni hizo zimetangazwa kupitia tangazo la Serikali Na. 333 la Disemba, 2016. Pia tumetoa mafunzo kwa Maafisa 65 wa Ununuzi na Ugavi Serikalini, lakini pia kuhusu mfumo wa malipo kwa njia ya *EPICOR 9*. Vile vile Serikali imefanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa Umma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ukaguzi wa hesabu za Serikali; Ofisi ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa mwaka 2015/2016 na *report* kuu tano zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi hiyo pia ilifanya ukaguzi wa hesabu za Taasisi za Serikali 199, Wizara na Idara

za Serikali zinazojitegemea 54, Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Wakala wa Serikali 30, Mifuko Maalum 13, Mabonde ya Maji tisa, Taasisi nyingine za Serikali 25 na Balozi za Tanzania nje ya nchi 34. Pia Ofisi ya CAG ilifanya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 171, Mashirika ya Umma 22 kati ya Mashirika 30 na Vyama vya Siasa vitatu kati ya vyama 22. Aidha, Ofisi ya CAG inaendelea na ukaguzi wa miradi ya maendeleo 492, lakini pia inaendelea na kutekeleza jukumu la ukaguzi katika taasisi 19 za Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Msajili wa Hazina, ofisi hiyo imeendelea na jukumu la kukusanya mapato yasiyo ya kodi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 500.13 zimekusanywa sawa na asilimia 121.3 ya makadirio. Makusanyo hayo yametokana na gawiwo la shilingi bilioni 352.69, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 136.48 na mawasilisho yanayotokana na mfumo wa udhibiti wa mawasiliano ya simu za mkononi (*Telecommunications Traffic Monitoring System - TTMS*) shilingi bilioni 10.96. Ofisi ya Msajili wa Hazina imekusanya shilingi bilioni 182.3 hadi Machi, 2017 sawa na asilimia 32.1 ikiwa ni makusanyo kutokana na marejesho ya mtaji uliozidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya ufuatiliaji na tathmini kwenye taasisi na mashirika ya umma 72 yaliyobinafishwa. Ufuatiliaji huo umeonesha kwamba wamiliki wa viwanda vinane wamekiuka masharti ya mikataba ya mauzo na kutoonyesha nia ya dhati ya kuvifufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo ni pamoja na *Tembo Chip Board, National Steel Corporation, Mang'ula Mechanical and Machine Tools, Mkata Sawmills, Tanganyika Packers* - Shinyanga; Kiwanda cha Korosho - Newala, Kiwanda cha Korosho - Lindi na Mgodi wa Pugu wa Kaolin. Aidha, hatua mbalimbali za kisheria dhidi ya baadhi ya wamiliki zimechukuliwa ikiwemo kuvirejesha chini ya umiliki wa Serikali. Kwa Mashirika na viwanda ambavyo bado vinasuasua, tumewataka wawekezaji kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mafao ya wastaafu, hadi kufikia Aprili, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 733.7 sawa na asilimia 73.8 kilitumika katika kulipa michango ya mwajiri kwa watumishi 540,530. Serikali imeendelea kuboresha huduma ya malipo kwa wastaafu ambao wanalipwa na Hazina kwa kulipa pensheni kila mwezi na mirathi moja kwa moja kwenye akaunti zao kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2017, shilingi bilioni 290.89 sawa na asilimia 97 kilitumika kulipa mafao ya wastaafu 1,775, mirathi 352 na pensheni kwa kila mwezi kwa wastaafu 55,481. Aidha, kumbukumbu za wastaafu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA ambao unajulikana kama *SAPERION* ambao hadi Aprili, 2017 kumbukumbu za wastaafu 95,092 zilikuwa zimewekwa. Kima cha chini cha pensheni cha Sh.100,000 ambacho wastaafu wa *PPF* walikuwa hawalipwi, kimeanza kulipwa tangu mwezi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi, kitengo husika (*Financial Intelligence Unit*) kimepokea na kuchambua taarifa 208 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Pia wamewasilisha taarifa fiche za fedha (*Financial Intelligence Packages*) 37 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na kufanya ukaguzi wa taasisi mbili za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kitengo hicho kimekamilisha kanuni za Taarifa za Usafirishaji na Uingizaji wa Fedha Taslimu kutoka na kwenda nje ya nchi (*Cross Border Declaration of Currency Reports Regulations*) na zimekwishachapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha rasimu ya stadi ya uwekezaji katika masuala mbalimbali ya Muungano, ambapo jumla ya mashirika tisa yamebainika kuwa yanatekeleza masuala

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya Muungano na kwa sehemu kubwa mtaji wake ulitokana na upande mmoja wa Muungano yaani Tanzania Bara. Pia Tume imekamilisha stadi ya kubainisha mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na stadi ya uchambuzi wa masuala ya fedha yanayohusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia kitengo cha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, imeendelea kuchambua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyofanyiwa uchambuzi ni pamoja na mradi wa barabara ya kulipia ya Dar es Salaam hadi Chalinze; mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam awamu ya pili; mradi wa kufua umeme *megawatt* 200 - 350 wa Somanga Fungu Mkuranga; mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi III na mradi wa kuzalisha dawa Bohari Kuu (*MSD*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto katika miradi ya ubia ikiwa ni pamoja na ukosefu wa wataalam wa kuchambua na kusimamia miradi katika sekta ya umma na sekta binafsi; uelewa mdogo wa jamii kuhusu miradi ya ubia na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa kifupi sana nieleze malengo ya mpango na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018. Naomba niyataje tu kwa sababu yanawiana na haya ambayo nimetoka kueleza kwa maana ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ambayo tutaendelea kusimamia katika mwaka ujao wa fedha ni:-

Kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; kuratibu mipango ya maendeleo ya Taifa; Kuratibu mikakati ya kupunguza umaskini; Kusimamia ukusanyaji wa mapato

ya Serikali ikiwemo mapato ya ndani, misaada na mikopo;Uandaaji na usimamizi wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali; Usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma; Usimamizi wa malipo; Usimamizi wa deni la Taifa; Usimamizi wa mifumo ya taarifa za kifedha na Usimamizi wa mali za Serikali; Ununuzi wa umma; Ukaguzi wa hesabu za Serikali; Usimamizi wa mashirika na taasisi za umma lakini pia kuhakikisha kwamba tutaendelea kuboresha taarifa za wastaafu na kusimamia malipo ya pensheni zinazolipwa moja kwa moja Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mwaka ujao wa fedha, tutaendeleza jitihada za kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi lakini pia kuhakikisha kwamba kazi ya Tume ya Pamoja ya Fedha inafanya kazi yake ipasavyo na pia kuendeleza ubia kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nilieleze Bunge lako Tukufu kuhusu Makadirio ya Mapato, Matumizi na maombi ya fedha kwa mwaka wa 2017/18. Katika mwaka 2017/2018, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 522.34 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi ya pango, mauzo ya leseni za udalali, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018. Wizara ya Fedha na Mipango imekadiria kutumia fedha kiasi cha shilingi bilioni 11,757.125 kwa mafungu yote tisa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10,328.04 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,429.084 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi bilioni 87.996 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 778.612 kwa ajili ya matumizi mengineyo yaani *other charges* na shilingi bilioni 9,461.433 ni Deni la Taifa na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

huduma nyingine. Aidha, katika fedha za matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 1,382.976 ambazo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 46.108 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango. Katika fungu hili kwa mwaka 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 55.04. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 8.08 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 46.96. Upande wa miradi ya maendeleo tunaomba shilingi bilioni 11.57 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 3.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 8.07 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21 – Hazina. Katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida tunaomba shilingi bilioni 570.43. Kati ya fedha hizo mishahara ya fungu hili ni shilingi bilioni 40.64 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 529.79 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya Idara, Taasisi zilizo chini ya fungu hili pamoja na matumizi maalum. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, tunaomba idhini ya shilingi bilioni 1,395.63 na kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 1,364, fedha za nje ni shilingi bilioni 31.63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 22 – Deni la Taifa. Katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha, matumizi ya kawaida shilingi bilioni 9,472.12 na kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 10.69, matumizi mengineyo ambayo ni malipo ya madeni na michango ya mifuko ya hifadhi za jamii shilingi bilioni 9,461.43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali. Katika Fungu hili mwaka 2017/2018, Wizara inaomba

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 45.96 na kati ya fedha hizo mishahara shilingi bilioni 8.4, matumizi mengineyo shilingi bilioni 37.56. Miradi ya maendeleo shilingi bilioni 3.6 ambapo kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 2.0 na fedha za nje shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu namba 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina. Katika Fungu hili kwa mwaka 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 104.92, ambapo kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 2.69 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 102.23. Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 2, kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 1 na fedha za nje shilingi bilioni 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha – Fungu Namba 10. Katika Fungu hili katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 1.39, kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 0.43 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 0.96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu. Katika Fungu hili kwa mwaka wa2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha, matumizi ya kawaida shilingi bilioni 1.52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 61.83 ambapo kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 17.31 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 44.52. Kwa upande wa miradi ya

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

maendeleo, tunaomba idhini ya shilingi bilioni 11.8 ambapo kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 8.0 na fedha za nje ni shilingi bilioni 3.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 66 – Tume ya Mipango. Katika Fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 4.93 ambapo mishahara ni shilingi bilioni 1.6 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 3.33. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 66 tunaomba idhini ya shilingi bilioni 4.47 ambazo zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii, kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo kwa namna moja au nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru sana wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha, [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango, ahsante sana.



**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT.  
PHILIP I. MPANGO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA  
2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2017/18.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/18.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Aidha, ninawapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanazofanya kwa dhati kumsaidia Rais katika utawala wa nchi yetu na kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, kumetokea matukio mbalimbali ambayo yamewagusa Watanzania. Katika kipindi hicho Bunge lako Tukufu lilipatwa na misiba ya kuondokewa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - CCM na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha

aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum-CHADEMA. Aidha, Taifa lilipata msiba mwingine wa aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la tisa Mheshimiwa Samwel John Sitta. Vile vile, Taifa lilipata maumivu makubwa kuondokewa na wanafunzi 32, walimu wawili (2) na dereva mmoja (1) wa shule ya Msingi Lucky Vicent kutokana na ajali iliyotokea Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha tarehe 6

Mei, 2017. Aidha, Taifa lilipoteza askari polisi wanane (8) waliouawa katika kijiji cha Uchembe Kata ya Mjawa Tarafa ya Kibiti na vile vile wananchi ambao walikatishwa maisha kwa nyakati tofauti mwaka huu na kundi la kihalifu katika Wilaya ya Rufiji. Taifa letu pia limekumbwa na maafa ya mafuriko kutokana na mvua zilizokuwa zinaendelea kunyesha hususan katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Dar es salaam pamoja na Zanzibar ambazo zilisababisha vifo, majeruhi pamoja na uharibifu mkubwa wa mali. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. na awaponye haraka majeruhi wote. **Amina!** Nitumie fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati wale wote waliotoa misaada ya hali na mali kwa familia za wahanga wa matukio hayo.

**5. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwapongeza Wabunge wapya wa Bunge lako hili Tukufu walioapishwa hivi karibuni ambao ni Mhe. Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Mhe. Anne Killango Malecela (Mb.), Mhe. Juma Ali Juma (Mb.), Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.), Mhe. Salma Rashidi Kikwete (Mb.), Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare (Mb.) na Mhe. Catherine Nyakao Ruge (Mb.). Ninawapongeza sana na kuwakaribisha katika Bunge hili ili kwa pamoja tuweze kuwatumikia wananchi. Aidha, kwa namna ya pekee ninampongeza Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Vivyo hivyo, ninampongeza M h e . Dkt. Harrison George Mwakyembe Mbunge wa Kyela, kwa kukabidhiwa dhamana ya Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

**6. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2017/18 kwa mafanikio makubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb.) kwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa umakini. Natoa shukurani nyingi kwa Kamati yake kutokana na maoni, ushauri na mapendekezo waliyotoa ambayo yamekuwa msaada mkubwa sana katika kuboresha Mpango na Bajeti ya Mwaka 2017/18. Aidha, ninawashukuru wenyeviti wa kamati za kudumu za Bunge kwa kuchambua na kutoa ushauri mzuri uliolenga kuboresha bajeti za kisekta ili ziendane na mahitaji ya wananchi.

**7. Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji Mbunge wa Kondo na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano na msaada anaonipatia katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu unafanikiwa. Aidha, nawashukuru Bw. Doto James (Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali), Naibu Makatibu Wakuu Bibi Dorothy S. Mwanyika, Bibi Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu kwa kusimamia shughuli za kila siku za kiutendaji za Wizara yangu kwa juhudi kubwa. Pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Prof. Benno Ndulu - Gavana wa Benki Kuu, Ndg. Charles E. Kichere - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Dkt. Oswald J. N. Mashindano - Msajili wa Hazina na Dkt. Albina Chuwa - Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kutekeleza majukumu ya kusimamia kwa weledi taasisi nyeti walizokabidhiwa. Taasisi hizi zinatoa mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nawashukuru pia, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zote zilizoko chini ya Wizara, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kutimiza wajibu wao vema wa kuwatumikia watanzania.

**8.** Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, yafuatayo ni maelezo ya majukumu ya Wizara katika

kujenga msingi wa uchumi imara, mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2016/17 na malengo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18.

## **2.0 MAJUKUMU YA WIZARA KATIKA KUJENGA MSINGI WA UCHUMI IMARA**

**9. Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha ujenzi wa uchumi imara, bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo: Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020; Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21; Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 lengo kuu ikiwa ni kutekeleza kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu. Ili kufikia lengo hili, Wizara imejikita katika kuhakikisha usimamizi bora na ukusanyaji wa mapato, kupanua wigo wa vyanzo vipya vya kodi, na kusimamia kwa umakini zaidi matumizi ya fedha za Umma na pia kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

**10. Mheshimiwa Spika**, katika kujenga uchumi imara, Wizara inaongozwa na Sera ya Fedha. Utekelezaji wa sera hii umejikita katika kuhakikisha kuwa kuna usimamizi wa malengo mapana ya kitaifa ya ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, na mapato na matumizi ya Serikali. Katika mwaka 2016/17, Serikali ilikusudia kutimiza malengo yafuatayo: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 7.3 kwa mwaka kutoka asilimia 7.2 kwa mwaka 2016 na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.4 kwa mwaka 2017; kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki kwenye kiwango cha tarakimu moja; na nakisi ya bajeti ya Serikali isiyozidi asilimia 4.5 ya Pato la Taifa.

**11. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha na kubakia katika wastani wa asilimia 7. Ukuaji huu ulitokana na ukuaji wa kasi wa shughuli za kiuchumi katika sekta ya mawasiliano asilimia 13.0, sekta ya ujenzi asilimia 13.0, sekta ya usafirishaji na uhifadhi asilimia 11.8, pamoja na sekta ya madini na uchimbaji mawe ambayo ilikua kwa asilimia 11.5.

Mchango mkubwa wa kiuchumi kwa mwaka 2016 ulitokana na sekta ya ujenzi (asilimia 20.2), usafirishaji na uhifadhi (asilimia 10.8), biashara ya jumla na rejareja (asilimia 9.9), mawasiliano (asilimia 8.3) na uzalishaji viwandani (asilimia 8.2).

**12. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji thabiti wa Sera ya Fedha na usimamizi madhubuti wa sera ya ukusanyaji mapato ya Serikali na matumizi ulisababisha kuwepo kwa utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na kushuka kwa bei ya nishati. Mfumuko wa bei uliendelea kubakia chini ya asilimia 7 katika kipindi chote cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2016/17, ukiwa ndani ya ukomo wa asilimia 8.0 chini ya makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mfumuko wa jumla wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.5 mwezi Juni 2016 hadi asilimia 5.0 mwezi Desemba 2016. Vile vile, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja katika siku zijazo kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta nchini inayotokana na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia na utulivu wa thamani ya shilingi.

### **3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17**

**13. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake kupitia mafungu tisa ya kibajeti na Taasisi na Mashirika yaliyo chini yake (**Jedwali na.1**). Mafungu hayo ni Fungu 50-Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 21-Hazina, Fungu 22-Deni la Taifa, Fungu 23-Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10-Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13-Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 7- Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 66-Tume ya Mipango na Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**14. Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla, katika mwaka 2016/17, Wizara ilipanga kutekeleza yafuatayo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla;
- ii. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa;
- iii. Kuratibu utekelezaji wa Mikakati ya Kupunguza Umasikini;
- iv. Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali;
- v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- vi. Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
- vii. Kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali kwenye mtandao wa malipo ya Serikali;
- viii. Kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje;
- ix. Kusimamia Mali za Serikali;
- x. Kukagua hesabu za Serikali;
- xi. Kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma;
- xii. Kuendelea kuboresha huduma za pensheni kwa wastaafu na malipo ya mirathi;
- xiii. Kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;
- xiv. Kuishauri Serikali katika masuala ya fedha za Jamhuri ya Muungano yanayohusu matumizi ya kawaida katika Serikali zote mbili;

xv. Kupokea na kuchambua miradi ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi;

xvi. Kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma; na

xvii. Kusimamia na kuratibu taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara.

### 3.1 MAPATO KWA MWAKA 2016/17

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 1,307,074,874,282 (Bilioni 1,307.07)** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi ya pango, mauzo ya leseni za minada, gawio, marejesho ya mikopo, michango ya asilimia 15 ya pato ghafi, mawasilisho kutoka Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya simu na marejesho ya mitaji iliyozidi kutoka katika taasisi na mashirika ya umma. Hadi Machi, 2017 jumla ya **Shilingi 500,274,001,756 (Bilioni 500.27)** zilikuwa zimekusanywa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada, gawio, marejesho ya mikopo, michango ya asilimia 15 ya pato ghafi na mawasilisho kutoka Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya simu sawa na asilimia **91** ya lengo la kukusanya **shilingi 550,464,547,282 (Bilioni 550.46)**. Aidha marejesho ya mtaji uliozidi wa **shilingi 182,327,655,320.84 (Bilioni 182.33)** zilikusanywa ikiwa sawa na asilimia **24.1** ya lengo ya kukusanya **shilingi 756,610,327,000 (Bilioni 756.61)**.

### 3.2 MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2016/17

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote tisa (9) iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **shilingi 8,716,493,400,510 (bilioni 8,716.49)** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 45,454,478,000 (bilioni**

45.45) zilikuwa kwa ajili ya mishahara na **shilingi 8,671,038,922,510 (bilioni 8,671.04)** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

17. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi mengineyo **shilingi 8,009,341,187,000 (bilioni 8,009.34)** zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa na huduma nyinginezo na **shilingi 661,697,735,510 (bilioni 661.70)** zilikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya **shilingi 6,901,168,195,852 (bilioni 6,901.17)** zilitumika, sawa na asilimia 79 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo, **shilingi 31,067,617,442 (bilioni 31.07)** ni kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 68 ya bajeti ya mishahara iliyoidhinishwa; na **shilingi 6,870,100,578,409 (bilioni 6,870.10)** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 79 ya bajeti ya matumizi mengineyo iliyoidhinishwa (**Jedwali Na. 2**).

### 3.3 MATUMIZI KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/17

18. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **shilingi 791,998,424,268 (bilioni 791.99)** ziliidhinishwa kutumika kwa mafungu yote tisa. Kati ya fedha hizo, jumla ya **shilingi 723,150,000,000 (bilioni 723.15)** ni fedha za ndani na **shilingi 68,848,424,268 (bilioni 68.84)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya **shilingi 18,898,317,854 (bilioni 18.89)** zimetumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,315,456,810 (bilioni 1.31)** ni fedha za ndani na **shilingi 17,582,861,044 (bilioni 17.58)** ni fedha za nje. Mchanganuo umeoneshwa katika **jedwali Na.3**.

### 3.4 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2016/17

19. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kuleleza Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17.



### 3.4.1 Kubuni na kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

**20. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo yenye jukumu la kusimamia na kuhakikisha Uchumi Jumla unakua na kuwanufaisha wananchi wote. Ili kufanikisha jukumu hili, Wizara imeendelea kuhakikisha sera za kukuza uchumi na kuondoa umasikini zinatungwa ili kusimamia sheria, kanuni na taratibu za fedha, Mapato na Matumizi ya fedha za Umma na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Sera ya Fedha inajumuisha viashiria vya mwenendo wa uchumi jumla kama vile: mfumuko wa bei, riba za mikopo na amana, thamani ya shilingi, akiba ya fedha za kigeni, na ujazi wa fedha na karadha. Sera ya Mapato na Matumizi inajumuisha mapato ya ndani (mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi na mikopo ya ndani) na mapato ya nje (misaada, mikopo yenye masharti nafuu na mikopo yenye masharti ya kibiashara). Kipengele cha matumizi kinajumuisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

**21. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuandaa na kutekeleza sera za fedha na kibajeti zinazolenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa. Hadi kufikia Machi, 2017 kasi ya ukuaji wa uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha na kubakia katika wastani wa asilimia 7 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

**22. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia iliendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Fedha, kutumia mwongozo wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha wa mwaka 2014-16, kusimamia Sheria ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015, Sheria ya Masoko ya Bidhaa ya Mwaka 2015 na kusimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali za fedha zilizotungwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata na kutumia huduma zilizo rasmi za fedha kwa lengo la kupunguza umasikini na kukuza Pato la Taifa. Aidha, Serikali ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2000 kwa kutunga Sera ya Taifa ya

Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2016 na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo. Lengo la sera hiyo ni kuimarisha huduma jumuishi za kifedha kwa kujenga mazingira wezeshi yatakayoleta ufanisi wa utoaji huduma kwenye sekta ndogo ya fedha nchini kwa wananchi wenye kipato cha chini, kaya na shughuli za biashara na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umasikini. Matokeo ya utekelezaji wa Sera hii yatakuwa ni urasimishaji wa huduma ndogo za fedha, kuhamasisha utamaduni wa kuweka akiba na kuanzisha mfumo wa kulinda na kushughulikia malalamiko ya watumiaji.

### **3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

**23. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Mipango imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo na kutoa elimu kwa wadau kwa kutekeleza yafuatayo: kuchapisha na kusambaza nakala 10,000 za Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), kutoa elimu kwa Maafisa Mipango 185 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Maafisa Mipango 237 kutoka Halmashauri kuhusu Mwongozo wa Uwekezaji wa Umma ili kuwajengea uwezo wa kutafsiri vipaumbele vya kitaifa katika mipango ya maendeleo katika maeneo yao; kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 930 za Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma; na kutoa elimu ya Mwongozo huo. Aidha, Tume ya Mipango iliandaa na kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18 katika mkutano wa Tano wa Bunge la 11, Novemba 2016.

**24. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Tume ya Mipango, kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta ilifanya ufuatiliaji wa miradi 42 ya Sekta ya Umma na binafsi hususan katika sekta ya viwanda, maji, kilimo, nishati na miundombinu katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara. Taarifa ya ufuatiliaji huo imewezesha Wizara

kubaini mafanikio na changamoto ambazo zimetumika kupanga hatua za kuchukua wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2017/18.

### **3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umasikini**

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea kuratibu jitihada za kupambana na umasikini nchini ikiwemo kuandaa Mpango wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Hali ya Umasikini Nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Sekta mbalimbali inaendelea kukamilisha Taarifa ya Hali ya Umasikini Nchini. Taarifa hii itaonesha hali ilivyokuwa mwaka 2016 nchi ilipoanza kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kurahisisha kufanyika kwa tathmini na utoaji wa taarifa kuhusu mwelekeo wa hali ya Umasikini hadi mwaka 2030.

**26. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliendesha mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Mipango na Wachumi kutoka idara mbalimbali za Halmashauri zote nchini kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu na Hali ya Umasikini Nchini. Mafunzo hayo yalilinga kuelimisha na kukuza uelewa wa wataalam mbalimbali kwa lengo la kuchambua na kujumuisha malengo hayo katika mipango na bajeti katika mwaka 2017/18. Jumla ya Maafisa 427 kutoka Halmashauri 185 na Maafisa 52 kutoka Sekretarieti za Mikoa yote nchini walihudhuria.

**27. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (Economic and Social Research Foundation -ESRF) ilifanya tathmini ya miradi inayotekelezwa ili kuondoa umasikini na kutunza mazingira katika wilaya za Bunda (Mara), Sengerema (Mwanza), Bukoba (Kagera), Ikungi (Singida), Ileje (Mbeya) na Nyasa (Ruvuma). Miradi hii inayotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na UNDP ni ufugaji wa samaki katika vizimba ndani ya Ziwa Victoria na

katika malambo nje ya ziwa, ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa na uzalishaji wa nishati mbadala (gesi) ya majumbani kwa kutumia samadi.

### 3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

#### (a) Mapato ya Ndani

**28. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, sera za mapato zililinga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 17,798.10 (ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa). Hadi Machi, 2017 jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) yalikuwa shilingi bilioni 12,469.9, sawa na asilimia 70 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 10,626.4 sawa na asilimia 70.3 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 15,105.1; mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 1,485.0 sawa na asilimia 73.2 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 2,027.6; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 358.5 sawa na asilimia 53.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 665.4 kwa mwaka. Vile vile, mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia shilingi bilioni 4,296.10, sawa na asilimia 80 ya shilingi bilioni 5,374.30 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka.

**29. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato; kupanua wigo wa walipa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kuingia katika mfumo wa kodi; kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake; kusimamia ulipaji ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo; na kuendelea kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu mapendekezo ya wadau mbalimbali ya kuboresha sera za bajeti hususan mapato kupitia Kikosi Kazi cha Maboresho na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016.

**(b) Misaada na Mikopo nafuu toka kwa Washirika wa Maendeleo**

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia Bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 3,600.8. Kati ya fedha hizo, Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS) ni shilingi bilioni 483, mifuko ya kisekta ni shilingi bilioni 372.1 na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 2,745.7.

**31. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 Serikali imepokea kiasi cha shilingi bilioni 2,247.9 sawa na asilimia 62 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi kilichopokelewa, shilingi bilioni 111.4 ni Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS) sawa na asilimia 23 ya ahadi ya mwaka, shilingi bilioni 292.9 ni za mifuko ya pamoja ya kisekta sawa na asilimia 79 na shilingi bilioni 1,843.6 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 67 ya lengo la mwaka.

**32. Mheshimiwa Spika**, kuchelewa kupatikana kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kunatokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kuchelewa kukamilika kwa vigezo na taratibu za kutoa fedha tofauti na ilivyokusudiwa kwa baadhi ya Washirika wa Maendeleo; taratibu za majadiliano kutokamilika kwa wakati; uthamini wa mali na ulipaji wa fidia kwa miradi mikubwa huchukua muda mrefu hivyo kuathiri utoaji wa fedha; na kasi ndogo ya utekelezaji wa baadhi ya miradi ya kisekta ambayo husababisha Washirika wa Maendeleo kuchelewa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika.

**3.4.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**33. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17, Wizara ilitekeleza yafuatayo: kuandaa, kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2017/18 kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Vitabu vya Makisio

ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 (Juzuu Na. I, II, III na IV) na kuviwasilisha Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa; na kijitabu cha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17 toleo la Wananchi (Citizen Budget). Aidha, Wizara ilivifanyia marekebisho na kuchapisha Vitabu vya Makisio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 (Juzuu Na. I, II, III na IV) kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

**34. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Bajeti ya Serikali inasimamiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa Sheria, Wizara iliandaa: Waraka wa Hazina Na.1 wa Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2016/17, Mwongozo wa Mafunzo ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kijitabu kinachofafanua Sheria ya Bajeti na kuendesha mafunzo ya Sheria ya Bajeti kwa Maofisa 187 kutoka kwa Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo ya Mfumo wa Matumizi wa Muda Kati (MTEF) kwa Maofisa 1,089 wakiwemo Wakurungezi wa Sera na Mipango, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mipango, Wakuu wa Idara za Mipango wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Maofisa wa Bajeti na Mipango kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kadhalika, Wizara iliendesha mafunzo mbalimbali juu ya uboreshaji wa mifumo ya uandaaji wa bajeti ikiwemo Mfumo wa Uandaaji wa Bajeti kwa kwa kuzingatia Programu (Programme Based Budgeting) pamoja na kuboresha Mfumo wa Takwimu za Fedha za Serikali (GFS) kwa kuzingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Takwimu za Fedha za Serikali wa mwaka 2014 (GFSM 2014).

**35. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha usimamizi wa Bajeti ya Serikali hususan kwenye miradi ya maendeleo, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha na kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2014/15 na 2015/16. Aidha, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma katika kipindi cha kufikia mwezi Machi, 2017 katika Halmashauri 73, Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Ofisi ya Rais – TAMISEMI na matumizi ya fedha za chakula cha wanafunzi wa bwani na fedha za uendeshaji wa shule katika mikoa 11. Vile vile, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za kutangaza utalii

ndani na nje ya nchi katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCCA). Taarifa zinazotokana na ufuataliaji zinaonesha kuwa bado zipo changamoto zinazotakiwa kufanyiwa kazi katika usimamizi na utekelezaji wa maeneo husika.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia ulipaji wa mishahara ya watumishi wa Serikali, Wizara imeendelea kufanya uhakiki wa taarifa za kiutumishi na mishahara katika Taasisi mbalimbali zikiwemo, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Chuo Kikuu Huria; kuhakiki na kufanya uchambuzi wa taarifa za michango katika Mfuko wa Pensheni wa PSPF kwa kipindi cha miaka tisa kuanzia mwaka 2006/07 hadi Juni, 2016; kufanya uhakiki wa mafao ya kiinua mgongo (gratuity) kwa Wanataaluma wenye ajira za mkataba katika vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Huria, Sokoine, Mzumbe, na Chuo cha Ufundi Arusha.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya utoaji wa taarifa za kibajeti kwa Umma, Wizara iliandaa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 zikiwemo: Taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; taarifa za migao ya fedha kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na taarifa ya uhamisho wa fedha katika Mafungu mbalimbali na kuziweka kwenye Tovuti ya Wizara. Utoaji wa taarifa hizi kwa wakati pia hutumiwa kama kigezo cha kutathmini uwazi wa Serikali katika utoaji wa taarifa za kibajeti kwa Umma pamoja na wadau wengine nje ya nchi chini ya mpango wa kimataifa unaojulikana kama "Open Budget Survey".

#### **3.4.6 Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali

imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa madeni ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 yakiwemo madeni ya walimu hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2015, uhakiki wa wastaafu wanaolipwa pensheni na Wizara na uhakiki wa matokeo ya mradi wa huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa unaofadhiliwa na Mfuko wa Afya na Benki ya Dunia.

**39. Mheshimiwa Spika**, majukumu mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kusimamia na kuendeleza Kada ya Ukaguzi wa Ndani na Kamati za Ukaguzi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Idara iliendesha mafunzo yanayohusu mbinu za kusimamia vihatarishi katika sekta ya Umma kwa wakaguzi wa ndani 552, wajumbe wa Kamati za Ukaguzi 312, wajumbe wa Kamati za fedha, Uongozi na Mipango 229 kutoka Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waratibu wa usimamizi wa vihatarishi 80 na Wajumbe wa menejimenti 75.

### 3.4.7 Usimamizi wa Malipo

**40. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa malipo kwa kuunganisha mfumo wa malipo wa TISS katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 zilizopo katika Mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Mbeya, Songwe, Arusha, Dodoma, Tanga na Morogoro. Mfumo wa Malipo wa EFT umeunganishwa katika malipo ya mishahara ya watumishi waliopo katika Wizara za: Fedha na Mipango; Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na Elimu, Sayansi na Teknolojia. Uunganishwaji wa Mifumo hii ya Malipo imeongeza ufanisi katika ulipaji wa malipo ya Serikali na kupunguza gharama za huduma za kibenki. Aidha, Wizara imeendelea kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 77 wa kada ya uhasibu, ugavi na kompyuta kutoka kwenye Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na kutoa mafunzo kwa Watumishi wapatao 928 wa kada ya uhasibu ya jinsi ya kutayarisha hesabu kwa kutumia viwango vya kimataifa vya Uhasibu (IPSAS Accrual).



### 3.4.8 Deni la Taifa

**41. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kusimamia Deni la Taifa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada **SURA 134**. Ili kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linahimilika, Serikali inakopa mikopo yenye masharti nafuu ambayo hutumika kwenye miradi ya maendeleo yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na ujenzi wa mitambo ya kufua Umeme. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau kila mwaka na robo mwaka inapitia viwango vya deni la Taifa ili kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu. Vile vile, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanya ukaguzi wa deni hilo na Serikali inapitia taarifa hiyo na itazingatia ushauri uliotolewa katika taarifa hiyo.

**42. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,218.10 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani ambapo hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 796.16 sawa na asilimia 65 zilitumika. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 617.10 kwa ajili ya kulipia riba ya deni la nje. Hadi Machi, 2017 shilingi bilioni 436.59 sawa na asilimia 71 zimetumika kulipia deni hilo.

**43. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Serikali ilitarajia kukopa kutoka soko la ndani kiasi cha shilingi bilioni 3,777.11 kwa ajili ya kulipia mtaji (rollover) wa deni la ndani. Hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 3,657.74 kilikopwa kutoka soko la ndani kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la ndani sawa na asilimia 97 ya lengo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 999.37 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje ambapo hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 766.02 sawa na asilimia 77 zilitumika kwa ajili hiyo.

### 3.4.9 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha

**44. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea na jukumu lake la uandaaji wa mishahara na usambazaji wa nyaraka za taarifa za mishahara ya watumishi wa umma. Aidha, Wizara inaendelea na kazi ya

kuboresha Mfumo wa kutolea taarifa za kulipia mishahara kwa watumishi wa Umma kwa njia ya Kielektroniki (Government Salaries Payment Platform and Government Online Salary Slip Portal) ambao uko kwenye hatua ya usimikaji na utumiaji. Mwezi Aprili, 2017 Wizara tatu ambazo ni Fedha na Mipango; Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na Elimu, Sayansi na Teknolojia zimeanza kulipa mishahara kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki na kuanzia mwezi Julai, 2017 Wizara, Mikoa, Halmashauri, Taasisi na Wakala za Serikali zilizobaki zitaanza rasmi kutumia mfumo huo.

**45. Mheshimiwa Spika**, kwa kutumia Mfumo huu wa Kielektroniki, kila ofisi ya Afisa Masuuli italazimika kuhakiki orodha ya malipo ya mishahara kwa njia ya Kielektroniki kabla ya malipo ya mishahara kufanyika. Orodha ya watumishi waliohakikiwa na kuidhinishwa na Afisa Masuuli ndiyo orodha itakayotumika kwa mwezi husika. Aidha, maboresho haya yatapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uandaaji na usambazaji wa taarifa za mishahara pamoja na mishahara hewa na kufanya Serikali kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kilikuwa kinalipwa kwa watumishi wasio stahili.

### **3.4.10 Usimamizi wa Mali za Serikali**

**46. Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora wa Mali za Serikali, Wizara imeendelea kufanya uhakiki wa mali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali ambapo jumla ya hakiki 160 zimefanyika. Aidha, Wizara imefanya uhakiki maalum wa mali za watu binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali katika vituo vya Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam. Uhakiki huu ni muhimu kwa Serikali kwa kuwa utaipunguzia mzigo wa kulipa fidia kutokana na mapungufu katika uangalizi na usimamizi wa mali hizo. Vile vile, Wizara imekamilisha kufanya uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali katika mafungu 16 ili kuwa na taarifa sahihi za mali za Serikali.

**47. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na zoezi la uondoshaji wa mali chakavu katika Wizara, Taasisi, Wakala,

Mikoa, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo jumla ya shilingi bilioni 8.42 zilikusanywa kutokana na mauzo ya mali hizo. Aidha, Wizara imekusanya kiasi cha shilingi milioni 91.71 ikiwa ni fidia kutoka kampuni za Bima kutokana na ajali zilizosababisha uharibifu wa magari ya Serikali na tozo kwa watumishi wa Umma kutokana na upotevu wa mali ya Serikali.

### **3.4.11 Ununuzi wa Umma**

**48. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara imetekeleza yafuatayo: kufanya mapitio ya Kanuni za Ununuzi wa Umma na kukamilisha marekebisho yake ambapo kanuni hizo zimetangazwa kupitia Tangazo la Serikali namba 333 la Desemba, 2016; kutoa mafunzo kwa maafisa 65 wa ununuzi na ugavi Serikalini juu ya matumizi ya mfumo wa malipo kwa njia ya EPICOR 9; kuboresha Daftari la Maafisa Ununuzi na Ugavi waliopo serikalini na kutoa mafunzo kwa watumiaji 82 wa Daftari hilo; kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Shughuli za Ununuzi na Ugavi Serikalini; na kukamilisha zoezi la kufanya tathmini ya ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma nchini.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Ununuzi wa Umma (PPRA) imefanya chunguzi za zabuni 11 zinazohusu ununuzi ambapo kati ya hizo chunguzi nne zimekamili na matokeo yake kuwasilishwa katika taasisi husika kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotokana na chunguzi hizo. Aidha, Mamlaka imefanya ukaguzi wa taratibu za utoaji wa zabuni na utekelezaji wa miradi na mikataba itokanayo na ununuzi wa Umma katika Taasisi 70, zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea 15, Mashirika ya Umma 30 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 25. Taarifa ya ukaguzi huo imebainisha mapungufu katika maeneo ya usimamizi wa mikataba, utunzaji wa nyaraka, utumiaji wa mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za ununuzi kwa njia ya kielektroniki pamoja na kushughulikia malalamiko ya wazabuni.

**50. Mheshimiwa Spika**, majukumu mengine yaliyotekelezwa na PPRA ni pamoja na: kutoa mafunzo ya Mfumo wa Utunzaji wa Taarifa za Ununuzi kwa watumishi 774 kutoka taasisi nunuzi za umma 472 na kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi ya Umma (Sura 410) na Kanuni zake kwa watumishi wa umma 711 wakiwemo Maafisa Masuuli, Wakuu wa Taasisi, Wajumbe wa Bodi za Zabuni, Wakaguzi wa ndani na wafanyakazi wa Idara mbalimbali kutoka Taasisi za Umma 118. Aidha, Mamlaka ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Mfumo kamili wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Mtandao kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, Idara ya Bohari ya Dawa, Wakala ya Serikali Mtandao na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora chini ya mpango wa Regional Communications Infrastructure Program (RCIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mfumo utaanza kutumika baada ya kukamilika kwa utoaji mafunzo kwa taasisi 100 za majaribio. Mfumo huu unatarajiwa kutumika kwa manunuzi ya umma yahasuyo dawa, vifaa tiba na bidhaa mtambuka kuanzia mwaka 2017/18.

**51. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini imenunua magari 415 kupitia utaratibu wa ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja na hivyo kuokoa shilingi bilioni 3.67. Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa Ofisi, ghala na kisima cha kuhifadhi mafuta katika mkoa wa Katavi.

**52. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma ilipokea jumla ya rufaa 31. Kati ya hizo, rufaa 21 zilishughulikiwa na kutolewa maamuzi, rufaa 4 ziliondolewa na walalamikaji wenyewe na rufaa 6 bado ziko kwenye hatua mbalimbali za kutolewa maamuzi.

**53. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 Wizara kupitia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ilitekeleza yafuatayo: ilisajili jumla ya Wataalam 1,275 wa fani ya Ununuzi na Ugavi kati ya wataalam 2,000 ambao ilipanga kuwasajili kwa mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 24 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Bodi katika ngazi mbalimbali kufikia 6,412

na kuendesha mitihani ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi katika ngazi mbalimbali ambapo watahiniwa 448 sawa na asilimia 35 walifaulu. Aidha, Bodi imezindua mtaala mpya wa mafunzo ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi ulioanza kutumika kuanzia Novemba, 2016 unaojikita katika kumjengea umahiri mtahiniwa ili kukidhi ushindani wa soko la ajira rasmi na isiyo rasmi.

**54. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Bodi ilifanya ukaguzi wa wanataaluma wenye sifa za kufanya kazi za Ununuzi na Ugavi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Bodi kwenye taasisi 24 katika mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo taasisi hizo zilishauriwa kuajiri wataalam waliosajiliwa na Bodi. Aidha, Bodi imekamilisha marekebisho ya Kanuni GN.364 na GN.365 za mwaka 2009 ili ziendane na marekebisho ya sheria Na. 23 ya mwaka 2007 kwa lengo la kuleta maboresho katika utendaji na ufanisi wa majukumu ya Bodi. Vile vile, Bodi imeendelea kutoa elimu kwa wataalam wa Ununuzi na Ugavi kupitia warsha za kila mwezi ambapo jumla ya warsha 9 ziliendeshwa na kuhudhuriwa na wanataaluma wapatao 343 kutoka mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar.

### **3.4.12 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

**55. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiyo yenye jukumu la kufanya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Katika kutimiza jukumu hilo, hadi kufikia Machi, 2017 ukaguzi wa mwaka 2015/16 umefanyika na ripoti kuu 5 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Machi, 2017. Ofisi ilifanya ukaguzi wa hesabu za taasisi za Serikali 199, Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea 54, Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Wakala wa Serikali 30, Mifuko maalum 13, Mabonde ya Maji 9, Taasisi nyingine za Serikali 25 na Balozi za Tanzania nje ya nchi 34. Aidha, Ofisi ilifanya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 171, Mashirika ya Umma 22 kati ya Mashirika 30 na Vyama vya siasa vitatu (3) kati ya vyama 22.

**56. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mdhidhibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea na ukaguzi wa miradi ya maendeleo 492 kwenye Halmashauri 171, miradi 40 inayofadhiliwa na Wakala za UNDP, SEDEP II kwa Halmashauri zote zilizopata fedha, TASAF III kwa Halmashauri zote zilizopata fedha za mradi na Global Fund kwa magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi. Hadi Machi, 2017 Ofisi ilikuwa imekamilisha kaguzi 10 za ufanisi na taarifa kuwasilishwa katika Mamlaka husika. Aidha, Ofisi za Ukaguzi katika mikoa 19 zimeunganishwa na Makao Makuu kwa njia ya mtandao. Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea na utekelezaji wa jukumu la ukaguzi katika taasisi 19 za Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2016/17.

### **3.4.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**57. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia rasilimali za Serikali ikiwemo uwekezaji wa Serikali katika Mashirika ya Umma na Kampuni binafsi. Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi ya Msajili wa Hazina husimamia utendaji wa mashirika na taasisi za umma na kutoa ushauri kwa Serikali wa namna ya kuimarisha uendeshaji wa taasisi, mashirika ya umma na kampuni zipatazo 264. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia mali ya Serikali ambazo zilibinafsishwa zinazojumuisha viwanda 153 na mashamba 184, lengo likiwa ni kuangalia tija iliyopo na utekelezaji wa mikataba ya mauzo.

**58. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu tajwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea na jukumu la kukusanya mapato yasiyo ya kodi. Hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 500.13 zimekusanywa kati ya shilingi bilioni 412.23 zilizopangwa kukusanywa katika kipindi hicho sawa na asilimia 121.32 ya makadirio. Makusanyo hayo yametokana na gawio shilingi bilioni 352.69, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 136.48 na mawasilisho yanayotokana na Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya simu za mkononi (Telecommunication Traffic Monitoring System - TTMS) shilingi bilioni 10.96. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekusanya shilingi bilioni 182.32 kati ya

shilingi bilioni 567.45 zilizokadiriwa kukusanywa hadi Machi, 2017 sawa na asilimia 32.13 ya makadirio ya makusanyo kutokana na marejesho ya mtaji uliozidi.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, kampuni zilizotoa gawio kutokana na uwekezaji wa Serikali ni Benki Kuu ya Tanzania, Inflight Catering Service Limited, National Housing Corporation, IPS, TANICA, TCC, TLLPPL na TPC. Aidha, taasisi na kampuni zilizowasilisha asilimia 15 za mapato ghafi katika mfuko mkuu wa Serikali ni BRELA, CMSA, DAWASA, EWURA, Gaming Board, Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, Bodi ya Sukari Tanzania, SSRA, SUMATRA, TANAPA, TANTRADE, TBA, TBS, TCAA, TCRA, TFDA, TIRA, TPA, TPRI, UTT AMIS, NACTE, NECTA, Mzinga, OSHA, Wakala wa Misitu na Wakala wa Vipimo na Mizani.

**60. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kufanya utafiti wa mashirika na taasisi ambazo zina vyanzo binafsi vya mapato kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kupunguza au kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali na kubainisha mashirika na taasisi zinazopaswa kuongezwa katika orodha ya taasisi zinazotakiwa kuanza kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**61. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha Taarifa ya Uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka 2015/16 na kuiwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria; kuingia mikataba ya utendaji na taasisi na mashirika 29; na kufanya ukaguzi wa kimenejimenti katika taasisi nane (8) ambapo taarifa ya ukaguzi huo imeandaliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka husika.

**62. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya ufuatiliaji na tathmini kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma 72 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti ya mikataba ya mauzo. Matokeo ya ufuatiliji huo pamoja na mambo mengine,

yameonesha kwamba viwanda nane (8) wamiliki wake wamekiuka masharti ya mikataba ya mauzo na kutoonesha nia ya dhati ya kuvifufua. Viwanda hivyo ni: Tembo Chip Board, National Steel Corporation, Mang'ula Mechanical & Machine Tools, Mkata Sawmills, Tanganyika Packers Shinyanga, Kiwanda cha Korosho Newala, Kiwanda cha Korosho Lindi na Mgodini wa Pugu Kaolin. Hatua za kisheria dhidi ya wamiliki hao zinafanywa kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kuendelea na hatua zaidi ikiwemo kuvirejesha chini ya umiliki wa Serikali. Aidha, baada ya ufuatiliaji huo Ofisi ya Msajili wa Hazina imechukua hatua mbalimbali kwa mashirika na viwanda vingine vinavyosuasua zikiwemo kuwataka wawekezaji kuongeza uzalishaji.

#### **3.4.14 Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

**63. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 993.61 kwa ajili ya kulipia michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 652.98 sawa na asilimia 65.7 kilitumika kulipia michango ya mwajiri kwa watumishi 541,002. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya malipo kwa wastaafu ambao wanalipwa na Hazina kwa kulipa pensheni kila mwezi na mirathi moja kwa moja kwenye akaunti zao kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa Benki Kuu ya Tanzania.

**64. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa mwaka 2016/17, ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 382.62 kwa ajili ya kulipa mafao ya wastaafu na mirathi kwa wastaafu wanaolipwa mafao na Hazina. Hadi Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 265.05 sawa na asilimia 69.3 kilitumika kulipia mafao ya wastaafu 1,645, mirathi 324 na pensheni kwa kila mwezi kwa wastaafu 55,443. Aidha, katika juhudi za kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wastaafu, kumbukumbu za wastaafu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA unaoitwa SAPERION ambapo hadi Machi, 2017 kumbukumbu za wastaafu 94,989 zilikuwa zimewekwa kwenye mfumo huo. Kuhusu kima cha



chini cha pensheni cha shilingi 100,000 ambacho wastaafu wa PPF walikuwa hawalipwi, kimeanza kulipwa tangu Januari, 2017.

### **3.4.15 Udhhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi**

**65. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhhibiti wa Fedha Haramu kwa kufanya yafuatayo: kupokea na kuchambua taarifa 208 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kuwasilisha taarifa fiche za fedha (Financial Intelligence Packages) 37 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; na kufanya ukaguzi wa taasisi mbili za kifedha. Aidha, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa wadau jinsi ya kutumia mfumo maalum wa uchambuzi wa taarifa wa kompyuta (goAML) kwa ajili ya kurahisisha uwasilishaji wa taarifa za miamala shuku kwa njia ya kielektroniki na uchambuzi . Vile vile, kitengo kimekamilisha kanuni za taarifa za usafirishaji na uingizaji wa fedha taslimu kutoka na kwenda nje ya nchi (Cross border declaration of currency reports Regulations) na zimekwishachapishwa. Kadhalika, Kitengo kinaandaa kanuni zitakazozitaka benki kutoa taarifa kwa FIU kila inapofanya miamala ya fedha taslim inayozidi ukomo au kiwango kitakachowekwa.

### **3.4.16 Tume ya Pamoja ya Fedha**

**66. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha rasimu ya Stadi ya Uwekezaji katika masuala mbalimbali ya Muungano ambapo jumla ya mashirika tisa (9) yalibainika kuwa yanatekeleza masuala ya Muungano na kwa sehemu kubwa mtaji wake ulitokana na upande mmoja wa Muungano, yaani Tanzania Bara. Mashirika hayo ni: Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Benki Kuu ya Tanzania (BOT); Shirika la Maendeleo la Mafuta Tanzania (TPDC); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL); Benki ya Posta Tanzania (TPB); National

Micro Finance Bank (NMB); na National Bank of Commerce (NBC). Vile vile, Tume imekamilisha mapitio ya stadi mbili (2), Stadi ya kubainisha mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Stadi ya Uchambuzi wa masuala ya fedha yanayohusu mambo ya Muungano. Katika mapitio ya stadi ya mfumo wa kodi, moja ya changamoto zilizofanyiwa kazi ni pamoja na kutambuliwa kwa Kamati za ushauri katika sera za kodi ambayo inajumuisha wajumbe kutoka pande mbili za Muungano kwa kuingizwa katika Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

### **3.4.17 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi**

**67. Mheshimiwa Spika**, ushirikishwaji wa sekta binafsi ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mahitaji ya miradi ya kiuchumi ni mengi na sekta ya umma pekee haiwezi kufadhili miradi yote. Kwa kuona umuhimu huo, Serikali ilianzisha Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambacho kiko katika Wizara yangu. Kitengo hiki kina kazi ya kuchambua miradi ya ubia ili kuainisha athari za kibajeti na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa miradi ya ubia; kutoa mafunzo kwa watekelezaji miradi; na kusimamia masuala ya fedha yanayohusiana na miradi ya ubia.

**68. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, imeendelea kuratibu miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kufanya uchambuzi wa miradi mbalimbali na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi iliyofanyiwa uchambuzi katika hatua mbalimbali ni pamoja na: Mradi wa Barabara ya Kulipia ya Dar es Salaam hadi Chalinze; Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam Awamu ya pili; Mradi wa Kufua Umeme Megawati 200-350 wa Somanga Fungu Mkuranga; Mradi wa Kufua Umeme wa Kinyerezi III; na Mradi wa Kuzalisha dawa wa Bohari Kuu (MSD).

**69. Mheshimiwa Spika**, Watanzania wameanza kupata mafanikio yanayotokana na miradi ya ubia hapa

nchini. Kwa mfano Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam umepunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam; muda wa kusafiri kwa mzunguko mmoja umepungua na kwa sababu hiyo huduma ya usafiri kwenye mradi huo imeongezeka kutoka watu 76,000 kwa siku kwa mwezi Mei, 2016 hadi 180,909 kwa siku kwa mwezi Machi, 2017; Baadhi ya safari kama vile kutoka Kimara hadi Kivukoni muda wake wakati wa msongamano mkali umepungua kutoka masaa mawili hadi dakika 40; ajira mpya zaidi ya 1,000 zimezalishwa zikihusisha madereva, mafundi karakana, walinzi na wahudumu. Wafanyakazi na wafanyabiashara kwa sasa wanawahi kazini ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya mradi na hivyo kuongeza ufanisi wa kazi; na mandhari ya Jiji la Dar es Salaam imeboreka.

**70. Mheshimiwa Spika**, ziko changamoto pia katika miradi ya ubia ikiwa ni pamoja na ukosefu wa wataalam wa kuchambua na kusimamia miradi katika sekta ya umma na sekta binafsi, uelewa mdogo wa jamii kuhusu miradi ya ubia, na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya ubia. Wizara yangu inaendelea kutoa mafunzo kwa sekta husika pamoja na kufadhili miradi inayokidhi vigezo. Miradi iliyofadhiliwa katika mwaka 2016/17 ni pamoja na Mradi wa Barabara ya kulipia ya Dar es Salaam hadi Chalinze, na mradi wa kuzalisha baadhi ya dawa muhimu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

### **3.5 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA**

**71. Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nieleze utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2016/17 kama ifuatavyo:-

#### **3.5.1 HUDUMA ZA KIBENKI**

##### **(i) Benki Kuu ya Tanzania**

**72. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ukuaji wa ujazi wa fedha na

mikopo kwa sekta binafsi umekuwa ukiongezeka kwa kasi ndogo ikilinganishwa na malengo, hali iliyochangiwa zaidi na kupungua kwa fedha za kibajeti kutoka nje ya nchi na kuchelewa kupatikana kwa mikopo ya kibiashara kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo. Kufuatia mwenendo huu, Benki Kuu kupitia sera ya fedha imechukua hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye mikataba ya muda mfupi ya kukopesha mabenki, kununua dola za Marekani katika soko la jumla la fedha za kigeni na kushiriki katika miamala ya kubadilishana na mabenki fedha za kigeni kwa shilingi ya Tanzania kwa muda maalum.

**73. Mheshimiwa Spika**, riba katika masoko ya fedha zimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti. Hali ya upungufu wa ukwasi hususan katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2016/17 ilijidhirisha kupitia kuongezeka kwa riba katika soko la fedha baina ya mabenki na kufikia wastani wa asilimia 16.15 mwezi Septemba, 2016 kutoka wastani wa asilimia 12.76 mwezi Juni 2016. Wastani wa riba za dhamana za Serikali uliongezeka kutoka asilimia 14.98 mwezi Juni, 2016 hadi asilimia 15.72 mwezi Oktoba, 2016, kabla ya kupungua kidogo na kufikia asilimia 14.52 mwezi Machi, 2017. Hali ya ukwasi ilianza kuwa ya kuridhisha baada ya Benki Kuu kuchukua hatua mbalimbali zilizolenga kuongeza ukwasi, hali iliyosababisha kushuka kwa riba katika soko la fedha baina ya mabenki kuanzia mwezi Oktoba 2016 na kufikia asilimia 8.16 mwezi Machi, 2017.

**74. Mheshimiwa Spika**, kutokana na mwenendo wa ukuaji mdogo wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi, Benki Kuu ya Tanzania imechukua hatua za ziada ili kusaidia kupanua uwezo wa mabenki katika kutoa mikopo na kuchangia ukuaji imara wa uchumi. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza riba ya Benki Kuu (discount rate) kutoka asilimia 16 hadi asilimia 12 na kupunguza sehemu ya kiwango cha amana za wateja kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu kisheria (Statutory Minimum Reserve Requirement) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 8. Hatua zote hizi zitasaidia kuongeza

ukwasi kwenye mabanki na hivyo kusaidia ukuaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi.

**75. Mheshimiwa Spika**, thamani ya shilingi imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha Julai,2016 hadi Machi, 2017 kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha pamoja na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kati ya shilingi 2,181 na shilingi 2,254, ikilinganishwa na kiwango cha shilingi 1,984 na shilingi 2,227 katika kipindi cha Julai,2015 hadi Machi, 2016.

**76. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya hali ya mabanki na taasisi za fedha inaonesha kuwa banki za biashara ni imara na salama, zikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Hadi kufikia Machi, 2017 kiwango cha mitaji kikilinganishwa na mali iliyowekezwa kilikuwa ni asilimia 20.3 kikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12.5. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi kilifikia asilimia 35.5 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 20.

**77. Mheshimiwa Spika**, matumizi ya mfumo wa malipo kwa kutumia simu za mikononi umeendelea kukua nchini kote. Malipo kwa simu za mikononi sasa yanatumika kwa miamala ya aina mbalimbali kama vile ankara za umeme, maji, kodi na ada mbalimbali na hivyo kuokoa muda na kupunguza misururu katika mabanki na sehemu mbalimbali zinazotoa huduma za kibiashara. Hadi Machi 2017, idadi ya watumiaji hai wa huduma za kifedha kwa njia ya simu za mikononi ilikuwa milioni 17 sawa na asilimia 77 ya watu wazima.

**(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)**

**78. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo kwa minyororo minne ya thamani ya mazao ya kilimo nchini. Mnyororo hiyo

ni pamoja na mahindi, mpunga, mbogamboga na miwa. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya mikopo iliyotolewa ina thamani ya shilingi bilioni 6.5. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wakulima 2,575 katika Wilaya za Kilolo, Mufindi, Iringa, Kilombero, Kilosa, Lushoto, Korogwe na Wakala wa Kuzalisha na Kusambaza Mbegu Tanzania.

**79. Mheshimiwa Spika**, Benki imeendelea kutoa mikopo kwa miradi ya kilimo cha umwagiliaji na mikopo kwa vyama sita vya wakulima vyenye jumla ya wakulima 1,216 vinavyojihusisha na kilimo cha umwagiliaji wa mazao ya mahindi, mpunga na mbogamboga katika wilaya za Mufindi, Kilombero, Iringa na Korogwe. Miradi hiyo inatekelezwa katika mashamba yenye jumla ya ekari 1,395.95 ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.2 zimetolewa kwa miradi hiyo. Aidha, Benki imevijengea uwezo vikundi 336 vya wakulima wadogowadogo vyenye jumla ya wanachama 44,400 katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga.

**(iii) Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI)**

**80. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Benki ya Maendeleo TIB imeendelea na jukumu la kukusanya amana kutoka kwa wateja na kutoa mikopo ya muda mrefu na wa kati kwa sekta mbalimbali za huduma na uzalishaji nchini. Aidha, Benki imeendelea kusimamia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya Mikopo kwenye dirisha la kilimo, Mfuko wa kilimo cha mbogamboga na maua, Mfuko wa nafuu ya kuagiza bidhaa nje ya nchi, Mfuko wa wachimbaji wadogo wadogo, Mfuko wa uendelezaji wa nishati, na Mfuko wa ufilisi wa iliyokuwa Benki ya Nyumba Tanzania (THB).

**81. Mheshimiwa Spika**, mikopo iliyotolewa na Benki iliongezeka kwa shilingi bilioni 641.85 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 538.67 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 19. Mikopo iliyotolewa inaonesha mikopo katika sekta ya mafuta na gesi ilikua kwa asilimia 28, sekta ya kilimo na usindikaji wa mazao asilimia 21, sekta ya viwanda asilimia

11, sekta ya madini asilimia 9 na sekta nyingine ikijumuisha ujenzi, umeme, hoteli, utalii, elimu, usafirishaji na nyinginezo asilimia 31. Kwa kipindi kilichoishia Desemba, 2016 Waraka mizania uliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 811.79 ikilinganishwa na shilingi bilioni 688.97 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 18.

**82. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Desemba, 2016 Benki ilikusanya amana kutoka kwa wateja kiasi cha shilingi bilioni 471.83 ikilinganishwa na shilingi bilioni 406.15 mwaka 2015. Mapato ya Benki yaliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 91.08 mwaka 2016 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 62.49 mwaka 2015.

**(iv) Benki ya TIB Corporate (TIB CBL)**

**83. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Benki imeendelea kutoa mikopo ya maendeleo katika sekta mbalimbali ambapo jumla ya shilingi billioni 31.9 zimetolewa. Sekta zilionufaika na mikopo hiyo ni pamoja na sekta ya viwanda shilingi bilioni 10.2, sekta ya biashara shilingi bilioni 21.1, na sekta nyingine shilingi milioni 600. Mikopo hii imeongezeka kutoka shilingi bilioni 77.27 Juni, 2016 na kufikia shilingi bilioni 104.77 Desemba, 2016. Amana za wateja zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 134.54 Juni, 2016 hadi kufikia shilingi bilioni 160.4 Desemba, 2016 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 25.86. Aidha, hadi Desemba, 2016 Benki ilipata faida baada ya makato ya kodi ya shilingi milioni 12 na kutoa dhamana za kibenki na barua za dhamana za mikopo za shilingi bilioni 15.15 .

**(v) Benki ya Posta Tanzania (TPB)**

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Benki ya Posta iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kibiashara kwa kutoa huduma kwa wananchi. Benki imetoa mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 298.05 ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 254.35 iliyotolewa mwaka 2015/16 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 43.70 sawa na asilimia 17. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2016 mapato ghafi ya Benki

yalikuwa shilingi bilioni 92 ikilinganishwa na mapato ghafi ya shilingi bilioni 74.48 Desemba, 2015. Benki imeendelea kupata faida katika uendeshaji wake ambapo hadi Desemba, 2016 faida ya shilingi bilioni 10.1 ilipatikana ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 8.26 iliyopatikana kwa mwaka ulioishia Desemba, 2015.

**(vi) Twiga Bancorp**

**85. Mheshimiwa Spika**, hadi Desemba, 2016 amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 95.53 ikilinganishwa na shilingi bilioni 87.71 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Mali za Taasisi ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 88.58 ikilinganishwa na shilingi bilioni 71.23 mwaka 2015. Aidha, mapato yatokanayo na riba yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 10.58 sawa na ongezeko la asilimia 53 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.9 mwaka 2015. Ongezeko hili limetokana na faida katika mikopo ya muda mfupi kwa benki na taasisi za fedha na uwekezaji katika dhamana za Serikali. Hata hivyo, mwezi Oktoba, 2016 Benki Kuu ya Tanzania ilichukua usimamizi wa Benki ya Twiga kutokana na upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kulinda usalama wa sekta ya fedha na amana za wateja wake.

**3.5.2 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**(i) Mfuko wa Pensheni wa PSPF**

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma umesajili jumla ya wanachama 1,405 na kufanya jumla ya wanachama kufikia 345,242. Aidha, katika kipindi hicho Mfuko umekusanya shilingi bilioni 697.08 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 634.98 ni makusanyo kutoka kwa wanachama, shilingi bilioni 22.44 kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi, shilingi bilioni 22.87 kutokana na vitega uchumi vilivyokomaa,



shilingi bilioni 16.32 kutokana na marejesho ya mikopo kutoka kwa wanachama na shilingi milioni 465.83 kutokana na vyanzo vingine vya mapato.

**(ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaafu wa GEPF**

**87. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Mfuko umesajili jumla ya wanachama 12,293 sawa na asilimia 37 ya lengo la kusajili wanachama 33,007 kwa mwaka. Ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanachama ilifikia shilingi bilioni 35.75 sawa na asilimia 43.79 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 81.64 kwa mwaka. Makusanyo ya mapato yatokanayo na vitega uchumi yalifikia shilingi bilioni 26.24 sawa na asilimia 49.36 ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 53.16 kwa mwaka. Aidha, hadi kufikia Machi, 2017 thamani ya Mfuko ilifikia shilingi bilioni 485.32 sawa na asilimia 96.43 ya lengo la kufikia shilingi bilioni 503.27.

**(iii) Mfuko wa Pensheni wa PPF**

**88. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Pensheni wa PPF kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 umetekeleza yafuatayo: kuandikisha wanachama 80,987 sawa na asilimia 65.9 ya malengo ya kuandikisha jumla ya wanachama 122,950; kukusanya shilingi bilioni 311.9 kutoka kwa wanachama wake ikiwa ni sawa na asilimia 94.6 ya malengo; na uwekezaji katika vitega uchumi ulifikia shilingi trilioni 2.1. Aidha, mapato kutokana na uwekezaji yalifikia shilingi bilioni 117.03 sawa na asilimia 64.97 ya lengo la shilingi bilioni 180.14. Vile vile, shilingi bilioni 140.1 zimetumika kulipia mafao sawa na asilimia 99.1 ya lengo la kulipia shilingi bilioni 141.4 na thamani ya Mfuko iliongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 2.55 Machi, 2017 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.29 Juni, 2016 sawa na ongezeko la asilimia 11.

**3.5.3 Rufani za Kodi**

**89. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB)

imesajili jumla ya kesi 219 ambapo kiasi cha kodi kinachobishaniwa ilikuwa shilingi bilioni 678.92 na Dola za kimarekani bilioni 0.14. Jumla ya kesi 134 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi, kati ya hizo Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshinda kesi 106 zenye jumla ya shilingi bilioni 192.68 na Dola za Kimarekani 63,175,700.54 (Milioni 63.17) na Walalamikaji wameshinda kesi 28 zenye jumla ya shilingi bilioni 412.17 ikijumuisha kesi ya BG Group iliyokuwa na shilingi bilioni 381.54. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) limesajili jumla ya kesi 100 ikijumuisha kesi 49 zilizosajiliwa kabla ya Juni 2016 ambapo kiasi cha kodi kinachobishaniwa ni shilingi bilioni 382.27 na Dola za Kimarekani Milioni 22.69. Hadi kufikia Machi 2017, Baraza lilisikiliza na kutolea maamuzi rufaa 41 ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishinda kesi 12 za kiasi cha shilingi bilioni 36.12 na Dola za Kimarekani Milioni 4.70 na Walalamikaji wameshinda kesi 29 zenye jumla ya shilingi bilioni 0.1.

### 3.5.4 Huduma za Bima

#### (i) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA)

**90. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini ilianzishwa na Serikali mwaka 2009 ili kusimamia shughuli za Bima kupitia Sheria ya Bima Na. 10 ya mwaka 1996. Serikali kupitia Mamlaka imeweza kupata mchango wa asilimia 1 kutoka sekta ndogo ya fedha ya bima katika Pato la Taifa. Aidha, Mamlaka imeboresha uendeshaji wa shughuli za Bima nchini kwa kuweka kanuni, miongozo na mifumo ambayo imesaidia kusajiliwa kampuni ya Bima 31, Madalali (Brokers) 133 na Wakala 575 hivyo kuongeza ajira, mapato yatokanayo na kodi na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima zinazokidhi mahitaji ya wananchi wa kada mbalimbali. Vile vile, Mamlaka imeendelea kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za bima na jamii kwa ujumla na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kusajili kampuni na huduma mpya za bima zinazojitokeza.

**91. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Mamlaka imekamilisha uandaaji wa Sera ya Bima ya Taifa inayotarajiwa kuanza kutumika katika mwaka 2017/18. Lengo kuu la sera hii ni kupanua wigo wa shughuli za Bima nchini ili Wananchi walio wengi waweze kunufaika na huduma za Bima ikiwa ni pamoja na Bima ya kilimo na Bima kwa watu wa kipato cha chini. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Bima kwa Umma ili kutoa elimu ya bima kwa Wananchi na makundi mbalimbali ikiwemo maeneo ya vijijini. Mamlaka ipo katika hatua za mwisho kukamilisha marejeo ya Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009 ili kufikia lengo la kukidhi mahitaji ya soko la bima.

**92. Mheshimiwa Spika**, mauzo ya soko la Bima katika mwaka 2016 yalikuwa kwa asilimia 8.4 na kufikia jumla ya shilingi bilioni 670.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 618.9 mwaka 2015. Bima za kawaida zilichangia asilimia 89.0 ya mauzo yote ya bima kwa mwaka 2016, wakati bima za maisha zilichangia asilimia 11.0 ya mauzo hayo. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yalikuwa kwa asilimia 8.5 na kufikia shilingi bilioni 596.9, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 550.2 mwaka 2015. Vile vile, mauzo ya bima za maisha yalikuwa kwa asilimia 7.8 na kufikia shilingi bilioni 74.1, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 68.7 mwaka 2015.

## **(ii) Shirika la Bima la Taifa (NIC)**

**93. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka 2016/17 utendaji wa Shirika la Bima Tanzania uliendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi, 2017 Shirika lilikusanya jumla ya shilingi bilioni 38.76, ikiwa ni utekelezaji wa asilimia 88.9 ya lengo, ikilinganishwa na shilingi bilioni 31.84 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16. Makusanyo haya yanajumuisha mapato kutokana na ada za bima shilingi bilioni 32.65, mapato kutokana na vitega uchumi shilingi bilioni 4.2, na mapato kutokana na Bima Mtawanyo shilingi bilioni 1.91.

### 3.5.5 Mitaji na Dhamana

#### (i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

**94. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 idadi ya kampuni zilizo rodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam iliongezeka kutoka 22 hadi 25. Kati ya hizo, 18 ni kampuni za ndani na 7 ni kampuni zilizo rodheshwa kutoka kwenye masoko ya hisa ya Nairobi na London. Aidha, hadi mwishoni mwa Desemba 2016 kampuni tano zimeorodheshwa kwenye safu ya soko la kukuza ujasiriamali.

**95. Mheshimiwa Spika**, matayarisho ya Soko la Bidhaa (Tanzania Merchantile Exchange) ya kimuundo, kisheria na mfumo wa mikataba itakayotumika katika uuzaji na ununuzi wa zao la korosho na ufuta yako tayari. Kanuni za usimamizi wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchanges Regulations) zimeandaliwa na Soko la Bidhaa la Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange) limepatiwa leseni na Mamlaka. Aidha, Mamlaka imekamilisha Kanuni za Soko la Bidhaa (Commodity Exchange Rules) ambalo linatarajiwa kuanza rasmi mwaka wa fedha 2017/18.

#### (ii) Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)

**96. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichoishia Machi, 2017 Soko la Hisa Dar es Salaam limeorodhesha kampuni tatu ambazo ni DSE yenyewe, Kampuni ya YETU Microfinance Limited (YETU) na Mufindi Community Bank (MUCOBA). Jumla ya mtaji wa kampuni zilizo rodheshwa umekua hadi kufika shilingi trilioni 20 na ukwasi umefikia wastani wa shilingi bilioni 500 kwa mwaka. Wawekezaji wameongezeka katika Soko hadi kufikia 475,000 ikilinganishwa na 460,000 Machi, 2016. Kuorodheshwa kwa DSE katika Soko lake lenyewe kumeifanya DSE kuwa ni Soko la tatu Afrika kufanya hivyo, baada ya Soko la Johannesburg Stock Exchange la Afrika ya Kusini na Nairobi Stock Exchange la Kenya. Aidha, Kampuni ya TCCIA Investment Plc imeuza hisa kwa umma na hisa zake zitaorodheshwa sokoni. Vile

vile, DSE imeshiriki katika kufanikisha utekelezaji wa sheria inayozitaka kampuni za simu kuuza asilimia 25 ya hisa zake kwa umma na kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Lengo likiwa ni kuwawezesha Watanzania kushiriki katika umiliki wa kampuni zilizo katika sekta hii muhimu kiuchumi. Kampuni ya kwanza ya simu kuuza asilimia 25 ya hisa zake ni Vodacom.

**97. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 DSE iliorodhesha Hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi trilioni 2.5. Aidha, DSE iliendelea na jitihada katika kuzishawishi Serikali za mitaa nchini kutumia Soko la Hisa kupata pesa kwa kutumia Hatifungani za Serikali za Mitaa kwa miradi ambayo inaweza kujiendesha yenyewe na kuleta tija kijamii na kiuchumi. DSE inafanya kazi kwa karibu na taasisi ya United Nations Capital Development Fund (UNCDF) kutoa msaada wa utaalamu na fedha za awali ili kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa katika masuala ya Hatifungani za Manispaa.

### **3.5.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania**

#### **(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI)**

**98. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI) imeendelea na jukumu la kutoa huduma shirikishi za kifedha na mikopo ya aina mbalimbali kwa watanzania wenye kipato cha chini na cha kati. Hadi Machi, 2017 mikopo iliyotolewa kwa wananchi 3,137 ina thamani ya shilingi bilioni 4.7 ambapo wanawake ni 2,154 sawa na asilimia 69 na wanaume 983 sawa na asilimia 31.

**99. Mheshimiwa Spika**, taasisi imeendelea kutoa elimu ya biashara na ujasiriamali kama vile ubunifu wa biashara zenye tija, nidhamu katika biashara, utunzaji wa kumbukumbu na tabia ya kujiwekea akiba ili hatimaye wajasiriamali wajitegemee na kutoendelea kuwa wakopaji wa kudumu. Hadi Machi, 2017 elimu imetolewa kwa wajasiriamali 12,795 katika vikundi 938.

**(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji (UTT AMIS)**

**100. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Kampuni ya UTT AMIS iliendelea kutekeleza jukumu la kusimamia mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kutoa huduma za ushauri katika uwekezaji. Hadi Machi, 2017 Kampuni imetekeleza yafuatayo: kusimamia mifuko mitano ya uwekezaji wa pamoja yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 244 yenye wawekezaji 134,688; kufanya mauzo ya vipande vyenye thamani ya shilingi bilioni 17.3 katika mifuko yake mitano; kununua vipande vyenye thamani ya shilingi bilioni 36 kutoka kwa wawekezaji wa mifuko yake; na kutoa gawio la shilingi bilioni 1.8 kwa wawekezaji wa mfuko wa Jikimu. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 37.8 zimetolewa kwenye mifuko kwenda kwa wawekezaji kusaidia mahitaji yao mbalimbali sambamba na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu faida zinazotokana na mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

**(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID)**

**101. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Miradi ya Maendeleo ya Miundombinu katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 imeweza kutekeleza majukumu yake yanayohusu miradi na maendeleo ya miundombinu kwa kuandaa nyaraka zinazohusu upatikanaji wa fedha zitakazowasilishwa CMSA na DSE, kupanua wigo wa shughuli zake katika maeneo ya miradi mbalimbali yenye manufaa kiuchumi na kijamii. Aidha, miradi mbalimbali iliyoanza kutekelezwa tangu mwaka wa fedha uliopita ipo katika hatua nzuri za kukamilika ikiwemo miradi ya ujenzi wa nyumba za mfano za askari wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na SUMA JKT. Vile vile, katika kutekeleza azma ya Serikali katika ujenzi wa nchi ya viwanda, taasisi ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha dawa za binadamu kitakachojengwa eneo la Zinga wilayani Bagamoyo.

### 3.5.7 Taasisi za Mafunzo

#### (i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo cha Usimamizi wa Fedha kimeendelea kutoa mafunzo katika matawi yake yaliyopo Dar es Salaam na Mwanza katika fani za usimamizi wa fedha, uhasibu, benki, bima, kodi, hifadhi za jamii, teknolojia ya mawasiliano ya habari na sayansi ya kompyuta. Katika mwaka 2016/17, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi, 8,787 ikilinganishwa na wanafunzi 7,977 waliidahiliwa mwaka 2015/16. Kati ya hao wanawake ni 3,584 sawa na asilimia 41 na wanaume ni 5,203 sawa na asilimia 59. Katika mwaka 2016/17, Chuo kimepata kibali cha kuanzisha programu tatu za mafunzo ambazo ni "Masters of Science in Insurance and Risk Management", "Masters of Science in Social Protection, Planning and Policy" na "Bachelor of Actuarial Sciences".

**103. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekelezwa na Chuo ni kama ifuatavyo: kukamilisha michoro ya mpango wa matumizi ya eneo lenye ukubwa wa ekari 1,500 lililoko Msata, Bagamoyo mkoani Pwani na tathmini ya athari ya mazingira; kuimarisha uwezo wa Chuo kutoa mafunzo kwa kuwapeleka masomoni watumishi kupata utaalamu zaidi ndani na nje ya nchi; kuimarisha utafiti na kutoa ushauri; kuongeza uwezo wa wahadhiri kuchapisha matokeo ya tafiti zao; na kupata ushauri katika fani za fedha na Teknolojia ya Habari.

#### (ii) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)

**104. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimedahili wanafunzi 5,852 ambapo wanaume ni 2,911 sawa na asilimia 50 na wanawake ni 2,941 sawa na asilimia 50. Aidha, Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na: kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka ya Serikali za Mitaa; kuwajengea uwezo watumishi 26 katika kozi

mbalimbali; kuboresha miundombinu ya Chuo; kutekeleza miradi mbalimbali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo; kuendesha mafunzo ya kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo ya sekta ya elimu ya msingi kwa maafisa elimu wa wilaya; na kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa mabadiliko ya tabianchi.

**(iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA)**

**105. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Taasisi ya Uhasibu Arusha imeendelea kutoa elimu katika nyanja za uhasibu, ugavi, usimamizi wa kodi, benki, utawala wa biashara, teknolojia ya habari na sayansi ya kompyuta katika ngazi mbalimbali. Idadi ya wahitimu imeongezeka kutoka 1,547 mwaka 2015/16 mpaka 1,700 mwaka 2016/17 na udahili wa wanafunzi uliongezeka kutoka 3,645 mwaka 2015/16 mpaka 3,711 mwaka 2016/17. Aidha, chuo kimetiliana saini Hati ya Makubaliano na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kupitia Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli ili kufundisha Shahada ya Sayansi ya Kijeshi na Stashahada ya Uzamili ya Sayansi ya Kijeshi. Vile vile, Chuo kimepata ithibati kutoka NACTE kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo. Chuo kimeanza kufundisha kwa kutumia mtandao ikiwa ni hatua muhimu ya kuanzisha kituo cha Elimu masafa.

**(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)**

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Uhasibu Tanzania iliendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika kampasi za Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Mbeya, Mwanza na Kigoma. Taasisi katika mwaka 2016/17 ilidahili wanafunzi 14,424 sawa na asilimia 96 ya lengo. Taasisi imekamilisha mitaala katika kozi ya Public Service Management na kusubiri kupitishwa na Mamlaka husika kabla ya kuanza kutumika. Aidha, Stashahada nne (4) za kwanza katika Kampasi ya Singida na Stashahada mbili (2) katika Kampasi ya Mwanza zimepitishwa na NACTE na zimeanza kufundishwa.



**(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC)**

**107. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili, Shahada, Stashahada na Cheti katika Takwimu rasmi kwa wanafunzi kutoka nchi za Afrika zinazozungumza kiingereza ambapo katika mwaka 2016/17 jumla ya wanafunzi waliodahiliwa ni 342 kutoka nchi 14. Aidha, Chuo kimeendelea kutekeleza makubaliano yaliyosainiwa kati ya Chuo na Shirika la Kimataifa la Ujerumani la Huduma ya Elimu ya Juu (DAAD-Deutscher Akademischer Austausch Dienst) kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi kwa ngazi ya elimu ya juu. Kwa kushirikiana na Kamisheni ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Uchumi na Maendeleo kwa Afrika, wakufunzi wameendelea kujengewa uwezo ili kuendesha mafunzo ya programu za Takwimu rasmi ambapo wanataaluma 11 wamehitimu Shahada ya Uzamili ya Takwimu Rasmi. Vile vile, Chuo kimeendesha mafunzo ya Cheti cha ukusanyaji wa Takwimu ikiwa ni mojawapo ya mikakati ya utekelezaji wa sheria mpya ya Takwimu ya Mwaka 2015 ambapo hadi Machi, 2017, wanafunzi 788 walidahiliwa.

**3.5.8 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo**

**(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

**108. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilitarajiwa kukusanya shilingi bilioni 15,105.1 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21.7 ikilinganishwa na makusanyo halisi katika mwaka wa fedha 2015/16. Hadi kufika Machi, 2017 mapato halisi ya kodi yalifikia shilingi bilioni 10,626.4 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 11,227.43 sawa na asilimia 95 ya lengo kwa kipindi hicho. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na makusanyo halisi yaliyofikiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16. **Jedwali Na.4.**

**109. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Zanzibar, Mamlaka ilitarajiwa kukusanya shilingi bilioni 188.79 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na makusanyo halisi

ya mwaka 2015/16. Hadi Machi, 2017 makusanyo yalifikia shilingi bilioni 152.6 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 139.75 sawa na ongezeko la asilimia 109 ya lengo katika kipindi hicho. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 46 ikilinganishwa na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2015/16. **Jedwali Na.5.**

**(ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

**110. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17 Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea na kazi za kufanya sensa ya viwanda; kufanya tafiti zilizoainishwa katika Kalenda ya Tafiti za Taifa; kuratibu na kusimamia mfumo wa kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu rasmi katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, na Sekta Binafsi; kufanya tafiti za kiuchumi ambazo zilitumika kuchambua takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo na nusu mwaka; kuandaa na kuboresha takwimu za Pato la Taifa, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya kurekebisha mwaka wa kizio wa bei za 2007 kwenda 2015; kutayarisha takwimu za ajira na kutoa takwimu za mfumuko wa bei kwa kila mwezi. Aidha, taasisi imeendelea kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kuboresha takwimu za utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhuisha Rejesta ya Wakazi katika mfumo wa kielektroniki.

**(iii) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)**

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kufanya yafuatayo: kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu nchini; kuhariri mitaala, silabi ya taaluma ya uhasibu; kuendeleza taaluma ya uhasibu; kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini; kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi; kutoa machapisho; kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu; na kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu.

**(iv) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (Gam- ing Board)**

**112. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Bodi imeendelea kusimamia, kuratibu sekta ya michezo ya kubahatisha nchini na kutoa leseni mbalimbali za michezo ya kubahatisha kwa wakati. Aidha, ukaguzi wa mara kwa mara kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha nchini uliendelea ili kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo hiyo pamoja na sheria nyingine za nchi.

**113. Mheshimiwa Spika**, Bodi imeendelea kukusanya kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha; yaani "gaming tax". Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Bodi ilikusanya shilingi bilioni 23.98, sawa na asilimia 92 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 26.04 kwa kipindi hicho. Lengo la Bodi ni kukusanya shilingi bilioni 34.72 hadi Juni, 2017 sawa na ongezeko la asilimia 42 ikilinganishwa na shilingi bilioni 24.5 zilizokusanywa mwaka 2015/16. Aidha, katika mwaka 2016/17 Bodi imechangia shilingi bilioni 2.87 katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo shilingi bilioni 1.42 ni mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi ya Bodi kwa mujibu wa Sheria na kiasi kingine cha shilingi bilioni 1.45 inahusiana na "mtaji" uliorejeshwa Hazina.

**(v) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (SELF Microfinance Fund)**

**114. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 Mfuko wa SELF ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 9.93, kati ya shilingi bilioni 12.5 zilizokuwa zimepangwa katika mwaka 2016/17. Kiasi hicho cha mikopo kilitolewa kwa asasi za fedha zipatazo 60, kati ya hizo asasi 33 ni SACCOS, 25 ni kampuni za fedha na 2 ni Benki za Jamii. Mikopo hiyo iliwanufaisha wajasiriamali wadogo wapatao 4,649, ambapo kati ya hao wanaume ni 2,500 sawa na asilimia 54 na wanawake ni 2,149 sawa na asilimia 46. Mikopo ilielekezwa katika sekta za biashara ndogo za ufugaji, uvuvi, usindikaji, madini, viwanda vidogo, huduma mbalimbali za kibiashara

pamoja na pembejeo za kilimo. Mikopo hii imechangia ajira zipatazo 5,617 katika kipindi husika. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, urejeshaji wa mikopo ya Mfuko wa SELF ulifikiwa kwa wastani wa asilimia 91.

### **3.5.9 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo mwaka 2016/17**

#### **(i) Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma**

**115. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kutekeleza yafuatayo: kuendelea na utekelezaji wa kubadilisha mfumo wa IPSAS Cash kwenda IPSAS Accrual; kupitia sheria mbalimbali za fedha pamoja na sheria ya Msajili wa Hazina kwa lengo la kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na udhibiti wa Fedha za Umma; na kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011. Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kusambaza mfumo wa taarifa za ununuzi wa Umma (PMIS) kwenda kwenye taasisi za ununuzi; kujengea uwezo PPRA na taasisi za Umma ili ziweze kuandaa na hatimaye kuanza kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki; na kuendelea kuioanisha na kuiunganisha mifumo mbalimbali ikiwemo Integrated Financial Management System (IFMS), Human Capital Management Information System (HCMIS), Advanced Loan System (ALS), Central Banking System (CBS) na Tourism Registration and Licensing Information System (TORLIS) .

**116. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kuwajengea uwezo watumishi wa kada za fedha, ununuzi wa Umma na TEHAMA; ukaguzi wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Serikali kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea na Halmashauri za Serikali za Mitaa katika kusimamia fedha na mali ya umma; wakaguzi wa ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na Kamati mbalimbali za Bunge katika masuala ya usimamizi na udhibiti wa rasilimali za Umma.

**(ii) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania (TSMP)**

**117. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS) zinaendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Nchini- (Tanzania Statistical Master Plan - TSMP). Lengo kuu la Mradi huu ni kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa Takwimu rasmi nchini. Katika mwaka 2016/17, Kanuni za Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 zimetayarishwa na kuanza kutumika. Takwimu mbalimbali zimeendelea kuboreshwa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa zikiwa zimeshirikisha wadau kutoka serikalini, Washirika wa Maendeleo na Sekta binafsi. Takwimu hizo ni pamoja na hali ya chakula nchini, Pato la Taifa, bei za mazao na Takwimu za Idadi ya Wafungwa na hali ya uhalifu nchini.

**118. Mheshimiwa Spika**, sambamba na uzalishaji wa takwimu hizi, NBS imeboresha tovuti yake ([www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz)) ili kuimarisha njia za usambazaji wa takwimu kwa watumiaji kwa njia ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano. Aidha, NBS imeboresha kanzidata za viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kijamii (Tanzania Socio-Economic Database - TSED) pamoja na kuhifadhi taarifa za kitaifa (National Data Archive – NADA) ili kuwapa fursa watumiaji wa takwimu kufanya uchambuzi zaidi kutokana na taarifa hizi. Vile vile, ujenzi wa jengo la NBS unaendelea Dodoma na unatarajiwa kukamilika Januari, 2018. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi unatarajiwa kukamilika Juni, 2017.

### **3.6 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO**

#### **3.6.1 MAFANIKIO**

**119. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 mafaniko yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/17 ni pamoja na: kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani; kuendelea kutengemaa na kukua kwa uchumi kwa asilimia 7 mwaka 2016; kuimarika

kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya kimarekani; mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja; utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kupitia mapato ya ndani kama vile malipo ya awali ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha "Standard Gauge" na Ununuzi wa ndege mbili sambamba na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege nne; na kupunguza malimbikizo ya madai ya watumishi, wazabuni na wakandarasi yaliyohakikiwa ambapo hadi Machi,2017 Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 796.38.

### 3.6.2 CHANGAMOTO

**120. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, changamoto zifuatazo zimejitokeza ambazo ni pamoja na: mwamko mdogo wa kulipa kodi na hususan kuzingatia matumizi ya mashine za kielektroniki; kuchelewa kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nje kutokana na majadiliano kuchukua muda mrefu hivyo kuchelewesha upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### 3.6.3 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

**121. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti kama zilivyobainishwa hapo juu, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo: kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari kupitia udhibiti wa matumizi ya mfumo wa EFDs; kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha fedha za misaada na mikopo nafuu zinapatikana kama zilivyoahidiwa; kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki; kuendelea kuisitiza nidhamu katika utekelezaji wa bajeti kama ilivyoidhinishwa kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti; kuendelea kuwianisha mapato na matumizi kwa kuhakikisha kuwa mgawo wa fedha utaendana na upatikanaji wa mapato; na kuendelea kuchukua hatua za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

## **4.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18**

**122. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2016/17, naomba niwasilishe malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18.

### **4.1 MAJUKUMU YA WIZARA**

#### **4.1.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Uchumi Jumla**

**123. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Wizara itaendelea kuimarisha Sera za uchumi jumla ikiwemo: kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2016; kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 5.0 Juni 2018; mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18; kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka asilimia 4.5 mwaka 2016/17 hadi asilimia 3.8 mwaka 2017/18; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

#### **4.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

**124. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21); kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/19; kufuatilia utekelezaji wa Mpango na miradi ya maendeleo; na kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma.

#### 4.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umasikini

**125. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, maeneo ya kipaumbele ni pamoja na: kukamilisha maandalizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Jitihada za kuondoa umasikini yakiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; kuandaa Taarifa ya Hali ya Umasikini na Malengo Endelevu nchini; kufanya uchambuzi na tathmini ya miradi ya kuondoa umasikini ili kuimarisha jitihada za kuondoa umasikini ngazi ya wilaya na vijiji; kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wadau kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu na jitihada za kuondoa umasikini; na kuandaa mfumo wa kuibua na kukuza Maendeleo ya Uchumi katika ngazi za chini.

#### 4.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

##### (a) Mapato ya Ndani

**126. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka 2017/18, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato; kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kuingia katika mfumo wa kodi; kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake; kufanya uthamini wa majengo na kusimamia ulipaji ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo; na kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija.

##### (b) Misaada na Mikopo

**127. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Washirika wa Maendeleo wameahidi kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kutekeleza programu na miradi ya kipaumbele iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ambapo wameahidi



kuchangia Bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 3,971.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 941.2 ni kwa ajili ya Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS), shilingi bilioni 556.1 kwa ajili ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na shilingi bilioni 2,473.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**128. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo, Serikali imeanza kufanyia kazi mapendekezo ya taarifa ya Washauri Elekezi walipopewa jukumu la kutathmini mfumo mzima wa ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaandaa Mwongozo mpya wa ushirikiano unaotarajiwa kutatua changamoto zilizokuwepo hapo awali ambazo zilikuwa zikidhoofisha utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

#### **4.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**129. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo: kuboresha mifumo ya uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; kuendesha mafunzo ya MTEF na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kwa wadau mbalimbali; kuandaa machapisho mbalimbali kuhusu Bajeti ya Serikali yakiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti, Makadirio ya Bajeti ya Serikali, Kijitabu cha Bajeti ya Serikali toleo la Wananchi (Citizen Budget) na Taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali za kila robo mwaka; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

**130. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengine Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya mishahara katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, katika kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma,

Wizara itafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa matumizi ya fedha za umma kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### **4.1.6 Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**131. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kufuatilia na kusimamia utendaji wa kada ya ukaguzi wa ndani pamoja na kamati za ukaguzi na kutoa mafunzo kwa kamati za ukaguzi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa vitengo vya ukaguzi na kamati za ukaguzi. Aidha, Wizara itafanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uhakiki wa madeni, uhakiki wa matokeo ya mradi wa huduma za afya kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa unaofadhiliwa na Mfuko wa Afya na Benki ya Dunia, ukaguzi maalumu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miongozo ya ukaguzi wa ndani.

#### **4.1.7 Usimamizi wa Malipo**

**132. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara imepanga kuendelea kuunganisha mfumo wa malipo wa TISS katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 139 zilizopo katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Njombe, Iringa, Pwani, Simiyu, Shinyanga, Mara, Geita, Kigoma na Kagera. Aidha, Wizara imepanga kuendelea kuunganisha mfumo wa malipo wa EFT katika Wizara na Idara zote za Serikali zilizobakia ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa. Vile vile, Wizara itaendelea kutoa udhamini wa masomo kwa wahasibu, wakaguzi, wagavi na wataalamu wa kompyuta kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa waliopo vyauni.

#### **4.1.8 Deni la Taifa**

**133. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa mwaka 2017/18, imepanga kuendelea kulipa madeni mbalimbali yaliyokopwa na Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo nchini na kulipa mafao ya wastaafu kwa watumishi

wanaolipwa mafao na Hazina mara wanapostaafu na mirathi kwa wategemezi mara mtumishi anapofariki. Aidha, Wizara itaendelea kuwasilisha michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii ukiwemo Mfuko wa Malipo ya Fidia kwa Wafanyakazi.

#### **4.1.9 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha**

**134. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara imepanga kusimika mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mapato yasiyokuwa ya kodi; kusimamia kazi ya utengenezaji na uunganishwaji wa mifumo mbalimbali ya kukusanya maduhuli kwenye mfumo mmoja wa Serikali unaoitwa Government Payment Gateway Platform (GePG). Mfumo huu utanza kutumika katika Taasisi na Idara za Serikali zinazokusanya mapato yasiyo ya kodi. Aidha, Wizara itaendelea kuoanisha na kuunganisha mifumo ya kielektroniki ya kifedha, kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na utumiaji wa mfumo wa taarifa za mishahara ya watumishi wa umma.

#### **4.1.10 Usimamizi wa Mali ya Serikali**

**135. Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia mali ya Serikali, katika mwaka 2017/18, Wizara imepanga kukamilisha uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali kwa Mafungu 36; kuendelea kuondosha mali chakavu, sinzia na zilizokwisha muda wake; na kufanya uhakiki maalum wa mali za watu binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali na zile zinazotokana na utaifishwaji katika vituo vya polisi nchini. Aidha, Wizara itahakiki mali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali ili kutoa ushauri wa kupunguza hasara zinazotokana na matumizi yasiyo ya lazima.

#### **4.1.11 Ununuzi wa Umma**

**136. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2017/18, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kuendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa EPICOR 9 katika

utekelezaji wa zabuni za umma kwa Maafisa Ununuzi na Ugavi, kutoa mafunzo mbalimbali yanayolenga kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na kanuni zake za Mwaka 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2016; na kuandaa na kutekeleza mikakati itakayohusiana na matokeo ya zoezi la Tathmini ya Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma nchini.

**137. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kusimika na kusimamia mfumo kamili wa ununuzi kwa njia ya mtandao kwenye ununuzi wa dawa, vifaa tiba na bidhaa mtambuka; kufanya ukaguzi kupima uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kupima thamani ya fedha kwa taasisi 120 zilizosajiliwa na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini; na kuendelelea kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake pamoja na mifumo na nyenzo za utekelezaji wa ununuzi.

**138. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Huduma wa Ununuzi Serikalini imepanga kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja, kuendelea kuandaa mikataba maalumu ya vifaa na huduma mtambuka kwa niaba ya taasisi za Serikali, kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta katika mikoa ya Kigoma, Lindi, Morogoro na Mtwara, na kuongeza kisima cha kuhifadhi mafuta katika mkoa wa Dodoma.

#### 4.1.12 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali na kuhakikisha uwepo wa uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya rasilimali za Umma. Ofisi imelenga kufanya yafuatayo: kutekeleza Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); kufanya ukaguzi wa mafungu ya bajeti ya Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani. Aidha, Ofisi imepanga kufanya ukaguzi wa

kiufanisi na kaguzi maalum katika maeneo yatakayoainishwa, kujenga uwezo wa Wakaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi yakiwemo sekta ya gesi, mafuta na madini, Serikali Mtandao na uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao na kuboresha mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA.

#### **4.1.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**140. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, itaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini wa Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa. Aidha, Wizara, itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mifuko ya Jamii, Taasisi za Fedha pamoja na wadau mbalimbali katika suala la uwekezaji na ufufuaji wa viwanda, kampuni na mashamba yaliyobinafsishwa.

**141. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea na uhakiki wa mali za taasisi na mashirika ya Umma zilizoingizwa katika Daftari la Mali; kufanya utafiti wa taasisi ambazo zina vyanzo binafsi vya mapato kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kupunguza au kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali; kuongeza mapato yasiyo ya kodi kwa kuimarisha ufuatiliaji wa ukusanyaji kodi kutoka kwa mashirika na taasisi za Umma; kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma kwa kuingia mikataba ya utendaji; kujenga uwezo wa wajumbe wapya wa Bodi za Wakurugenzi katika usimamizi wa taasisi na mashirika ya Umma; na kuendelea na ukaguzi wa kimenejimenti kwa taasisi na mashirika ya Umma.

#### **4.1.14 Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kuboresha taarifa za wastaafu na kusimamia malipo ya pensheni zinazolipwa moja kwa moja na Hazina.

#### 4.1.15 Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

**143. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2012 na Sheria ya Udhibiti Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar ya Mwaka 2009. Shughuli zifuatazo zitatekelezwa: kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na taarifa za usafirishaji wa fedha kutoka na kuingia nchini kupitia mipakani; kuendelea kuwasilisha taarifa za intelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na kukamilisha taarifa ya zoezi la kutathmini mianya na viashiria ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi nchini.

**144. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizopangwa ni: kufanya ukaguzi wa watoa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za fedha; kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria na watoa taarifa wa Tanzania bara na Zanzibar; kuboresha mifumo ya mawasiliano na kompyuta; na kuwajengea uwezo watumishi kujifunza mambo mbalimbali katika nyanja ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

#### 4.1.16 Tume ya Pamoja ya Fedha

**145. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Tume imepanga kukamilisha Stadi ya Uwekezaji katika Mambo ya Muungano, kufanya Mapitio ya Stadi kuhusu Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha na kufanya uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi ya Muungano kwa lengo la kuwa na kanzidata ya taarifa za fedha zinazohusu mambo ya Muungano.

#### 4.1.17 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

**146. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kufanya yafuatayo: kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha; kutoa

mafunzo ya namna ya kuibua, kuchambua na kutekeleza miradi ya ubia kwenye Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na taasisi binafsi; na kuziwezesha Taasisi zenye miradi ya ubia kuajiri washauri elekezi kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa Ubia. Aidha, pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu sera, sheria na kanuni za miradi ya ubia.

## **4.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA**

### **4.2.1 Huduma za kibenki**

#### **(i) Benki Kuu ya Tanzania (BOT)**

**147. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kutekeleza yafuatayo: kufanya tathmini ya mpango jumuishi wa huduma za kifedha ulioishia Desemba 2016; kufanya utafiti wa upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo nchini; kufanya utafiti wa upatikanaji wa huduma za kifedha nchini (Finscope Survey, 2017); na kusimamia majukumu yake ya msingi na kuhakikisha kuwa mabanki na mifumo ya malipo inaendelea kuwa imara na salama katika soko huru la fedha. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuhakikisha uwepo wa ujazi wa fedha na ukwasi utakaochangia upatikanaji wa mikopo unaoendana na malengo ya Serikali ya kukuza uchumi bila kuongeza mfumuko wa bei. Vile vile, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia utulivu katika masoko ya fedha wakati riba na thamani ya shilingi zikiendelea kuamuliwa na nguvu ya soko ili kuongeza ufanisi katika mgawanyo wa rasilimali za nchi.

#### **(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)**

**148. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Benki ya Maendeleo ya Kilimo itaboresha huduma za kibenki kwa kuanzisha mazao maalum kwa wakulima wadogowadogo kulingana na mnyororo husika wa thamani kulingana na vipaumbele vya Mikoa husika. Aidha,

Benki imepanga kufanya maandalizi ya kutoa mikopo ya kuendeleza miradi ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yaliyoainishwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Vile vile, Benki imepanga kuwajengea uwezo wakulima wadogowadogo, wafanyakazi wa TADB, benki nyingine na wadau mbalimbali wa kilimo; kuitangaza Benki na huduma zake kwa wananchi ili waweze kuzielewa shughuli zake na jinsi benki itakavyowahudumia; kusimamia utoaji na usimamizi wa fedha kwenye uendeshaji wa miradi mbalimbali ya kilimo hapa nchini; na kuratibu upatikanaji wa dhamana mbalimbali kwa ajili ya mikopo kwa wakulima ili mabenki yaweze kuelekeza nguvu zao kuwakopesha wakulima wengi zaidi.

**(i) Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI)**

**149. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Benki ya Maendeleo ya TIB imepanga kutoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 671.37. Aidha, Waraka Mizania wa benki unatarajiwa kukua hadi kufikia shilingi bilioni 842.93 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5. Vile vile, Benki inatarajia kupata faida ya shilingi bilioni 12.36.

**(ii) Benki ya Biashara TIB (TIB CBL)**

**150. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Benki inatarajia kutoa mikopo ya shilingi bilioni 244 na dhamana za kibenki na barua za dhamana ya mikopo za shilingi bilioni 70. Aidha, Benki inatarajia kutoa dhamana ya malipo na barua za dhamana ya mikopo ya shilingi bilioni 182 na kupata faida ya shilingi bilioni 3.81.

**(i) Benki ya Posta Tanzania (TPB)**

**151. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Benki ya Posta Tanzania imeweka lengo la kukamilisha taratibu za kuuza Hisa kwa Watanzania ili kuwawezesha kumiliki benki na kukuza mtaji wa Benki. Aidha, Benki imepanga kuongeza mapato hadi kufikia shilingi bilioni 94, kukuza amana hadi kufikia shilingi bilioni 320, kuongeza thamani ya mikopo



husususan kwa wananchi wa kipato cha chini hadi kufikia shilingi bilioni 311, na kukuza thamani ya mtaji wa Wanahisa hadi kufikia shilingi bilioni 61.

**(ii) Twiga Bancorp**

**152. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18 Benki imeweka malengo yafuatayo: kuongeza amana za wateja kufikia shilingi bilioni 89.64 sawa na asilimia 6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 95.53 mwaka 2016/17; kuongeza mapato yatokanayo na riba kufikia shilingi bilioni 10.89 sawa na asilimia 3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.58 mwaka 2016/17; na kukusanya shilingi bilioni 3.1 toka mikopo chechefu.

**4.2.2 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**(i) Mfuko wa Pensheni wa PSPF**

**153. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Mfuko unatarajia kusajili wanachama wapya 15,000 na kuongeza idadi ya wanachama hadi kufikia 374,840 ifikapo Juni, 2018. Mfuko unatarajia kukusanya shilingi bilioni 793.27 kutokana na michango ya wanachama; shilingi bilioni 62.16 kutokana na vitega uchumi; na shilingi bilioni 18.13 kutokana na vitega uchumi vilivyokomaa. Aidha, Mfuko umepanga kuwekeza shilingi bilioni 73.43 kwenye vitega uchumi ambapo uwekezaji huo utaoongeza thamani ya Mfuko kutoka shilingi trilioni 1.42 zinazotarajiwa ifikapo Juni, 2017 hadi kufikia shilingi trilioni 1.78 Juni, 2018.

**(ii) Mfuko wa Pensheni wa GEPF**

**154. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18 Mfuko unatarajia kufanya yafuatayo: kusajili wanachama 36,988; kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 89.35; kukusanya mapato ya shilingi bilioni 67.36 kutokana na uwekezaji; na kuboresha huduma kwa wanachama kwa kuwekeza zaidi katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Aidha, thamani ya Mfuko inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 669.68.

**(iii) Mfuko wa Pensheni wa PPF**

**155. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18 Mfuko unatarajia kufanya yafuatayo: kukusanya michango ya shilingi bilioni 526.4 kutoka kwa wanachama; shilingi bilioni 361.4 kutokana na uwekezaji; kuandikisha wanaachama wapya 200,000; na kushiriki ujenzi wa viwanda vikubwa vya kisasa vya kuzalisha sukari na bidhaa za ngozi kwa kushirikiana na taasisi nyingine. Uwekezaji huu unatarajia kuongeza thamani ya Mfuko hadi kufikia shilingi triloni 3.3.

**4.2.3 Rufani za Kodi**

**156. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) itaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi ya rufaa za kodi ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) linatarajia kutatua asilimia 90 ya rufani zote za migogoro ya kodi itakayosajiliwa. Baraza litaendelea na utaratibu wa utoaji wa machapisho ya mkusanyiko wa kesi za kodi zilizoamuliwa katika kipindi husika ambazo hutumika na wadau na wanazuoni kama vitabu vya rejea.

**4.2.4 Huduma za Bima**

**(i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA)**

**157. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Mamlaka imepanga kutekeleza yafuatayo: kutekeleza Sera ya Bima, Mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Bima kwa Umma na Mkakati wa Kitaifa wa kutoa huduma za Bima kwa watu wenye kipato cha chini; kufanya marejeo ya Sheria ya Bima na kanuni zake; kudhibiti mwenendo wa soko kwa kutumia TEHAMA; kuimarisha ukusanyaji wa tozo za ada za bima katika soko; na kuanzisha Bima za Kiislamu baada ya kanuni kupitishwa.

**(ii) Shirika la Bima la Taifa (NIC)**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Shirika linalenga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 90.48. Kati ya mapato hayo shilingi bilioni 43.54 zitatokana na ada ya bima za mali na ajali, shilingi bilioni 36.08 zitatokana na ada ya bima za maisha, shilingi bilioni 7.42 zitatokana na vitega uchumi, na shilingi bilioni 3.44 zitatokana na ada za bima mtawanyo.

**4.2.5 Mitaji na Dhamana**

**(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)**

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kufanya yafuatayo: kukamilisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Maendeleo ya Masoko ya Mitaji; kuandaa rasimu ya sheria mpya ya Masoko ya Mitaji; kutoa elimu kwa umma na kukuza masoko ya mitaji nchini; kuendelea kushawishi kampuni za umma zinazofanya vizuri kuorodhesha hisa zake katika soko la hisa; na kukamilisha hatua za mwisho na kuhakikisha biashara katika Soko la Bidhaa linaanza kufanya kazi kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa.

**(ii) Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)**

**160. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Soko la Hisa la Dar Es Salaam linalenga kufanya yafuatayo: kuendelea kutoa elimu kwa Umma juu ya matumizi ya soko la hisa kwa wawekezaji na watafuta mitaji; kuendeleza jitihada za kuishawishi Serikali kutumia Soko la Hisa katika utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji; kutambulisha bidhaa mpya sokoni kama Hatifungani za Manispaa; kuendelea kuboresha utendaji kazi wa soko; na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kukuza na kuendeleza sekta ya viwanda nchini.

#### 4.2.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania

##### (i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI)

161. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Taasisi inatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 22 kwa watumishi wa Umma, wafanyabiashara na wakulima wapatao 9,000; kupokea amana kutoka kwa wateja baada ya kupata leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania; na kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kuuza hisa kwa Watanzania.

##### (ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji (UTT AMIS)

162. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Kampuni imepanga kufanya yafuatayo: kuongeza rasilimali inazosisimamia kwa kiwango cha asilimia 15 na idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; kuzindua uwekezaji na usimamizi wa rasilimali za mifuko ya Pansheni; kuzindua uwekezaji na usimamizi wa rasilimali za fedha za taasisi za Serikali katika masoko ya fedha na Hatifungani; na kutoa kiwango shindani cha faida pamoja na huduma kwa wawekezaji kwa kutumia fursa za uwekezaji zilizoko kwenye soko.

##### (iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID)

163. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, UTT PID inatarajia kuingia ubia na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa umeme na nishati wa Kinyerezi III; uzalishaji wa Saruji; usafishaji mafuta; uendelezaji wa viwanja kwenye Balozi za Tanzania nchi za nje; kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa; ujenzi wa nyumba za askari wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na SUMA JKT; na uendelezaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

#### 4.2.7 Taasisi za Mafunzo

##### (i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

**164. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18 Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatarajia kufanya yafuatayo: kudahili wanafunzi 8,820 katika fani mbalimbali; kufanya tafiti; kutoa huduma za ushauri elekezi na machapisho /majarida; kuendeleza kampasi ya Mwanza; na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Chuo na utoaji huduma kwa wadau.

##### (ii) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)

**165. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Chuo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 5,852 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanafunzi 6,500 mwaka 2017/18. Aidha, Chuo kimepanga kuanzisha Shahada ya Uzamili katika fani za: Idadi ya watu; Mipango ya Maendeleo Vijijini; Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi; Utawala na Usimamizi wa Serikali za Mitaa; na Shahada ya kwanza katika fani za Mipango na Usimamizi wa Miradi; Utawala na Usimamizi wa Serikali za Mitaa; na Mipango na Usimamizi wa Biashara. Vile vile, chuo kitaendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali za Mitaa katika kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo.

##### (iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA)

**166. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Taasisi inatarajia kutekeleza yafuatayo: kudahili wanafunzi 5,000 kutoka 3,723 waliopo sasa; kukamilisha maandalizi ya mitaala mipya kwa ajili ya kupata ithibati kutoka NACTE; kuanza kuendesha programu za "Military Science" kwa ushirikiano na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi – Monduli; kutafuta mwekezaji kwa mpango wa PPP ili kujenga madarasa, kumbi za mikutano ya kisasa na mabweni; na kufanya utafiti kwa kushirikiana na Chuo cha Coventry katika sekta ya mafuta na gesi.

**(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)**

**167. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Taasisi imepanga kuongeza idadi ya udahili kutoka wanafunzi 14,424 hadi kufikia wanafunzi 17,708; kuendelea kuboresha huduma za maktaba kwa kuzipatia vitabu vipya na kuziunganisha maktaba zote kwenye mfumo wa maktaba mtandao (e-library); na kudhamini wahadhiri wanaojiunga na kozi za Uzamili na Uzamivu.

**(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afri- ka (EASTC)**

**168. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Chuo kimepanga kuendelea kutoa mafunzo ya takwimu rasmi katika ngazi za Cheti cha awali, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kinatarajia kutoa mafunzo ya Uzamili katika eneo la Utawala na Biashara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Nagarjuna kilichopo nchini India ambapo mafunzo haya yanatarajia kuanza Septemba, 2017.

**4.2.8 Taasisi za kitaalam na Huduma nyinginezo**

**(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

**169. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni **17,106.33** sawa na ongezeko la asilimia 14.2 ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya mwaka 2016/17.

**170. Mheshimiwa Spika**, mikakati ya kufikia lengo la 2017/18 ni pamoja na Kupanua wigo wa kodi kwa kuendelea kusajili na kuhakiki taarifa za walipakodi kwenye mifumo ya kodi ya TRA; kuendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi kwa kubadilishana taarifa ili kuweza kupata taarifa sahihi za walipakodi; kuendelea kusimamia na kuhamasisha utumiaji sahihi wa mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFDs); kudhibiti ukwepaji wa kodi kwa

kuendelea kufanya ukaguzi na uchunguzi; kuboresha shughuli za ukaguzi wa mizigo kutoka bandarini (post clearance); kuimarisha ukaguzi wa mizigo gatini Dar es Salaam (Dar Wharf); kuendelea kudhibiti utoaji wa misamaha kwa mizigo inayoingia nchini; na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa ukusanyaji wa malimbikizo /madeni ya kodi.

**(ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

**171. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga kuendelea kukusanya, kuchambua, kusambaza, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi pamoja na kuratibu takwimu hizi kwa lengo la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika sera za maendeleo katika sekta zote za kiuchumi na kijamii na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/17-2020/21). Hii ni pamoja na kufanya tafiti na sensa mbalimbali ili kukidhi mahitaji yaliyopo katika Mpango huo.

**(iii) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)**

**172. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo: kusajili watahiniwa, wanachama na kampuni za uhasibu na ukaguzi; kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi; kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na u k a g u z i ; kuendeleza taaluma ya uhasibu; kutunga na kusimamia mitihani; kusimamia mradi wa maboresho ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu; na kusimamia uanzishaji wa mitaala mipya katika kuendesha mitihani ya Uhasibu.

**(iv) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (Gaming Board)**

**173. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Bodi inatarajia kukusanya kodi ya shilingi bilioni 39.11 sawa na ongezeko la asilimia 12.64 ikilinganishwa na shilingi bilioni 34.72 inayotarajiwa kukusanywa hadi kufikia Juni, 2017. Aidha, Bodi imepanga kuendelea kusimamia sekta ya michezo ya kubahatisha nchini na kuhakikisha kwamba inaendelea kuendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo

hiyo pamoja na sheria nyingine za nchi. Bodi inatarajia kuchangia shilingi bilioni 2.37 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali katika mwaka wa 2017/18 sawa na ongezeko la asilimia 9.72.

**(v) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (SELF Microfinance Fund)**

**174. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Mfuko unatarajia kutoa mikopo ya shilingi bilioni 20 kwa walengwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na SACCOS, Kampuni za fedha na Benki za Jamii. Aidha, Mfuko umepanga kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa asasi 160 na wajasiriamali 200; kutafuta vyanzo zaidi vya fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo; na kujenga uwezo wa asasi na wajasiriamali wadogowadogo ili waweze kukua na kuwa wawekezaji wenye tija. Vile vile, Mfuko unatarajia kuongeza ufanisi wa urejeshaji wa mikopo kutoka asilimia 91 ya mwaka 2016/17 hadi kufikia asilimia 95 kwa mwaka 2017/18.

**5.0 MPANGO WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18**

**175. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Awamu ya Tano wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kufanya yafuatayo: kuboresha usimamizi wa mapato na matumizi; kuboresha mifumo ya fedha katika Serikali za Mitaa; kuboresha taasisi za ukaguzi ili ziweze kusimamia fedha za Umma, kuimarisha udhibiti wa ndani na kuboresha ununuzi wa Umma ili kuongeza uwajibikaji; kuboresha sera za fedha, kodi na madeni; kuendelea kuunganisha mifumo ya fedha; kuimarisha ununuzi wa Umma kwa kuzingatia thamani ya fedha, kuweka udhibiti na usimamizi, na kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Hesabu za Serikali, Wahasibu, Maafisa TEHAMA, Bajeti, Ugavi na Ununuzi pamoja na wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia Hesabu za Serikali.



**176. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/18, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu chini ya mradi wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania imepanga kuendelea na uzalishaji wa takwimu na kukamilisha ujenzi wa Jengo la Takwimu mjini Dodoma. Aidha, Ofisi imepanga kukamilisha kazi ya kubadilisha mwaka wa kizio wa Pato la Taifa kuwa 2015 badala ya 2007.

**177. Mheshimiwa Spika**, chini ya Mradi wa Kusaidia Ufanisi wa Bajeti za Wizara na Idara za Serikali, Wizara inatarajia kuongeza mtaji wa Benki ya TIB Development ili kugharamia utekelezaji wa miradi mikubwa inayoweza kujiendesha kibiashara; kuendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa katika Wizara, idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kugharamia ujenzi wa nyumba na ofisi za Serikali mjini Dodoma. Aidha, kupitia Programu ya Uwezeshaji Wananchi Vijijini, Serikali imepanga kugharamia utoaji wa mikopo ya vikundi vya uzalishaji mali katika vijiji vya majaribio kupitia Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

**178. Mheshimiwa Spika**, kupitia Mradi wa Regional Support on Budget Process, Wizara imepanga kufanya mafunzo ya uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21) na kuendelea kutoa mafunzo ya uzingatiaji wa Sheria ya Bajeti na kanuni zake. Aidha, kupitia Mradi wa EDF Support, Wizara imepanga kuendesha ofisi inayoratibu miradi inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya sambamba na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu katika sekta ya barabara, maji na nishati inayofadhiliwa na Umoja huo. Vile vile, kupitia Mradi wa PPP Facilitation Fund, imepanga kuziwezesha taasisi zenye miradi ya ubia kuajiri washauri elekezi, kusimamia sera na shughuli za ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kuishauri Serikali kuwekeza kwenye miradi yenye manufaa kwa Taifa.

**179. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Tume ya Mipango kwa mwaka 2017/18 chini ya Mradi wa Kuhamasisha

Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umasikini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira, imepanga kuwezesha majadiliano ya wadau kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), kuendesha utafiti kuhusu hali ya umasikini katika ngazi ya kitaifa na vikwazo vya kitaasisi; na kuandaa na kusambaza majarida kwa wadau yanayohusu utunzaji endelevu wa mazingira, ustawi na usawa wa kijinsia, na uwezeshaji wa wanawake nchini. Aidha, kupitia Mipango ya Masuala ya Idadi ya Watu, Tume imepanga kukamilisha Mapitio ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Mwaka 2006; kuandaa taarifa ya hali ya Idadi ya Watu Tanzania kwa Mwaka 2016; na kuendesha utafiti kuhusu Afya na Idadi ya Watu.

**180. Mheshimiwa Spika,** Tume kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imepanga kutekeleza yafuatayo: kuratibu kanzidata ya kuhifadhi na kutoa taarifa za miradi ya maendeleo; kujenga uwezo na kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma; kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kila robo mwaka; kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara, Idara na Wakala za Serikali katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## **6.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18**

### **6.1 MAKADIRIO YA MAPATO**

**181. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/18 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi **522,342,627,291 (Bilioni 522.34)** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

## 6.2 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18

**182. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Fedha na Mipango imekadiria kutumia kiasi cha jumla ya **shilingi 11,752,225,182,252 (Bilioni 11,752.225)** kwa mafungu yote tisa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 10,323,141,232,511 (Bilioni 10,323.141)** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,429,083,949,741 (Bilioni 1,429.084)** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **shilingi 89,847,360,068 (Bilioni 89.847)** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 771,860,872,443 (Bilioni 771.861)** kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 9,461,433,000,000 (Bilioni 9,461.433)** ni Deni la Taifa na Huduma nyingine. Aidha, katika fedha za matumizi ya maendeleo, **shilingi 1,382,975,800,000 (Bilioni 1,382.976)** ni fedha za ndani na **shilingi 46,108,149,741 (Bilioni 46.108)** ni fedha za nje.

### 6.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**183. Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 55,039,643,000 (bilioni 55.04)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 8,077,009,000 (bilioni 8.08)**.

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 46,962,634,000 (bilioni 46.96)**.

(b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 11,570,500,000 (bilioni 11.57)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 3,500,000,000 (bilioni 3.5)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 8,070,500,000 (bilioni 8.07)**.

## 6.2.2 FUNGU 21 - HAZINA

**184. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya Kawaida -  
**Shilingi 570,429,248,000 (bilioni 570.43)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara ya fungu hili - **Shilingi 40,643,601,000 (bilioni 40.64)**.

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 529,785,647,000 (bilioni 529.79)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.

(b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 1,395,636,701,741 (Bilioni 1,395.63)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 1,364,000,000,000 (Bilioni 1,364.00)**.

(ii) Fedha za Nje - **S h i l i n g i 31,636,701,741 (bilioni 31.63)**.

## 6.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA

**185. Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida -  
**Shilingi 9,472,122,300,000.00 (bilioni 9,472.12)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara-**Shilingi10,689,300,000.00 (bilioni 10.69)**.

(ii)Matumizi Mengineyo (Malipo ya Deni la Taifa na Michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii) - **Shilingi 9,461,433,000,000.00 (bilioni 9,461.43)**.

#### 6.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI

**186. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 45,960,838,000.00 (bilioni 45.96)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara – **Shilingi 8,404,104,000.00 (bilioni 8.40)**.

(ii) Matumizi Mengineyo - **S h i l i n g i 37,556,734,000.00 (bilioni 37.56)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 3,600,000,000.00 (bilioni 3.60)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 2,000,000,000.00 (bilioni 2.00)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,600,000,000.00 (bilioni 1.60)**.

#### 6.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

**187. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 104,917,488,000.00 (bilioni 104.92)**. Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 2,687,702,000.00(bilioni 2.69)**.

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 102,229,786,000.00 (bilioni102.23)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 2,000,000,000.00 (bilioni 2)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani – **S h i l i n g i 1,000,000,000.00 (bilioni 1).**

(ii) Fedha za Nje -**Shilingi 1,000,000,000.00 (bilioni 1).**

#### **6.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA**

**188. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 1,386,817,511.00 (bilioni 1.39).** Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 428,676,000.00 (bilioni 0.43).**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 958,141,511.00 (bilioni 0.96).**

#### **6.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU**

**189. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

Matumizi ya kawaida - **Shilingi 1,515,586,000.00 (bilioni 1.52).**

#### **6.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

**190. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida – **Shilingi 61,832,948,000.00 (bilioni 61.83).** Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 17,313,756,068.00**  
**(bilioni 17.31).**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi**  
**44,519,191,932.00 (bilioni 44.52).**

(b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi**  
**11,800,948,000.00 (bilioni 11.80).** Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi**  
**8,000,000,000.00 (bilioni 8.00).**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 3,800,948,000.00 (bilioni 3.80).**

### 6.2.9 FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO

**191. Mheshimiwa Spika,** katika Fungu hili kwa mwaka 2017/18, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi**  
**4,936,364,000.00 (bilioni 4.93).** Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara – **Shilingi 1,603,212,000.00 (bilioni 1.60).**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi**  
**3,333,152,000.00 (bilioni 3.33).**

(b) Miradi ya Maendeleo - **Shilingi**  
**4,475,800,000.00 (bilioni 4.47)** ambazo ni fedha za Ndani.

### 7.0 SHUKRANI

**192. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru sana Wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu.

**193. Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ([www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz)).

**194. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili aweze kuwasilisha taarifa ya Kamati. Karibu mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama leo nikiwa mwenye afya ya kutosha. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, naomba niwasilishe na kusoma taarifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo inajumuisha Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu; Fungu 21- Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Fungu 66 - Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilitekeleza jukumu lake la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango ikiwemo kulishauri Bunge ipasavyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali



(Fungu 45). Kamati ilitekeleza jukumu hili na kufanya mashauriano na Serikali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu haya, Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Fedha na Mipango kati ya mwezi Machi na Aprili, 2017 Dodoma na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya ujumla kuhusu Utekelezaji Wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mafungu yote tisa (9) iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 8,716.49 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 45.45 zilikuwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 8,671.04 zilikuwa kwa ajili matumizi mengineyo kwa mchanganuo ufutao:-

Kulipia deni la Taifa kiasi cha shilingi bilioni 8,009.34 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 661.70. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo iliidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 791.998 ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 723.150 na fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 68.84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 6,901.17 kimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 79 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 18.89 kilikuwa kimetumika kugharamia miradi ya maendeleo hii ikiwa sawa na asilimia mbili ya fedha yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya

utekelezaji wa bajeti ya mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati imefanya tathmini katika mafungu tisa yaliyo chini ya Wizara hii na kuona yapo baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, yapo mafungu ambayo hayajapatiwa fedha za kutosha na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mafungu haya utaona kuwa kati ya mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango ni mafungu matano (5) tu, Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 66 - Tume ya Mipango; Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali ndiyo yaliyoweza kupokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mafungu mengine manne yamepokea fedha chini ya asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo ni Fungu moja tu la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali limepata zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yake iliyooidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa kwa Wizara hii kuweza kulihakikishia Bunge kwamba inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri ukizingatia hata mafungu yake mwenyewe yamepokea fedha pungufu (rejea Jedwali Na.1 la taarifa hii).  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 50. Wizara hii ndiyo kitovu cha kusimamia uchumi jumla na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi kupitia sera bora za fedha na mapato na matumizi. Kushindwa kuwajibika vema kwa Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake kunapelekea kushindwa kufikia malengo kwa Wizara nyingine. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kutekeleza mipango yake kwa umakini na uangalifu mkubwa ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa mafungu yake mbalimbali

pamoja na kuhakisha mafungu mengine ya Wizara yanapata fedha za bajeti zao kama ilivyo dhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21 – Hazina. Jukumu kubwa la Hazina ni kuandaa na kusimamia Sera ya Fedha (*Monitory Policy*) na Sera ya Mapato na Matumizi (*Fiscal Policy*) pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Pamoja na jukumu hilo zito, fungu hili limepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha Sh.196,000,000,000 kati ya shilingi bilioni 411.27 sawa na asilimia 48. Aidha, kwa fedha za maendeleo limepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.8 kati ya shilingi bilioni 740.15 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge sawa na asilimia 0.8. Kwa mwenendo huu wa utolewaji hafifu wa fedha, Kamati inaona ni dhahiri Hazina haijaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa katika upande wa usimamizi wa Sera ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 22 - Deni la Taifa. Kamati inajua umuhimu wa kuwepo kwa kitengo hiki ili kihakikishe kinatunza na kusimamia taarifa muhimu za madeni yaani *public debt database* pamoja na kutoa kwa wakati taarifa muhimu za ulipaji wa madeni ya ndani na nje (*domestic and external debts*), ni muhimu kitengo hiki kikasaidia kufanya tathmini ya ulipaji wa deni la Taifa kwa kuzingatia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa kiasi kikubwa cha mapato ya ndani kimekwenda kulipia deni la Taifa na hivyo Serikali kushindwa kugharamia masuala mengine ya maendeleo. Takwimu zinaonesha kati ya kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017, Serikali imelipa deni la Taifa kiasi cha shilingi trilioni 4.64. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu. Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu (*Financial Intelligence Unit*) kinapambana na aina yoyote ya utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini. Kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi

milioni 861.3 kati ya shilingi bilioni 1.6 kilichoidhinishwa, hii ni sawasawa na asilimia 54 ya fedha yote. Hali hii inarudisha nyuma juhudi za kupambana na masuala ya fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 50 - Tume ya Pamoja ya Fedha. Majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha yamewekwa na Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 133 na 134, majukumu hayo ni pamoja na kutunza Akaunti ya Pamoja ambayo ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuchambua mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa masuala ya Muungano. Hadi kufika mwezi Machi 2017, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi milioni 797.96 kati ya shilingi bilioni 1.37 iliyoidhinishwa sawasawa na asilimia 58 ya bajeti yake. Kutokana na majukumu yake ya kimsingi, Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwa Tume hii ili iweze kukamilisha majukumu yake ya kimsingi kama ilivyoelezwa kwenye Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kamati inatambua jukumu la msingi la Ofisi ya Msajili wa Hazina kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370. Hata hivyo, utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii unaathiriwa na bajeti ndogo inayoidhinishwa pamoja na kiasi kinachotolewa. Takwimu zinaonesha hadi kufikia Machi 2017, kiasi cha shilingi bilioni 160.18 kilichoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida wamepewa kiasi cha shilingi bilioni 12.07 tu. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, kati ya kiasi cha shilingi bilioni 3.22 kilichoidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo ni kiasi cha shilingi milioni 493.7 tu kimetolewa sawa na asilimia 15.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 66 - Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ndiyo chombo kikuu kinachoishauri Serikali kuhusu sera za usimamizi wa uchumi na mikakati ya maendeleo ya Taifa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, fungu hili liliidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 4.03 kwa matumizi ya kawaida. Hata hivyo, hadi kufika Machi 2017,

kiasi cha shilingi bilioni 2.047 ndicho kilitolewa na Hazina. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kutoa kiasi cha shilingi bilioni 1.99 kilichobaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kamati inasisitiza kuwa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ihakikishe inaendelea kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha kwa kuzingatia Sheria za Usimamizi wa Fedha. Kamati inaipongeza idara hii kwa kuweza kusimamia na kuboresha mfumo wa malipo Serikalini yaani *Integrated Financial Management System (IFMS)*. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa maoteo ya mahitaji ya fedha kwa kila mwaka yazingatie mahitaji na majukumu ya kazi ya mafungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 44.6. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13.8 ni kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 18.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 12.2 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za ndani ikiwa ni Sh.8,000,000,000 na za nje ikiwa shilingi bilioni 4.3. Aidha, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli, ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 14.3 kutoka vyanzo mbalimbali chini ya ofisi hii. Hadi kufikia Machi, 2017, ofisi hii ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 9.5 za maduhuli ikiwa ni sawasawa na asilimia 66 ya makadirio kwa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti wa ofisi hii unaonesha kuwa hadi Machi, 2017, ofisi hii, Fungu 45 lilikuwa limepokea jumla ya shilingi bilioni 32.6 zilizotolewa na Hazina ikiwa ni sawa na asilimia 73.05 ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.4 ni matumizi ya mishahara na shilingi bilioni 22.1 ni fedha za matumizi mengineyo ikiwa ni sawa na asilimia 115 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, ilipofika mwezi Disemba 2016, ofisi ilibaini

kuwa isingeweza kumudu kutimiza majukumu yake ya Kikatiba hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha kwa maana ya Juni, 2017. Hivyo, ofisi ililazimika kuandika barua Hazina kuomba nyongeza ya bajeti ya Sh.15,000,000,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi mengineyo pamoja na kukamilisha utayarishaji wa ripoti za ukaguzi za mwaka 2015/2016. Wizara ya Fedha na Mipango iliipatia ofisi hii kiasi cha Sh.5,000,000,000 kati ya fedha zilizoombwa. Ni matumaini ya Kamati kuwa kiasi cha fedha kilichobakia yaani Sh.10,000,000,000 kitatolewa na Wizara kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maendeleo, ofisi ilipokea shilingi bilioni 1.2 tu ikiwa ni sawasawa na asilimia 9.98 tu ya bajeti iliyopangwa ya shilingi bilioni 12.2. Kamati inaiomba Serikali ipeleke kiasi cha fedha kilichobaki cha shilingi bilioni 11.05 za fedha za maendeleo ili kuisaidia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kukamilisha miradi ya maendeleo inayotakiwa kukamilishwa kabla ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka wa fedha 2017/2018 imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 11.752 kwa mafungu yote tisa, kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 10.323 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.429 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha kiasi cha Sh.89,000,000,000 kwa ajili ya mishahara, Sh.771,000,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na shilingi trilioni 9.4 ni kwa ajili ya ulipaji wa deni la Taifa na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa fedha za matumizi ya maendeleo, shilingi trilioni 1.382 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 46.108 ni fedha za nje. Makadirio ya mapato na matumizi haya yanahusisha pia Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao ufafanuzi wake nitautoa hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilijadili na kufanya kikao cha mashauriano na Waziri wa Fedha na Mipango na Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mashauriano haya yalizingatia majukumu ya msingi ya Ofisi hii kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yaani NAOT uliidhinishiwa fedha zake kama ilivyoomba kwenye mapendekezo ya bajeti yao yaani kiasi cha shilingi bilioni 73.633 ikijumuisha na Sh.12,000,000,000 zinazotarajiwa kukusanywa na Ofisi yaani *reimbursable costs*. Hatua hii ilifikiwa baada ya mashauriano na Wizara ya Fedha na hivyo kuongeza kiasi cha shilingi bilioni 3.9 kwenye Mfuko husika na kufikia kiasi hicho cha fedha. Kamati ya Bajeti inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua hii muhimu. Kamati inasisitiza bado kuna umuhimu wa kuhakikisha Mfuko huu, Mfuko wa Mahakama na Mfuko wa Bunge inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi kama kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinavyoelekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti inaomba Bunge lako Tukufu liridhie Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote tisa ya Wizara ya Fedha ya jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 11.752.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti. Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango inayojumuisha mafungu tisa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maombi ya fedha ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mipango. Tume ya Mipango imekuwa ikitoa dira

na miongozo mbalimbali ya kukuza uchumi wa Taifa kwa kubuni sera za kiuchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa. Kamati imefanya tathmini na kuona kuwa utendaji wa Tume hii ikiwa chini ya Wizara ya Fedha unakuwa siyo huru ukizingatia kuwa wao ndiyo wanaopanga mipango ya nini kifanyike na Wizara ya Fedha ndio watafutaji wakuu wa fedha ili kukamilisha mipango husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kuwa Tume ya Mipango irudishwe kuwa chini ya Ofisi ya Rais, hii itasaidia kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi kuliko ikiwemo kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga mipango husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ni pamoja na kusimamia uwekezaji wa mitaji na kulinda rasilimali zilizowekwa na Serikali katika mashirika na taasisi kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370. Ofisi hii pia inasimamia mali za Serikali ambazo zilibinafsishwa, viwanda 153 na mashamba 184 kwa lengo la kuangalia ni kwa namna gani Serikali itafaidika na mikataba iliyoingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, majukumu haya mazito yamekuwa hayaendani na utolewaji wa fedha kwenye ofisi husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Mfano katika mwaka wa fedha 2016/2017, ofisi hii iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi bilioni 160 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2017, kiasi cha shilingi bilioni 12.7 kimetolewa kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 8 tu na kiasi cha shilingi milioni 493.7 kimetolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inamalizia kutoa fedha zilizobaki kabla ya tarehe 31Juni, 2017 ukizingatia kuwa dhamana iliyoopewa ofisi hii ni kubwa kuliko kiasi cha bajeti wanachotengewa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa madeni ya watumishi na watoa huduma. Kamati bado inaendelea kusisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kuhakiki na kulipa madeni mbalimbali ya ndani hasa ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma wengine ambao baadhi yao walikopa benki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali. Ingawa Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 796.22 kati ya kiasi kinachokadiriwa kuwa shilingi trilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwahimiza Maafisa Masuuli kudhibiti ulimbikizaji wa madeni kwa kuingia mikataba isiyokuwa na fedha, Kamati inashauri kuwa ufumbuzi wa tatizo hili ni Wizara ya Fedha na Mipango kukusanya mapato ili yajitosheleze katika kugharamia bajeti ya Serikali ikiwemo kulipa madeni haya pamoja na kutoa fedha za matumizi mengineyo kwa wakati na kama zilivyopangwa na Maafisa Masuuli ili waweze kutoa huduma kwa wakati kwa kadiri ya majukumu yao kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumiaji wa mashine za kieletroniki (*EFD*). Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ihakikishe inasimamia Wizara, Idara na taasisi zake kuhakikisha zinatumia mashine za kieletroniki katika ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Mfano mdogo tunauona katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ukurasa 153, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 wakala 11 zililipa kiasi cha takribani shilingi bilioni 2.97 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kieletroniki (*EFD*). Hali hii inasababisha walipa kodi kukwepa kodi na hivyo kuikoshesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa vijiji maarufu kama *Village Empowerment* wa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Fedha na Mipango ilitenga kiasi cha Sh.59,000,000 kwa ajili ya kufanya *pilot study* kwa baadhi ya mitaa, vijiji, kata na shaiya kwa

ajili ya kutekeleza mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama milioni 50,000,000 kwa kila kijiji. Mradi huu ulilenga kutenga kiasi cha shilingi milioni 50,000,000 kwa Kila kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa kwa maana ya *SACCOS* katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha hadi kufikia Machi, 2017, Wizara haijapeleka fedha yoyote kwenye mradi huo. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Fedha na Mipango imetenga kiasi cha Sh.50,000,000 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Kamati ingependa Bunge lako Tukufu lipewe taarifa ya utekelezaji wa mradi huu ikiwemo *piloty study* husika ili lipate fursa ya kuishauri tena Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa wastaafu. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuboresha huduma kwa wastaafu ikiwepo kuwapokea, kuwahakiki na kuweka kumbukumbu bora za wastaafu katika mfumo wa kompyuta na kufanya mfumo mzima wa pensheni kuwa wa kompyuta pamoja na kuunganisha katika masijala kuu. Huduma zote hizi zinasaidia kupunguza msongamano na usumbufu kwa wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hii nzuri ya Wizara, Kamati inashauri kuhakikisha pensheni kwa wastaafu inatoka haraka kwa wakati unaostahili ili kuwapunguzia wastaafu hawa makali ya maisha baada ya kuitumikia Serikali kwa muda mrefu. Aidha, ni vyema Serikali ikaendelea kulipa deni la *PSPF* na Mifuko mingine ili iweze kuhudumia malipo ya wastaafu hawa kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye mabadiliko yaliyotolewa kupitia *GN.No. 209* ya mwaka 2009 ya kurekebisha pensheni zao za kila mwezi. Serikali itimize ahadi yake ya kutoa *Non Cash Bond* ya shilingi trilioni 2.6 kwa Mfuko wa *PSPF* ili uweze kupunguza mzigo mkubwa wa malipo ya wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo katika mabenki ili kumiliki sehemu za majengo. Itakumbukwa kuwa mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali kuwezesha ardhi kutumika kupata mikopo ya kibenki kupitia *Mortgage Finance Act, 2008*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uhitimisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nikushukuru wewe, nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na wataalaam wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadilio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano walioutoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, baada ya maelezo haya naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu tisa yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU  
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO  
KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 PAMOJA NA MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA  
WA FEDHA 2017/18 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/18 ambayo inajumuisha Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Fungu 66 - Tume ya Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilitekeleza Jukumu lake la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango ikiwemo kulishauri Bunge ipasavyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo. Aidha, Kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Fungu 45). Kamati ilitekeleza jukumu hili na kufanya mashauriano na Serikali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu haya, Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Fedha na Mipango kati ya mwezi Machi na Aprili, 2017 Dodoma na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

## 2.0 MAPITIO YA UJUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

### 2.1 Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote Tisa (9) iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 8,716.49**. kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 45.45** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi bilioni 8,671.04** zilikuwa kwa ajili matumizi mengineyo kwa mchanganuo ufutao; kulipia deni la Taifa kiasi cha **Shilingi bilioni 8,009.34**; na matumizi mengineyo shilingi **bilioni 661.70**. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 791.998** ambapo fedha za ndani zilikuwa **Shilingi bilioni 723.150** na fedha za nje zilikuwa **Shilingi bilioni 68.84**.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi cha shilingi **bilioni 6,901.17** kilikuwa kimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na **asilimia 79** ya fedha yote iliyoidhinishwa. Aidha kwa upande wa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi **bilioni 18.89** kilikuwa kimetumika kugharamia miradi ya maendeleo hii ikiwa sawa na asilimia 2 ya fedha yote iliyoidhinishwa.

### 2.2 Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2016/17. Kamati imefanya tathmini katika mafungu Tisa yaliyo chini ya Wizara hii na kuona yapo baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, yapo mafungu ambayo hayajapatiwa fedha za kutosha na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia mafungu haya utaona kuwa kati ya mafungu Tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango; ni mafungu matano (5) tu (Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 66 - Tume ya Mipango, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali) ndio yaliyopokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge. Mafungu mengine manne yamepokea fedha chini ya asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha kwa upande wa miradi ya maendeleo ni fungu moja tu la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali limepata zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yake iliyoidhinishwa na Bunge. Hii ni changamoto kubwa kwa Wizara hii kuweza kulihakikishia Bunge kwamba inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri ukizingatia hata mafungu yake yenyewe yamepokea fedha pungufu. (Rejea Jedwali Namba 1)

### 2.2.1 Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii ndio kitovu cha kusimamia uchumi jumla na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi kupitia sera bora za fedha, Mapato na Matumizi. Kushindwa kuwajibika vema kwa Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake, kunapelekea kushindwa kufikia malengo kwa Wizara nyingine. Kwa mantiki hiyo Kamati inaishauri Wizara kutekeleza mipango yake kwa umakini na uangalifu mkubwa ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa mafungu yake mbalimbali pamoja na kuhakikisha mafungu mengine ya Wizara yanapata fedha za bajeti zao kama zilivyoidhinishwa na Bunge

### 2.2.2 Fungu 21- Hazina

**Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la hazina ni kuandaa na kusimamia sera ya fedha (monetary policy) na sera ya mapato na matumizi (fiscal policy) pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Pamoja na jukumu hilo zito fungu hili limepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi bilioni 196 kati ya bilioni 411.27 (sawa na asilimia 48);

aidha kwa fedha za maendeleo limepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.8 kati ya shilingi bilioni 740.15 ya fedha yote zilizo dhinishwa na Bunge (sawa na asilimia 0.8). Kwa mwenendo huu wa utolewaji hafifu wa fedha, Kamati inaona ni dhahiri Hazina haijaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa katika upande wa usimamizi wa sera ya mapato na matumizi.

### 2.2.3 Fungu 22 – Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inajua umuhimu wa kuwepo kwa kitengo hiki ili kihakikishe kinatunza na kusimamia taarifa muhimu za madeni (Public Debt Database) pamoja na kutoa kwa wakati taarifa muhimu za ulipaji wa madeni ya ndani na nje (Domestic and External Debts). Ni muhimu kitengo hiki kikasaidia kufanya tathmini ya ulipaji wa Deni la Taifa kwa kuzingatia mapato. Takwimu zinaonyesha kuwa kiasi kikubwa cha mapato ya ndani kinakwenda kulipia Deni la Taifa na hivyo Serikali kushindwa kugharamia masuala mengine ya maendeleo. Takwimu zinaonyesha kati ya kipindi cha Julai 2016 hadi Februari 2017 Serikali imelipa Deni la Taifa kiasi cha shilingi trilioni 4.64.

### 2.2.4 Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika**, kitengo cha udhibiti wa fedha haramu (*Financial Intelligence Unit*) kinapambana na aina yoyote ya kutakatisha fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini. Kiasi cha fedha kilichotolewa cha shilingi milioni 861.3 kati ya bilioni 1.60 kilicho dhinishwa (asilimia 54 ya fedha yote) kinarudisha nyuma juhudi za kupambana na masuala ya fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi

### 2.2.5 Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

**Mheshimiwa spika**, majukumu ya Tume ya pamoja ya Fedha yanamewekwa Katiba kwa mujibu Ibara 133 na 134. Majukumu hayo ni pamoja na kutunza akaunti ya pamoja ambayo ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuchambua

mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa masuala ya Muungano. Hadi kufikia mwezi Machi 2017, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi milioni 797.96 kati ya shilingi bilioni 1.37 iliyoidhinishiwa (Sawa na asilimia 58 ya fedha yote). Kutokana na majukumu yake ya Msingi Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inatoa fedha za kutosha kwa tume hii ili iweze kukamilisha majukumu yake ya kimsingi kama yalivyoainishwa kwenye Katiba.

### 2.2.6 Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jukumu la msingi la Ofisi ya Msajili wa Hazina kama yalivyoainishwa kwenye sheria ya Msajili wa Hazina SURA Na. 370. Hata hivyo utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii yanaathiriwa na bajeti ndogo inayoidhinishwa pamoja na kiasi kinachotolewa. Takwimu zinaonesha hadi kufikia mwezi Machi 2017 kiasi cha shilingi bilioni 160.18 kilichoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida, wamepewa kiasi cha shilingi bilioni 12.07 tu; aidha kwa upande wa fedha za maendeleo kati ya kiasi cha shilingi bilioni 3.22 kilichoidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo, ni kiasi cha shilingi milioni 493.7 tu kimetolewa (sawa na asilimia 15.3).

### 2.2.7 Fungu 66 – Tume ya Mipango

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango ndio chombo kikuu kinacho ishauri Serikali kuhusu sera za usimamizi wa uchumi na mikakati ya Maendeleo ya Taifa. Katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Fungu hili liliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 4.03 kwa matumizi ya kawaida. Hata hivyo hadi kufikia mwezi Machi 2017 kiasi cha shilingi bilioni 2.047 ndicho kimetolewa na Hazina. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kutoa kiasi cha shilingi bilioni 1.99 kilichobaki.

### 2.2.8 Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuwa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ihakikishe inaendelea kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha



kwa kuzingatia sheria za usimamizi wa fedha. Kamati inaipongeza Idara hii kwa kuweza kusimamia na kuboresha mfumo wa malipo Serikalini – *Integrated Financial Management system (IFMS)*. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa maoteo ya mahitaji ya fedha kwa kila fungu yazingatie mahitaji na majukumu ya kazi ya mafungu husika.

**JEDWALI NAMBA 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17**

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI ILIYODHINISHWA	FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI , 2017	ASILIMIA YA KIASI KILICHOTOLEWA (%)
50	Wizara ya Fedha na Mipango	Bilioni 50.71 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 38.89 (Matumizi ya Kawaida)	76
		Bilioni 26.03 (Matumizi ya Maendeleo)	Bilioni 8.8 (Matumizi ya Maendeleo)	33.9
21	Hazina	Bilioni 411.27 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 196.86 (Matumizi ya Kawaida)	48
		Bilioni 740.15 (Matumizi ya Maendeleo)	Bilioni 5.8 (Matumizi ya Maendeleo)	0.8
22	Deni la Taifa	Trilioni 8.00 (Matumizi ya Kawaida)	Trilioni 6.58 (Matumizi ya Kawaida)	82
		-	-	-
13	Kitengo cha Udhhibiti Fedha Haramu	Bilioni 1.6 (Matumizi ya Kawaida)	Milioni 861 (Matumizi ya Kawaida)	54
		-	-	-
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	Bilioni 1.37 (Matumizi ya Kawaida)	Milioni 797 (Matumizi ya Kawaida)	58
		-	-	-
07	Msajili wa Hazina	Bilioni 160 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 12.07 (Matumizi ya Kawaida)	8
		Bilioni 3.22 (Matumizi ya Maendeleo)	Milioni 493.7 (Matumizi ya Maendeleo)	15.3
66	Tume ya Mipango	Bilioni 4.03 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 2.47 (Matumizi ya Kawaida)	61
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	Bilioni 45.58 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 36.23 (Matumizi ya Kawaida)	79
		Bilioni 4.49 (Matumizi ya Maendeleo)	Bilioni 2.45 (Matumizi ya Maendeleo)	54.6
45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali	Bilioni 32.37 (Matumizi ya Kawaida)	Bilioni 29.29 (Matumizi ya Kawaida)	90
		Bilioni 12.28 (Matumizi ya Maendeleo)	Milioni 494.39 (Matumizi ya Maendeleo)	4

### 2.2.9 Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 44,658,523,368** kati ya fedha hizo **Shilingi 13,870,774,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 18,502,322,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 12,285,427,368** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo (Fedha za ndani kiasi cha **shilingi bilioni 8.0** na nje kiasi cha **shilingi bilioni 4.3**). Aidha, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli Ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni 14.3** kutoka vyanzo mbalimbali chini ya ofisi hii. Hadi kufikia Machi, 2017, Ofisi ilikuwa imekusanya **Shilingi 9,581,191,930** za maduhuli ikiwa ni sawa na **asilimia 66** ya makadirio kwa mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii unaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 Ofisi hii (Fungu 45) ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 32,622,888,212** zilizotolewa na Hazina; ikiwa ni sawa na **asilimia 73.05** ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,494,131,641** ni matumizi ya mishahara na **Shilingi 22,128,756,571** ni fedha za matumizi mengineyo ikiwa ni sawa na asilimia 115 ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, ilipofika mwezi Disemba 2016, Ofisi ilibaini kuwa isingeweza kumudu kutimiza majukumu yake ya Kikatiba hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha Juni, 2017. Hivyo Ofisi ililazimika kuandika barua Hazina kuomba nyongeza ya bajeti ya **Shilingi 15,000,000,000** kwa ajili ya bajeti ya matumizi mengineyo pamoja na kukamilisha utayarishaji wa ripoti za ukaguzi za mwaka 2015/16. Wizara ya Fedha na Mipango iliipatia Ofisi hii kiasi cha **Shilingi 5,000,000,000** kati ya fedha zilizombwa. Ni matumaini ya Kamati kuwa kiasi cha fedha kilichobakia (shilingi bilioni 10) kitatolewa na Wizara kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maendeleo, Ofisi ilipokea **Shilingi 1,225,634,000** tu ikiwa ni sawa na **asilimia 9.98** tu ya bajeti iliyopangwa (Bilioni 12.2). Kamati inaiomba Serikali

ipeleke kiasi cha fedha kilichobaki cha **shilingi 11,059,793,368** za fedha za maendeleo, ili kuisaidia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kukamilisha miradi ya maendeleo inayotakiwa kukamilishwa kabla ya mwaka huu wa fedha 2016/17 kumalizika.

### **3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18.**

#### **3.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18.**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2017/18 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 11,752,225,182,252** kwa mafungu yote Tisa (9). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,323,141,232,511** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,429,083,949,741** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha kiasi cha **shilingi 89,847,360,068** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 771,860,872,443** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 9,461,433,000,000** ni kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa na Huduma nyingine. Aidha kwa upande wa fedha za Matumizi ya Maendeleo, **shilingi 1,382,975,800,000** ni fedha za ndani na **shilingi 46,108,149,741** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya mapato na matumizi haya yanahusisha pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:-

#### **3.2 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilijadili na kufanya kikao cha mashauriano na Waziri wa Fedha na Mipango na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/18. Mashauriano haya yalizingatia majukumu ya msingi ya Ofisi hii kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) uliidhinishiwa

fedha zake kama walivyoomba kwenye mapendekezo ya bajeti yao ya kiasi cha **shilingi 73,633,896,000** (ukijumuisha na shilingi **bilioni 12** zinazotarajiwa kukusanywa na Ofisi (Reimbursable costs). Hatua hii ilifikiwa baada ya mashauriano na Wizara ya Fedha na hivyo kuongeza kiasi cha **shilingi bilioni 3.9** kwenye Mfuko husika na kufikia kiasi hicho cha fedha. Kamati ya Bajeti inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua hii muhimu. Kamati inasisitiza bado kuna umuhimu wa kuhakikisha Mfuko huu, Mfuko wa Mahakama na Mfuko wa Bunge inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi kama kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Bajeti (2015) kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inaomba Bunge lako tukufu liridhie Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote Tisa ya Wizara ya Fedha ya Jumla ya kiasi cha shilingi **11,752,225,182,252**.

#### **4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango inayojumuisha mafungu Tisa (9) kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 pamoja na maombi ya Fedha ya mafungu husika kwa Mwaka wa Fedha 2017/18; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

##### **4.1. Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango imekuwa ikitoa dira na miongozo mbalimbali ya kukuza uchumi wa Taifa kwa kubuni sera za kiuchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa. Kamati imefanya tathmini na kuona kuwa utendaji wa Tume hii ukiwa chini ya Wizara ya Fedha unakuwa sio huru ukizingatia kuwa wao ndio wanaopanga mipango ya nini kifanyike na Wizara ya Fedha ndio watafutaji wakuu wa fedha ili kukamilisha mipango husika. Ni maoni ya Kamati kuwa Tume ya Fedha na Mipango irudishwe kuwa chini ya

Ofisi ya Rais hii itasaidia kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi ikiwemo kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga mipango husika.

#### **4.2. Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ni pamoja na kusimamia uwekezaji wa mitaji na kulinda rasilimali zilizowekwa na Serikali katika Mashirika na Taasisi kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina SURA Na. 370. Ofisi hii pia inasimamia Mali za Serikali ambazo zilibinafsishwa (viwanda 153 na mashamba 184) kwa lengo la kuangalia ni kwa namna gani Serikali itafaidiaka na mikataba iliyoingia.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo majukumu haya mazito yamekuwa hayaendani na utolewaji wa fedha kwenye Ofisi husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Mfano katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi hii iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha shilingi bilioni 160 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2017, kiasi cha shilingi bilioni 12.07 kimetolewa kwa matumizi ya kawaida (sawa na asilimia 8) na kiasi cha shilingi milioni 493.7 kimetolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inamalizia kutoa fedha zilizobaki kabla ya tarehe 31 Juni 2017 ukizingatia kuwa dhamana iliypewa ofisi hii ni kubwa kuliko kiasi cha Bajeti wanachotengewa.

#### **4.3. Uhakiki wa madeni ya watumishi na watoa huduma**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati bado inaendelea kusesitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kuhakiki na kulipa madeni mbalimbali ya ndani hasa ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma wengine ambao baadhi yao walikopa benki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali. Ingawa Serikali imelipa kiasi cha **shilingi bilioni 796.22** kati ya kiasi cha takribani shilingi **trilioni 3** inachodaiwa; pamoja na kuwahimiza Maafisa Masuuli kudhibiti ulimbikizaji wa madeni kwa kuingia mikataba isiyokuwa na fedha,

Kamati inashauri kuwa ufumbuzi wa tatizo hili ni Wizara ya Fedha na Mipango kukusanya mapato ili yajitosheleze katika kugharamia bajeti ya Serikali ikiwemo kulipa madeni haya pamoja na kutoa fedha za matumizi mengineyo kwa wakati na kama zilivyopangwa na Maaifisa Masuuli ili waweze kutoa huduma kwa wakati kwa kadiri ya majukumu yao kisheria.

#### **4.4. Utumiaji wa mashine za kieletroniki (EFD) katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ihakikishe inasimamia Wizara, Idara na Taasisi zake zinatumia mashine za kieletroniki katika ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Mfano mdogo tunauona katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali (ukurasa 153); katika mwaka wa fedha wa 2015/16 wakala 11 zililipa kiasi cha takribani shilingi bilioni 2.97 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za keletroniki (EFD), hii inasababisha walipakodi kukwepa kodi na hivyo kuikoshesha Serikali mapato.

#### **4.5. Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. (Fungu 21)**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango ilitenga kiasi cha **Shilingi bilioni 59 kwa ajili ya** kufanya '*pilot study*' kwa baadhi ya mitaa, vijiji, kata na shaiya kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. Mradi huu ulilenga "*Kutenga Kiasi cha Milioni 50 kwa Kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika*". Takwimu zinaonyesha hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara haijapeleka fedha yoyote kwenye mradi huo. Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2017/18 Wizara ya Fedha na Mipango imetenga tena kiasi cha **shilingi bilioni 60** kwa ajili ya kuteleza mradi huu. Kamati ingependa Bunge lako tukufu lipewe taarifa ya utekelezaji wa mradi huu ikiwemo '*pilot study*' husika ili lipate fursa ya kuishauri Serikali tena kuhusu utekelezaji wa mradi huu.

#### 4.6. Huduma kwa wastaafu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuboresha huduma kwa wastaafu ikiwemo kuwapokea, kuwahakiki na kuweka kumbukumbu bora za wastaafu katika mfumo wa kompyuta na kufanya mfumo mzima wa pensheni kuwa wa kompyuta pamoja na kuunganisha katika masijala kuu. Huduma zote hizi zinasaidia kupunguza msongamano na usumbufu kwa wastaafu. Pamoja na hatua hii nzuri ya Wizara, Kamati inashauri kuhakikisha pensheni kwa wastaafu inatoka haraka kwa wakati unaostahili ili kuwapunguzia wastaafu hawa makali ya maisha baada ya kuitumikia Serikali kwa muda mrefu. Aidha, Ni vyema Serikali ikaendelea kulipa deni la PSPF na Mifuko mingine ili iweze kuhudumia malipo ya wastaafu hawa kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye mabadiliko yaliyotolewa kupitia GN No 209 ya mwaka 2009 ya kurekebisha pensheni zao za kila mwezi. Serikali itimize ahadi yake ya kutoa *Non Cash Bond* ya trilioni 2.6 kwa Mfuko wa PSPF ili uweze kupunguza mzigo mkubwa wa malipo ya wastaafu.

#### 4.7. Mikopo katika mabenki ili kumiliki sehemu za majengo

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa Mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa sheria ya kurekebisha sheria mbalimbali kuwezesha ardhi kutumika kupata mikopo ya kibenki kupitia '**Mortgage Finance Act, 2008**', na Muswada wa sheria ya miliki za sehemu za majengo '**The Unit Titles Act, 2008**' ambao uliweka utaratibu kisheria wa kutoa miliki za sehemu za majengo. Lengo kuu la sheria hizi lilikuwa ni kuwawezesha Watanzania hasa wenye kipato cha chini kukopa kupitia ardhi au kupata nyumba au fedha za kujenga nyumba na kumilikishwa sehemu ya jengo husika. Hata hivyo ni miaka nane (8) imepita, sheria hizi pamoja na ile ya *lease financing* hazijaeleweka vizuri kwa wananchi na pia Benki zetu bado hazijapewa msukumo wa kutosha na Serikali wa kuwakopesha wananchi wenye kipato cha chini ili waweze kufaidika na huduma hizi kwa gharama nafuu. Kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira na kuweka mfumo wa

upatikanaji wa mikopo hii kwa urahisi na uwazi, kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa sehemu ya nyumba kwa gharama nafuu pamoja na kumlinda mkopaji na mkopeshaji kwa kuzingatia sheria husika.

#### **4.8 Marekebisho ya Sheria mbalimbali za usimamizi na upatikanaji wa fedha kwa halmashauri toka kwa wahisani mbalimbali.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuna mkanganyiko wa sheria mbalimbali za usimamizi na upatikanaji wa fedha kwa halmashauri toka kwa wahisani pindi wanapoingia mikataba ya kuendeleza miradi ya maendeleo ya halmashauri husika. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuzifanyia tathmini sheria mbalimbali za usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma ili kutoa fursa kwa halmashauri mbalimbali kufaidika na fedha za wahisani pindi wanapoingia mikataba ya kugharamia miradi ya maendeleo bila kulazimika kulipa kodi mbalimbali kama vile Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

#### **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Josephat S. Kandenge, Mbunge wa Kalambo na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano anaonipatia. Pia, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb



9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
16. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
17. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
18. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
19. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
22. Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb
25. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga, Mb
26. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
27. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
28. Mhe. Joseph Roman selasini, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Philip Mpango Mb, Naibu Waziri Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizochini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika Dkt. Tulia Akson, Mb na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii na kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu Tisa (9) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

30 Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Sasa tunakaribisha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, kabla haujaanza tu, naomba nikukumbushe kwamba ukurasa wa 18 vitabu ambavyo Waheshimiwa Wabunge tumepewa kuna maneno yameondolewa na Mheshimiwa Spika na katika kabrasha ambalo unalisoma ni ukurasa wa 22. Kwa hiyo, naomba tafadhali tufuate maagizo ya Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Hawajakusikia Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa wamenisikia, naomba uendelee.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya kuanza kusoma hotuba yangu, nitaomba baadaye utoa utaratibu, leo kwa mara ya kwanza wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha hotuba hapa Bungeni pamoja na Kamati wataalam wa Wizara ya Fedha hawakuwepo kabisa katika

eneo la Bunge. Kwa hiyo, ni vizuri sasa utaratibu ujulikane kwa sababu wao ndio wenye jukumu la kusimamia. Naomba utoe utaratibu juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee kuhusu bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ni ndefu na naomba iingie kama ilivyo kwenye *Hansard* kwa sababu nitasoma kwa kurukaruka baadhi ya vipengele..

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ni utangulizi. Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kuchukua fursa hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele na kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Halima James Mdee ambaye ndiye Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu kama Naibu wake. Kimsingi najivunia kufanya kazi na Waziri Kivuli mchapa kazi, msikivu, mweledi, jasiri, Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nitumie fursa hii kuishukuru Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

kwa msaada wao katika kufanya utafiti wa kina ambao ndiyo umekuwa msingi wa maandalizi ya hotuba hii. Niwatie moyo, waendeleo kufanya kazi yao kwa weledi kwa manufaa ya Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuungana na Watanzania wenzangu wote na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa pole kwa wazazi, familia na uongozi wa shule kwa wanafunzi 32, Walimu na dereva wa Shule ya Lucky Vincent waliopoteza maisha Mkoani Arusha mnamo tarehe 6 Mei, 2017 katika maeneo ya Rhotia Marera, wakiwa njiani kuelekea Wilaya ya Karatu kwa ajili ya mitihani ya ujirani mwema kujipima uwezo na shule ya wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza utangulizi wangu wa hotuba hii napenda nimnukuu Bw. Adam Smith katika kitabu chake cha *Wealth of Nations*. Mtaalam huyo alipata kusema kuwa, nitanukuu:

*“No society can surely be flourishing and happy, of which the far greater part of the members are poor and miserable.”* Akimaanisha kuwa, “hakuna jamii ambayo inaweza kuwa na uhakika wa furaha na kufanikiwa endapo sehemu kubwa ya watu wake ni maskini na walala hoi” Wizara hii ikitimiza majukumu yake kwa ufanisi, Watanzania walio wengi hawatakuwa maskini kama walivyo hivi leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inahusu majukumu ya Wizara ya Fedha, mtaisoma kama ilivyo katika kitabu chetu. Nakwenda sehemu ya tatu maoni ya zamani kwa maana ya siku za nyuma ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2012/13 na 2013/2014, kuna mambo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza yafanyiwe kazi na Serikali ili kuleta tija na ufanisi katika utendaji wa Wizara. Kuna ambayo yalifanyiwa kazi, kuna

yanayoendelea kufanyiwa kazi na kuna ambayo hayajafanyiwa kazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo hayajafanyiwa kazi kwa ufanisi ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia chini ya asilimia moja ya Pato la Taifa. Serikali imechukua hatua kadhaa za kupunguza misahama ya kodi. Hata hivyo, hatua husika bado haijafikia lengo la Taifa ambalo lilikuwa ni kupunguza misamaha hadi kufikia chini ya asilimia moja ya pato la Taifa. Kiasi kinachosamehewa kodi kwa mujibu wa ripoti ya CAG Machi, 2017 ni shilingi trilioni 1.1 tu, kiasi hicho ambacho kinazidi zaidi ya asilimia moja ya pato la Taifa. Hivyo basi, bado Serikali inatakiwa kuendelea kuchukua hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali itaendelea kupitia upya motisha za kodi zinazotolewa kwa lengo la kupunguza viwango vya misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia 1 au pungufu ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika bado kuna tatizo sugu katika uhibitaji wa kodi ya mafuta hususan kwenye kampuni za uchimbaji wa madini. Ripoti ya hivi karibuni ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainisha kwamba, kuna kampuni ambazo zilipata msamaha wa kodi ya mafuta ambazo hazikustahili kupata misamaha hiyo. Mathalani ripoti hiyo inaonesha kwamba, lita 20,791,072 za mafuta katika kipindi cha miezi 18 kuanzia Julai, 2014 na Desemba, 2015 yalisafirishwa kwenda kwa Mkandarasi *M/S Agreko Company Limited* ambaye hakustahili kupewa msahama wa kodi. Jumla ya thamani ya mafuta hayo ilikuwa ni shilingi bilioni 10.174. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo pendekezo hili lingetekelezwa ipasavyo, mapato ya Serikali yangeongezeka. Pia, ingesaidia kupunguza nakisi ya bajeti ya Serikali kwa

kutegemea misaada na mikopo ya nje pamoja na mikopo ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kufanya uchunguzi kupitia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (*PPRA*) kuhusu manunuzi ya mafuta ya kuendesha mitambo ya *IPTL* ya kuzalisha umeme. Pendekezo hili lilitokana na matumizi yenye mashaka ya shilingi bilioni 1.4 kwa siku kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendesha mitambo hiyo. Katika pendekezo hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tuliitaka Serikali kuleta taarifa ya uchunguzi huo Bungeni. Mpaka sasa, taarifa rasmi ya uchunguzi huo haijawahi kuletwa katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ikumbukwe kuwa ni kwa kipindi kirefu sasa Serikali ilitoa ahadi ya kubadilisha mitambo ya *IPTL* itumie gesi badala ya mafuta yenye gharama kubwa lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa. Kwa mujibu wa *CAG*, moja ya sababu zinazoifanya *TANESCO* kuwa na malimbikizo makubwa ya madeni kunatokana na madeni katika manunuzi ya umeme kutoka kwa wazalishaji huru wa nishati (*IPP*) na wazalishaji wa dharura wa nishati (*EPPs*) watano. Hii inatokana na *TANESCO* kununua umeme kwa bei ya wastani wa shilingi 544 na kuuza shilingi 276 kwa kila *unit* hivyo kusababisha hasara ya shilingi 265.30 kwa *unit* moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kuielekeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kama vile reli na bandari. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa pendekezo hili kwa kuwa uwekezaji wa mifuko hii ulikuwa umelenga kwenye ujenzi wa majengo makubwa ya makazi na biashara ambao unatumia fedha nyingi, huku mapato yanayopatikana (*return on investment*) yakiwa ni kidogo, jambo lililosababisha kuchukua kipindi kirefu kurudisha gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwekeza katika eneo moja na kumlenga mteja mmoja, majengo mengi yalikosa wapangaji na hivyo kufanya mradi mzima

uwe ni wa hasara. Pendekezo hili bado halijafanyiwa kazi na kwa sababu hiyo, bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea na msimamo wake wa kuendelea kuitaka Serikali kuelekeza Mifuko ya Hifadhi za Jamii kuwekeza kwenye miradi yenye faida za haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, kutoa taarifa ya hesabu za robo mwaka za kila Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kama ilivyo katika mabenki ili wanachama waweze kupata fursa za kuona utendaji wa mifuko wanayohifadhi fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, kuhamisha Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwenye Wizara ya Kazi na Ajira ambayo kimsingi ndiyo inayohusika na hifadhi ya jamii kwa maana ya *social security*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kwa muda mrefu sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha imekuwa ama ikichelewa kupeleka fedha kwenye Wizara na Idara mbalimbali za Serikali au kutoa fedha pungufu na katika mazingira mengine kutokutoa fedha kabisa kama ambavyo zimeidhinishwa na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuandaa makisio yake ya mwaka yanayoshabihiana na makusanyo ya mapato. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zako za Kudumu za Bunge, rejea Taarifa za Kamati za Bunge kwa mfano Bunge la Bajeti la 2017, nazo zimeona tatizo hilo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika Wizara na Idara za Serikali wanazosisimamia utoaji wa fedha za maendeleo umekuwa finyu sana. Hali hii inaondoa umuhimu wa Bunge kukaa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi la kujuliza hapa ni kwamba; hizo fedha ambazo Serikali inajisifu kukusanya kwa wingi zinakwenda wapi? Au zinatumika vibaya, kwa maana ya matumizi ambayo hayajaidhinishwa

na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini haikutoa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo kwa takriban Wizara zote, kwa kisingizio kwamba kulikuwa na upungufu wa fedha lakini wakati huo huo inautangazia umma kwamba imekusanya mapato mengi kuzidi lengo la makusanyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache ya jinsi ambavyo Serikali haikutoa fedha za maendeleo kwa ukamilifu wake katika baadhi ya Wizara ili tuweze kujipima kama tunasonga mbele kama Taifa, kuiendeleza Tanzania ya viwanda au Serikali inawahadua wananchi.

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Kati shilingi bilioni 10.9 za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 1.2 tu sawa na asilimia 11.3 ya fedha hizo zilitolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(ii) Tume ya Kudhibiti Ukimwi. Kati ya shilingi bilioni 10.1 za fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 2.7 tu sawa na asilimia 27 ya bajeti ndiyo zimetolewa.

(iii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kati ya shilingi bilioni 897.6 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ni shilingi bilioni 500, sawa na asilimia 55 ndizo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2017. Hata hivyo, mchanganuo wa fedha hizo ni kwamba, shilingi bilioni 427 sawa na asilimia 48 zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na shilingi bilioni 470 sawa na asilimia 52 zilikuwa ni kwa ajili ya kugharamia miradi halisi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo katika sekta ya elimu zinaonekana kuwa nyingi kwa kuwa zimechanganywa pamoja na fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba ni muhimu tukatenganisha kati ya miradi halisi ya maendeleo na mikopo ya wanafunzi ili kuweza kupata picha



halisi ya nini kinakwenda kutumika kutatua changamoto za uboreshaji, upanuzi, ujenzi wa miundombinu na shughuli za utafiti katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye miradi halisi ya maendeleo, kati ya miradi 16 ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ya Bunge ya Maendeleo na Huduma za Jamii ilifanya ukaguzi wa miradi mitano tu sawa na asilimia 12 ya miradi yote. Kati ya miradi hiyo mitano, ni miwili tu iliyopatiwa fedha tena kwa kiwango kidogo sana. Ifuatayo ni hali halisi ya miradi.

(a) Mradi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, mradi namba 6361, ulitengewa shilingi bilioni nne lakini hawakupeleka hata shilingi moja.

(b) Mradi wa ukarabati wa Chuo Kikuu uliidhinishiwa shilingi bilioni 9.4 lakini hakuna hata shilingi moja iliyopeleka. *(Makofi)*

(c) Mradi wa Hospitali ya Mloganzila uliombewa shilingi bilioni 14.5 lakini mpaka kufikia tarehe 13 Mei, hakuna fedha yoyote iliyopeleka. *(Makofi)*

(d) Mradi wa Mfuko wa Utafiti wa Maendeleo (*COSTECH*), mradi namba 6345. Katika malengo ambayo nchi imejiwekea, ni kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa. Hata hivyo, mfuko huu ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 12.8, sawa na asilimia 0.012 ya pato la Taifa. Pamoja na udogo huo, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 4.7 tu, sawa na asilimia 31.7. *(Makofi)*

(e) Mradi wa ujenzi wa *DIT Teaching Tower*, mradi namba 4384. Mradi huu una umri wa miaka 11 bado unasuasua, hakuna pesa na matokeo yake gharama za mradi zimeongezeka kutoka shilingi bilioni tano mpaka shilingi bilioni tisa. *(Makofi)*

(iv) Wizara ya Maji, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Kati ya shilingi bilioni 35.3 za miradi ya maendeleo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

zilizodhinishwa na Bunge, ni shilingi bilioni 2.9 tu sawa na asilimia 8.4 zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa upande wa usambazaji wa maji, mijini na vijijini kati ya shilingi bilioni 915.1 zilizotengwa, zilizotolewa ni shilingi bilioni 181.2 sawa na asilimia 19.8 ya fedha zote za miradi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utekelezaji duni namna hii wa bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji ni matusi kwa Watanzania ambao uhaba wa maji umewafanya waishi kama wanyama. Ule usemi wa Serikali wa 'kumtua mama ndoo ya maji', katika mazingira haya ni dhihaka kwa akinamama wote wa nchi hii ambao wanaendelea kusota na kukumbana na kila aina ya kadhia katika kutafuta maji. Ikumbukwe kwamba hawa ndiyo mtaji mkubwa wa kura waliyoipa ushindi Serikali iliyopo madarakani. *(Makofi)*

(v) Wizara ya Viwanda. Kati ya shilingi bilioni 42.1 zilizotengwa, Wizara ilipokea shilingi bilioni 7.6 tu sawa na asilimia 18.6. Kwa utekelezaji huu wa bajeti, ni aibu kwa Serikali kutumia Kauli Mbiu ya Tanzania ya Viwanda kama kampeni ya kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia viwanda wakati umetenga asilimia 18 tu. *(Makofi)*

(vi) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wizara hii ambayo ni nyeti kwa usalama wa nchi yetu, nayo ilikumbana na panga ambalo limezikumba Wizara mbalimbali. Moja ya mradi muhimu sana ni mradi wa *Defence Scheme*, mradi namba 6103 na tumeweka kielelezo hapo, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 151.1 mpaka Machi, ikiwa ni robo ya tatu ya mwaka Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 30 tu sawa na asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mradi tajwa hapo juu kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, fedha ya miradi ya maendeleo iliyowasilishwa ni asilimia 14 tu yaani Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 230, pesa zilizotolewa hadi Machi ni shilingi bilioni 33.9. Halafu tunaitangazia dunia kwamba tuna

lengo la kuwa na jeshi dogo la kisasa lenye weledi, kwa bajeti ipi? (Makofi)

(vii) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa shilingi bilioni 101, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 3.36 sawa na asilimia 3.31. Kwa upande wa mifugo na uvuvi, ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 15.8 kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 1.2 sawa na asilimia nane. Kwa maneno mengine, kilimo ambacho tunasema kwamba ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania bajeti yake ya maendeleo haikuteklezwa kwa takriban asilimia 97. Serikali inahubiri Uchumi wa Viwanda ikijua fika kwamba viwanda hivyo haviwezi kuendelea bila ukuaji katika sekta ya kilimo, lakini haitoi fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba ama Serikali imefilisika ila haitaki kukiri hivyo, au kuna tatizo kubwa katika *mental health* miongoni mwa watendaji wa Serikali. Haingii akilini kwamba ile sekta ambayo inategemewa kuleta hayo mapinduzi ya viwanda haipewi fedha za kutosha halafu Serikali inaendelea kuhubiri viwanda, vitatoka wapi kwa asilimia tatu? (Makofi)

(viii) Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika fedha za ndani za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni mbili, fedha zilizopelekwa ni shilingi milioni 156, sawa na 8%.

(ix) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 25.3 lakini fedha zilizopelekwa mpaka sasa ni shilingi bilioni 7.63 tu.

(x) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Wizara hii ilitengewa fedha za maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

- Ujenzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.17, zilizotolewa ni trilioni 1.07, sawa na asilimia 58.7

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- Uchukuzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.49, zilizotolewa ni shilingi bilioni 761.5 sawa na asilimia 30.5

(xi) Wizara ya Fedha na Mipango. Fedha za maendeleo zilizoidhinishiwa katika Wizara ya Fedha na Mipango ni shilingi bilioni 791.99, fedha za ndani ni shilingi bilioni 723.15 na fedha za nje ni shilingi bilioni 68.84. Hadi kufikia Machi fedha zilizotumika ni shilingi bilioni 18.89 sawa na asilimia 2.3 ya shilingi bilioni 700. Kati ya shilingi bilioni 18.89, shilingi bilioni 1.31 ni fedha za ndani sawa na asilimia 0.18 na shilingi bilioni 17.58 ni fedha za nje sawa na asilimia 25. Sasa hii ndiyo Wizara inayosimamia mipango ya nchi hii yenyewe tu inajichechemea haiwezi kujihudumia, itahudumia Wizara nyingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa hapo juu unaonyesha wazi kwamba, ufanisi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo na mpango wa kuwaondolea umasikini wananchi ni kwa wastani wa 0%- 20%. Wizara pekee iliyoweza kuvuka ni Wizara ya Ujenzi na inafahamika kwamba yapo maslahi mapana ya kitaifa yanayohitaji kulindwa katika Wizara hii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM katika vipindi mbalimbali, imekuwa ikituambia kwamba Chama hicho kupitia Dira ya Maendeleo ya 2025 na 2020 ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwelekeo wa sera za CCM katika miaka 2000 -2010-2015 imeelekeza suluhisho la kuondokana na hali ya uchumi kuwa nyuma na tegemezi ni kufanya *modernization* ya uchumi. Mchakato wa *modernization* ya uchumi na kuitoa nchi yenye uchumi tegemezi kuelekea uchumi wa kisasa utazingatia vipaumbele vifuatavyo:-

- (i) Kutilia Mkazo katika matumizi ya maarifa ya kisasa, sayansi na teknolojia;
- (ii) Kuandaa rasilimali watu katika maarifa na mwelekeo;

- (iii) Kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi;
- (iv) Kufanya mapinduzi ya viwanda ambavyo ndiyo kiongozi wa uchumi wa kisasa; na
- (v) Mapinduzi katika nishati na miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msingi ambalo Wabunge wa pande zote mbili tunapaswa kutafakari na kujuliza, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hapo juu, hivi ni kweli itakapofika mwaka 2020 ama 2025 malengo (i)-(v) yatatimia? Kama nafsi zetu zinatumia kwamba hayatatimia, tunajipanga vipi kutumia kipindi hiki cha bajeti kujisahisha ili mwaka ujao wa fedha tusijulize maswali hayahaya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne, Ofisi ya Msajili wa Hazina, mtasoma pale mwanzoni, nakwenda chini narukaruka. Taarifa ya Mdhimitina Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetaja baadhi ya mashirika ya umma pamoja na changamoto zinazoyakabili mashirika hayo na kushauri hatua za haraka zichukuliwe ili kuyanusuru. Miongoni mwa Mashirika hayo ni kama ifuatavyo: Wameeleza *TANESCO*, nimeshaisoma hapo mwanzoni; kuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa maana *NSSF, PPF, PSPF* na *LAPF*, nitaisoma hii kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko hii inakabiliwa na tatizo la kushuka kwa mapato ya uwekezaji kutokana na kutokuwepo kwa ufanisi wa menejimenti katika kusimamia mikopo iliyotolewa. Aidha, kuna usimamizi hafifu wa utaratibu na kudhibiti madeni ya muda mrefu na kuchelewa kulipwa kwa madeni ambayo mifuko inaidai Serikali. Serikali imekuwa na tabia ya kutumia huduma au kukopa katika taasisi zake bila kufanya malipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika mengine utaona kuna Mfuko wa Bima ya Afya (*NHIF*); Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*) na Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano, inahusu Msajili wa Hazina kutokuwa na uwezo wa kusimamia Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Tumeieleza hapo mpaka chini na nieleze tu kutokana na ukosefu wa umakini katika kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yapo matukio ambayo kwa hali zote hayakuzingatia weledi jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kubwa katika mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya ni pamoja na mkopo wa *PSPF* shilingi bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo na marejesho ya mikopo ya wanafunzi shilingi bilioni 51.1 ya *NSSF*. Taarifa za fedha za *NSSF*, nimeainisha hapo itasomwa. Niseme tu mifano hiyo hapo juu inadhirisha kwamba Wizara ya Fedha haitimizi majukumu yake ipasavyo na haiko makini katika kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita, Ripoti ya Msajili Wa Hazina kuhusu utendaji wa Kampuni ya Ndege ya Taifa. Kampuni hii ilianzishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura 212 kama kampuni ya biashara ya usafiri wa anga. Mwezi Oktoba, 2016, Serikali ilinunua ndege sita, mbili kati ya hizo zimeshafika na kuanza kazi. Kwa mujibu wa kitabu cha mpango wa maendeleo 2017/2018, katika mwaka wa fedha 2017/2018, zimetengwa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege tatu zilizosalia. Kwa lugha nyingine ndege zote sita zitaligharimu Taifa si pungufu ya shilingi trillion moja. Kwa hiyo, mtasoma yale maelekezo yapo hapo tumelielezea Shirika la Ndege vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba inahusu mafao ya wastaafu; mafao ya watumishi wa umma; dhuluma dhidi ya waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeeleza namna ambavyo Serikali inatakiwa iwasaidie hawa wazee wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane tumezungumzia hali ya uchumi wa nchi na kuendelea kupanda kwa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei umeendelea kupanda siku hadi siku kutokana na sera mbovu jambo ambalo linalopelekea wananchi wenye kipato duni

kuumia. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu (*Monthly Economic Review*) iliyotolewa Aprili, 2017, mfumuko wa bei umepanda kutoka asilimia 5.4 Machi, 2016 mpaka asilimia 6.4 Machi, 2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda huku kwa mfumuko wa bei kumeathiri kupanda kwa bei za chakula kama vile mahindi, mihogo, mtama, mchele, ndizi, dagaa na vitu vingine. Katika gazeti la kila siku la Mwananchi limeripoti tarehe 3 Aprili, 2017, kupitia uchunguzi uliofanywa katika masoko mbalimbali na kubaini kuwa bei za mazao zimepanda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, bei ya maharage imepanda kutoka Sh.1,800 kwa kilogramu mpaka Sh.2,700 mpaka Sh.3,000. Mazao mengine yaliyopanda bei kwa ukubwa usiokuwa wa kawaida ni pamoja na sukari kutoka bei elekezi ya Sh.1,800 kwa kilo moja mpaka kufikia Sh.2,500; mchele umepanda kutoka Sh.1,200 kwa kilo moja mpaka kufikia Sh.2,600 ; na unga wa sembe nao umepanda kutoka Sh.1,000 mpaka kufikia Sh.2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu juu ya hatua stahiki zinachokuliwa ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ndani ya Bunge lako Tukufu kuwa ni lini itabadilisha Sera zake za Fedha na matumizi ya Serikali ili kudhibiti mfumuko wa bei unaofanya maisha ya wananchi wa Tanzania kuwa duni na kushindwa kumudu gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sehemu hii tumeongelea kuhusu uwepo wa njaa na hifadhi duni ya chakula na mzunguko wa fedha, riba na hali ya mikopo, mtaipitia hapo. Ningesoma kidogo hapa ili muone; kwa mujibu wa Ripoti ya Benki Kuu ya Aprili, 2016 na Machi, 2017, mikopo ya kibiashara kwa sekta binafsi ilishuhudia ukuaji wa asilimia 23.6 kwa mwaka 2016 na ilipofika Machi, 2017 ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umepungua kwa kasi ya ajabu

mpaka kufikia asilimia 3.7 kwa mwaka. Kwa hiyo, tunataka Serikali ichukue tahadhari ione namna gani ambavyo uchumi umezidi kuporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumezungumzia tafrani ya sera ya Serikali kuweka fedha *BoT* na athari zake na tumeainisha baadhi ya mabenki, mpaka sasa kuna benki kadhaa za kibiashara zimerekodi hasara zake katika hesabu zao. Kwa mfano, benki ya Barclays imepata hasara ya bilioni bilioni 8.2; *TBI Tanzania Development Bank* imepata hasara ya shilingi bilioni 6.27; *Stanbic Bank Tanzania* imepata hasara ya shilingi bilioni 2.4; *CRDB Bank* imepata hasara ya shilingi bilioni 1.9 na *Amana Bank* imepata hasara ya shilingi milioni 195. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ikubaliane na hoja ya kuamua kuwa na falsafa moja ya ujenzi wa uchumi na kuacha kutokueleweka kuwa inasimamia mfumo upi wa uchumi. Falsafa hii itajenga misingi itakayozuia viongozi wa kisiasa wasio na ujuzi wala weledi na taaluma ya uchumi kuacha kuibuka na matamko yanayopelekea anguko la uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali ikubaliane na ukweli kuwa kuzipeleka fedha za mashirika ya Serikali na kuzitunza katika akaunti maalum zilizopo Benki Kuu siyo suluhisho la kudumu la kuzuia matumizi mabaya ya fedha wala siyo tija ya kuzuia wizi na ubadhirifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya Awamu ya Tano kuelewa kuwa njia salama ya Serikali kuzuia wizi wa fedha za umma siyo kuzificha katika akaunti maalum kwa kuwa kwa vyovyote vile lazima zitatolewa ili zitatumike kugharamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya umma. Njia sahihi ya kuzuia wizi ni kuimarisha usimamizi wa fedha (*finance management*) ndani



ya mashirika ya umma na Serikali; kuimarisha sera ya matumizi ya fedha kwenye miradi ya kimkakati na kuziba mianya ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kuna hoja kweli kweli za msingi, ningeomba yote niliyoyazungumza na yale ambayo sijayasema yaingie katika *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Silinde. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA  
HALIMA JAMES MDEE (MB), KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI  
WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2016/17, PAMOJA NA MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2017/18 KAMA  
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/17, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kuchukua fursa hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele na kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Momba. Pili, napenda kutumia fursa hii kumshukuru, na pia kumpongeza Mheshimiwa Halima James

Mdee (Mb) ambaye ndiye Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu kama Naibu wake. Kimsingi najivunia kufanya kazi na Waziri Kivuli mchapa kazi, msikivu na mwenye weledi, kama Mheshimiwa Halima Mdee.

**Mheshimiwa Spika**, hali kadhalika nitumie pia fursa hii kuishukuru Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa msaada wao katika kufanya utafiti wa kina ambao ndio umekuwa msingi wa maandalizi ya hotuba hii. Ninawatia moyo, waendeele kufanya kazi yao kwa weledi kwa manufaa ya taifa hili.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuungana na Watanzania wenzangu wote na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa pole kwa wazazi, familia na uongozi wa shule kwa wanafunzi 32, walimu na dereva wa Shule ya Lucky Vincent waliopoteza maisha mkoani Arusha mnamo tarehe 6 Mei, 2017 katika maeneo ya Rhotia Marera, wakiwa njiani kuelekea wilayani Karatu kwa ajili ya mitihani ya ujirani mwema kujipima uwezo na shule ya wenzao.

**Mheshimiwa Spika**, ninapomalizia utangulizi wangu napenda kila Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwa ujumla wafahamu kuwa Wizara hii ya fedha ndio inaweza kuwatoa Watanzania kwenye umasikini kama sio kuendelea kuwabakiza katika hali hiyo, kama alivyosema Mtaalamu wa masuala ya fedha na uchumi duniani Bw. Adam Smith<sup>1</sup> katika kitabu chake cha Wealth of Nations. Mtaalamu huyo alipata kusema kuwa, nitanukuu ***“no society can surely be flourishing and happy, of which the far greater part of the members are poor and miserable.”*** Akimaanisha kuwa *“hakuna jamii ambayo inaweza kuwa na uhakika wa furaha na kufanikiwa endapo sehemu kubwa ya watu wake ni masikini na walalahoi”* Wizara hii ikitimiza majukumu yake kwa ufanisi, Watanzania walio wengi hawatakuwa masikini kama walivyo hivi leo!

---

<sup>1</sup> Wealth of Nations, Book V, Chapter I, Part III, Article II, p. 764, para. 15.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na umuhimu wa Wizara hii katika maendeleo ya nchi yetu, Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inao wajibu wa kuwakumbusha wabunge majukumu ya Wizara hii, ambayo ni:

- i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla,
- ii) Kusimamia ukusanyaji wa **mapato** ya ndani na nje ya nchi pamoja na **matumizi** yake,
- iii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali,
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umasikini katika sekta mbali mbali,
- v) Kusimamia deni la Taifa,
- vi) Kusimamia upatikanaji wa rasilimali fedha zinazopatikana katika miradi ya ubia baina ya Serikali na sekta binafsi,
- vii) Kusimamia sera, sheria ,kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa Umma,
- viii) Kusimamia Mali za Serikali,taasisi na mashirika ya Umma (treasurer registrar),
- ix) Kusimamia masuala ya Tume ya Pamoja ya fedha,
- x) Kuandaa na kulipa mishahara watumishi Serikalini,
- xi) Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni ya wastaafu,
- xii) Kudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa majukumu hayo ya wizara, ni dhahiri kwamba mafanikio ya mipango yote tunayopanga kama Taifa unategemea ufanisi katika Wizara hii.

### 3.0 MAONI YA NYUMA YA KAMBI YA UPINZANI

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka 2012/13 na 2013/ 2014, kuna mambo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza yafanyiwe kazi na Serikali ili kuleta tija na ufanisi katika utendaji wa wizara. Kuna ambayo yalifanyiwa kazi, kuna yanayoendelea kufanyiwa kazi na kuna ambayo hayajafanyiwa kazi kabisa.

Mambo ambayo hayajafanyiwa kazi kwa ufanisi ni pamoja na haya yafuatayo:

*i. Kupunguza Misamaha ya Kodi hadi kufikia chini ya Asilimia 1 ya Pato la Taifa.*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imechukua hatua kadhaa za kupunguza misamaha ya kodi. Hata hivyo, hatua husika bado haijafikia lengo la Taifa ambalo lilikuwa ni kukupunguza misamaha hiyo hadi kufikia chini ya asilimia 1 ya pato la Taifa. Kiasi kinachosamehewa kodi kwa mujibu wa ripoti ya CAG (Machi 2017) ni shilingi Trillion 1.1 tu, kiasi ambacho bado kinazidi asilimia 1 ya pato la taifa. Hivyo, bado Serikali inatakiwa kuendelea kuchukua hatua zaidi . Ni rai ya kambi ya upinzani kwamba Serikali itaendelea kupitia upya motisha za kodi zinazotolewa kwa lengo la kupunguza viwango vya misamaha ya kodi hadi kufikia 1% au pungufu ya hapo.

**Mheshimiwa Spika**, halikadhalika bado kuna tatizo sugu katika udhibiti wa kodi ya mafuta hususan kwenye kampuni za uchimbaji madini. Ripoti ya hivi karibuni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainisha kwamba, kuna kampuni ambazo zilipata msamaha wa kodi ya mafuta ambazo hazikustahili kupata misamaha hiyo. Mathalani ripoti hiyo inaonyesha kwamba, **lita 20,791,072** za mafuta katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Julai 2014 na Desemba 2015 yalisafirishwa kwenda kwa mkandarasi M/S Agreko Company Limited ambaye hakustahili kupewa msamaha wa kodi . Jumla ya tamani ya mafuta ilikuwa ni **shilingi 10,174,646,166**.

**Mheshimiwa Spika**, endapo pendekezo hili lingetekelezwa ipasavyo, mapato ya Serikali yangeongezeka. Pia, ingesaidia kupunguza nakisi ya bajeti ya Serikali kwa kutegemea misaada na mikopo ya nje pamoja na mikopo ya ndani.

*ii. Kufanya uchunguzi kupitia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) kuhusu manunuzi ya mafuta ya kuendesha mitambo ya IPTL ya kuzalisha umeme.* **Mheshimiwa Spika**, pendekezo hili lilitokana na matumizi yenye mashaka ya **shilingi bilioni 1.4** kila siku kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendesha mitambo hiyo. Katika pendekezo hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tuliitaka Serikali kuleta taarifa ya uchunguzi huo Bungeni. Mpaka sasa, taarifa rasmi ya uchunguzi huo haijawahi kuletwa katika Bunge hili tukufu. Pia, ikumbukwe kuwa ni kwa kipindi kirefu sasa Serikali ilitoa ahadi ya kubadilisha mitambo ya IPTL itumie gesi badala ya mafuta yenye gharama kubwa, lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa. Kwa mujibu wa CAG moja ya sababu zinazofanya Tanesco kuwa na Malimbikizo makubwa ya madeni kunatokana na madeni katika manunuzi ya umeme kutoka kwa **wazalishaji huru** wa nishati (IPPs) na **wazalishaji wa dharura wa nishati** (EPPs) watano. Hii inatokana na Tanesco kununua umeme kwa bei ya wastani wa **shilingi 544.65** na kuuza **shilingi 279.30** kwa kila unit hivyo kusababisha hasara ya **shilingi 265.30** kwa kila unit.

*ii) Kuelekeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye Maeneo yanayochochea Ukuaji wa Uchumi kama vile Reli na Bandari.*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa pendekezo hili kwa kuwa uwekezaji wa mifuko hii ulikuwa umelenga kwenye ujenzi wa majengo makubwa ya makazi na biashara ambao unatumia fedha nyingi, huku mapato yanayopatikana (return on investment) yakiwa ni kidogo jambo linalosababisha kuchukua kipindi kirefu kurudisha gharama (Payback period). Kutokana na kuwekeza katika eneo moja, na kumlenga mteja mmoja, majengo mengi yalikosa wapangaji na hivyo kufanya mradi mzima uwe ni wa hasara. Pendekezo hili bado halijafanyiwa kazi na kwa

sababu hiyo, bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea na msimamo wake wa kuendelea kuitaka Serikali kuielekeza mifuko ya hifadhi za jamii kuwekeza kwenye miradi yenye faida ya haraka.

iii) Kutoa taarifa ya hesabu za robo mwaka za kila mfuko wa hifadhi ya Jamii kama ilivyo katika mabenki ili wanachama waweze kupata fursa za kuona utendaji wa mifuko wanakohifadhi fedha zao.

iv) ***Kuhamishia mifuko yote ya hifadhi ya Jamii kwenye Wizara ya Kazi na Ajira ambayo kimsingi ndiyo inayohusika na hifadhi ya jamii (Social Security). Mheshimiwa Spika,*** pendekezo hili lilitokana na kwamba kwa hali ilivyo sasa mifuko hii iko katika Wizara tofauti tofauti jambo ambalo linaleta ugumu katika kuidhibiti na kuisimamia. Hoja hiyo mpaka sasa haijatekelezwa. Mamlaka ya Kusimamia mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) haijaweza kudhibiti kwa ufasaha mifuko yote ya hifadhi ya Jamii nchini.

#### 4.0 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa Serikali kupitia Wizara ya fedha imekuwa ama ikichelewa kupeleka fedha kwenye Wizara na idara mbalimbali za Serikali au kutoa fedha pungufu na katika mazingira mengine kutokutoa fedha kabisa kama ambayo zimeidhinishwa na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuandaa makisio yake ya mwaka, yanayoshihiana na makusanyo ya mapato!!Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama zilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati zako za kudumu za Bunge (Rejea Taarifa zote za Kamati, Bunge la Bajeti 2017), nazo zimeona tatizo hili kutokana na ukweli kwamba katika Wizara na idara za Serikali wanazosisimamia utoaji wa fedha za maendeleo **umekuwa finyu sana!** Hali hii inaondoa umuhimu wa Bunge kukaa kwa gharama kubwa kupitisha bajeti ya Serikali ambayo haitekelezwi ipasavyo. Tofauti na awamu za utawala zilizotangulia, Serikali hii ya awamu ya tano

ambayo imekuwa ikijigamba kwamba imefanikiwa kukusanya mapato kwa kiwango cha hali ya juu kuzidi makisio iliyoyaweka, kila mwezi imekuwa na hali mbaya zaidi katika utekelezaji wa bajeti na hasa bajeti ya maendeleo kuliko awamu zilizopita.

**Mheshimiwa Spika**, Swali la msingi la kujiuliza hapa ni kwamba; hizo fedha ambazo Serikali inajisifu kukusanya kwa wingi zinakwenda wapi?? Au zinatumika vibaya – kwa maana ya matumizi ambayo hayajaidhinishwa na bunge? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kwa nini haikutoa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo kwa takriban Wizara zote, kwa kisingizio kwamba kulikuwa na upungufu wa fedha lakini wakati huo huo inautangazia umma kwamba imekusanya mapato mengi kuzidi lengo la makusanyo?

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe mifano michache ya jinsi ambavyo Serikali haikutoa fedha za maendeleo kwa ukamilifu wake katika baadhi ya Wizara ili tuweze kujipima kama tunasonga mbele kama taifa kuiendea Tanzania ya viwanda au Serikali inawahadaa wananchi kama ilivyozea.

1. Ofisi ya Makamu wa Rais ( Mazingira)

**Mheshimiwa Spika**, Kati **shilingi bilioni 10.9** za miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, ni shilingi **bilioni 1.2** tu sawa na asilimia **11.3** ya fedha hizo zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa maneno mengine bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira haikutekelezwa **kwa asilimia 88.7**. Ikimbukwe kwamba fedha hizi ndizo hutumika kupambana na uharibifu wa mazingira yetu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamekuwa na athari kubwa sana kwa wananchi kama vile ukame, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, njaa nk. Serikali kutotoa fedha za maendeleo katika Ofisi hii, ili kulinda mazingira yasiharibiwe maana yake ni kubariki athari mbaya zinazotokana na uharibifu wa mazingira ziendelee kuwaangamiza wananchi. Ndio maana hatushangai kuona mkuu wetu akikataza

tuzungumzie habari za njaa, mafuriko au matetemeko kwa kuwa hana mpango nazo, na ndio maana fedha hazitoki.

## 2. Tume ya kudhibiti Ukimwi :

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya shilingi bilioni 10.1 za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, ni shilingi bilioni 2.7 tu sawa na asilimia 27 ya bajeti ndio zimetolewa. Kwa maneno mengine vita dhidi ya maambukizi ya UKIMWI hapa nchini si kipaumbele cha Serikali hii ya awamu ya tano.

## 3. Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya shilingi bilioni 897.6 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ni shilingi bilioni 500.4 sawa na asilimia 55 ndizo ambazo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2017. Hata hivyo, mchanganuo wa fedha hizo ni kwamba, shilingi bilioni 427 (asilimia 48) zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na shilingi bilioni 470 (asilimia 52) zilikuwa ni kwa ajili ya kugharamia miradi halisi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha za maendeleo katika sekta ya elimu zinaonekana kuwa nyingi kwa kuwa zimechanganywa pamoja na fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba; ni muhimu tukatenganisha kati ya miradi 'halisi ya maendeleo' na ' Mikopo ya wanafunzi' ili kuweza kupata picha halisi ya nini hasa kinakwenda kutumika kutatua changamoto za uboreshaji/ upanuzi/ujenzi wa miundombinu na shughuli za utafiti katika sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, tukija kwenye miradi halisi ya maendeleo, kati ya miradi 16 ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/17 Kamati ya Bunge ya Maendeleo na Huduma za Jamii ilifanya ukaguzi wa miradi 5 tu sawa na 12% ya miradi yote. Kati ya miradi hiyo mitano, ni miwili tu iliyopatiwa fedha! Tena kwa kiwango kidogo sana. Ikuatayo ni Hali halisi ya miradi mitano iliyokaguliwa:



(i) Mradi wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) – Mradi namba 6361. Bunge liliidhinisha **shilingi bilioni 4, hakuna fedha yoyote iliyopelekwa**

(ii) Mradi wa ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam (Mradi namba 6350). **Bunge iliidhinisha shilingi bilioni 9.4, hakuna fedha yoyote iliyopelekwa**

(iii) Mradi wa Hospitali ya Mloganzila (Namba ya Mradi 6364). Chuo kiliomba shilingi 14,549,727,933 (BN. 14.5) hakuna fedha iliyopelekwa mpaka 13/Mei /2017 wakati wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya elimu inasomwa.

(iv) Mradi wa Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH (Namba ya Mradi 6345. Katika Malengo ambayo nchi imejiwekea , ni kutenga 1% ya Pato la Taifa. Hata hivyo, mfuko huu ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 12.8 tu sawa na 0.012% ya pato la Taifa** . Pamoja na udogo huo , kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 4.07 tu (sawa na 31.7%). Kati ya hizo fedha **Mfuko mkuu wa Hazina uliotakiwa kutoa bilioni 8 ilitoa shilingi bilioni 1.5 tu** na TCRA iliyotakiwa kutoa shilingi bilioni 4.8 ilitoa shilingi bilioni 2.57 tu.

(v) Mradi wa ujenzi wa DIT Teaching Tower (Namba ya Mradi 4384). Mradi huu una umri wa miaka 11 (2006-2017)...bado unasuasua, hakuna pesa na matokeo yake gharama za mradi zimeongezeka toka bilioni 5 mpaka bilioni 9.

#### 4. Wizara ya Maji

- Tume ya Taifa ya umwagiliaji- Fungu 05:

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya **shilingi bilioni 35.3** za miradi ya maendeleo zilizodhinishwa na Bunge, ni **shilingi bilioni 2.9 tu** sawa na **asilimia 8.4** zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa upande wa **usambazaji wa maji ,mijini na vijijini** kati ya shilingi bilioni 915.1 zilizotengwa, zilizotolewa ni shilingi bilioni 181.2 **sawa na 19.8%** ya fedha zote za miradi ya Maendeleo ndizo zilizotolewa. Kwa utekelezaji duni

namna hii wa bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji ni matusi kwa watanzania ambao uhaba wa maji umewafanya waishi kama wanyama. Ule usemi wa Serikali wa kumtua mama ndoo ya maji, kwa mazingira haya ni dhihaka kwa akina mama wote wa nchi hii ambao wanaendelea kusota na kukumbana na kila aina ya kadhia katika kutafuta maji. Ikumbukwe kwamba hawa ndio mtaji mkubwa wa kura waliyoipa ushindi Serikali hii na sasa imeshindwa kutimiza ahadi yake ya kuwatua akina mama ndoo za maji kwa kushindwa kutekeleza bajeti ya maendeleo iliyodhinishwa na Bunge.

#### 5. Wizara ya Viwanda:

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya shilingi **bilioni 42.1** zilizotengwa, Wizara ilipokea shilingi **bilioni 7.6 tu sawa na 18.6%**. Kwa utekelezaji huo wa bajeti, ni aibu kwa Serikali kutumia Kauli mbiu ya *'Tanzania ya Viwanda'* kama kampeni ya kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia viwanda.

#### 6. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii, ambayo ni nyeti kwa usalama wa nchi yetu, nayo ilikumbana na panga ambalo limezikumba Wizara mbalimbali. **Moja ya mradi muhimu sana ni mradi wa Defence Scheme ( mradi namba 6103) na kutekelezwa chini ya Kifungu namba 2002- Military Research na Development Fungu 57.** Mradi huu, ulitengewa jumla ya **shilingi bilioni 151.1**. Mpaka mwezi Machi, 2017 - ikiwa ni robo ya tatu ya mwaka Wizara ilikuwa imepokea shilingi **bilioni 30 tu sawa na 20% tu!** Mbali na mradi tajwa hapo juu kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama<sup>2</sup> fedha za miradi ya maendeleo ziliwasilishwa ni **14.5% tu, yaani Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 230 , pesa zilizotolewa hadi Machi 2017 ni shilingi bilioni 33.9.** Halafu tunaitangazia dunia kwamba tuna lengo la kuwa na jeshi dogo la kisasa lenye weledi- kwa bajeti ipi?

---

<sup>2</sup> Iliyowasilishwa tarehe 16/5/2017

**7. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi:**

**Mheshimiwa Spika**, Kilimo kiliidhinishiwa shilingi 101,527,497,000 (bilioni 101). Kiasi kilichotolewa ni shilingi 3,369,416,66 (bilioni. 3.369) **sawa na 3.31%**. Kwa upande wa mifugo na uvuvi, kiasi cha shilingi 15,873,215,000 (bilioni 15.8) kiasi kilichotolewa ni bilioni 1.2. **Sawa na 8%**. Kwa maneno mengine, Kilimo ambacho tunasema kwamba ndio uti wa mngongo wa uchumi wa Tanzania, bajeti yake ya maendeleo haikutekelezwa kwa takriban asilimia 97. Serikali inahubiri Uchumi wa Viwanda ikijua fika kwamba viwanda hivyo haviwezi kuendelea bila ukuaji katika sekta ya kilimo, lakini haitoi fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya Kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba; ama Serikali imefilisika ila haitaki kukiri hivyo, au kuna tatizo kubwa la afya ya akili (mental health) miongoni mwa watendaji wa Serikali. Haingii akilini kwamba ile sekta ambayo inategemewa kuleta hayo mapinduzi ya viwanda haipewi fedha za kutosha, halafu Serikali inaendelea kuhubiri viwanda – vitatoka wapi?

8. Wizara ya Maliasili na Utalii, fedha za ndani za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 2. Fedha zilizotolewa ni mil 156,688,000 sawa na **8%**

9. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni **25.30**. Fedha zilizotolewa mpaka sasa ni shilingi bilioni **7.63** tu.

**10. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii ilitengewa fedha za maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:

- Ujenzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.17 zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.07 sawa na asilimia 58.7
- Uchukuzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.49 zilizotolewa ni shilingi bilioni 761.5 sawa na asilimia 30.5

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanywa hapo juu unaonyesha wazi kwamba, ufanisi wa Serikali ya awamu ya tano katika utekelezaji bajeti ya miradi ya maendeleo na mpango wa kuwaondolea umasikini watanzania ni kwa wastani wa 0%- 20%. Wizara pekee iliyoweza kuvuka 50% ni Wizara ya Ujenzi na inafahamika kwamba yapo *'maslahi mapana'* yanayohitaji kulindwa katika Wizara hiyo. .

**Mheshimiwa Spika**, Ilani ya CCM katika vipindi mbalimbali , imekuwa ikituambia kwamba Chama hicho kupitia Dira 2025, na 2020 (SMZ), Mwelekeo wa sera za CCM katika miaka 2000 -2010-2015 kimeelekeza suluhisho la kuondokana na hali ya uchumi kuwa nyuma na tegemezi na kufanya modenaizesheni ya uchumi. Mchakato wa Modenization ya uchumi na kutoa nchi yenye uchumi tegemezi kuelekea uchumi wa kisasa utazingatia vipaumbele vifuatavyo:

- (i) Kutilia Mkazo katika matumizi ya maarifa ya kisasa (Sayansi na Teknolojia)
- (ii) Kuandaa rasilimali watu katika maarifa na mwelekeo
- (iii) Kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi
- (iv) Kufanya mapinduzi ya viwanda ambavyo ndivyo kiongozi wa uchumi wa kisasa
- (v) Mapinduzi katika nishati na miundombinu ya kisasa

**Mheshimiwa Spika**, Suala la msingi ambalo Wabunge wa pande zote mbili tunapaswa kutafakari na kujuliza, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hapo juu, hivi kweli itakapofika 2020 na 2025 malengo (i-v) yatatimia? Na kama nafsi zetu zinatambia kwamba hayatatimia, tunajipanga vipi kutumia kipindi hiki cha bajeti KUJISAHIHISHA ili mwaka ujao wa fedha TUSIJIULIZE maswali hayahaya?!

#### 4.0 OFISI YA MSAJILI WA HAZINA NA UHAI WA MASHIRIKA YA UMMA

**Mheshimiwa Spika**, Kulingana na Sheria ya Msajili wa Hazina na kifungu Na. 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1992, Msajili wa Hazina ana majukumu ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi nyinginezo za umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika. Hata hivyo, hali ya baadhi mashirika yetu sio ya kuridhisha, na kwa sababu hiyo, hatua za haraka zinahitajika ili kuweza kuyanusuuru.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetaja baadhi ya mashirika ya umma pamoja na changamoto zinazoyakabili mashirika hayo na kushauri hatua za haraka zichukuliwe ili kuyanusuuru. Miongoni mwa Mashirika hayo ni kama ifuatavyo:

i. **TANESCO:**

**Mheshimwa Spika**, TANESCO inakabiliwa na malimbikizo makubwa ya madeni yanayotokana na manunuzi ya umeme kutoka kwa **wazalishaji huru** wa nishati ( IPPs) na **wazalishaji wa dharura wa nishati** (EPPs). Hii inatokana na Tanesco kununua umeme kwa bei ya wastani wa shilingi **544.65** na kuuza shilingi **279.30** kwa kila unit hivyo kusababisha hasara ya shilingi **265.30** kwa kila unit. Kwa upande mwingine TANESCO inadai taasisi mbalimbali za Serikali fedha nyingi ambapo inashindwa kujiendesha kutokana na kutolipwa kwa fedha hizo. Mathalani TANESCO inaidai Wizara ya Nishati na Madini kodi ya pango ya **shilingi bilioni 1.12 Kwa ujumla TANESCO inaidai Serikali ( Mpaka tarehe 30 Juni 2016) shilingi bilioni 144,854 sawa na 67.4% ya deni lote la umeme**. Deni lililobaki kwa wateja binafsi ni shilingi bilioni **70 sawa na asilimia 33**

ii. **Mifuko ya Hifadhi ya NSSF, PPF, PSPF na LAPF:**

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko hii inakabiliwa na tatizo la kushuika kwa mapato ya uwekezaji kunakotokana na

kutokuwepo kwa ufanisi wa menejimenti katika kusimamia mikopo iliyotolewa. Aidha, kuna usimamizi hafifu wa kuratibu na kudhibiti madeni ya muda mrefu na kuchelewa kulipwa kwa madeni ambayo mifuko inaidai Serikali. Serikali imekuwa na tabia ya kutumia huduma au kukopa katika taasisi zake bila kufanya malipo.

**iii. Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika**, NHIF ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 44.29 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma. Mkopo ulitolewa bila mkataba wala uthibitisho wa udhamini. Matokeo yake mpaka sasa haijulikani haki na wajibu wa kila upande, utaratibu wa urejeshwaji wa mkopo halikadhalika ulipaji wa riba ya mkopo! hali hii inaisababishia mfuko kupoteza fedha za wanachama endapo mkopaji atashindwa kuwa mwaminifu (kama ambavyo viashiria vinavyojionyesha) na itakuwa ngumu kupata haki mahakamani.

**iv. Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF)**

**Mheshimiwa Spika**, mfuko huu ni mhanga wa kurushwa fedha zake na Serikali. Kutorejeshwa kwa gharama za uendeshaji za mfuko wa afya ya jamii (CHF) shilingi bilioni 1.20 kunaiweka CHF kwenye wakati mgumu kujiendesha. Fedha hizi zilitakiwa ziwe zimerejeshwa na Serikali kutokana na gharama ilizotumia kwenye miradi ya CHF kama ilivyoainishwa kwenye hati ya makubaliano. Kutokulipwa kwa madeni haya na Serikali kunaongezea mfuko mzigo mkubwa wa kifedha hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kushindwa kupanua wigo wa shughuli zake.

**v. Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

**Mheshimiwa Spika**, shirika hili nalo lina changamoto ya kutolipwa deni na Serikali. TANAPA inaidai Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki jumla ya shilingi

bilioni 2.4 ikiwa ni kodi ya pango ya ofisi za Wizara zilizopo katika jengo la TANAPA mkoani Arusha.

## **5.0 MSAJILI WA HAZINA KUTOKUWA NA UWEZO WA KUSIMAMIA MIFUKO YA HIFADHI ZA JAMII**

**Mheshimiwa Spika**, Ukirejea hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzai Bungeni ya mwaka 2012/13 na 2013/2014 tulitoa ushauri kwa Serikali kufanya mambo yafuatayo kuhusu mifuko ya hifadhi za jamii kama ifuatavyo:

Kwamba; Serikali ihamishie mifuko yote ya hifadhi ya Jamii kwenye Wizara ya Kazi na Ajira ambayo kimsingi ndiyo inayohusika na hifadhi ya jamii (Social Security). Pendekezo hili lilitokana na ukweli kwamba kwa hali ilivyo sasa mifuko hii iko katika Wizara tofauti tofauti jambo ambalo linaleta ugumu katika kuidhibiti na kuisimamia. Na ni ukweli usiopingika kwamba Mamlaka ya kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) imeshindwa kuisimamia mifuko kwa ufasaha.<sup>3</sup>

Na kwamba; Msajili wa Hazina awe na mamlaka ya kuisimamia kama anavyofanya kwenye Mashirika mengine ili kumwezesha kufuatilia ipasavyo utendaji na uwekezaji unaofanywa na mifuko hiyo. Hoja hizi mpaka sasa hazijapatiwa majibu, hali ambayo inazidi kuhatarisha uhai wa mifuko yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukosefu wa umakini katika kusimamia mifuko ya hifadhi ya jamii, yapo matukio ambayo kwa hali zote hayakuzingatia weledi jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kubwa katika mifuko hiyo. Matukio hayo ni pamoja na:

---

<sup>3</sup> Mifuko ya hifadhi ya jamii inaelekezwa na sharia zilizoanzisha mifuko hiyo kuwasilisha Taarifa za uwekezaji na utendaji kwa mamlaka ya udhibiti wa mifuko ya hifadhi ya Jamii na Benki Kuu ya Tanzania. Hii inakinzana na masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina , Sura 370 inayotaka taasisi zote za Umma kuwasilisha Taarifa zake za uwekezaji na utendaji kwa Msajili wa Hazina.

- Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1 NSSF
- Taarifa za fedha za NSSF zinaonyesha kwamba waliwekeza kwenye viwanja (Benki ya Ardhi) vyenye thamani ya shilingi bilioni 97.2 wakati kukiwa hakuna mipango na upembuzi yakinifu kuhalalisha sababu za kuwekeza katika rasilimali kinyume na aya 3.3 ya sera ya uwekezaji ya mwaka 2012 inayoitaka NSSF kuwekeza rasilimali zake katika uwekezaji unaolipa zaidi ili kuweza kuleta mafanikio kwa wanachama wake.
- Shirika pia linakopesha taasisi ambazo hazikidhi vigezo na masharti kutokana na ukweli kwamba wakopeshwaji wanapaswa kuwa wanachama wa NSSF, lakini mikopo imekuwa ikitolewa kwa watu ambao sio wanachama !
- Mradi wa Tuangoma ambapo mfuko uliingia mikataba mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 165.4 kwa ajili ya kijiji cha setilaiti katika shamba la Dungu Tuangoma Kigamboni pasipo kufanya upembuzi yakinifu...

### [MANENO YALIONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]

**Mheshimiwa Spika**, mifano hiyo hapo juu inadhirisha kwamba Wizara ya Fedha haitimizi majukumu yake ipasavyo na haiko makini katika kuisimamia mifuko ya hifadhi ya Jamii.

### 6.0 RIPOTI YA MSAJILI WA HAZINA KUHUSU UTENDAJI WA KAMPUNI YA NDEGE

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni hii ilianzishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa sheria ya Makampuni sura 212 kama kampuni ya biashara ya usafiri wa anga. Mwezi Oktoba, 2016, 'Serikali ilinunua ndege sita (mbili kati ya hizo zimeshafika na kuanza kazi). Kwa mujibu wa kitabu cha Mpango wa maendeleo 2017/18<sup>4</sup>, katika mwaka wa fedha 2017/18 zimetengwa shilingi

---

<sup>4</sup>Tume ya Mipango, Wizara ya fedha na Mipango , Machi 2017 uk.83



bilioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege 3 zilizosalia. Kwa lugha nyingine ndege zote sita zitaligharimu Taifa si pungufu ya shilingi bilioni 1000 (Trillion 1).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya ofisi ya Msajili wa Hazina kwenda kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu ya tarehe 29 Machi 2017 inabainisha mambo yafuatayo:

i) Imekuwa vigumu kwa ofisi ya msajili kufanya uchambuzi wa kina wa utendaji wa ATCL kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za kutosha za kampuni.

ii) Mahesabu ya kampuni yaliyokamilika ni ya mwaka 2014/15. Mahesabu hayo hayajatomizwa na kupitishwa na bodi, hali ambayo imemsababishia Msajili wa Hazina kutoweza kuchambua na kubainisha hali halisi ya uwekezaji ilivyo sasa hususani madeni na mali za kampuni.

iii) Imekuwa vigumu kubaini hali halisi ya utendaji na hali ya ukwasi (liquidity ratio) wa kampuni kwa kutumia viashiria vya utendaji kutokana na kampuni kutokuwa na hesabu (financial statements) kwa muda mrefu.

iv) Uongozi ulilizwe kueleza mikakati iliyonayo kuwezesha kampuni kujijendesha kwa faida na tija.

v) ATCL inatakiwa kuhakikisha inakuwa na hesabu zilizokaguliwa kila mwaka, mpango wa biashara, mpango au sera ya uwekezaji, mpango wa kurithisha utaalum. (Taarifa inaonyesha kwamba uongozi wa ATCL umeahidi kwamba ifikapo June 2017 mpango wa biashara na sera ya uwekezaji vitakuwa tayari).

vi) Kutokuwa na wataalam wa kutosha katika masuala ya usafiri wa anga hususan marubani, wahandisi, wataalam wa uongozi na uendeshaji wa biashara ya usafiri wa anga na waongoza ndege

vii) Kampuni inakabiliwa na madeni makubwa ambayo yanachangia ukuaji wa matumizi ya kampuni na hatimaye

kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zake za maendeleo!

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maelezo hayo ya ofisi ya msajili wa hazina , Kambi ya upinzani inataka Serikali ilieleze Bunge hili tukufu ni kwa nini inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyingine ikiwa kampuni yetu ya ndege ina mapungufu makubwa namna hii? Je Serikali haioni kwamba kwa kuendelea na mpango wa kununua ndege ikiwa shirika la ndege lina matatizo makubwa namna hiyo ni kupoteza fedha za walipa kodi kwa kuwa kuna dalili zote shirika hilo kuanguka kama ilivyotokea awali?

## 7.0 MAFAO YA WASTAAFU (PENSHENI)

**Mheshimiwa Spika**, Mafao ya wastaafu katika nchi hii yameendelea kuzua migogoro mbalimbali na manung'uniko katika jamii. Kuna makundi mengi yenye malalamiko, kuanzia Wanajeshi, waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wastaafu waliokuwa watumishi wa Umma ambao wamebaguliwa na Sheria ya Mafao kwa Watumishi wa Umma, ya mwaka 1999 (The Public Service Retirement Benefits Act, Cap. 371, R.E. 2002).

### 7.1 SHERIA YA MAFAO YA UTUMISHI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii, pamoja na kufuta Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954 (The Pensions Ordinance of 1954, Cap. 371 of the Laws of Tanzania), bado ilibakiza matumizi ya Sheria hiyo kwa watumishi wa umma waliokuwa wakipokea mafao yao kwa Sheria na kanuni za Sheria iliyofutwa. Hali hii inajidhihirisha kwenye kifungu cha 73 na 84 cha Sheria ya mwaka 1999.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa asilimia kubwa ya watumishi hao wanalipwa mafao yasiyoendana na hali halisi ya maisha. Wako kwenye hali ngumu ya udhalilishwaji na umaskini uliopindukia. Wengi wao hupewa shilingi elfu ishirini (Sh. 20,000/=) tu kwa mwezi! Huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za Binadamu na aibu kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafanywe mabadiliko ya Sheria zote zinazohusu mafao kwa wafanyakazi katika sekta zote za ajira nchini. Pia, kipaumbele kiwekwe kwenye marekebisho ya Sheria ya Pensheni ya mwaka 1999 na kuwafanya wale wote waliokuwa wakistahili kupewa pensheni zao kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954 wanapewa pensheni hizo kwa kuzingatia viwango vipya vinavyokidhi mahitaji ya msingi ya Binadamu na Utu, siyo viwango vya mwaka 1954.

## **7.2 DHULUMA DHIDI KWA WALIOKUWA WAFANYAKAZI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 24/02/2016 wawakilishi wa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki walimwandikia barua<sup>5</sup> Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakimtaka aingilie kati dhuluma waliofanyiwa na Serikali ya CCM kwa kutokulipwa stahiki zao kikamilifu baada ya Jumuiya kuvunjika na kila nchi kupewa mgao wake kwa malipo ya wafanyakazi wa Jumuiya wanaotoka katika nchi zao!

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka mmoja na miezi minne imepita, Wastaafu hawa hawajapata majibu, Kambi Rasmi ya Upinzani ni sauti ya wasio na sauti, ikiwa ni miaka 40 toka Jumuiya hiyo ivunjike inalileta suala hili mbele ya Bunge lako tukufu ili Serikali itoe ufafanuzi wa madai ya watanzania hawa wanaodai kwamba bado hawajaaalipwa kikamilifu stahiki zao zilizotokana na ajira zao kwa kuzingatia kumbukumbu,taratibu na Sharia za ajira zao ambazo zilihitimishwa kwa nguvu ya Mkataba wa East African Community Mediation Agreement 1984 ulioidhinishwa na kutiwa saini na Mamlaka (The Authority ) ambao ni marais wa Afrika Mashariki wakati huo. Pamoja na Mkataba huo kulitayarishwa pia Acturial Report ya 1986 iliyotoa ufafanuzi wa malipo hayo.

---

5 Ref. Ikulu/ EAC /1/01/2016

**Mheshimiwa Spika**, Viashiria vya wizi na dhuluma dhidi ya watanzania hawa vilianza mwaka 1987 pale Mkataba wa The East African Community Mediation Agreement 1984 (Ulioidhinishwa na kusainiwa na Marais wa nchi wanachama, akiwemo hayati Julius Kambarage Nyerere) ulipoletwa kwenye Bunge ili upate uthibitisho kama sheria rasmi ya nchi . Katika hali ya kushangaza Serikali ilinyofoa baadhi ya vipengele muhimu vya Mkataba mama ( Article 1,2,6,13,16,17 na 18) kabla ya kuupeleka Bungeni kwa uthibitisho. Tendo hili la Serikali lilikuwa ni kinyume kabisa na mwongozo wa Article 95 ya Mkataba wa Jumuiya ya Africa Mashariki (The Treaty for East African Co-operation) .

**Mheshimiwa Spika**, Kitendo hichi cha dhuluma kilichofanywa na Serikali ya CCM kilipunguza nguvu nna thamani ya mafao ya watanzania hawa na hususani kifungu cha 1(n) ambacho kiliweka bayana kwa kutoa maagizo na mwongozo uliotakiwa kufuatwa katika ukokotoaji na ulipaji wa mafao. Hatua hii ya Serikali kwa kiwango kikubwa imekuwa ikiathiri wazee wetu hawa kwani Mahakama zetu zimekuwa zikitoa uamuzi wake kwa kutumia Mkataba wa ndani uliochakachuliwa !

**Mheshimiwa Spika**, Swala la wazee hawa ( Watanzania zaidi ya 28,831) halitofautiani sana migogoro ya mirathi , hasa pale baba mkubwa anapoteuliwa kusimamia mirathi ya marehemi ndugu yake ambae aliacha mali na watoto wadogo. Mara nyingi ndugu hawa wa baba hugeuka wakatili , hunyanyasa na kuwadhulumu au mara nyingine kuwapunja haki mayatima hao pale wanapoanza kudai mali zao kwa kisingizio eti waliwalea na kuwasomesha! Hichi ndicho kilichowakuta wafanyakazi wa Jumuiya mbele ya baba yao Mlezi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano!

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2005 iliundwa Kamati ya muafaka baada ya Serikali kuomba suala limalizwe nje ya Mahakama. Kwa ridhaa ya Mahakama Kuu, Kamati husikwa iliundwa na watu 10 toka Serikali Kuu ikiongozwa na Bwn. Ramadhani Khija (ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Muafaka

na baadae alikuwa Katibu Mkuu Hazina. Na watu 10 wakiwakilishwa upande wa wastaafu wakiongozwa na Ndugu Alfred Kinyondo kama Mwenyekiti wa Wastaaafu. Baada ya majadiliano ya ya miezi mitatu Muafaka ulifikiwa na kupelekwa kwa Waziri wa Fedha , wakati huo Bwana Basil Mramba. Makubaliano yakiwa Serikali itawalipa jumla ya shilingi billion 450 kwa wastaafu 28,831

**Mheshimiwa Spika**, Makubaliano haya yalithibitishwa na kauli ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Benjamin Mkapa katika kilele cha sherehe za wafanyakazi za Mei Mosi tarehe 1/05/2005 Songea, alitamka rasmi kwamba Serikali yake imeridhai kulipa Tshs. 419 bilioni ikiwa ni malipo ya wastaafu wa Jumuiya hiyo na mashirika yake japo kwa awamu na alimuagiza Waziri wa Fedha wakati huo ndugu Basil Mramba kutekeleza maamuzi hayo kwa haraka ( Kiambatanisho)!

**Mheshimiwa Spika**, Katika hali ile ile ya dhuluma kama ilivyotokea katika uchakachujaji wa Mkataba kama nilivyoainisha hapo juu, Serikali hiyo hiyo iliyoingia makubaliano katika Kamati ya mwafaka, ikaandaa Deed of Settlement yenye kuonyesha kwamba kiasi cha shilingi bilioni 117 zitalipwa kwa wastaafu 31,831, kutoa shinikizo kwa wastaafu kupitia wakili wa ndugu Lukwaro wasaini. Mkataba ulisainiwa Kwa shinikizo (21/09/2005) Mahakama ikatoa hukumu siku hiyo hiyo!..Siku ya pili 22/09/2005 Serikali ikachapisha majina ya wastaafu 28,831 na kuagiza wakachukue malipo yao kuanzia tarehe hiyo hiyo 22/09/2005!!

**Mheshimiwa Spika**, Swali la kujjuliza hapa ni kwa miujiza gani Serikali iliweza kukokotoa ndani ya siku moja stahiki za watumishi wote 28,831 ambao wako kada tofauti na waliohudumu kwa muda , mishahara na vyeo tofauti ndani ya nusu siku/siku moja??

Serikali ikijua kwamba inafanya hila ilifanya siri sana katika 'kukokotoa mahesabu' bila hata kuwashirikisha wawakilishi

wa wastaafu, ni pale tu Mstaafu alipofika kuchukua hundi yake na kuona payment voucher , ndipo alipoweza tambua kuwa alicholipwa hakiendani na stahihi yake!

**Mheshimiwa Spika**, Dhuluma kama hii hatuwezi kuacha iendelee kutafuna Taifa letu kudhulumu wazee waliolitumikia Taifa na Jumuiya ni laana kubwa, laana ambayo haturuhusiwi kuiacha kama Taifa! Hivi kwa nini hatujiulizi kwa nini hawa wazee wetu kwa miaka yote wamekuwa wakisisitiza kwamba wamedhulumiwa?? Kwa nini nafsi yao hairudi nyuma licha ya vitisho mbalimbali wanavyokabiliana navyo?? Kwa nini ni wastaafu hawa tu kati ya wengi ambao hawachoki kuililia Serikali yao (baba yao Mlezi) iwape urithi halali walioachiwa na baba yao (Jumuiya) wakati anafariki??

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kupitia Waziri wa Fedha ambaye Hazina iko chini yake, ilieleze Bunge hili tukufu ni lini Serikali itafanyia kazi kwa usahihi na haki madai ya wastaafu hawa??

## 8.0 HALI YA UCHUMI WA NCHI

### 8.1 Kuendelea Kupanda kwa Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei umeendelea kupanda siku hadi siku kutokana na sera mbovu za Serikali ya CCM jambo linalopelekea wananchi wengi wenye kipato duni kuumia.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu (Monthly Economic Review) iliyotolewa mwezi Aprili, 2017 mfumuko wa bei umepanda kutoka asilimia 5.4 mwezi Machi, 2016 mpaka kufikia asilima 6.4 mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kupanda huku kwa mfumuko wa bei kumeathiri kupanda kwa bei za chakula kama vile mahindi, mihogo, mtama, mchele, ndizi, dagaa wakavu, sukari na mboga za majani. Gazeti la kila siku, **Mwananchi**, limeripoti tarehe **3 Aprili, 2017** kupitia uchunguzi uliofanywa katika masoko mbalimbali na kubaini kuwa bei za mazao

zimepanda sana. Kwa mfano bei ya maharage imepanda kutoka shilingi 1,800 kwa kilogramu 1, mpaka kufikia kati ya shilingi 2,700 mpaka 3,000.

**Mheshimiwa Spika**, mazao mengine yaliyopanda bei kwa ukubwa usiokuwa wa kawaida ni pamoja na Sukari kutoka bei elekezi ya Serikali shilingi 1,800 kwa kilogramu 1, mpaka kufikia shilingi 2,500. Mchele nao umepanda kutoka 1,200 kwa kilogramu 1 mpaka kufikia 2,600. Unga wa Sembe nao umepanda kutoka shilingi 1,200 kwa kilogramu 1 mpaka kufikia shilingi 2,000.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu juu ya hatua stahiki zinachokuliwa ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ndani ya Bunge lako tukufu kuwa ni lini itabadilisha sera zake za fedha na matumizi ya Serikali ili kudhibiti mfumuko wa bei unaofanya maisha ya wananchi wa Tanzania kuwa duni na kushindwa kumudu gharama za maisha.

## **8.2 Uwepo wa Njaa na Hifadhi Duni ya Chakula**

**Mheshimiwa Spika**, tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani njaa imeendelea kuiathiri nchi kwa kiwango cha kutisha. Serikali ya Rais Kikwete katika awamu ya nne ilipofika mwezi Machi, 2015 iliacha hifadhi ya chakula katika Ghala la Taifa jumla ya tani **452,054**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya tano, haina mpango wa kununua chakula cha hifadhi, ilipofika Mwezi Machi, 2016 miezi mitano tu baada ya Rais Magufuli kuapishwa, hifadhi ya chakula katika ghala la Taifa ikashuka kwa **asilimia 85** mpaka kufikia kiasi cha **tani 68,727**.

**Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni sera ya Serikali ya awamu ya tano kutonunua chakula cha kutosha kwa ajili ya akiba katika

ghala la Taifa. Ilipofika mwezi Machi, 2017 akiba ya chakula katika ghala la Taifa la hifadhi ya chakula ilikuwa ni **tani 86,444**

**Mheshimiwa Spika**, ripoti ya Benki Kuu (Monthly Economic Review) iliyotolewa mwezi Aprili, 2017 imeonesha kuwa Serikali ya awamu ya tano haijanunua chakula chochote wala kuuza ndani ya mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Serikali ya awamu ya tano kutonunua hifadhi ya chakula ni hatua ya kuwatia kitanzi na kufanikiwa kuwanyonga kiuchumi Watanzania zaidi ya asilimia 70 ambao kazi yao kubwa ni kulima mazao ya chakula na kuuza katika ghala la hifadhi la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali itoe majibu mbele ya Bunge lako tukufu na mbele ya Watanzania wote, kuwa ni kwanini Serikali hainunui tena chakula kwa ajili ya kuweka akiba na kuwainua wananchi wake kiuchumi kutokana na wengi wao kutegemea kilimo kama chanzo cha mapato yao.

### **8.3 Mzunguko wa fedha, Riba na Hali ya Mikopo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu (Monthly Economic Review) iliyotolewa mwezi Aprili, 2016 na Aprili, 2017 ilipofika mwezi Machi, 2016 mikopo ya Benki za Kibiashara kwa sekta binafsi ilishuhudia ukuaji wa asilimia 23.6 kwa mwaka, na ilipofika mwezi Machi, 2017 ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ukapungua kwa kasi ya ajabu mpaka kufikia asilima 3.7 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya Benki Kuu inasema kuwa upunguaji huo wa mikopo kwa sekta binafsi unapunguza ukuaji wa mzunguko wa fedha. Sehemu ya ripoti hiyo ukurasa wa 3 inasema kuwa *"This development mirrors the slowdown in the growth of money supply"*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ***kuhakikisha inaboresha sera za Benki kuu juu ya uratibu madhubuti ya mzunguko wa fedha ili kuzuia anguko la kiuchumi litakalotokana na sekta binafsi kutopata fedha***



*za mikopo zinazotarajiwa kutumiwa katika usisimujaji wa uchumi kutokana na shughuli za kiuchumi kuongezeka.*

**Mheshimiwa Spika**, Kinachoendelea hivi sasa kwa sekta binafsi kukosa mikopo ya kibiashara na mikopo binafsi kunaathiri ukuaji wa pato la mwananchi mmoja mmoja hivyo kuongeza mzigo wa ugumu wa maisha kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo kutokana na sera zisizotabirika za Serikali ya awamu ya tano, sekta ya mikopo hususani katika riba ya mikopo imeendelea kuathirika. Ripoti ya Benki kuu imendelea kusema kuwa kiwango cha riba ya mikopo (lending rate) kiliendelea kupanda kutoka asilimia 16.26 mwezi Machi, 2016 mpaka kufikia asilima 17.58 mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kiwango kikubwa cha riba kinachotozwa nchini kinarudisha nyuma juhudi za kuwakwamua Watanzania kiuchumi, hivyo basi, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya awamu ya tano, kuhakikisha inatoa majibu ya haraka iwezekanavyo juu ya hatua inazozichukua kuhakikisha kiwango cha riba za mikopo kinapungua ili kurahisisha ongezeko la wakopaji miongoni mwa Watanzania wenye nia ya kukopa na uwezo wa kurudisha unaozuiliwa na kiwango kikubwa cha riba ya mikopo.

#### **8.4 Tafrani ya Sera ya Serikali kuweka Fedha BoT**

**Mheshimiwa Spika**, haijaeleweka (uncertainties) mpaka sasa endapo Serikali ya awamu ya tano inafuata falsafa ipi katika ujenzi wa uchumi wa nchi kutokana na Sera yake ya kuzuia mashirika ya Serikali kutunza fedha katika mabanki ya kibiashara, kuondoa jumla ya bilioni 5 kutoka mabanki ya biashara na kuzitunza katika akaunti za Benki Kuu (BoT).

**Mheshimiwa Spika**, hata ongezeko la riba za mikopo katika benki za biashara linatokana na uamuzi wa Serikali ya awamu ya tano kuondoa fedha katika mabanki ya biashara jambo lililopunguza kiasi cha fedha 'liquidity' na kupelekea kupungua kwa amana katika benki hizo jambo

linalolazimisha benki za biashara kuongeza kiwango cha riba ili kujipatia unafuu wa kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, wachambuzi mbalimbali wa masuala ya uchumi, wameonya kuwa kitendo cha Serikali kukosa falsafa inayoisimamia katika ujenzi wa uchumi na kitendo cha Serikali kufanya maamuzi yasiyotabirika (uncertainties) kunatuma 'signal' kwa wawekezaji kusita kuwekeza fedha zao ndani ya uchumi wa Tanzania kutokana na hofu zinazotokana na Serikali ya awamu ya tano kuibuka na sera zisizoshirikishi kila mara.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali kuondoa fedha katika mabanki ya biashara ni hatua ya kuamua kuiangamiza sekta binafsi ambayo inauhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa pato la kila Mtanzania na pia ukuaji wa pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Benki kadhaa za kibiashara zimerekodi hasara katika hesabu zao kutokana na uamuzi huo. *Gazeti la The Citizen, tarehe 11 mwezi Agosti, 2016<sup>6</sup>* liliripoti kuwa uamuzi wa Serikali kuhamisha fedha kwenye mabanki ya biashara kumesababisha benki kadhaa kupata hasara. Benki zilizorekodi hasara ni pamoja na *Barclays Bank Tanzania (hasara ya Shilingi bilioni 8.2)*, *TBI Development Bank (hasara ya Shilingi bilioni 6.27)*, *Stanbic Bank Tanzania (hasara ya shilingi bilioni 2.40)*

**Mheshimiwa Spika**, Gazeti hilo hilo la The Citizen, tarehe 31 mwezi Oktoba, 2016<sup>7</sup> liliripoti benki kadhaa kuendelea kupata hasara iliyopelekewa na uamuzi wa Serikali kuondoa fedha katika mabanki ya biashara. Benki zilizorekodi hasara ni pamoja na *CRDB Bank (hasara ya shilingi bilioni 1.9) na Amana Bank (hasara ya milioni 195)*

---

<sup>6</sup> Banks hit by public entities' withdrawal of Sh500bn, imetolewa <http://www.thecitizen.co.tz/magazine/businessweek/1843772-3340626-57jbnmz/index.html>

---

<sup>7</sup> Tanzania's largest bank posts Sh2bn quarterly loss, imetolewa: <http://www.thecitizen.co.tz/News/Tanzania-s-largest-bank-posts-Sh2bn-quarterly-loss/1840340-3435694-2cwx6vz/index.html>

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ikubaliane na hoja ya kuamua kuwa na falsafa moja ya ujenzi wa uchumi na kuacha kutoeleweka kuwa inasimamia mfumo upi wa uchumi. Falsafa hii itajenga misingi itakayozuia viongozi wa kisiasa wasio na ujuzi wala weledi na taaluma ya uchumi kuacha kuibuka na matamko yanayopelekea anguko la uchumi wan chi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kukubaliana na ukweli kuwa kuzipeleka fedha za mashirika ya Serikali kutunza katika akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu sio suluhisho la kuzuia matumizi mabaya ya fedha wala sio njia ya kuzuia wizi na ubadhirifu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Ramsi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya awamu ya tano kuelewa kuwa njia salama ya Serikali kuzuia wizi wa fedha za umma sio kuzificha fedha katika akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu; ***kwa kuwa kwa vyovyote vile lazima zitatolewa ili zitatumike kugharamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya umma***, njia sahihi ya kuzuia wizi ni ***kuimarisha usimamizi wa fedha (finance management) ndani ya mashirika ya umma na Serikali, kuimarisha sera za matumizi ya fedha kwenye miradi ya kimkakati na kuziba mianya ya rushwa katika mifumo rasmi ya matumizi ya fedha za umma.***

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuanza kuzitunza fedha za umma kwenye akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu, sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezea Bunge lako tukufu kuwa ni hatua zipi inazozichukua ili kuhakikisha mifumo ya matumizi ya fedha za umma katika mashirika ya umma na Serikali kuu inaimarishwa ili kuziba mianya ya rushwa kubwa kubwa za kimfumo zinazowanufaisha 'PEP' (Political Exposed Personalities) kama vile Wakurugenzi, Makatibu wakuu, na Mawaziri.

**Mheshimiwa Spika**, Mtindo unaotumiwa na Serikali ya awamu ya tano kutuza fedha za umma Benki Kuu badala ya kuziweka kwenye benki za biashara ili zisisimue uchumi wa

nchi na kuimarisha sekta binafsi na kukuza biashara nchini ni njia za kizamani (**traditional methods**), zimepitwa na wakati na hazina tofauti na baba wa nyumba anayeficha fedha kwenye kibubu chini ya uvungu wa kitanda wakati angeweza kwenda kuzihifadhi katika amana za benki ili ziingizwe katika mfumo rasmi wa mzunguko wa fedha.

## 9.0 TUME YA PAMOJA YA FEDHA (FUNGU 10)

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 133 inatambua uwepo wa Tume ya Pamoja ya Fedha na Ibara ya 134 inaelezea majukumu ya Tume kuwa ni yafuatayo:

- a) Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo ya Serikali hizo;
- b) Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;
- c) Kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza, na kwa mujibu wa sheria iliyoitungwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 18(3) cha Sheria ya Tume (The Joint Finance Commission Act) ya mwaka 1996, Sura ya 140, Tume itawasilisha mapendekezo yake au ushauri unaohusiana na kazi yake Serikalini kupitia kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia Kifungu cha 18 cha Sheria, Tume imekuwa inawasilisha mapendekezo yake Serikalini kupitia Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania, ambaye humpatia mapendekezo hayo Waziri mwenye dhamana ya Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baada ya hapo kila upande hupeleka mapendekezo hayo kwenye Baraza la Mawaziri kwa kupitia utaratibu wa kawaida wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na kilio kikubwa toka upande wa pili wa muungano kuhusu Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa faida ya Benki Kuu,

### **9.1. KANUNI (FORMULA) YA KUCHANGIA GHARAMA ZA MUUNGANO**

**Mheshimiwa Spika**, Kumbukumbu zinaonyesha kuwepo kwa makubaliano kati ya Mawaziri wa Fedha na SMT na SMZ ikionyesha kima cha mchango wa Zanzibar kuwa ni wastani wa shilingi milioni 12 kwa mwaka kuanzia mwaka wa 1964/65 mpaka machi, 1977. Kiwango hiki kilikatwa kutokana na pato la Ushuru wa Forodha na kodi ya Mapato iliyokuwa inakusanywa na SMT kutoka upande wa Zanzibar. Kufuatia agizo la Halmashauri Kuu ya CCM kuwa mapato ya kila upande yaingie kwenye Hazina ya SMT kwa Tanzania Bara na Hazina ya SMZ kwa Tanzania Zanzibar, yalifikwiwa makubaliano kwamba kila upande uchangie gharama za mambo ya Muungano kwa msingi (fomula) wa uwiano wa idadi ya watu na pato la Taifa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kadhaa kuhusu uchangiaji wa gharama zikiwemo zifuatazo;

1) **Mheshimiwa Spika**, SMZ inatoa hoja kwamba “formula” hiyo inaelekea kuchangisha kila Mtanzania wa Tanzania Zanzibar kiasi kikubwa zaidi ya kiwango anachochangishwa kila Mtanzania wa Tanzania Bara.

2) SMZ inatoa hoja kuwa baadhi ya shughuli ambazo zimehusishwa katika mambo ya kuchangia kimuungano siyo mambo ya Muungano na hivyo kutaka yafanyiwe mchanganuo na ufafanuzi zaidi ili kufikia maelewano. Maeneo hayo ni pamoja na yanayohusisha gharama ya;

(i) Michango kwa mikataba ya kimataifa (External Contributions) ambayo imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano kama vile ILO, GATT, PTA, SADC, WHO, UNEP, UNIDO, UNDP, CCC na IBRD.

(ii) Pensheni za Viongozi wa kisiasa.

- (iii) Pensheni za marupurupu ya viongozi wa Kitaifa.
- (iv) Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano hususani Usalama wa Taifa.
- (v) Mahakama ya Rufani na sikukuu za kitaifa.
- (vi) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya SMT; na
- (vii) Mambo mengine ya kimuungano ambayo hayakuorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

3) SMZ kutokuwa na mapato ya kutosheleza mahitaji ya bajeti yake.

4) SMZ inatoa hoja kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ni lazima mchango wa SMZ utolewe baada ya SMZ kukubali ushauri na mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha iliyoundwa na Katiba ya Muungano Ibara ya 133. Hadi sasa wajumbe wa Tume hiyo hawajateuliwa na Sheria ya kuiwezesha kutekeleza kazi zake haijatangwa.

## **9.2. MAPENDEKEZO KWA MUJIBU WA UTAFITI WA TUME YA MAREKEBISHO YA KATIBA**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa Masuala ya Fedha yanayohusu Mambo ya Muungano masuala mbalimbali yamejitokeza ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi;

*(i) Ugumu wa kubaini mapato na matumizi ya Muungano yasiyotokana na kodi*

*(ii) Kutoanzishwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja*

Kutokuanzishwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja<sup>1</sup>, kunasababisha kutokuwekwa pamoja mapato ya Muungano kwenye Akaunti hiyo ambayo ni mchango wa Serikali mbili (SMT na SMZ) kwa ajili ya kugharamia Mambo ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mrejesho ni kwanini hadi sasa akaunti ya pamoja ya fedha kati ya Serikali hizi mbili haijafunguliwa na ni hatua gani hadi sasa zinatumiwa kubaini matumizi halali ya Muungano na matumizi ambayo siyo ya muungano?

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017 tume ya pamoja ya fedha ilitengewa bil 1.374 lakini hadi feb 2017 Tume ilikuwa imepatiwa mil 686 sawa na 50%. Mhe Spika mwenendo wa upelekaji wa fedha kidogo imegeuka kuwa tabia ya serikali kwenye kila fungu. Kwa mwenendo huu hali ya nchi ni itaendelea kudumaa kila kukicha. Pamoja na umuhimu wa tume kusimamia masuala ya fedha za muungano lakini bado serikali haioni umuhimu wa kitengo hichi mana sera tuliyojiwekea ya mgawanyo bado ni kitendawili kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, kama taifa tunapaswa kuheshimu makubaliano yetu ili tuweze kuulinda muungano wetu kwa vitendo. Maana kwa mwenendo wa sasa wa magawanyo serikali ya mapinduzi Zanzibar inapaswa kupokea 21% na serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania 79%, hii ni kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri anayesimamia masuala ya Muungano aliyotoa Bungeni tarehe 24/04/2017. Pamoja na umuhimu wa makubaliano bado serikali haiyafuati kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali ilieleze bunge lako tukufu ni kwa nini mgawanyo wa fedha wenye lengo la kudumisha muungano na kusaidia usawa wa kimaendeleo haufuatwi? Na kwa nini fedha zinazotengwa kwa ajili ya Tume hii haziendi kama zilizotengwa?

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 Tume inaliomba Bunge kuwapatia shilingi bilioni 1.286 kiwango hiki kikiwa pungufu kwa asilimia 6 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/17. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu kupungua huku kwa bajeti hasa ni kutokana na nini?

## 10.0 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya kisheria ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi ya Umma, Na. 11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, Icha ya Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuanzishwa na Katiba ya Nchi, na majukumu yake kuainishwa na Katiba pamoja na sheria ya ukaguzi ya Umma, Ofisi hii imekuwa haitendewi haki kibajeti. Katika mwaka wa fedha 2016/17 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi ya CAG jumla ya shilingi bilioni 44.7 zilitengwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13.8 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 18.5 fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 12.2 ni fedha za maendeleo. Hata hivyo fedha zilizopokelewa kutoka hazina hadi mwezi februari 2017, ni shilingi bilioni 31.699 sawa na asilimia 54.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Serikali kushindwa kupeleka fedha kama inavyotakiwa kwa ofisi hii ya Mkaguzi, kumepelekea ofisi hii kukumbana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kushindwa kufanya ukaguzi katika maeneo yafuatayo;

- a. Sekretariat ya SADC
- b. Vyama vya siasa
- c. Ofisi za Mahakama katika mikoa 21(Mahakama za mwanzo, mahakama za wilaya na mahakama kuu)
- d. Kaguzi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika halmashauri 105
- e. Wakala za Serikali (GPSA, TIA, TIRA,SELF na PPAA)



f. Ukaguzi wa mafuta yanayo safirishwa kwenda nchi jirani Pia ofisi hiyo imeshindwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa vyombo vya kusimamia fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina fahamu kwamba Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ndiyo imeokoa fedha nyingi za Serikali kutokana na matumizi au ubadhirifu unaofanywa na watendaji wasio waaminifu. Hivyo basi, kitendo cha kutokuipatia fedha kiukamilifu maana yake ni kutoa mwanya kwa matumizi mabaya ya fedha za serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inadhani kutokuipatia fedha ofisi hii ni kitendo cha makusudi kutokana na ukweli kwamba matumizi mengi ya serikali ya awamu ya tano hayafuati taratibu za kiuhasibu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kulieleza Bunge hili kwa nini haikutoa fedha za kutosha kwa CAG na pia ilileze Bunge nini madhara ya kufanya ukaguzi katika taasisi zilizotajwa.

## 11. MPANGO WA MATOKEO MAKUBWA SASA (BRN)

**Mheshimiwa Spika**, kulikuwa na utaratibu wa mpango wa matokeo makubwa sasa, mpango huu ulitoka nchini Malaysia ambapo Serikali ya awamu ya Nne ilikwenda huko na kuja nao hapa kwetu, na kitendo hicho kikawa chini ya kitengo cha *“Presidential Delivery Bureau*. Tatizo kuwa ni kwamba “copy and paste” haikuangalia ni mazingira gani wenzetu wa Malaysia wanaifanyia kazi hiyo BRN kwenye sekta mbalimbali, Mfano kwenye sekta ya elimu Malyasia ilikuwa na mkakati kama nchi kusomesha wanafunzi 10,000 nje ya nchi kila mwaka. Tanzania ilichotoka nacho ni kuongeza ufaulu wa sekondari kwa kushusha alama za ufaulu, maana yake ni kuongeza watu wasiokuwa na uwezo wa kushindana katika soko la ajira.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba kitengo hicho ambacho kilikuwa chini ya ofisi ya Rais hakikufanya kazi yake vyema na hivyo Serikali ya awamu ya tano ikaamua kukivunja. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta

Bungeni utendaji wa miradi yote iliyokuwa inatekelezwa chini na BRN.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuanzishwa kwa BRN ulikuwa ni maanuzi ya baraza la Mawaziri kama ilivyokuwa uamuzi wa kuuzwa kwa nyumba za Serikali umamuzi ambao hadi leo umelitia hasara kubwa Taifa letu na kuleta kashfa mbaya kwa viongozi wetu wakuu wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Mpango wa Matokeo makubwa sasa ulitumia fedha nyingi za walipa kodi, Na kwa kuwa Mpango huo umeshindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa; Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta mchanganuo wa matumizi ya fedha zilizotumika kutekeleza mpango huo ambao umeshindwa na kulieleza Bunge hili namna itakavyotekeleza yale malengo ya mpango huo.

## 10.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumnukuu mtaalam wa masuala ya fedha Bw. Adam Smith aliyesema: *“ A man whose whole life is spent in performing a few simple operations, of which the effects are perhaps always the same, or very nearly the same, has no occasion to exert his understanding or to exercise his invention in finding out expedients for removing difficulties which never occur. He naturally loses, therefore, the habit of such exertion, and generally becomes as stupid and ignorant as it is possible for a human creature to become.”*

Kwa tafsiri isiyo rasmi alisema kuwa *“Mtu ambaye maisha yake yote yanatumika kufanya mambo machache marahisi ambayo labda kila mara huwa yale yale, anakosa muda wa kuongeza ufahamu wake au kutumia ubunifu wake kutafuta njia za mafanikio ambayo katu hayawezi kutokea.*

***Mtu huyo mara zote hushindwa, na hivyo juhdi zake zote hugeuka kuwa ujinga na upumbavu kama ambavyo ni rahisi kwa mwanadamu kuwa hivyo”***

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itimize wajibu wake ipasavyo katika kusimamia masuala ya fedha, ili isije ikaingia katika kundi hili analozungumzia Adam Smith.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

David Ernest Silinde (Mb)

**K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
KATIKAWIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

30 Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza taarifa hizo sasa moja kwa moja tunaingia kwenye mjadala wa ujumla na tutaanza na Mheshimiwa Godbless Lema na baadaye atafuatia Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa niipongeze kwa nguvu zote hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ni hotuba muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikipigia kelele sana habari ya viwanda lakini katika bajeti inayoishia kati ya shilingi bilioni 42.1, Serikali ilipeleka shilingi bilioni 7.6 asilimia 18 tu. Ndiyo maana Mheshimiwa Mwijage anavyosema cherehani nne ni viwanda halafu watu wakamshangaa mimi nawashangaa wanaomshangaa, ni ukweli viwanda vya Serikali ya awamu hii ni cherehani nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo agenda kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano, viwanda, viwanda, viwanda, kati ya shilingi bilioni 42 mnapeleka bilioni saba, asilimia 18. Hamtaweza ku-*transform* nchi hii ili iende katika kuwa Taifa la viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji, maji ni biashara, najiuliza kwa nini nchi hii haijawahi kuona maji ni biashara, tena maji ni biashara ambayo haihitaji matangazo, maji ni biashara ambapo kila mtu anahitaji maji. Mahitaji namba moja ya binadamu anayeishi ni maji. Maana yake mmeshindwa ku-*connect pipe*, mmeshindwa ku-*connect* vyanzo na kuweka mita Serikali ikusanye fedha kutoka kwenye maji. Kama mmeshindwa kuona maji ni biashara cherehani nne lazima iwe ni viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maji shilingi bilioni 33 ambayo walikuwa wapeleke wamepeleka shilingi bilioni 2.9 asilimia 8.4. Ukienda kwenye kilimo na mifugo ambayo ni uti wa mgongo unaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Taifa hili fedha iliyokuwa inapaswa kupelekwa ni shilingi bilioni 101, wamepeleka shilingi bilioni 3.3 sawasawa na asilimia 3.31. Waheshimwa sio rahisi kukiri kwamba mmechoka, sio rahisi kabisa, lakini Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kazi yenu siyo kuitetea Serikali ni kuisaidia Serikali ifikie malengo muhimu ya Taifa letu. Leo kama kwenye kilimo kati ya shilingi bilioni 100 wanapeleka shilingi bilioni 3 hiyo *transformation* ya *agriculture* itatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazingira kwanza wamepanga hela ndogo kabisa, wamepanga shilingi bilioni 10.9. Leo ukiongelea tishio lingine la ulimwengu katika vizazi vinavyokuja ni mazingira. Mazingira ambayo yalipaswa kutengewa fedha nyingi kama ambavyo Jeshi la Ulinzi linatengewa. Leo Mheshimiwa January wamempa shilingi bilioni 10 halafu wakampeleka shilingi bilioni 1.2 sawa na asilimia 11.3, maana yake wao ambao wanasema wanajenga amani na imani ya kizazi kinachokuja kama hawawezi kuona mazingira ni jambo muhimu, kama

hawawezi kuona mazingira ndiyo yata-*sustain future* za watoto wenu maana yake ni kwamba hawajui wanachokifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ni *very seriously* na Mheshimiwa Dkt. Mpango haya mambo lazima ayaelewe. Leo wanatoa makandarasi wa barabara, mimi niliongea na Mheshimiwa January nikamwambia habari ya mazingira ni habari *sensitive* na kwenye hotuba yangu ya Wizara ya Mambo ya Ndani niliweka, nikasema tishio lingine la amani ya Taifa hili ni uharibifu wa mazingira kwa sababu yatakuja kusababisha njaa kali sana tunakoenda na Bob Marley alisema mtu mwenye njaa ni mtu mwenye hasira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zinajengwa, makandarasi wanaojenga barabara kuanzia sasa wapewe na *contract* ya kupanda miti. Wakati wanaendelea kujenga urefu wa barabara wapande miti na maji wanayojengea barabara hayo maji wajinyweshee miti. Mti ukiumwagia kwa mwaka mmoja huo mti hauhitaji tena kumwagiwa utakuwa umeota wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nirudi kwenye mambo ya msingi. Mheshimiwa Dkt. Mpango, kauli zao wanazoongea katika jamii zimefanya wafanyabiashara wamerudi nyuma. Leo hawatangazi tena mapato ya *TRA* kwa sababu wanajua nini kinaendelea. Ikiendelea hivi mwezi unaokuja Taifa hili litashindwa kulipa mishahara. Lugha za viongozi wa juu ni tishio kwa usalama wa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yetu imesema, leo wafanyabiashara hawana amani. Mheshimiwa Mpango amshauri Mheshimiwa Rais na hao watu wa TAKUKURU hii biashara wanapita Mbezi wanaona nyumba nzuri, wanachukua *plot* namba, wanakwenda kuanza kutishia watu, watu watahamisha pesa. Wakati Rais anasema fedha imehamishwa ilikuwa haijahamishwa lakini sasa ninavyokwambia watu wanahamisha fedha katika Taifa hili kwa sababu mazingira ya *investment* yamekuwa ni magumu,

vitisho vimekuwa ni vingi, Wakuu wa Mikoa na ma-DC wanajiita ni Marais wa Mikoa, ni Marais wa Wilaya. Kila wakienda kutishia wafanyabiashara wanasema kuna maelekezo kutoka juu. Wafanyabishara wamevunjika moyo, wafanyabiashara wanaogopa kufanya *investment* kwa sababu ya kauli za viongozi, kauli za viongozi zinaua *morale* na Mheshimwa Mpango anafahamu uchumi ni *confidence*, kama huna *confidence* na Taifa, huna *confidence* na maisha yako mambo yatakuwa ni mabaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda magereza watu wote wenye fedha kwenye akaunti mbalimbali wanahojiwa na Polisi na TAKUKURU, wanatishiwa kupewa *money laundering*. Mfumo wenu ambapo nyie mlikuwa watawala uliruhusu hata mtu kununua *round about*. Nchi hii miaka iliyopita na hata sasa hata ungetaka kununua *round about*, hata ungetaka uziwe Ikulu miaka iliyopita ungeuziwa. Ni Serikali hii ilishawahi kutaka kuuza Mahakama ya Rufaa iwe *parking* ya Kempinski. Kwa uchumi ulivyoyumba ...

## T A A R I F A

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mbunge anayezungumza kuwa Mwenyekiti wa Chama chake Mheshimiwa Freeman Mbowe alitaka kuitapeli *Bilicanas* na alitumia pesa nyingi sana lakini ikashindikana. Hiyo inamthibitishia kuwa Serikali yetu hainunuliwi ingekuwa kama kununuliwa angeuziwa *Bilicanas* ile. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema unapokea taarifa hiyo.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie dakika zangu, tuendelee na mambo ya msingi, nilisema toka mwanzo mnamjua huyu kijana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema siku za nyuma wote mnakubaliana na ndiyo sababu mnauona huu ukali wa Rais kwamba mfumo haukuwa rasmi sana kuzuia baadhi ya mambo. Hawa watu muwa-*engage* kwenye uchumi, msiwa-*disengage*. Kama mnafikiri kuna hela chafu zilitoka ndani ya mfumo wa nchi hii, ni muhimu mkafanya *engagement* na siyo *disengagement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Putin wakati anaingia madarakani alikuta hali kama hii Russia, lakini wale wote ambao walikuwa wamepata hela katika mfumo usiokuwa rasmi hela ambazo zilikuwa kodi, wakiwaza kuwatisha, wakawapa kesi mbalimbali kama *money laundering*, watahamisha fedha katika njia isiyokuwa stahili na wataogopa kufanya *investment* katika Taifa hili, watapoteza fedha nyingi sana kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Mpango hali inavyoendelea sasa, hali ni mbaya kupita kiasi. Namna pekee ya kusaidia uchumi wa Taifa hili namba moja ni lazima wafanyabiashara warudi kwenye *confidence* waliyokuwa nayo. Leo watu hawalipwi fedha, biashara za ndani hazilipwi fedha. Hapo Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu amekuwa ndiyo *Governor*, tunajua! Haya mambo tunaambiwa kutoka huko huko kwenye *corridor* zenu, Katibu Mkuu ndiyo kila kitu. Fedha hazilipwi, mambo hayaendi na kama fedha hazilipwi, Mheshimiwa Mpango yeye ni mtaalam wa uchumi, ili uchumi uweze kupanda lazima watu wa-*spend* kama watu hawawezi ku-*spend* watapata wapi kodi? Leo nenda hata kwenye mahoteli hapa Dodoma, pamoja na kwamba Wizara nyingi zimehamishia makazi hapa watu hawana uwezo wa kufanya *purchasing*, watu hawawezi kununua, hoteli zinafungwa, biashara zinafungwa, watu wanahama kwa sababu wamekosa *confidence* ya kufanya *investment*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mheshimiwa Mpango namwomba sana aelewe *confidence* ni muhimu katika *investment* katika Taifa. Leo *TRA* wamekuwa kama polisi, ukimuona mtu wa *TRA* ni hatari. Leo *TRA* wanakwenda kukusanya kodi wakiwa na Usalama wa Taifa na TAKUKURU. Nawahakikishia, hawatajenga uchumi kwa ukali wanaou-*pose* katika *society*. Watajenga uchumi kwa wanasiasa ambaye ni pamoja na Rais, kujenga mahusiano mazuri na kuwapa *confidence* wafanyabiashara. Bakhresa alikuwa anaondoka nchi hii, wakaenda wakampa eneo la bure ili abaki, wanaoondoka ni wengi. *Shares* za *DSE* Mheshimiwa Mpango zinaporomoka mpaka kwa asilimia 90, Serikali imekaa kimya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri afanye bidii ya namna yoyote ile arudishe *confidence* ya wafanyabiashara. Wakati tunawaambia bandarini meli haziji walisema bora zisije, wakaambiwa na *TATO*A kwamba *truck* zimepungua kwa asilimia 80, wakasema bora zipungua...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, naomba umalizie sentensi yako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, naomba dakika mbili za yule kijana aliyekuwa amenipotezea kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa hotuba ya Mheshimiwa Mpango mwenyewe, matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016. Kati ya shilingi bilioni 791 zilizoidhinishwa kutumika katika Mafungu yote tisa jumla ya shilingi bilioni 323 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 68 ni fedha za nje. Hadi kufikia Machi, jumla ya shilingi bilioni 18 zimetumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni moja ni fedha za ndani, shilingi bilioni 17 ndiyo fedha za nje. Sasa hizi fedha za nje bado hata hao Wazungu wanaendelea kuwazingua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu ambacho ningependa nisisitize kwenye mchango wangu *confidence*



ya wafanyabiashara imepotea, vitisho kwa wafanyabiashara zimekuwa nyingi, wataharibu na kuua uchumi kwa sababu ya sifa na kiki ambazo hazina msingi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lema. Tunaendelea na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Waziri lakini nianze kwa ku-*quote* maneno aliyoyasema *Deputy Managing Director* wa *IMF* Dar es Salaam kuhusu kodi. Pamoja na kutusifia lakini alisema maneno yafuatayo:

*“It is crucial to mobilize more private public resource within Tanzania especially by strengthening tax collection and fair and predictable tax regime. Ametumia maneno, strong, fair and predictable tax regime. Anasema, this is an area where Tanzania has fallen behind its neighbours. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema la kodi kwa sababu biashara, Waziri wa Fedha naomba hili likae kichwani, wafanyabiashara wote Tanzania ni *partner* wake, wafanyabiashara wa nchi hii ni *partner* wa nchi hii na nitasema kwa nini ni *partner*. Wafanyabiashara wa nchi hii wanatupa asilimia 30 ya *corporate tax* kila mwaka, kwa hiyo, maana yake na sisi tunazo sababu za kufanya biashara iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ikienda vizuri, Serikali inapata asilimia 30, Serikali itapata *Pay As You Earn*, itapata kwenye *insurance*, itapata kwenye *pension funds*. Kwa hiyo, tunalo jukumu kama Serikali na niwaombe sana watu wa Wizara ya Fedha, tufanye kazi ya kukuza biashara Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda leo Kariakoo, yuko mfanyabiashara mmoja ni mdogo sana, natoa mfano, mwaka 2005 alikuwa anaingiza makontena manne kila mwezi analipa shilingi milioni 72, leo hii mambo yamekuwa magumu anaingiza kontena moja kila baada ya miezi miwili,

aliyepoteza ni nani? Ni sisi Serikali. Hii nasema lazima niwaombe sana tujitahidi tuwalee wafanyabiashara. Kudhani wafanyabiashara ni wezi, wanatuibia siyo sahihi sana, naombeni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili wameanzisha *task force*, *task force* inakwenda kwa wafanyabiashara imerudi mpaka 2009. Wanajua maana yake ni nini? Kwa sababu walikwepa kodi kule zamani wakiwaambia leo wailipe, yes watalipa lakini hao wanakufa kibiashara. Kwa hiyo, mwezi unaofuata hawataweza kulipa kodi. Ama kitakachotokea ile *task force*, wanakwenda wanakaa mezani, ni rushwa! Mtu atakuja anadaiwa shilingi bilioni tano hajalipa miaka sita, anaambiwa sasa sikiliza, lipa shilingi bilioni moja, tupe shilingi bilioni moja, shilingi bilioni tatu tunakusamehe, ndiyo kinachoendelea huko mtaani. Niwaombe sana watu wa Wizara ya Fedha, tuamue sasa, tusiende nyuma, tuanzie sasa kwenda mbele kuhakikisha kila mtu analipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Sheria ya VAT. Sheria yetu ya VAT haitambui vivutio tunavyowapa wawekezaji, kwa maana ya *capital goods* na *deemed capital goods*. Nimwombe Waziri, tutoze kodi kwenye bidhaa siyo kwenye *production*. Tukianza kudhani unataka kuwekeza leo unataka uanze kupata, hakuna atakayewekeza. Mimi nasema jamani haya yanayofanyika, duniani wenzetu wanafanya, ukimuachia mtu azalishe, Dangote alienda pale Ethiopia akaambiwa tunakupa umeme rahisi, vivutio, baada ya kuanza kuzalisha bei ya *cement* ikashuka *by 60%* maana yake watu wengi wakajenga, utapata kodi kule mbele. Kwa hiyo, niwaombe wenzetu wa Wizara ya Fedha tuyasimamie haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba tu-*harmonise NIC* pamoja na Sheria ya Fedha. Kama inatokea *NIC* inatoa vivutio *under TIC*, Sheria ya Fedha inakuja hapa haivikubali ni *contradiction*, hatueleweki. Ndiyo maana tumeambiwa *our tax regime is unpredictable*, wenzetu ndivyo wanavyotuona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *TIB*, Waziri wa Fedha, naomba leo atuambie anaihitaji *TIB* ama haihitaji? Kutoweka fedha *TIB* mimi sielewi maana yake ni nini. Duniani kote wanaweka hela kwenye Benki zao za Maendeleo ili zisaidie katika maendeleo hasa ya viwanda na kila kitu. Sisi tunasema tuna maendeleo ya viwanda, tunataka kwenda kwenye viwanda lakini hakuna hela *TIB*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninacho kitabu cha maendeleo cha mwaka mmoja, *TIB* imetajwa *by the way*. Hakuna *anywhere* imetajwa *TIB* inawekwa pesa. Tuliambiwa watapewa shilingi trilioni moja, najua mwaka huu wamepanga kuwapa shilingi bilioni 94, watafanya nini kwenye maendeleo? Jamani ukienda China, Brazil, wapi wana *embrace Development Banks* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana watu wa Wizara ya Fedha, waweke *commitment* hapa. Leo *TIB* ukimpa shilingi trilioni moja anazi-*leverage* atapata hata zaidi ya bilioni nyingi tu, anakwenda kwenye masoko nje, analeta *through DIF*, anachangia kwenye maendeleo yetu. Mimi sijui kuna nini pale Wizara ya Fedha, hawataki kuisaidia *TIB*. Watuambie, kama hawaitaki tuifunge lakini kila siku ukisoma kwenye vitabu humu inashangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *investment model* yetu. Waziri wa Fedha, lazima tuchanganye *tax, debt* na *investment*. Kwa nini nasema *investment*, ili sasa uweze kuleta *PPP*. Ukisoma kwenye kitabu *PPP* haisemwi, ukisoma kwenye hii ya maendeleo, hakuna *PPP* tunaisema *by the way*. Hivi mbona wenzetu wote, China, Malaysia na kadhalika wana *embrace PPP, what is wrong with us?* Hatuwezi kujenga nchi hii kwa kodi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu barabara, umeme, wanajenga kwa hela za watu, unaweka *legal framework* yenye *clarity*. Hata *agriculture*, mimi nawasikia wenzangu wanasema tuweke hela kwenye *agriculture*, tusipo-*embrace* kwenye *commercial farming* hatutaendelea. *Commercial*

*farming ni more capital*, itaajiri watu wengi na italeta hela kwenye *products* za kwenye viwanda lakini wakubwa hawasemi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa, wanasema linahimilika, linahimilika *yes*, kwa sababu wanachukua *debt sustainability ratio*, *fine*. Mimi naomba, umefika wakati tuliangalie deni la Taifa na *revenue base yetu* ndiyo watajua kwamba deni letu halihimiliki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *transit trade*, *VAT*. Jamani tumesema mwaka jana, *auxiliary VAT* kwenye *transport* inaua hii *industry*. Waziri hapa anasema uchumi umekua kwa asilimia saba na moja ya mchango ni kwenye *transport*, Waziri wa Fedha, *transport* imeshuka. Aende akaulize wenye malori, malori yaliyokuwa yanakwenda nje yalikuwa 23,000 leo yamebaki malori 11,000.

Yakibaki malori 11,000 maana yake ni nini? Mafuta hawanywi, madereva hawana kazi, tairi hakuna, magari 12,000 yako nyumbani, mabenki hayalipwi kwasababu tumeua hii *industry*. *This is our dear country*, naombeni tufanye wanavyofanya wengine. Nimesikia *auxiliary VAT* hawataki kuitoa, hawataki kuitoa kwa sababu gani? Wanapata nini kwa kuiweka? Ni kama vile ambavyo tunasema suala la kuwakusanyia Congo kodi tuache, haitusaidii ni *disincentive* kwenye *economy* yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni deni la ndani, Waziri naomba tulipe deni la ndani. Leo hali iliyoko nchini ni kwa sababu hatulipi deni la ndani. Naombeni sana tuhangaika na kulipa deni la ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *Federal Reserve* zimepanda *interest rate*. Mimi niliisema mwaka jana, naomba leo niiseme, najua watu wa Wizara ya Fedha hili hawataki hata kulisikia. Leo hii *Federal Reserve* imepanda *to 0.75* maana yake ni nini? Kwa sababu mikopo yetu yote ni *faulting libel* maana yake inakwenda kupanda, maana yake Waziri wa Fedha utakapoanza kulipa deni la Taifa kesho siyo

hela uliyolipa mwaka huu, *revenue* inashuka, deni la Taifa linapanda kwa sababu ya *interest rates, what do we do?* Wenzetu wana-*swap, let us fix this interest.* Jamani wote wanafanya, Kenya wamefanya, Uganda wamefanya, wamezi-*fix interest rates* kwa sababu *vitality* kwenye *economy* ya Marekani ni kubwa, inatu-*affect* sisi ambao tumekopa kwa dola lakini wenzetu hawataki kusema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifuko, nasikia mnataka kuunganisha mifuko ya *pension fund*, jambo jema lakini niwaombe Waziri wa Fedha, kabla hawajaiunganisha tulipe madeni yao yote. Maana hii itakuwa ni kukwepa majukumu yetu. Mifuko inaidai Serikali, hakikisheni mifuko yote inalipwa, tufanye hesabu za mwisho ndiyo tuamue kuiunganisha. Kwa kufanya hivyo, tutafanya vizuri sana kama nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kusema suala la mwisho na narudia kwa kweli ni suala la biashara. Nawaombeni sana wakubwa, tu-*embrace* biashara Tanzania. Ukienda leo Kariakoo jamani siyo Kariakoo ya miaka mitatu iliyopita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaambieni kwa mtu aliyesoma *tax, somebody* akiwa analeta makontena 100, akakwepa makontena 50 akalipa kodi ya makontena 50 anaingiza kwenye *market*, uwe na hakika atakapoenda mwezi ujao ataleta makontena 150. Kwa hiyo, anapokuja anakukuta umejiandaa unampiga kodi makontena 120 maana yake wewe *base* yako ya kodi imepanda. Akileta 100 ukasema lazima ulipe yote, *fine, it is a good idea* lakini mwezi unaokwenda ataleta makontena 70, aliye-*loose* ni wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutengeneza utaratibu wafanyabiashara wakue na sisi tukue. Ukidhani unaweza ukafunga milango kwamba hapa hakitoki kitu ni jambo jema lakini mwisho wa siku *we will be a loser as a country.* Kwa sababu ukiangalia *trend* ya kodi imekuwa

inapanda, kama inanza kushuka lazima tujulize haraka sana, tatizo kwa vyovyote vile ni suala tunavyo-*handle business as a country*. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, naomba umalize sentensi yako.

**MHE PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la miradi ya maendeleo. Katika bajeti ya mwaka jana, hii ambayo sasa tunamalizia mwaka wa Serikali tarehe 30 mwezi Juni, Serikali imetuahidi kwamba asilimia 40 ya bajeti yake itakwenda kwenye maendeleo. Mpaka leo hii fedha ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri ni kidogo sana, hazitoshi kabisa na kuna miradi ambayo hajiatekelezwa, viporo ni vingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka jana Bunge tumeidhinisha fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 791.99 lakini hadi Machi mwaka huu fedha ambayo imetumika ni shilingi bilioni 18 na miradi ni mingi katika nchi hii na katika Halmashauri zetu. Nimuulize Mheshimiwa Waziri wa fedha, hii asilimia ya fedha iliyobaki ambapo miradi hajakamilika, mtaleta lini fedha zote ili tukamilishe miradi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Jimbo langu la Mpwapwa kuna miradi mingi ya maji ambayo haijakamilika. Kuna visima vitatu sasa ni mwaka mmoja tangu vimechimbwa, hakuna cha *pump*, hakuna cha bomba ambalo limewekwa. Kuna vituo vya afya viwili ambavyo vimeanza kujengwa zaidi ya miaka 10 havijakamilika ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, naishauri Serikali, *TRA* wanakusanya vizuri sana mapato, niwapongeze sana *TRA* lakini pamoja na mapato, tudhibiti fedha za Serikali ili fedha zote ziende kwenye miradi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu *TRA* kukusanya kodi ya majengo ya Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji. Nataka kupata maelezo, hii kodi ya majengo walikuwa wanakusanya Halmashauri wenyewe kuna sababu gani za msingi ikahamishiwa *TRA*? *TRA* watakwenda mpaka kwenye *grass root*, mpaka chini nyumba za mbali kwenye vijiji huko kukusanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wamekusanya kwa sababu Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilikuwa imetenga kama Halmashauri thelathini ndiyo *TRA* ikusanye, tupate maelezo, *TRA* wamekusanya kiasi gani na hizo Halmashauri zimeshapelekewa fedha kiasi gani kwa sababu Halmashauri hizi zina miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, nataka nipate maelezo kwa nini suala hili limekwenda *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu vyanzo vya mapato vya Halmashauri za Wilaya. Halmashauri za Wilaya zina hali mbaya sana, hasa mapato ya ndani kwa sababu vyanzo vingi vimechukuliwa na Serikali Kuu na fedha toka Serikali Kuu zinazopelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha awarudishie baadhi ya vyanzo vya mapato Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji ili wakusanye wenyewe kwa sababu hali

ni mbaya. Wanashindwa kuendesha Halmashauri zao kwa sababu vyanzo vingi vimepelekwa kwenye Halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna madeni ya ndani, wenzangu wamezungumzia pamoja na kulipa deni la nje ambalo ni lazima tulipe kwa sababu bila kulipa huwezi kupata mkopo tena lakini haya madeni ya ndani kwa mfano wakandarasi kama wasipolipwa barabara haziendelei kutengenezwa na madeni ya ndani ni pamoja na hao wazabuni wanaohudumia kwa mfano shule. Wilayani kwangu kuna wazabuni watatu wanahudumia chakula katika shule za sekondari, Mpwapwa *High School*, Shule ya *Maza Girls'* na Shule za Berege, wanadai zaidi ya shilingi milioni 300 hawajalipwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, siyo Halmashauri ya Mpwapwa tu ni maeneo mengi katika nchi hii, wazabuni hawalipwi sasa kama hawalipwi watahudumia shule hizi na wanafunzi wanatakiwa kupata chakula? Hivi leo wazabuni wanaohudumia vyakula katika shule wakigoma si shule zitafungwa? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha walipe wazabuni hawa ili waendeleo kuhudumia hizi shule zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wastaafu, wanalalamika pamoja na kuwa wanawalipa kila mwezi, lakini fedha ni kidogo waongeze fedha, wawe wanapata angalau fedha za kutosha badala ya hii Sh.100,000/= sijui Sh.200,000/=. Nataka niwaambie hapa wengi tumeshastaafu na tunakwenda kwenye uzee na sisi wengine tumefika kwenye uzee, mtu unatoka kwa mfano Rudi, Malolo unafuata Sh.100,000/= wakati nauli tu peke yake ya kwenda na kurudi ni Sh.30,000/= unapata nini hapo? Kwa hiyo, nashauri hiki kipato cha wastaafu kiongezwe ili waweze kupata fedha za kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ila ninachoomba tu ni kwamba Serikali ijitahidi



kupeleka fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri *otherwise* miradi mingi itakwama. Sisi ni Wabunge wa kuchaguliwa na tumeahidi katika Ilani ya Uchaguzi kutekeleza miradi mbalimbali, tusipotekeleza mwaka 2020 wananchi hawaturudishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lubeleje, tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nitoe tu mchango wa kushauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, mfumo wetu wa kukusanya mapato hivi sasa si mzuri. Tungeweza kukusanya kodi na ushuru au nchi ingeweza kupata hela ya kutosha hasa katika viwanda kwa kudhibiti mianya na kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mfumo mzima wa kusanyaji kodi utazamwe. Hivi sasa kodi zinalipwa katika utaratibu ambapo wale wanaolipa wanapangiwa kiwango kikubwa sana kutokana kwamba wengi wao huwa hawako kwenye mfumo ambao unaipa Serikali kodi. Ukusanyaji huu uungane na ule wa viwanda vikubwa sasa tunapata wakati mgumu pale ambapo mfumo wa ukusanyaji wa kodi ndani ya viwanda na makampuni haujakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hivi sasa Watanzania wanaogopa sana kutumia mfumo hii ya kielektroniki katika kukusanya mapato. Mfumo huu ni mzuri, mimi ni mdau wake kwa takribani miaka 10, shida iliyopo ni uelewa kwa wafanyabiashara na wadau wanaopaswa kutumia mfumo huu ili nchi ipate mapato ya kutosha. Kwa hiyo, nashauri

kama itawezekana kufanyike utaratibu wa mfumo huu na viwango vile vya kodi kupungua ili kundi kubwa la ukusanyaji wa mapato waweze kuingia katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, katika taarifa hizi tulizowasilishiwa, upelekaji wa fedha katika ngazi za Serikali za Mitaa hasa fedha za miradi ni mdogo sana. Tunapata wakati mgumu sana sisi Wabunge, bajeti hii tunapokaa hapa hatimaye tunapopitisha lakini mwishoni tunaenda kuwaambia wananchi malengo ya Serikali yetu au Serikali yao kuhusu miradi ya maendeleo. Sasa pale ambapo fedha za miradi ya maendeleo hazitapelekwa katika ngazi za Serikali za Mitaa miradi mingi ya maendeleo inakosa fedha na hatimaye sasa tunaingia mgogoro wa wachaguliwa na wananchi waliotuchagua lakini pia miradi mingi inakosekana na huduma inakuwa duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upelekaji huu wa fedha ukisimamiwa kwa kuzingatia mpango mzima wa bajeti na kwa kuona kwamba umuhimu wa miradi ya maendeleo na uendeshaji wa Serikali unapelekewa fedha kwa vyovyote vile miradi mingi ya maendeleo itafanikiwa. Hivi leo hata tukipiga kelele kwa Waziri na timu yake bila pesa kupatikana nadhani Waziri hatabadilika kuwa fedha na hatutaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni suala la Mfuko wa Maji. Naomba jambo hili litazamwe na namna pekee ya kuondoa kero ya maji nchini ni kutafuta mfumo mzuri wa kuona fedha za miradi ya maji zinapatikana kama ilivyo kwa Mfuko wa Mawasiliano na huu Mfuko wa Maji upate fedha za kutosha na pengine taarifa yetu iletwe baadaye ili tuweze kuona na kuishauri Serikali namna gani Mfuko huu wa Maji unapata fedha za kutosha ili miradi ya maji vijijini iweze kutatuliwa. Hivi sasa hali ni mbaya sana katika miradi ya maji na hasa miradi mipya na vile viporo lakini pia hali ni mbaya katika upatikanaji wa fedha na kwa vyovyote vile hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, madeni ya watumishi na wazabuni wenzangu walishaongea sitaongelea, nashauri malipo ya wastaafu yawe na mfumo wa wazi ambao unaonesha dira sahihi na kiwango kizuri. Hivi sasa wastaafu wetu au watumishi wanapoelekea kustaafu wengi wao wanakata tamaa na kuona kwamba ni wakati mgumu sasa unakuja kwao. Pengine tuone namna ya kuboresha malipo yale ya wastaafu na utaratibu wa wazi ambao hauwabugudhi wala kuwatesa wale wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, tulifanya ziara mimi na timu yetu ya Kamati ya TAMISEMI, tulienda kule Njombe, jengo la Hospitali ya Mkoa wa Njombe ni kubwa na linajengwa kwa shilingi bilioni 3.2 mpaka kukamilika, lakini miradi kama hiyo katika mikoa mingine nchini na katika Wilaya zingine inajengwa kwa shilingi milioni karibu nane mpaka tisa na hata zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na mfumo na utaratibu unaoangalia matumizi ya fedha katika manunuzi ya umma na jinsi ya kutekeleza miradi kwa kuzingatia mfano wa Hospitali ya Njombe. Matumizi sahihi ya fedha yanaweza yakasaidia nchi pia kuona ni namna gani kile kidogo kinachopatikana kinakuwa na thamani katika utekelezaji wa miradi ya wananchi na miradi ya huduma na utoaji wa huduma Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, ni Wakaguzi wa Ndani katika Halmashauri, wakaguzi hao mara nyingi wanafanya kazi katika utaratibu ambao sio mzuri. Nashauri Idara ya Ukaguzi wa Ndani katika Halmashauri zetu wapewe nafasi ya kuwa Idara inayojitegemea na Serikali ianzishe mfumo huu toka Taifa hadi Halmashauri ili wasiwe wategemezi kwa Wakurugenzi na watendaji wa Halmashauri kwa jinsi ambavyo wao ndiyo jicho la Halmashauri pale walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, semina kwa Madiwani. Madiwani bila kufanyiwa semina wakapewa kazi

ya kusimamia miradi ya maendeleo ni kazi bure. Nashauri Serikali ione umuhimu ya kutenga fedha kwa ajili ya semina za majukumu, wajibu na usimamizi na uendeshaji wa Halmashauri wao kama wawakilishi wa wananchi ili waweze kufanya kazi yao na kwa makusudi yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, ajira Serikalini. Tunashindwa kuajiri watu sasa kwa sababu hata mfumo ule wa kuwastaafisha watu unakuwa si rafiki kwa wale wanaoelekea kustaafu na kwa hivyo hela hatuna hivyo vijana wengi wanakosa ajira. Ingewezekana tungepunguza hata umri wa kustaafu sasa lakini tuboreshe pensheni ya kustaafu ili kustaafu kuwe miaka 50 kwa hiari na lazima 55. Hali hii itafanya wastaafu waone wanalipwa pensheni inayolingana na maisha yao yajao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, kuimarisha Benki ya Kilimo. Hivi sasa tunazungumza suala zima la upatikanaji wa fedha, lakini bila kuboresha Benki ya Kilimo ambayo ndiyo itachukua wananchi wengi na watanufaika na huduma yake na kutazama utaratibu wao ulio rafiki katika kukopesha wakulima, kwa vyovyote si rahisi uchumi wa kawaida ukamfikia mwananchi na mzalishaji na mjenga uchumi wa nchi kwa kadri ambavyo inawezekana kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, Tume ya Mipango iboreshwe, irudi Ofisi ya Rais kama Kamati ilivyoomba lakini ijengewe uwezo na iweze kuwa chombo/taasisi inayoweza kushauri Serikali kuhusu uchumi wa nchi. Chombo hiki kikisimamiwa kikakaa vizuri kinaweza kitatufikisha katika hali ambayo itatujenga zaidi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni misamaha ya kodi isiyo na tija. Hivi sasa si kweli kwamba misamaha yote ya kodi inayotolewa ina tija kwa nchi yetu. Kama itawezekana nashauri kuwe na chombo kinachosimamia mfumo huu na kutazama msamaha uliotolewa kwenye kampuni au taasisi fulani una tija kwa nchi, kizazi kijacho na uchumi wa nchi kwa siku za baadaye. Misamaha haiwezi

kuepukika kutokana na hali halisi inayojitokeza, lakini si misamaha yote ina tija kwa hivi sasa. Naona jambo hili likitazamwa linaweza likajenga uchumi wa nchi lakini likaongeza pia mapato Serikalini na tutafanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Issaay. Muda wetu uliobaki tutamalizia dakika tano tano na Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa dakika tano na mimi niseme machache kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutumia muda wangu vizuri, niseme tu kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Kambi, hotuba ya Mheshimiwa Lema na hotuba ya Mheshimiwa Peter Serukamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme jambo ambalo kwa kweli ningelizungumza kwenye *briefing* wakati tukitengeneza ratiba ya Mkutano huu wa Bajeti. Bajeti ni kuhusu mapato na matumizi, kwa muda wa siku 90, Wabunge tunakaa hapa kupanga matumizi lakini tukimaliza hizo siku 90 tunapewa siku moja au mbili kuzungumza habari ya mapato. Kwa jinsi hii sioni ni namna gani sisi Wabunge tunaishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa Mabunge mengine ukienda Bunge la Kenya hapa, juzi Kamati ya Bajeti ilikuwa Finland, ukienda Bunge la Uingereza muda wa kujadili vyanzo vya mapato katika nchi ni mkubwa sana Bungeni kuliko muda wa kujadili matumizi. Sasa sisi tunajadili matumizi ambayo hatujui tutayapata wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Makinda alianza vizuri na Bunge la Tano, aliunda Kamati ile tuliita Chenge *One* ilitoa

mawazo, ilitoa mapendekezo namna ya kuongeza vyanzo vipya vya mapato lakini sisi kila mmoja wetu analalamika, kila mmoja wetu anataka mradi lakini ukweli ambao tunauona sasa hivi Mheshimiwa Mpango tunamwonea pesa zipo wapi? Kwa hiyo, lazima tuamue, Bunge litengeneze ratiba inayofaa tupate muda wa kutosha kuweza kuishauri Serikali kuhusu vyanzo vya mapato, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda kulisema ni kuhusu vyanzo ambavyo tayari tunavyo. Bunge lililopita tulifanya uamuzi wa makusudi kunyang'anya *property tax* kwenye Halmashauri na kuwapa *TRA*. Kwa mfano Jiji la Dar es Salaam walikuwa wameweka maoteo ya Sh.33,100,000,000/=, lakini katika uhalisia wamekusanya shilingi bilioni 6.5 tu ina maana shilingi bilioni 26.59 hazikukusanywa na *TRA*, jambo ambalo Halmashauri na Majiji wangeachiwa kukusanya zile fedha pengine zingepatikana fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo Hazina imeendelea kutoa pesa kwa ajili ya Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuufikirie huu uamuzi wa kuchukua chanzo hiki cha mapato kutoka Majiji na Halmashauri na kukipeleka *TRA*, tuwarudishie Majiji na Halmashauri ili fedha ambazo zingeenda kwenye miradi ya maendeleo kwenye Majiji na Halmashauri kutoka Hazina zisiende na pengine haya majiji yanaweza kusaidia Hazina katika mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Tume ya Mipango. Ni ushauri wa Kamati ya Bajeti, ni ushauri wa wengi hapa, Tume ya Mipango irudi Ofisi ya Rais au iundiwe Wizara. Sababu ni kwamba Tume ya Mipango imeenda imejificha pale Hazina hakuna anayeitambua sasa Waziri na Naibu Waziri na wengine wako *busy* kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya mipango mingine kwa ajili ya kuhakikisha bajeti inaenda vizuri lakini Tume ya Mipango imesahauliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari za kwenye *corridor* Mheshimiwa Waziri ni kwamba Katibu Mkuu wa Hazina amekuwa *so powerful* kiasi kwamba hakuna mtu anayemsikiliza, kwa hiyo Tume imebaki inaeleaelea tu pale. Tume kama chombo cha kutunga sera za uchumi, kusimamia sera za uchumi, kusimamia hii miradi ya maendeleo kimebaki kinaelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwa Mheshimiwa Rais aone uwezekano wa kutoa Tume ya Mipango Hazina, aiundie Wizara au airudishe kwenye Ofisi yake kama ilivyokuwa zamani ili Tume iwe huru katika kupanga sera za uchumi za nchi na kuzisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini tunamalizia na Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hatuwezi kuendelea kukaa hapa tunaambiwa Wizara inakusanya, watu wanafungiwa maduka kwa kudaiwa kodi, watu wanafunga biashara kwa kulemewa mizigo, wanataka kukamuliwa huku hakuna mashudu, maziwa sijui yatoke wapi, wakati Waziri na Timu zake na vyombo vyake wanakusanyia kwenye pakacha linalovuja. Ukweli wenyewe tunapigwa mno, tunakusanyia kwenye pakacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi juzi inaripotiwa kwamba kuna mtumishi wa TAKUKURU amepiga ile mbaya, hebu Waheshimiwa Wabunge fikirieni vyombo ambavyo Mheshimiwa Rais amezungumza kwamba sasa anaviamini, vyombo vya ulinzi na usalama ndiyo vimsaidie kudhibiti mapato na mianya ya rushwa, TAKUKURU anakuwa ndiyo mpigaji mkubwa, hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri anapokuja hapa kuhitimisha atueleze yeye na timu yake sasa kwa awamu

hii wamejipangaje kuzuia pakacha hili linavyovuja vinginevyo watu wanakatishwa tamaa na wanapata hofu, tunawaonea watu kwa kuwatoza kodi inayokwenda kuvuja, hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kila Kamati ya Bunge iliyokuja hapa na Mawaziri wengi waliokuja hapa wanalalamika bajeti haitoshi yaani kwa maana nyingine Mheshimiwa Mpango na Naibu wake shemeji yangu, kwa lugha nyepesi ya Mheshimiwa Rais wanatuletea bajeti hewa, hizi ni bajeti hewa yaani watu wanapewa *eight percent* ya bajeti yao ambayo sisi kama Wabunge tunakuja kukaa hapa Madaktari, Profesa na watu wa kada mbalimbali mnakuja mnapitisha 100 kwa 100, mwisho wa siku ripoti inakuja kwamba mnapitisha *eight percent* maana yake ni kwamba hata *performance* ya Serikali ni *eight percent* katika eneo hilo husika, tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa akija hapa atueleze tunamalizianaje, hizi bajeti hewa, bajeti hewa ya safari hii iwe ya mwisho, hatutaki tena bajeti hewa. Tunataka apange mambo machache yanayoendana na kile anachokusanya, asijipangie mambo mengi akawapa watu kiu kumbe wanaishia kunawa kula hawali, hilo haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanazungumza kwamba wawape pesa kwa muda mchache uliobaki, ukitoa pesa mwishoni ni sawa na una gari la *V8* unaweka mafuta ukiongeza *speed* ikaanza 200 ujue *valve* zimefunguka zinakunywa mafuta ile mbaya, sasa hii pesa ya kutolewa mwishoni, zinapigwa hatutaki mchezo huo. Pesa zitoke kwa ratiba ambayo imepangwa na kwa muda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafanyabiashara wa *Bukoba Town*, nimekuwa napiga kelele hapa, Mheshimiwa tutataka *Marshall Plan* ya Bukoba – Kagera, tumeumia sana na shemeji yangu amekuwa anakuja ukweni unapendelea watu waendeleo kulala maturubai? Tunataka



*Marshall Plan* ya *Bukoba Town*, wafanyabiashara wana madeni hamuwalipi, walipeni basi madeni yao ya ku-*supply* huduma Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni *road license*, wadau wanaomba hii *road license* ya kutoza gari ambalo liko *under grounded* miaka saba au nane na mbaya zaidi unakamata gari linalotembea lipo kwenye biashara eti mpaka lile deni la gari ambalo lipo *garage* liligongwa au lilianguka lilipiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utaratibu huo ubadilishwe hata kama ni kuweka kwenye mafuta bora *road license* iwekwe kwenye mafuta, kwa njia hiyo hutalipata gari linalotembea kwa sababu limekwenda kunywa mafuta na tutakuwa tumemalizana kuliko kuwaonea watu, watu wanakamatiwa vyombo vyao, watu wanashindwa kuelewa na imekuwa ni chanzo cha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sitaki kugongewa kengele, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lwakatare.

## **MAJIBU YA MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Kabla sijawataja Wabunge ambao watachangia jioni, naomba nisome mwongozo wa Spika kuhusu haya yaliyooombewa mwongozo na Mheshimiwa Godbless Lema leo tarehe 30 Mei, 2017.

Waheshimiwa Wabunge, leo tarehe 30 Mei, 2017, Mheshimiwa Godbless Lema aliomba mwongozo wa Spika akitaka kufahamu iwapo kuna utaratibu wa michango ya Wabunge hapa Bungeni kuhaririwa na *Studio* ya Bunge. Mheshimiwa Godbless Lema alieleza kwamba aliomba *video clip* ya mchango wake alioutoa jana tarehe 29 Mei, 2017

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki lakini alipopewa *video clip* alishangaa kuona sehemu kubwa ya mchango wake imeondolewa.

Waheshimiwa Wabunge, nimefuatilia suala hili na maelekezo ni kwamba Studio ya Bunge na Ofisi ya Bunge kwa ujumla haina utaratibu wa kuhariri michango ya Wabunge isipokuwa tu pale ambapo kunakuwa na maelekezo ya Kiti yanayotolewa hapa Bungeni kwamba maneno fulani yaondolewe. Kwa maana hiyo, mchango wa Mbunge hapa Bungeni *Hansard* na *video clip* husika vinatakiwa vioane. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kilichotokea kwa suala la Mheshimiwa Godbless Lema ni kosa la kiufundi na linaendelea kufanyiwa kazi ili kurekebishwa. Hivyo, tatizo hilo litakapotatuliwa, Mheshimiwa Godbless Lema anaweza kupata *video clip* yenye mchango wake kamili kama alivyoutoa hapa Bungeni na kwa Mbunge yeyote ambaye atakuwa amepatwa na jambo hilo anaweza kupeleka malalamiko yake kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nataja wale wachangiaji ambao wataanza jioni tukijaliwa, tutaanza na Mheshimiwa Ally Salim Khamis, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Akbar, Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Ruth Mollel, halafu tutaendelea na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu umemalizika na shughuli zetu zimekwisha kwa asubuhi hii, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge Ilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na majadiliano yetu na tunaanza kama tulivyoagana asubuhi, tutaanza na Mheshimiwa Ali Salim Khamis.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kunipa afya njema na niwatakie Waislam wote duniani Ramadhan Kareem. Pia niwape pole wale wote ambao wamepatwa na maafa, ajali iliyotokea kule Karatu Arusha na wale wote waliopata majanga ya mafuriko hasa Visiwa vya Zanzibar ambapo pia kulitokea upepo mkali ulioezua majumba zaidi ya 70 na mvua ambazo zilisababisha maafa makubwa na majumba mengi kuharibika kutokana na mafuriko hayo ya mvua. Kwa hiyo, nawapa pole wote ambao wamefikwa na maafa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba utumie busara yako ya kiti kama vile ambavyo tuliwafariji hawa ambao walipatwa na tetemeko kule Bukoba na watoto wetu kule Karatu tukajitolea Wabunge ile posho yetu ya siku moja basi ningepomba busara yako itumike ili siku hii ya leo basi ichangie maafa ambayo yametokea kule Zanzibar, ukilinganisha sasa hivi kuna maradhi ya mlipuko ya kipindupindu, ningepomba busara yako ya Kiti itumike ili kuweza kudumisha muungano wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Utadumu muungano. *(Kicheko)*

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, leo nataka nijikite katika jambo moja tu ambalo linahusiana na hii Tume ya Pamoja ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwanza Tume hii ya Pamoja, ipo kikatiba, tokea mwaka 1977 jambo hili liliridhiwa katika Katiba yetu lakini kwa masikitiko makubwa tokea 1977 jambo hili lilipopitishwa katika Katiba yetu limekuja kutungiwa sheria mwaka 1996, miaka 19 baadaye. Kama hiyo haitoshi, jambo hili baada ya kupitishiwa sheria kuundwa kwa Tume yenyewe imekuja kuundwa mwaka 2003 miaka saba baadaye, baada ya kupitishwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo la masikitiko na ni jambo la aibu kwamba leo tumeunganisha nchi zetu hizi kwa ajili ya mustakabali wa vizazi vyetu na jamii zetu kutokana na nchi zetu hizi ambazo zimeungana. Ukija katika masuala ya Muungano, yameelezwa katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano na naomba leo niyasome ili kuweka *Hansard* vizuri, inaonekana pengine baadhi ya watu hatuna uelewa wa haya mambo ya Muungano, lakini ukiisoma Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano mambo haya 22 inaonesha wazi kwamba mambo yote katika nchi hii ni ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo haya ya muungano, ni Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, pili ni mambo ya nchi za nje, ulinzi na usalama, Polisi, mamlaka ya mambo yanayohusiana na hali ya hatari, uraia, uhamiaji, mikopo na biashara ya nchi za nje, utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na idara ya forodha, bandari, mambo yanayohusiana na usafirishaji wa anga, posta na simu, mambo yote yanayohusiana na sarafu na fedha, leseni ya viwanda na takwimu, elimu ya juu, maliasili ya mafuta pamoja na mafuta yasiyochujwa na motokaa na mafuta ya aina ya petrol, Baraza la Taifa la Mitihani ya Tanzania, usafiri na usafirishaji wa anga, utafiti, utabiri wa hali ya hewa, takwimu, Mahakama ya Rufaa, uandikishaji wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiyataja maeneo haya yote ukizungumzia ukusanyaji wa kodi ni jambo la Muungano, kwa hiyo kodi zote zinazokusanywa hapa ndani ya nchi hii ni mambo ya muungano. Leo kuna tozo mbalimbali zinazotozwa ambazo hizi si za kodi zimeainishwa pia katika taasisi mbalimbali. Kwa mfano, Ofisi ya Rais ni ya Muungano lakini yenyewe inakusanya tozo ambazo hizi zinatakiwa zije katika Mfuko wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu hii ni sehemu ya ofisi ya Muungano, lakini Msajili wa Vyama vya Siasa, Mahakama ya Rufaa kama ilivyotajwa huku lakini kuna mashirika mbalimbali, mashirika ya ndege na kadhalika, mpaka leo hii mwongozo umetoka kwamba iwekwe akaunti ya pamoja kati ya nchi hizi mbili ili kutunza haya mapato ya Jamhuri ya Muungano na kuzinufaisha hizi nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo miaka 40 umri wa mtu mzima, zimeundwa Tume chungu nzima. Ukiangalia utafiti huu ambao umefanywa na Tume ya Katiba kuna tume zimeundwa zaidi ya 11 humu ndani ya *book* hili ambalo limetolewa kuna Tume ya Mark Bomani, na Tume ya Shellukindo na wengine ambao imeelezea jinsi ya kuifanya Tanzania iondokane na hizi kero za Muungano. Hata hivyo, mpaka leo hii cha ajabu na cha kusikitisha suala hili halijapatiwa ufumbuzi miaka 40, halafu tunaambiwa kwamba Serikali hii ni Serikali sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali hii kumbe yale ambayo yametokea kwa nchi hii kwa ajili ya mchanga wa madini kwamba, nchi hii imedhulumiwa na wawekezaji hakuna tofauti na dhuluma ambayo Zanzibar imefanyiwa muda wote huu wa makusanyo ya Muungano hayakuwekwa katika sehemu ya Muungano ili kunufaisha hizi nchi mbili, hakuna tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia kwa *ratio* ya asilimia 21 katika mgao katika mambo ya muungano, ukiangalia hii trilioni 1.4 ambayo ameitaja Rais, siku ile Tume

ilivyowasilisha taarifa yake, Zanzibar tulitakiwa tupate karibu bilioni 66. Sasa ina maana sio ninyi tu mnaoathirika pia Zanzibar nayo inaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulivyokwenda kwenye uchaguzi mwaka 2015 tulisema kwamba, Zanzibar hii itajitegemea kwa uchumi wa huduma na hii Tanganyika ina rasilimali, madini, kilimo na kadhalika. Leo ukiangalia nchi kama Malaysia imestawi katika uchumi kwa sababu ya Singapore. Singapore haina *resource* ya aina yoyote lakini imewekeza katika huduma, leo Malaysia inanufuka kupitia Singapore. Sasa sisi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu liangalieni hili, ikiwa jambo hili halitapatwiwa ufumbuzi wa haraka basi inaonesha wazi kwamba wenzetu wa Tanganyika hamko tayari kulipatia ufumbuzi jambo hili na inabidi sasa tukazungumze lugha nyingine kule kwetu kwa ajili ya kuwaambia Wazanzibari Muungano huu imetosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na baadaye Mheshimiwa Akbar na Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye hii hoja muhimu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Niungane na wenzangu niwatakie wote waliofunga wawe na funga yenye heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza hii Wizara, nimpongeze Waziri Mpango, Naibu wake, Watendaji wote na Taasisi nyingi ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa mafaniko makubwa. Kwa sababu ukiangalia *parameter* za uchumi, utaona kwamba tunaenda vizuri, bila kuwa na *coordination* nzuri ya Wizara hii isingewezekana. Kwa hiyo nawapongeza sana wote. Niipongeze pia Mamlaka ya Mapato kwa makusanyo, napongeza pia usimamizi kwenye

idara ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kipindi hiki tumepokea ripoti nyingi sana, ukiangalia hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ripoti zaidi ya 600 kwenye majumuisho yake siyo kazi ndogo, kwa hiyo nitumie fursa hii kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo moja kuhusu Wizara hii ya Fedha inayo mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya kilimo. Nataka nijikite kwenye eneo hilo. Nitapenda nizungumzie taasisi mbili kwa maana ya hii Benki ya Kilimo na kampuni ya mbolea. Kwa sababu kilimo kwa ujumla wake kina mchango mkubwa sana kwenye ukuaji wa uchumi, kwa hiyo nafikiri nizungumzie haya maeneo mawili ili nione kwa namna gani naweza kushauri Serikali kupitia Wizara hii muhimu itusaidie wakulima wa Tanzania, wakulima wa Ushetu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kabisa katika kilimo kweli tutapata chakula, biashara zitashamiri lakini pia ni sehemu kubwa ya kutoa mchango wa mapato yasiyo ya kodi (*non tax revenue*) inatoka katika eneo hili la kilimo kama Wizara hii itasukuma vizuri na kilimo chetu kiwe chenye tija, ili tuweze kuondokana na kilimo hiki kwa ajili ya kujikimu, ili tuweze kwenda kwenye kilimo cha kibiashara na mapinduzi ya kilimo hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona yako mambo mengi mazuri ambayo kama Serikali imeyaandaa yanahitaji sasa msukumo wa kipekee ili kuona mchango wake unakuwa mkubwa. Kilimo hiki kitachangia ajira, kilimo hiki pia kitachangia malighafi ya viwanda na katika hali ya ukuaji wa uchumi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia hata kwenye mfumuko wa bei tumekwenda vizuri sana tuko kwenye digiti moja kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa akizungumza, tuko kwenye karibu asilimia sita, lakini ukiiona hii kwenye upande wa chakula bado mfumuko wa bei siyo mzuri. Tungekuwa na *indicator* kwa ujumla wake ingeshuka sana kama eneo hili la kilimo litakwenda vizuri. Kwa mfano,

sasa hivi kwenye chakula peke yake mfumuko wake wa bei uko kwenye asilimia 11 hivi, ukisoma kwenye tafiti mbalimbali. Kwa hiyo utaona kabisa kwamba tunavyokwenda kuiona *inflation* kwa ujumla wake kwenye asilimia sita lakini upande wa kilimo imejaribu kutupandisha juu, tungeweza kushuka chini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko juhudi mbalimbali Serikali ikiwa inafanya ili kuhakikisha kwamba kiwango cha uzalishaji kinakuwa kina tija kwenye kilimo. Kwamba tuende kwenye ukulima ambao unatumia pembejeo za kutosha pia teknolojia ya kisasa, bado kuna matumizi madogo kwenye upande wa umwagiliaji. Sasa bila Wizara hii kuweka nguvu yake na kuwezesha vile vyombo ambavyo kimsingi vinasaidia sio moja kwa moja inaweza ikasaidia pia kwenda kupandisha uzalishaji kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji wakulima waende kulima kisasa, wawe na mashamba makubwa, wawe na mitaji ya kilimo, pamoja na kuwa kuna sekta zingine zinasimamiwa na Wizara zingine lakini bila Wizara hii ya Fedha utagundua kabisa kwamba hatuwezi kwenda kuwa na kilimo kikubwa ambacho kitachangia katika ukuaji wa haraka wa uchumi wetu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba lazima Serikali kupitia Wizara hii ituangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia hata mikopo inayotoka ina riba kubwa na bado kuna uchache wa maghala ya kuhifadhia chakula, mara nyingi nimekuwa nikizungumza, naona iko haja ya kuwa na tafiti za kutosha ili kwanza tuwe na chakula cha kutosha ili tuende kwa usalama zaidi. Pia tunahitaji kuchakata mazao yetu ili yaweze kuongeza ubora wake hatimaye yatingizie fedha za kutosha. Kuna madhara mengi pia katika uhifadhi wa mazingira, kwa hiyo uko umuhimu wa Serikali kupitia Wizara hii kutazama sana kwenye eneo hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo imeanzishwa mwaka 2014 lakini bado msukumo na mtaji ni mdogo sana. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aiongelee.



Nimeiona kwenye hotuba yake nzuri hii, katika ukurasa wa 47 ameizungumza lakini kidogo sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, tulipozungumza na benki hii tunaona yako mahitaji ya kuiongezea mtaji. Kwa hiyo, niombe sana Serikali itazame kwa sababu ilikuwa hairidhishi pale ambapo tunaona benki hii imejipanga kutoa mikopo yenye riba ambayo ni nafuu, sasa kama hawana mtaji wanahitaji nao waende kwenye *Commercial Bank* ili wakakope fedha halafu waje wakopeshe wakulima wetu, haitawezekana hizi *rate* ambazo wamezionesha kwenye sera yao. Kukopesha mikopo ya bei nafuu haitawezekana kama na wao wanaenda kwenye mabanki mengine yenye riba kubwa kwa sababu mtaji wao bado ni mdogo. Mtaji wao uko kwenye bilioni 60 lakini Serikali ilikuwa imeahidi kusaidia angalau bilioni 100 kila mwaka kwa miaka nane ili benki hii iende kwenye mtaji wa bilioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa muda umekuwa mwingi bado benki hii haina mtaji wa kutosha. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana aitazame benki hii ili mwisho wa safari tuweze kuona kwamba wakulima wetu wananufaika. Utaona kabisa kati ya majukumu mazuri ambayo benki hii tumeipa baada ya kuianzisha inatakiwa iweze kutoa mikopo yenye riba nafuu, itatakiwa ifanye tafiti za kifedha, tafiti za kiuchumi katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kabisa kwamba ukienda kwenye maeneo ya vijiji bado tuna shida hata hii mikopo inayotoka tunaona ina sura nzuri ya riba ya asilimia 18 lakini *effective rate* yake kama hatufanyi tafiti za kutosha wakulima wale wanachajiwa kwa mwezi, ukifika mwisho wa safari utaona zile *rate* zina-*attract cost* kubwa ambayo ukirudisha ukafanya *re-alculation* utaona inakwenda mpaka zaidi ya asilimia 30. Kwa hiyo, wakulima wetu wanaumia hawawezi kufanya kilimo ambacho kitaweza kuwapa faida kama hii haitazamwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo benki hii ikiwezesha inaweza ikasaidia kuweza kufanya tafiti na kuona kama maeneo yanawapunja sana wananchi iweze

kusaidia. Pia itakuwa zoezi zuri la kutoa elimu na kujenga uwezo kwa wakulima, kujenga uwezo kwa ushirika, kujenga uwezo kwenye taasisi zingine za kifedha kama hizi *micro-finance* hizi zinazokuwepo zinategemea sana chombo kuwe na ambacho itazisaidia ili mwisho wa safari wakulima wetu waweze kunufaika. Kwa hiyo, nafikiri iko haja ya kuiangalia benki hii iweze kupata mtaji ambao utaiwezesha kuweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu niliona kwamba kulikuwepo na utaratibu wa benki hii kupata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri tumefikia wapi? Kwa sababu ilikuwa inatia matumaini angalau wangepata hizi dola milioni 93.5 ambazo tulizungumza kwenye Kamati, kama bilioni 204 angalau ingekuwa nusu ya safari tunaanza kusonga mbele. Sasa tumefikia wapi na huu mchakato wa kuisaidia hii benki kupitia huu mkopo ambao Serikali kupitia Wizara hii ilikuwa imefanya *arrangement*, napenda tujue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado iko *pledge* nzuri sana kuelekea mwaka 2020/2021 kwamba tuwe tumefikisha hii benki kuwa na mtaji wa trilioni tatu, ingeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa sana katika hii sekta ya kilimo. Kwa hiyo, nafikiri tuitazame kwa nia ya kuiboresha lakini mwisho wa safari tunavyokwenda kwenye uchumi wa kati tutawasaidia sana wananchi wetu ambao wana utayari sana wa kuzalisha kwa tija ili iweze kuleta mchango mkubwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kampuni ya mbolea. Kampuni ya mbolea imeanzishwa miaka mingi, imeanzishwa mwaka 1968 lakini ilikuwa na shughuli moja tu ya kushughulikia uzalishaji wa pembejeo pamoja na mbolea kule Tanga. Hata hivyo, hapa mbele ya safari tumekuwa na mkwamo, matokeo yake sasa imekuwa ikiendelea kuwa na jukumu moja la kusambaza mbolea. Usimamizi wake haukuwa mzuri kwa sababu mbolea imekuwa ikitufikia huko vijijini ikiwa na gharama kubwa. Nashukuru Wizara ya Kilimo kuja na mpango wa kununua

mbolea kwa pamoja. Bado natazama na chombo hiki kitaingia wapi ili kiweze kusaidia? Kwa sababu chombo hiki kimekuwa na msukosuko mkubwa sana, kina changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali inadaiwa na kampuni hii, lakini pia utaona kwamba, imekuwa ikipata hasara kubwa sana. Mpaka kufikia mwaka 2015 ilikuwa na *accumulated losses* ya 30 billion, lakini hawa wanahitaji mtaji, walikuwa wanaomba wapewe kama bilioni 27. Sasa haipendezi kuona wanaomba shilingi bilioni 27 wakati wana madeni zaidi ya shilingi bilioni 30. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba aitazame hii taasisi ili iweze pia kutoa mchango wake katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Akbar baadaye Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Ruth Mollel wajandae.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai mpaka jioni hii ya leo, ili tuje tushiriki katika mjadala huu wa kuchangia Wizara hii muhimu. Nakushukuru wewe mwenyewe kwa kuweza kutupa nafasi hii na kutoa mchango mdogo kama huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wamezungumza Wabunge wenzangu, nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mpango kwa hii *graph* ya maendeleo ambayo inaonesha kabisa kwamba asilimia saba kwa kweli kwa uchumi kukua ni asilimia kubwa sana. Kwa kweli kwa hili, Mheshimiwa Mpango amejitahidi sana, namshukuru sana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni juu ya Kiwanda cha Newala ambacho ameahidi kwamba, anafikiria

kukichukua kukirejesha tena Serikalini. Nampongeza sana na achukue kile kiwanda sio asubiri tena aangalie uwezekano akakichukue kesho na aangalie namna gani auaweza akakigawa. Kwa sababu, vile viwanda vilikuwa vingi, Mkoa wa Mtwara na Kusini kote kulikuwa na viwanda zaidi ya 10 ambapo Serikali ilikuwa imekopa fedha nyingi sana na vile viwanda vilivyopo Newala ilikuwa ni Mkopo wa Benki ya Dunia kupitia wallokuwa wajenzi *Itaro Fame*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mtu yule anapewa kwa bei poa kabisa, Serikali ilikuwa imeingia kwenye deni kubwa ambalo kwa kweli ilikuwa inalilipa, lakini yule mtu mpaka leo hajafanya uzalishaji wowote wa msingi na anachokifanya yeye ni ghala tu. Sasa sio Newala tu, angalia maeneo mengine ambayo kuna viwanda kama vile, wale watu ambao tumewapa vile viwanda hawavitumii kwa yale makusudio ambayo tumewapa na badala yake wanatumia kwa madhumuni mengine. Hivyo viwanda ni vingi sana na ni kweli akichukua hatua Mheshimiwa Waziri tutamwona kwamba, sasa kweli amekuja kivinginevyo, nampongeza katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nishauri, Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano hizi taasisi kutoa fedha, kwa mfano; *CAG* anampa fedha kidogo sana na zile taasisi ambazo ni muhimu ambazo anadhani kwamba tunawapa mabillioni ya fedha, lakini huyu msimamizi wa fedha anampa fedha kiasi kwamba anashindwa kwenda kufanya ile kazi. Je, haitakuwa kazi ngumu sana kwa sababu, mtu umempa nyama lakini yule Mkaguzi wa kwenda kukagua kile kiwanda hana uwezo wa kwenda kumfikia yule mtu kwenda kukagua? Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri naomba afanye jitihada zozote ili hii Ofisi ya *CAG* aweze kuisaidia iweze kupata fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimepata athari vilevile kutokana na huu ukata. Toka enzi za Waziri Maghembe akiwa Waziri wa Maji, yeye likuja akaahidi pale akasema kwamba, atatupa mradi wa maji kutoka Mitema

kwenda kwenye Kijiji cha Chihangu, Chilangala, Miyuyu, Mikumbi na pale maji yatakwenda kwa *gravitation force* hadi yafike Nnyambe. Kwa hiyo, kile chanzo cha maji kilichopo Mbwinji kikachukuliwa kikapelekwa Masasi hadi Nachingwea. Hatuna tatizo kuhusu maji kwenda Nachingwea, tatizo ni hapa toka akiwa Waziri Maghembe yule Mheshimiwa Maghembe hakuonekana tena mpaka leo kuna Waziri mwingine, kile chanzo wale watu hawajapata maji na yale maji sasa kule eneo lingine yanatoka. Kwa hiyo, wanajiuliza, hawa watu wamekuja kuchukua chanzo hiki cha maji, halafu wao waliahidi kabisa kwamba, wataleta fedha kwa ajili ya kuchukua maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachohitajika pale ni fedha tu kwa sababu, yale matenki alishajenga Mwalimu Nyerere yako pale Mikumbi, Miyuyi, kwa hiyo maji kutoka Mitema pale ni mabomba tu, ni kununua tu kwa kutumia fedha hadi kufika Mikumbi kupitia Chihangu. Sasa vinginevyo Mheshimiwa Waziri atakuwa ananigombanisha mimi na wananchi wangu. Sio mimi tu, vilevile wale wananchi watakuwa wanagombana kati ya kijiji na kijiji, wilaya na wilaya na mkoa na mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki wananchi wangu waende wakagombane na wananchi wa Masasi, kwa sababu wale wananchi wa Masasi ni ndugu zetu, ila nimwombe Mheshimiwa Waziri, hebu akae na Waziri mwenzake wa Maji, ni namna gani watawapelekea maji wale wananchi wa Newala ili wapate maji, tuangalie uwezekano wa kulitatua tatizo hili, kuliko hii ambayo sasa hivi inakuja kiduchukiduchu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuongea na Waziri wa Maji amesema kwamba tutaangalia uwezekano wa kumpata Mkandarasi, lakini hatutawaleteeni fedha; hatuhitaji fedha sisi tunachohitaji ni huduma. Mheshimiwa Waziri hebu aliangalie hilo kama limekaaje, kama limekaa vibaya, vinginevyo huu ushauri wangu utakwenda *at negative attitude*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nimshauri ni kuhusu wafanyabiashara na huu ugawaji wa *TIN Number*; inawezekana hawa *TRA* wanamdanganya Mheshimiwa. Mimi mwenyewe haya yamenikuta, nilienda nikasajili kampuni ambayo ilikuwa mimi mwenyewe ni Mkurugenzi pamoja na watoto wangu wanne, jumla tukawa watano, tulivyokwenda kusajili nikategemea kwamba, nitapata *TIN Number* bure, lakini tulivyokwenda pale tulipewa masharti kwamba, wewe ni lazima uwe na *TIN Number* ya kampuni, lakini na wewe mwenyewe uwe na *TIN Number* na Wakurugenzi wawili wawe na *TIN Number*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kampuni tukailipia 1,000,000/= na kila mtu ambaye ni Mkurugenzi mle akalipia laki tano na biashara hatujafungua. Mheshimiwa Waziri haoni kama hapo ni *double taxation*? Hilo nimelifanya Dar-es-Salaam. *Double taxation* ipo nchi hii, inaonesha si kwamba unapewa tu *TIN Number*. Unapewa *TIN Number* ya kampuni ambayo ni *Limited Liability Company* na Wakurugenzi wote wanalipia laki tano, laki tano kutokana na ile *TIN Number* na biashara na duka sijafungua mpaka leo. Kwa hiyo, tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri angekuwa na *alternative*, hawa ni watu wake, hebu awaache wafanye biashara waingie kwenye dema, hana sababu ya kuwatafutia manati hawa watu wake, wanakuwa wengi halafu baadaye anawatoza tozo kidogo kidogo. Hiyo namwambia kabisa kwamba inawezekana ndiyo maana wale wafanyabiashara wa Kariakoo wamekimbia. Mimi ni mfanyabiashara wa Kariakoo, asituone tumekaa hapa, sisi wengine ni Wamachinga. Hicho kitu ninachomwambia na inawezekana ile milango ndiyo maana wale watu wamefunga, wamekimbia wanaogopa *double taxation* ya *TIN Number*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika 2,500,000/= mtu hujafungua biashara. Mheshimiwa Waziri asifikirie kwamba, wananchi wake anaowadai kodi wana hela, hawa wananchi wengi milioni mbili ni hela nyingi sana, hebu afikirie, *don't*

*look far*, asifikirie mbali sana akadhani kwamba wananchi wake wana hela, hawa watu anaowaongoza ni maskini sana wana mtaji wa Sh.500,000/=, Sh.1,000,000/= na Sh.2,000,000/= . Huyo mwenye Sh.2,000,000/= ndio ana mtaji mkubwa sana. Kwa hiyo, anapofikiria kumtoa mtu kodi ya Sh.2,000,000/= *in advance* na hajafungua duka asitarajie yeye akapata kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa Waziri aache watu wa Kariakoo wafanye biashara kama walivyokuwa wanafanya *then* anawatoza kodi, tena sio nyingi, hata akiwaambia kwamba, walipe laki tano atapata pesa nyingi tena za kutisha. Hayo mambo yapo, lakini inawezekana watu wanashindwa kumweleza au yeye mwenyewe aende kufanya utafiti pale Kariakoo, hayo mambo atayakuta kule, nadhani atakuja kuniambia ni kweli, sasa hayo mambo ni mazuri, hao watu wanamdanganya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, hebu kama tunaingia kweli kwenye sekta ya viwanda, tuangalie namna gani wenzetu Wachina wameendelea. Kwa sababu, wale wenzetu walikuwa na mfumo wa *Commune*, ile *Commune* mwaka 1967 ilikuwa inakopa duniani, lakini leo ndio *shareholder* wa *Exim Bank* ambako leo tunataka kwenda kukopa. Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi ya kukaa na Jeshi, kwa maana JKT aangalie *pilot areas* ambako wanaweza wakapeleka vijana wa JKT wakawa wanalima, lakini wakawa wanazalisha, viwanda vilevile tukawa tumekaa na mtu wa viwanda tunaangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tutakuwa tumetengeneza ajira, maana leo ukiwa na *pilot area* kama 10 na kila *pilot area* kuna vijana 8,000 utakuwa umeshaajiri vijana 8,000 x 10 utakuwa umeajiri vijana 80,000. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Akbar, muda wako umeisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na baadae Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Massare wajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote naomba niwatakie ndugu zangu Waislam mfungo mwema, ili waendelee kupata baraka za Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikikipitia kitabu cha Waziri na taarifa za Kamati, nikaanza na sehemu ambayo ilikuwa inazungumzia hoja mbalimbali na hatua ambazo Wizara imekusudia kuchukua kwa maana ya kukabili changamoto. Wanasema kuendelea kuwianisha mapato na matumizi kwa kuhakikisha kuwa mgawo wa fedha utaendana na upatikanaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema jambo hili ni jema, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba, kuhakikisha kuwa mgawo wa fedha utaendana na upatikanaji wa mapato, fedha hizo zinazopatikana bila kuwafikia walengwa tabu ipo na ni tabu kubwa. Kwa hiyo, naomba ikiwa amesema hizo ni hatua za kukabili, kweli hilo jambo tulifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nafahamu. Kuna changamoto kwa maana ya mashine za kielektroniki, niendeleo kusema jambo hili ni jema, lakini waendeleo kufuatilia suala la udanganyifu katika mashine hizo za kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo inaendelea kutukumbusha kwamba, ni vizuri tukajenga uwezo wetu binafsi kwa sababu unapokuwa unatamani kusafiri, lakini kwa nauli ya kutoka kwa jirani, hiyo safari iko mashakani. Niendeleo kuomba Mheshimiwa Waziri kwa maana ya



kujenga uwezo wetu wa ndani, ili hata kama fedha za wadau wa maendeleo zitakuwa hazipatikani tutakuwa tuko sehemu salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba elimu kwa maana ya miradi ya ubia kwa wadau mbalimbali, wadau hao tusiwasahau Madiwani. Tutakapokuwa tukizungumzia elimu kwa miradi ya ubia Madiwani ni kiungo muhimu kwa sababu wanatufanyia kazi kubwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio Mheshimiwa Waziri amezungumzia mafanikio kwa maana ya kupunguza malimbikizo ya madai ya Watumishi, Wazabuni na Wakandarasi yaliyohakikiwa hadi Machi, 2017, Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 796.3. Nasema kwa hatua hiyo ni jambo jema, lakini tuendeleo, malalamiko huko ni mengi na kwa kweli eneo hili tukilifanyia kazi tunaamsha ari ya watu kufanya kazi, lakini na wale wengine kama ni Wazabuni au ni wadau muhimu wa maendeleo wanapokuwa wakilipwa, maana yake wanashiriki zaidi kwenye kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la upelekaji fedha za maendeleo. Mimi kule kwangu Katavi hivi ninavyoongea hawajapata OC, hawajapata fidia ya vyanzo vya mapato kwa maana ya *General Purpose Grant*, suala la *National Water Supply Sanitation Program*, hawa watu fedha zote katika maeneo hayo hawajapata. Kwa hiyo, tunapozungumzia suala zima la kupeleka mbele maendeleo naiona shida kubwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ya kuenzi watumishi na hasa wale wastaafu, mafao ya wastaafu na mirathi ilipwe kwa wakati. Hapa nilikuwa naendelea kupongeza, najua kuna *program* wanasema mfumo wa TEHAMA unaoitwa *Saperion* mpaka Machi, 2017 inaonesha wastaafu 96,989 wamewekwa kwenye mfumo, hili ni jambo jema, lakini niendeleo kuisitiza namna pekee ya kuwaenzi

wastaafu ni kuwalipa kwa wakati ili watu hawa waone kwamba, nchi inawaheshimu kwa utumishi walioufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza suala la utoaji elimu kwa Maafisa Mipango. Hapa kuna Maafisa Mipango 183 kutoka Sekretarieti za Mikoa na 237 kutoka Halmashauri kwa maana ya kuwajengea uwezo wa kutafsiri vipaumbele vya Kitaifa. Ni vizuri kuwajengea uwezo kwa sababu, watu hawa tunao kule katika maeneo yetu, wanapokuwa wanafahamu nini tufanye, elimu hiyo wataishusha kwa watu wengine pale, kwa hiyo tutakuwa tunaimba wimbo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu tunaambiwa kwamba, 2016/2017 kukua kwa Pato la Taifa ilitoka 7.2 kwenda 7.3 na kwa maana ya 2017 tunakusudia kukua kwenda 7.4 ni jambo jema, lakini ninachoomba Mheshimiwa Waziri wananchi hawa wanatamani tunapozungumzia habari hii ya ukuaji huu wa uchumi walione bubujiko kwenye mifuko yao. Namna pekee ya kuweza kuimba ukuaji wa uchumi uende sambamba na hali halisi katika mifuko yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo yote, najua pia kwamba, mfumuko wa bei unabaki tarakimu moja na nakisi ya bajeti ya Serikali isiyozidi asilimia 4.5 ya Pato la Taifa yote hayo nasema ni mema. Eneo la sekta ya ujenzi, naona hapa tunaambiwa kwamba, imekua kwa asilimia 13. Sekta ya Ujenzi kwa mimi ninayetoka Katavi naona namna pekee tutakayoweza kufanya kwa sababu, leo ukiuzungumzia mfuko wa simenti katika maeneo ya kwetu, bei ya mfuko wa simenti wakati nikiona sekta hii inakua, natamani tuone namna ambapo mkazi wa Katavi anapokwenda kuununua mfuko 20,000/= anapokwenda kununua mfuko zaidi ya 20,000/= ni namna gani na yeye atakuwa sambamba na ukuaji wa sekta hii ya ujenzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa upande wangu naomba niishie hapo. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapufi. Tunaendelea na Mheshimiwa Ruth Mollél, baadaye Mheshimiwa Massare, Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Kiteto Kushuma wajandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Na nichukue nafasi hii pia niwatakie kheri ndugu zetu Waislam, Ramadhan Karim kwa wote, Mungu awajalie mmalize mfungo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Fedha na Mipango ni moyo wa Serikali. Nasema moyo wa Serikali ni kama moyo wa binadamu unavyofanya kazi, kama usipofanya kazi vizuri kila kitu kinatetereka. Kwa hiyo, ninapenda kusisitiza unyeti wa Wizara hii ya Fedha na mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua katika mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kwamba, hii ni Serikali ya Viwanda. Katika kuangalia mpango wa miaka mitano, nikaangalia mpango ule wa mwaka mmoja, nikaangalia pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, vimetajwa viwanda vingi sana ambavyo vinahitajika kufanyiwa kazi, vingine kufufuliwa, vingine kujengwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake atuambie hii Tanzania yetu ya viwanda ni viwanda vya aina gani? Kwa sababu ni lazima tujue kama viwanda tunavyozungumzia ni *agro-processing*, kama ni *textile industries*, kama ni *machinery*, ili tuweze kuwa na lengo ambalo Serikali iweze kujipanga maana unapoinisha kabisa, kwamba, kama alivyofanya Mwalimu Nyerere yeye alikwenda kwenye *Textile Industry*, tukaona viwanda vingi vya nguo na *resources* zote zikapelekwa kwenye hayo maeneo kwa ajili ya kuleta ufanisi na ku-*create* ajira. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake atufungue macho kidogo, kujua hivi viwanda tunavyovizungumzia ni vipi ambavyo Serikali inajikita kuviamsha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona viwanda vingi, ni jambo jema, lakini kwa *resources* tulizonazo hatuwezi tukapeleka hapa kidogo, hapa kidogo, hapa kidogo. Ni lazima tuainishe maeneo madhubuti ambayo tunajua baada ya miaka mitano tunajua hii Serikali tutaipima kwa viwanda gani vilivyokamilika na vinavyofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo pia linaendana na kuelimisha Watanzania. Nchi nyingine za duniani ukienda Mauritius au Singapore au Malaysia unakuta mpaka *tax driver* anajua mwelekeo wa nchi yake. Je, Watanzania wote tunajua mwelekeo wa nchi yetu? Kama ni laa, basi kazi kubwa ifanyike ili kusudi kila mtu aweze kujua nini mwelekeo wa nchi yetu katika hii Sera ya Viwanda Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itasaidia hata na wakulima kama ni *agro-processing*, wakulima watajipanga, kila mtu atajipanga na Serikali pia itajipanga kama ni kupeleka mbolea, kama ni kuhakikisha mashamba makubwa ya pamba, itajipanga vizuri na wataalam. Maana mwaka 2015 tulihitajika tuwe na *Mechanical Engineering, Manufacturing Engineering*, kama 17,000, lakini lengo halikufikiwa, kwa nini halikufikiwa? Ni kwa sababu bado hatujaainisha ni kitu gani tunataka kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mapato ya ndani. Hili jambo limezungumziwa na watu wengi kuhusu kodi ya majengo. Kodi ya majengo ina historia, Mheshimiwa Waziri anafahamu. Kwanza walikuwa wanakusanya *TRA* wakashindwa, jukumu hili likapelekwa kwa Halmashauri (TAMISEMI) wakafanya vizuri sana wakakusanya, sijui ni kitu gani sasa kimekuja hapa katikati kuona kwamba hili suala tena lirudishwe *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa kidogo tu ya mkoani kwangu Dar es Salaam, Kinondoni na Ubungo walikuwa wamepanga kukusanya bilioni 10.5 Kinondoni ilikuwa wakusanye bilioni 7.5, Ubungo shilingi bilioni 3.0, wote ilikuwa wakusanye hizo pesa. Jukumu hili lilipoondolewa

wakaambiwa watapewa bilioni mbili, mpaka leo hawajapewa hata senti tano na hatujui kama hizi pesa zimekusanywa au hazijakusanywa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunakubaliana kwamba Serikali imeingia katika Sera ya *D by D* na unapotekeleza Sera ya *D by D* upeleke *resources*, upeleke na wataalam. Kitendo cha kunyang'anya *property tax* kwenye Halmashauri za Jiji na Manispaa ni sawa na kuwaambia wasifanye kazi, kwa sababu huduma zote za jamii zinapatikana kwenye Serikali za Mitaa ndiko kwenye afya, maji, barabara, ndiko kwenye kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuwaje kwa sababu Serikali Kuu imekasimu madaraka kwa *Local Government*, ni kama baba unasema mtoto wangu wewe nenda ukafanye *A, B, C, D*, chukua hela hizi, chukua *resources* hizi, sasa unainyang'anya tena halafu unategemea itafanya nini? Tunaomba Mheshimiwa Waziri ili akajitafakari, najua Sheria ilipita hapa lakini hiyo sheria ikatazamwe upya, kwa sababu mpaka sasa *TRA* wameshindwa kukusanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa lringa tumekuta *TRA* lringa wameshindwa kukusanya, wanawatumia tena hao hao watu wa *Local Government* kukusanya kuwatumia kama *agency*. Kama wao hawawezi kukusanya kwa nini wasiwaachie *Local Government* wazikusanye hizi pesa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye suala la fedha za miradi. Fedha za miradi tumekwenda kwenye Mikoa fedha za miradi hakuna, tumekuja hata kwenye Wizara, fedha za miradi hazipo hata kwenye Wizara katika taarifa zilizopita sasa hivi kwa mfano kilimo wanapata *three percent*, viwanda *eighteen percent*. Sasa ni kwanini Wizara isiende na *realist budget*. Kama bajeti ya kupeleka kwenye Wizara fulani ni bilioni mbili basi ipelekwe hiyo bilioni mbili na ipatikane, kuliko kusema unapeleka bilioni 100 kwa mfano

kilimo halafu hakuna pesa inayokwenda. Hii ni *unacceptable* kwa kweli. Twende na uhalisia ile pesa iliyokusanya ndiyo hiyo igawanywe na hiyo iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kidogo kwenye suala la Muundo wa Wizara. Najua Tume ya Mipango iko chini ya Wizara sasa hivi, Tume ya Mipango ndiyo *think tank* ya uchumi na mipango. Nikiangalia hata bajeti waliyopelekewa haitoshi, sasa katika hii dhana ya Tanzania ya viwanda ikiwa Tume ya Mipango ambayo ndiyo *think tank* ambayo inatakwa ikae na kufikiri, kupanga na kupangua haipati bajeti, tutafika huko tunakwenda? Sioni kama tutafika huko tunakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kumaliza hoja yake atuambie mwelekeo wetu wa viwanda ni upi na ni viwanda gani ambavyo Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba itakapofika 2020 vitakuwa vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare, halafu Mheshimiwa Abdallah Chikota na baadaye Mheshimiwa Kiteto Koshuma na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk wajandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara hii ya Fedha na Mipango katika kufanya nchi yetu iende. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Waisalam wenzangu wanaoendelea na mfungo huu wa mwezi Mtukufu mwezi wa Radhamani, nawaombea Ramadhani Mubarak. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii ya Fedha kwa juhudi na kazi nzuri ilizoonessa hasa katika suala zima la kusimamia kulipa deni letu la nje. Wizara ya Fedha imesimamia kwa ukamilifu kwa mwaka uliokwisha na

naomba sasa waendeleo kusimama imara kuhakikisha nchi hii inaaminika baadaye ili tuweze kufanya maendeleo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Wizara ya Fedha kwa usimamizi wao madhubuti sana ambao ulikutana na changamoto mbalimbali katika kusimamia mashine hizi za elektroniki (*EFDs*) kwa wajasiriamali wahakikishe wanazitumia ili kurahisisha makusanyo ya kodi za Serikali. Ni ukweli usiopingika kwamba Wizara hii ina mafanikio kiasi kikubwa na niwapongeze sana. Nataka kushauri Serikali yangu na Wizara hii tujaribu kuweka sera ambayo itaeleweka juu ya watu wetu, Serikali tusiwe na sera za mlipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nataka kulisemea na hata Mheshimiwa Waziri amelionyesha katika ukurasa wa 41 kwamba sasa tunatoa nafasi kubwa kwa sekta binafsi kusaidia katika uchumi na hasa kuweza katika maeneo mbalimbali. Tukikumbuka kule nyuma Serikali ilikuwa ikifanya biashara kupitia mashika yake ikiwemo *RTC*, *NMC* na hata mashirika kama *GAPEX*, badala ya mashirika haya kulipa kodi yalikuwa yanachukua ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoondoka kule nilitegemea kwamba sasa Serikali haitajiingiza tena katika biashara, kuna viashiria vidogo vidogo vinaoonesha kwamba Serikali inataka ijaribu kuingilia katika biashara. Niombe sana Mheshimiwa Waziri ang'ang'ane hapo alipoonesha ukurasa wa 41 kwamba sasa sekta binafsi itawekeza maeneo mbalimbali na ametolea mifano ambayo iko hai, gari za mwendo kasi pale Dar es Salaam lakini barabara ya Dar es Salaam Chalinze ambayo inategemea iwe ya kutoza *toll* kwa maana ya *road toll*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejifunza kutoka nchi mbalimbali walioendelea waliachia sekta binafsi, Serikali kwa uwezo wake haiwezi kufanya kila kitu, lakini sekta binafsi inashindwa kuja katika nchi hii kwa sababu ya kutokuwa na uwazi katika sera za nchi. Hatuna sera, akija Waziri huyu ana tamko lake, akija huyu ana tamko lake. Tukiweka hilo

itatusaida na wadau mbalimbali kutoka nchi mbalimbali miongoni mwetu Wabunge na hata wananchi na wafanyabiashara mbalimbali wanaweza kuleta watu wa kuwekeza katika maeneo mbalimbali kama tu tutakuwa na Sera ambayo itaeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vya kuimarisha ili sekta hii binafsi ambayo tunaitegemea isaidiane na Serikali katika kuboresha maendeleo ya nchi yetu ikiwemo miundombinu, maeneo mbalimbali ni lazima tuboreshe, Benki ya *TIB*. Mheshimiwa Waziri ameonesha kwa vipengele vifupi tu ukurasa wa 49 na ukurasa wa 90. Naomba sasa juhudi za makusudi benki hii ya *TIB* ndiyo mkombozi wa sekta binafsi, kwa sababu benki hii itahusisha mwekezaji yeyote anaweza kwenda pale na akapewa mkopo ambao ataulipa kwa kile alichowekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, benki hii inasuasua, mtu akihitaji mkopo mkubwa Waziri mwenyewe ni shahidi na ameonesha katika kurasa hizi kwanza benki haijawa sawasawa. Kwa hiyo tumwombe sana Mheshimiwa Waziri asimame imara kuisaidia nchi yako. Tuna mategemeo mkubwa na yeye lakini safu yake na Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara yake, tunaamini kwamba wataisaidia Serikali hii ya Awamu ya Tano kwenda na fikira ambazo Mheshimiwa Rais anadhani na anafikiri ni vizuri kwamba siku moja baada ya kipindi chake nchi hii itakuwa imesimama yenyewe kwa miguu yake, lakini inasimamaje kwa miguu yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuondokane na fikira za kwamba Serikali inaweza kufanya biashara, Serikali kazi yake ni kusaidia miundombinu, kurahisisha mambo yaende ili sasa sekta binafsi nayo ichukue nafasi. Mfano ni huo kama nilivyotolea pale Dar es Salaam. Tulivyojenga miundombinu ya barabara. Leo mtu kutoka Kimara mpaka posta haizidi dakika 40. Ni mfano kama huo na iko mifano mingi ambayo itawekezwa. Hata Mheshimiwa Mwijage anapokuja na viwanda vyake vile vya mwendo kasi kama Serikali tutaifanya benki hii ya *TIB* iweze kuwa na nguvu basi



wale wajasiriamali tukiwemo Wabunge kama anavyosema viwanda vidogo tunaweza tukawekeza, kupitia benki hii tunaweza kwa mawazo yake Mheshimiwa Mwijage. Mheshimiwa Waziri wa Fedha akisaidiana kama Serikali na Mheshimiwa Mwijage naamini hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Wizara hii, mashirika wanayoyasimamia yakiwemo mashirika ya hifadhi ya jamii, yameonesha mfano nzuri sana katika kuwekeza. Nimwombe Mheshimiwa Waziri asimamie hilo, sekta binafsi na sekta ya umma lakini wanawekeza katika sekta binafsi naamini siku moja yatakuja kuwa mwarobani wa shida zetu na ajira za vijana wetu ambao wako na wanaosoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo katika huduma ya mfuko wa huduma ndogo za fedha, ukurasa 202, Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba watakopesha wajasiriamali vikundi vidogo vidogo vile bilioni 20, sijui wamefikia wapi, sijui wanakwenda kweli, au ndiyo tunakwenda kisiasa. Niwaombe sana wale watu wetu wa SACCOS za vijijini wana dhamira njema na kama tutawawezesha tutaondokana na mpango huu wa kuitegemea Serikali ituletee viwanda vya kutengeneza chaki kule katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mipango ndiyo kitu ambacho naamini kama kitaweka mipango iliyo sawasawa, chuo hiki kinatengeneza wataalam ambao wanaamini wao wataenda kufanya kazi tu Serikalini. Ni vizuri tukabadilisha mfumo na mawazo ya watu wanaotokana na chuo hiki waweze kuangalia na sekta binafsi ili waweze kutoa utaalam wanaoupata. Nchi hii ili iweze kwenda mbele kama nilivyosema ni lazima sekta binafsi kwa asilimia kubwa nayo ihusishwe. Mifano kwa nchi zote ambazo zimeendelea, leo tunalitolea mfano Taifa la India, wamehusishwa sana wananchi pia watu ambao wako nje ya nchi ile ambao wana nguvu ya kiuchumi wameitwa, wamekuja kuwekeza maeneo mbalimbali na sisi tunayo fursa hii, lakini Chuo cha Mipango kikifanya kazi hii kwa weledi naamini hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu pia kwa jitihada zinazosimamiwa na Wizara hii hasa katika suala la kulipa wazabuni ambao walikuwa wanahudumia katika taasisi za Kiserikali kama Magereza na maeneo mengine, leo wameanza kulipa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri waongeze juhudi kuhakikisha wale watu ambao walikuwa wanadai, wana madeni mbalimbali katika mabenki, wengine nyumba zao zimetaka kuuzwa na nyingine zimeuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili watu hao waondokane na hali hii, kwa sababu walikuwa wanaisaidia Serikali yetu, wakisaidia watu wetu, wakisaidia wafungwa wetu na pia Majeshi yetu, leo kwa kuwa wameonesha dalili ya kuwajali naomba tu waongeze nguvu ili watu hawa nao waweze kulipwa kwa wakati ili kesho na kesho kutwa mpango uende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru kwa nafasi hii ambayo umenipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Massare. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota baadaye Mheshimiwa Kiteto Koshuma, Mussa Bakari na Mheshimiwa Richard Mbogo wajandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na niungane na Wabunge wenzangu kwa kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii Mheshimiwa Waziri Mpango na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi pamoja na Kamshina wa Bajeti kwa kazi nzuri wanayoifanya Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utaanza na Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kama nilivyochangia wakati wa uchangiaji wa Wizara ya Kilimo ningeomba sasa benki hii ijikite kwenye mazao ya biashara. Kwanza benki hii ina tatizo la mtaji; kwa hiyo nashauri Serikali sasa iongeze mtaji wa benki hii vilevile bado matawi ni machache,

nilishauri kwamba miongoni mwa maeneo ambayo yanatakiwa benki hii sasa ipeleke nguvu zake ni Kanda ya Kusini ambapo kuna uzalishaji mkubwa wa zao la korosho na kama mnavyofahamu zao la korosho mwaka huu ni zao ambalo linaongeza kwa kutuletea fedha za kigeni. Limeingiza zaidi ya dola milioni 700 kwa hiyo ni zao ambalo siyo la kubeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba benki hii sasa ijikite katika kutoa mikopo ya muda mfupi ili wakulima wetu wa korosho waweze kuwa na uwezo wa kununua pembejeo. Mkulima wa korosho anahangaika na shamba lake wakati wa palizi lakini unapofika wakati wa pembejeo anahitaji kupewa msaada. Kwa hiyo, naomba benki hii sasa ifungue matawi Kanda ya Kusini ili itoe mikopo kwa wakulima wa korosho na isijikite tu kwenye mazao ya chakula, kwa sababu ukiangalia kwenye kitabu cha Waziri ambacho amewasilisha kwenye mnyororo wa thamani. Mazao ambayo yameorodheshwa pale ni mazao ya chakula kuna mahindi, mpunga kwa hiyo tunaomba twende sasa kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namba ya wakulima ambayo wamefaidika na benki hii ni wachache. Kwenye taarifa ya Waziri inaonesha kwamba ni wakulima 2,575, sasa hebu angalia nchi takriban asilimia 75 ya wananchi wanategemea kilimo, kwa kundi hili dogo ambalo limepata msaada ni kiasi kidogo sana. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri tuwe na mkakati kwanza tuongeze matawi tuongeze mtaji, lakini tuongeze na idadi ya wananchi ambao watafaidika na benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, utahusika na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii. Nizungumzie taasisi hiyo ya Uhasibu na nitajikita kwenye taasisi ya Uhasibu kwenye tawi la Mtwara. Taasisi hii ni nyeti na inatoa taaluma ambayo ni muhimu kwa sasa lakini mazingira ya kujifunzia na kujifundishia hasa kwa tawi la Mtwara hayaridhishi, hivyo naomba Wizara itenge fedha za kutosha

ili ukarabati mkubwa ufanywe kwenye taasisi hii na hasa tawi la Mtwara ambapo vyumba vya madarasa havitoshi, hawana hosteli za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto ambao wako pale wanahangaika kupanga mitaani na wanafunzi hususan wa kike si vema sana kwa sababu pale wanatoa *certificate*. Wengine wamemaliza *Form Four* juzi tu hawawezi kukaa nje ya familia yao, kwa hiyo wanafunzi wale wanaangaika. Ni vema kukawa na hosteli kubwa inayochukua wanafunzi wengi ili watoto wote ambao watapata udahili pale wakae katika mazingira ya Chuo cha Uhasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu nitajikita kwenye usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, hapa kwenye kitabu chake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atajikita katika kuimarisha Kamati za Ukaguzi kwenye taasisi mbalimbali, lakini nimsihi sio Kamati za Ukaguzi tu, hebu atuelekeze katika kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani hasa kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa, tutakuwa tumeokoa mambo mengi sana kwa sababu Mkaguzi wa Ndani ndiyo jicho la kwanza la Afisa Masuuli kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hivyo naomba tujikite katika kuimarisha Kamati za Ukaguzi lakini ofisi ya wakaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hali ilivyo sasa hivi kwa kweli inasikitisha, utakuta kwenye Halmashauri nyingine mkaguzi wa ndani ni mmoja hana gari, hana vifaa vya kufanyia kazi, kwa hiyo hawezi kufanya kazi yake vizuri, akitaka kwenda kukagua usambazaji wa madawa na utoaji wa huduma katika zahanati anamwomba msaada *DMO*, sasa yule mkaguliwa ndiyo anampa posho, anampa gari, hata nguvu ya kukagua pale inapungua. Kwa hiyo, naomba

Wizara sasa ijikite licha ya kuangalia tu Kamati za Ukaguzi tuangalie na kitengo hicho ambacho ni muhimu na nyeti katika kudhibiti matumizi ya fedha zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu katika suala la Usimamizi wa Fedha za Serikali tuingalie kwa jicho la pekee Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mwaka jana tullona alivyofanya kazi nzuri, alikagua taasisi nyingi lakini fedha hakupewa kwa wakati. Kwa hiyo ilibidi aji-*stress*, naomba CAG apewe fedha za kutosha lakini siyo za kutosha tu, bali kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi una misimu yake, ukimpa CAG fedha kuanzia Januari hazimsaidii sana, kwa sababu wakati ule na timu yake wanajifungia mahali kwa ajili ya *report writing*. Tujitahidi kutoa fedha za kutosha kama ilivyo kwenye bajeti yake kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, tukifanya hivyo tutakuwa tumemsaidia CAG na atafanya kazi yake kwa ufanisi na atakuwa amekwenda kuangalia fedha zetu ambazo tumepeleka katika miradi yetu ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine utajikita kwenye uhakiki na ulipaji wa madeni ya Watumishi wa Umma na Wazabuni. Kama walivyosema wenzangu kwamba tuongeze kasi ya uhakiki wa haya madeni. Kwenye taarifa pale imeonekana kwamba tumeshaanza kulipa madeni ya wazabuni, kwenye deni la trilioni tatu tumelipa milioni 796. Ningeomba Serikali yangu isiwe chanzo cha kuu mitaji ya wafanyabiashara wadogo, tulipe madeni kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulipe madeni ya Watumishi kwa wakati ili kuongeza morali kwa watumishi. Watumishi wakilipwa stahili zao morali inaongezeka, lakini madeni kwa watumishi yasipolipwa kwa wakati kwanza yanafifisha ari kwa watumishi na hivyo mtumishi anakwenda kazini wakati hana ari ya kufanya kazi. Kwa hiyo, naomba kwenye trilioni tatu kwa sababu tumeana kulipa milioni 796

basi tujitahidi ili tulipe deni hili ili wazabuni waweze kutoa huduma lakini na watumishi waweze kufanya kazi ili tuliyoitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho unahusu mfuko wa huduma ndogo za fedha (*microfinance*) na hii ni taasisi muhimu sana. Nchi za wenzetu wanawapa kipaumbele sana *SMEs*, kwa hiyo na sisi hizi taasisi za *microfinance* hebu tuzipatie fedha za kutosha na tupunguze mifuko. Kwenye Mfuko wa Uwezeshaji tumeambiwa kuna mifuko 19, sasa ile mifuko ni mingi sana. Tupunguze tuwe na mifuko miwili au mitatu ambayo itatoa huduma ambayo inajulikana na wananchi watakuwa na taarifa za kutosha. Kwa hiyo, itakuwa wanapohitaji mikopo midogo midogo au uwezeshwaji wanakwenda kwenye taasisi hizo na kuhudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chikota. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niendeleo kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu lakini niendeleo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunjalia afya njema ili niendeleo kutoa michango yangu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Fedha ninaomba nianze kwa kuchangia suala la ukusanyaji wa mapato. Ni jambo ambalo nimekuwa nikilifikiria sana pamoja na kulifikiria hata Mheshimiwa Rais amewahi kuliongelea katika kampeni zake na hata wakati wa kufungua Bunge hili. Suala hilo ni suala la wafanyabiashara kuombwa kulipa kodi wakati hata biashara yenyewe hajaianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo imani kubwa sana kwamba Wizara ya Fedha ndiyo Wizara ambayo inahusika

kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu makusanyo haya ya mapato ya kodi yanakusanywa na TRA. Mfanyabiashara kama hajaanza biashara yake amechukua mtaji wake, anaanza biashara, maana yake ni kwamba anaanza kwanza kwa kulipia kama ni chumba cha kufanyia biashara, pili anaweka bidhaa anazotaka kuziuzua. Sasa kama mfanyabiashara huyu unaanza kumwambia kwamba alipe kodi kwanza ndipo aendelee na biashara yake ina maana pesa hiyo anaitoa kutoka kwenye mfuko wake ambao ndio mtaji wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninaona kabisa suala hili ni kuwadhulumu wafanyabiashara na sio tu kuwadhulumu bali ni kuwafanya wafanyabiashara wasiwe na moyo wa kulipa kodi. Ndio maana unakuta hapa Tanzania unaona watu hawana moyo wa kulipa kodi. Sio kwamba wafanyabiashara hawataki kulipa kodi, wanapenda sana kulipa kodi lakini kama mtu unataka kuanza biashara unaenda kuomba leseni kwenye Halmashauri, Halmashauri wanakwambia hatuwezi kukupa leseni pamoja na kwamba umejaza fomu mpaka utuletee *tax clearance*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linawaumiza sana Watanzania na mimi sitapenda kuona watanzania wakiendelea kuumia kwa sababu wanaoumia ni wafanyabiashara wale ambao ni wadogo wadogo ambao pesa zao wanazipata kwa taabu sana, halafu anapokuwa amepata mtaji wake ili aanzishe biashara Serikali na yenyewe inasogea inaanza kumwambia lipa kwanza kodi ndio uende kufanya biashara. Kwa akili tu za kawaida, hata hazihitaji uende darasani, hivi unawezaje mtu ukaanza kulipa kodi kabla hata biashara yenyewe hujaiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa sana kwamba nifikungua biashara yangu nikaanza kuifanya ndipo mtu anijije aniambie lipa kodi, kwa sababu moja kwa moja nitakuwa nimejua baada ya zile *administration cost* na

*operation cost*, sasa faida yangu ni kiasi gani. Kwa hiyo, hata ukija kuniuliza mapato yangu ninayajua kwa kichwa kwa sababu tayari nimeianza biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri sana Serikali iweze kuangalia na kutekeleza kwa sababu hili ni agizo la Mheshimiwa Rais. Wakati Mheshimiwa Rais anazunguka kwenye kampeni yake, alikuwa anaongea kwa uchungu sana na mimi namwamini sana Mheshimiwa Rais nikiamini yeye anayo nia ya kuwasaidia watanzania ambao ni wa hali ya chini, namwamini sana Mheshimiwa Rais. Sasa sisi watendaji ambao tunamsaidia Mheshimiwa Rais hatupo tayari kumsaidia kwa sababu yale anayoyasema hatuyaweki kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii, Mheshimiwa Waziri wa Fedha uweze kufanyia kazi masuala ya *TRA* kuanza kukusanya kodi wakati mfanyabiashara bado hajaanza kufanya biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kuhusu suala la shilingi milioni 50 katika kila Kijiji. Sitawahi kukaa ninyamaze hata siku moja kwa sababu mimi ni mwakilishi wa wanawake na kila siku nimekuwa nikisema mimi ni mwakilishi wa wanawake sio tu Mkoa wa Mwanza bali Tanzania nzima. Shilingi milioni 50 katika kila kijiji ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Waziri wa Fedha ameeleza kabisa mwanzo kabisa wa ukurasa wake kwamba anatengeneza bajeti hii kutokana na mambo mengi tu lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi ndio ambayo inamuelekeza ni namna gani aweze kutekeleza bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shilingi milioni 50 kila kijiji sielewi nianzie wapi, nikiangalia katika kitabu hiki cha Waziri sijaona ni sehemu gani inaonekana shilingi milioni 50 kila kijiji itatoka. Mwaka jana nilisimama hapa hapa Bungeni kwa kutumia kitabu hiki cha Wizara ya Fedha cha mwaka 2016/2017 shilingi milioni 50 katika kila kijiji ilikuwepo, ilikuwa imetengwa. Nashukuru kwamba Kamati imeweza kutusaidia kutuonyesha kwamba katika mwaka wa fedha 2016/2017



shilingi milioni 50 kila kijiji ilikuwa imetengwa shilingi bilioni 59 na kwa mwaka huu wa fedha Kamati imetuambia kwamba katika ukurasa wake wa 20, Kamati inaeleza kabisa wazi pale kwamba...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kamati imeeleza ukurasa wa 20 kwamba shilingi bilioni 59, zilizotengwa 2016/2017 bado hazijatoka lakini kwa sasa Kamati imeeleza kwamba shilingi bilioni 60 sasa imetengwa kwa ajili ya kutekeleza suala la shilingi milioni 50 katika kila kijiji.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Taarifa hii sio ya bajeti...

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Nashangaa sana Mheshimiwa Mbunge sijui anataka kunipa taarifa gani, sijamuelewa, kwa sababu gani, suala ninaloliongea lipo katika kitabu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo mimi najitahidi kuhoji hapa ni kwamba kwa nini kamati imeeleza kwamba shilingi bilioni 60 imetengwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, lakini katika kitabu chake cha Wizara shilingi bilioni 60 siioni. Kwa hiyo, naomba atakapokuja kusimama pale kuhitimisha hoja yake Mheshimiwa Waziri aweze kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba hii shilingi bilioni 60 ambayo Kamati ya Bajeti inaiongelea kwenye kitabu chake ipo ukurasa wa ngapi, aweze kutuelezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda wangu haujaisha ninaomba niseme kwamba pamoja na kwamba hii shilingi milioni 50 kila kijiji imeelekezwa, lakini hizi fedha kama tutakuwa tunazitenga kila mwaka halafu haziendi, ninaiomba Serikali wakati wanakuja kuhitimisha watueleze ni lini itaanza kwenda. Tumekuwa tukijibiwa humu majibu, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiuliza maswali mara

kwa mara na kujibiwa kwamba fedha hizi zitaanza kupelekwa pale ambapo utaratibu utakuwa umekamilika wa kupeleka fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi sasa hivi ukiniuliza tuanze na mradi gani, tupeleke katika vijiji gani, tupeleke katika Mikoa gani, ninaweza nikaisaidia Wizara ya Fedha. Hii ni kwa sababu mwaka jana wakati tunajadili hapa bajeti kuna mikoa ilitajwa kwamba ni Mikoa maskini, ikiwemo Kagera na Kigoma. Tunaomba Wizara hii ilipokuwa imeeleza mwaka jana kwamba wataanza na mikoa mitatu ambayo itakuwa ni mikoa ya *pilot study*, tunaomba basi hiyo mikoa mitatu watuambie ni Mikoa gani na kama wameshapeleka watueleze ni Wilaya zipi na kama wameshapeleka watueleze vijiji gani ambavyo vimepata pesa hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaamini kwamba Watanzania watakuwa wamesikia ni kwa namna gani nimeweza kuwawakilisha katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tena niweze kuongelea suala la *allocation* ya bajeti, naamini Wizara hii ndiyo inahusika katika kuandaa bajeti, katika kuweka *allocation* ya *resources*. Suala la *allocation* ya bajeti naomba iwe inaangalia zile Wizara ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya Watanzania. Naomba niishauri Serikali inapokuwa inaweka *allocation* ya bajeti, iangalie Wizara ya Maji. Wizara ya Maji iwekewe fedha za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa Wizara ya Maji ikiwekewa fedha za kutosha wananchi wakipata maji wataweza kulima, baada ya kulima ndipo tutaweza kuanza kuongelea viwanda. Hatuwezi tukaanza kusema viwanda wakati hata kilimo hatukioni. Kilimo hakina dira kabisa, hatuwezi kulima kwenye ardhi ambayo ina ukame... (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa, naomba ukae kidogo...

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti .....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto naomba ukae tusikilize taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji, hii sio bajeti, sio kitabu cha bajeti, hii ni bajeti ya Wizara ya Fedha sio bajeti ya nchi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio bajeti ya nchi kusema kwamba wametenga kiasi fulani, tuchangieni Wizara ya Fedha kama Wizara nyingine. Hii ni bajeti ya Wizara ya Fedha, siyo bajeti ya Serikali Kuu, hii sio bajeti. Muwe mnachangia inavyotakiwa sio kuchangia hovyoya hovyoya.Changieni jinsi inavyohusika siyo kuchangia hovyoya.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Keissy.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Namna gani ninyi! Mnaropoka ropoka tu huko.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Keissy naomba ukae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Keissy *ambulance* hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini unapokuwa Mbunge, unapokuwa kiongozi katika nchi hii, lazima ujitofautishe. Ninamshangaa sana Mheshimiwa Keissy kwa sababu haelewi kitu anachokiongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeenda shule, hivi Hazina *accountability* yake iko wapi? Si ipo kwenye Wizara ya Fedha? Sasa unaponiambia kwamba hii shilingi bilioni 50 haihusiki katika Wizara hii, naomba niikatae taarifa yake na niendeleo na mchango wangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie nina dakika tano ambazo Mheshimiwa Keissy amenipotezea...

**MWENYEKITI:** Una nusu dakika Mheshimiwa.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kuchangia suala la Benki ya Wanawake. Nimekwisha kujitambulisha mimi ni Mbunge na mwakilishi wa wanawake Mkoa wa Mwanza na Tanzania nzima. Suala la Benki ya Wanawake tumekuwa tukilipigia kelele sana humu ndani. Nitaendelea kusema nina amini Wizara ya Fedha ndio ambayo inahusika kupitia Hazina. *Treasury* ndiyo wanahusika kupeleka fedha, walioenda shule wote watakuwa wananielewa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali itusaidie kupeleka fedha katika benki hii ili kuiongezea mtaji ili wanawake waweze kukopa kila sehemu. Matawi yawepo Tanzania nzima ili wanawake waweze kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika zangu mbili kuhusu suala la malipo ya watu ambao walikuwa wanafanya kazi Afrika Mashariki. Ninaamini suala hili la watu ambao walikua wanafanya kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki linamgusa kama sio mimi, litakugusa wewe na litamgusa Mbunge mwingine... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk na baadae Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Oran Njeza wajjandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo kama manne hivi, nitazungumzia kwanza suala la *road licence* na *motor vehicle*, lakini nitazungumzia pia udhaifu na uchakavu wa fedha zetu, vilevile udhaifu wa *EFD receipts* na utozwaji kodi mara mbili pale unaposhusha mizigo Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema nikaweza kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Vilevile niungane na wenzangu kuwatakia waislamu wenzangu wale ambao tunafunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani na wasiofunga pia Mwenyezi Mungu awafanye wavae vizuri kusudi tuweke swaumu zetu sawa. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Baada ya kusema hayo niseme tu kwamba palikuwa na utaratibu hapo zamani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kutoa taarifa ya makusanyo ya fedha kila mwezi, lakini mpaka sasa hivi hatujui utaratibu umepotelea wapi. Hili tunaliona ni tatizo, namshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha utaratibu ule uendelee, kila mwezi *TRA* inapokusanya fedha tupewe taarifa za mapato ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia *road licence*, hii ni kodi ambayo inalipwa kwa vyombo vinavyotumia barabara. Baada ya wananchi kulalamika

tulibadilisha tukaletewa *motor vehicle* lakini sasa kinachotushanganza *motor vehicle* inakuwa inalipwa hata kwa vyombo ambavyo vimeshakufa zamani au vimepata ajali na havipo barabarani kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali *motor vehicle* badala ya kushikwa katika vyombo ambavyo hata vimekufa au havipo barabarani basi sasa hivi *motor vehicle* tuingize kwenye mafuta ili iwe chombo kinachotumia mafuta moja kwa moja kiwe kinalipa kodi ya Serikali, lakini kulipisha kodi chombo ambacho pengine kama ni gari limeshakufa au lipo *garage* miaka mingi au limeshatengenezwa majiko ya kupikia huko lakini bado linatozwa kodi, hii ni dhuluma ya mchana kweupe. Kwa hiyo, naishauri Serikali tuingize kodi ya *motor vehicle* kwenye mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kodi nyingine naishukuru Serikali kwamba imeondoa *motor vehicle* katika pikipiki, lakini cha kushangaza pikipiki imewekewa kuna kitu kinaitwa *fire extinguisher*. Ukienda TRA unalipishwa shilingi 10,000 unapotoa shilingi 10,000 kwanza unaelekezwa ukalipie *Max Malipo*, risiti unapewa *Max Malipo* lakini hupewi hiyo *fire extinguisher* yenyewe. Sasa hii nayo ni dhuluma ya Serikali kwa wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, ndugu zangu wa bodaboda na wamiliki wa pikipiki nafikiri mtaona jinsi gani Wabunge tunavyowatetea katika Bunge letu hili. Kwa hiyo, naishauri Serikali *fire extinguisher* katika pikipiki nayo iondolewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kuzungumzia suala hili la *motor vehicle* na *road licence* jirani zetu Kenya hapa hawana. Kenya unalipia *insurance* ime-*contain* vitu vyote, lakini Tanzania kuna kodi lukuki mpaka tunawachanganya Watanzania, tunawachanganya wafanyabiashara. Naomba ikibidi hili suala la *motor vehicle* viondolewe pia. Vilevile pia tuige kwa wenzetu kwa sababu kama ikiwa kumbe unapolipa *insurance* unaweza ukawa umelipia vitu vyote na sisi tungeiga mfano wa wenzetu Kenya

kwa sababu ni jirani zetu na katika baadhi ya mambo ni kama walimu wetu. Kwa hiyo, nafikiri hilo litakuwa limeeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuzungumzia ni suala la wafanyabiashara kulipishwa kodi kabla hawajafanya biashara, hii nayo mimi naona ni dhuluma ya wazi. Ilikuwa kwanza Watanzania kuna kitu unataka kufanya biashara unaambiwa ufanyiwe *assessment*, wakati kodi inatakiwa ulipe baada ya kupata faida, Watanzania walipolalamika wakaletewa kitu kinaitwa hiyo *assessment* lakini unailipa kabla hujafanya biashara. Sasa wenzetu Kenya unapewa *tax holiday* ya karibu miezi sita, ina maana ufanye biashara, uwe umejiweka vizuri lakini wakati huo huo unapitiwa katika vitabu vyako, na sisi tuombe Tanzania tuwaige wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini mtu kabla hajafanya biashara unamlipisha kodi, hii ni dhuluma vilevile kwa wafanyabiashara. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwaache wafanyabiashara pale wanapotaka kufanya biashara kwanza wafanye biashara, baadaye Maafisa wa *TRA* wakakague vitabu vyao ndiyo watoze kodi, lakini Tanzania tunakwenda kinyume kabisa, matokeo yake biashara nyingi zinafungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tulisikia taarifa ya Wizara ya Fedha, kwamba kuna biashara zaidi ya 300 Dar es Salaam zimefungwa, yaani katika mafanikio ya Wizara ya Fedha ni pamoja na kufungia biashara 300 ambazo hazilipi kodi. Mimi nasema haya sio mafanikio, haya ni matatizo. Hizi biashara zinapofungwa zimeondoa Watanzania wangapi katika ajira, zimewafanya watu wangapi maskini? Hata mfanyabiashara mwenyewe anakuwa hana kipato tena, ina maana unahatarisha maisha yake kwa kumkosesha kupata mkate wake wa kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wananchi kulalamika sana, kuna kitu kililetwa kinaitwa *presumptive tax*. Hii *TRA* waliweka kwamba yeyote anayeza kuanzia shilingi

milioni nne mpaka shilingi milioni saba na nusu anatakiwa alipe shilingi 150,000 kwa mwaka, na anayeuzua shilingi milioni 16 mpaka shilingi milioni 20 alipe shilingi 862,000. Sasa mtu analipaje fedha zote hizi kabla hajafanya biashara? Naishauri Serikali, kwanza tuwaache wafanyabiashara wafanye biashara halafu ndiyo tushike hizi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine pia twende mbali zaidi, hizi *assessment* zinakuwa ni kubwa sana, naishauri Serikali tungetumia ile *third law of demand, in the high price low demanded, in the low price high demanded*. Sasa sisi hatuendi huko, matokeo yake tunakosa fedha nyingi katika makusanyo ya kodi kwa sababu kodi zetu sio rafiki kwa wafanyabiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni *EFD machines*. Mashine hizi kwa kweli ni utaratibu mzuri, lakini hapa kwetu Tanzania utaratibu huu tumeukosea. Kwanza, haioneshi kuwa mfanyabiashara aliuzua kwa mkopo kwa mteja au anaporudishiwa mali endapo ina dosari risiti ile inamsaidiaje, mwisho wa mwaka anapofanya mahesabu inakuwa ni usumbufu na matatizo makubwa. Vilevile *EFD machines* zinafutika haraka, sio za madukani tunaponunua bidhaa wala kwenye *ATM* unapokwenda kutoa fedha benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunatunza vitabu vyetu vya mahesabu ikiwa risiti ndani ya siku nne mpaka saba imefutika, mimi nasema huu ni sawasawa na utapeli, kwa sababu kama inavyosemekana kwamba unapokuwa una risiti ndiyo unajua pia takwimu zako za makusanyo zikoje, sasa sisi risiti zetu mbovu. Niliwahi kuwauliza wataalam wa *TRA* wakasema *quality* ya zile karatasi za risiti zipo *grades* tatu, sasa kwa nini tuweke *grades* tatu kama sio utapeli huu, kwa nini tusiweke *grade* moja tu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, risiti za *EFD machines* ikibidi zibadilishwe ziwe za *plastic material* kwa sababu zitakuwa hazifutiki, kama vile ambavyo fedha ya



Msumbiji ilivyo, ni ya *plastic*, hata uichovye kwenye maji haifutiki. Kwa hiyo, nashauri *EFD machine receipts* ziwe za *plastic*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhaifu wa fedha zetu, fedha zetu za Tanzania zinatia aibu, nchi kama sisi wenye historia kubwa na pana duniani lakini ukishika shilingi 50, ukishika shilingi 100 ya *coin*, ukishika shilingi 500 ya noti, ukishika shilingi 1,000, ukishika 2,000 aibu tupu. Pesa ya noti ikipita kwa muuza mkaa, ikaenda kwa muuza samaki, ikiingia kwa muuza juisi hapo ndipo *wabillahi taufiq* na mchezo umekwisha! pesa imeoza, haifai hata kumzawadia mtu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, narudi tena, tuitazame dola *material* yake ilivyo, tuitazame *Riyal* ya Saudi Arabia jinsi ilivyo, lakini pia tuiangalie pesa ya nchi kama Msumbiji ambayo tumechangia katika kuitetea kupata uhuru, leo wana fedha bora kuliko fedha yetu ya Tanzania, hii ni aibu. Kwa hiyo naishauri Serikali, tuboreshe *material* ya fedha zetu tunazotumia kila siku. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nizungumzie suala la mafao ya wazee wetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mussa, muda wako umemalizika.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** ...atakapokuja Mheshimiwa Waziri atuambie, deni la wastaafu wa Afrika Mashariki litakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunisikiliza. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika tafadhali naomba, umeeleweka, ahsante. Tuendeleo na Mheshimiwa Richard Mbogo baadae Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru Mungu kwa nafasi hii na pia nimpongeze Waziri na timu yake kwa kazi ambayo wameweza kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza na Mamlaka ya Mapato (*TRA*), suala la *EFD*. Niliwahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba *TRA* katika kudhibiti mapato na kuweka uwazi, Serikali ilianzisha *EFDs* na *ESDs*, lakini kilichopo ni kwamba tuna matatizo ya kimtandao kwenye hizi mashine, kwa hiyo tunaomba *TRA* iweze kuangalia. Katika uhasibu tunajua katika kurekebisha mahesabu ya kiuhasibu unatoa *credit note* au *debit note*, sasa hizi *signatures* hazichukui taarifa za marekebisha ya kiuhasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililopo *TRA*, tunapata malalamiko sana kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu wanavyofanya makadirio. Wenyewe wako ofisini lakini na mteja mwenyewe ndio anajikadiria kama anavyotakiwa kufanya, lakini wanakadiriwa kwenye hali ya juu tofauti na uhalisia wa biashara walizonazo. Kwa hiyo, tunaomba *TRA* waangalie ikiwezekana waangalie na hali halisi ya biashara mtu anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Wizara hii ni kufuatilia mapato, lakini tunaomba, bajeti ya mwaka jana tumezungumza, kuna ripoti nyingi na Kamati ziliundwa na Bunge hili huko nyuma na maarufu sana ripoti ya Mheshimiwa Chenge, kuna *Chenge One* na *Chenge Two*. Sasa hizi mpaka sasa hivi kama Wizara wamefanyia kazi kiasi gani? Tunaomba Wizara zote kwa ujumla ziweze kufanya mawasilisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa *property tax* ni majukumu ya *TRA*, lakini nimeangalia katika

*website* katika ripoti yao makusanyo wameweka mwezi Novemba, 2016 tu, sasa je, mpaka sasa hivi wamekusanya kiasi gani, tutaomba Waziri wakati wa majumuisho utueleze upande aw *property tax TRA* wameweza kufanikisha kiasi gani kwenye makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia kwenye ripoti za *TRA* kuna maeneo *VAT* baadhi ya *categories* sijaona wameripoti makusanyo, je, hatuna makampuni yanayo-*fall* kwenye hizo *categories*? Kwa mfano *electrical products, aluminium, motor vehicle spares and bicycle*, sijaona kwenye *VAT on local*, hawajaripoti. Kwa hiyo, tutaomba tupate kujua nini wanachotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uandaaji wa mahesabu, *TRA* wakija kukagua kuna wakati wanahitaji ushahidi wa risiti, lakini sasa hivi dunia imekuwa inaenda kimtandao zaidi. Kwa mfano, unaweza kulipia umeme, kununua *airtime* kwa kutumia Tigo Pesa, M Pesa, sasa unavyoandika mahesabu yako unaweka *reference* ipi ambapo yeye *staff* wa *TRA* atakuja aridhike kwamba kweli muamala huu uliufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaomba Waziri haya malipo ya sasa hivi ya miamala kwenye gharama zetu za uendeshaji atueleze Serikali wataridhika kwa maandishi yoyote ambayo mtu atasema alilipa kwa *Tigo Pesa, M Pesa, Halopesa* au *Airtel Money* au kwa njia nyingine za kibenki kwa njia ya simu, kwa hiyo tutaomba utueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafao, watumishi wa Posta walipandishiwa mafao toka shilingi 50,000 mpaka 100,000 Julai, mwaka 2015 lakini kuna baadhi mpaka sasa hawajaanza kulipwa. Waziri, tutaomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *PPRA*, tuna Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011, kuna kipengele cha 77(4) mambo ya *liquidated damage* na ukienda kwenye *regulation* ya mwaka 2013 naomba *PPRA* watupe mwongozo mzuri, wanavyoandaa zile *Standard Tender Documents*

kwenye *general conditions* zinatofautiana kabisa juu ya *liquidated damage* na sheria mama pamoja na kanuni. Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri tutahitaji majibu kwa nini zinatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia bajeti ya Wizara ya Kilimo, nilizungumzia kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Serikali mpaka sasa haijaongeza mtaji, Mheshimiwa Waziri tutaomba utuambie ni lini Serikali itaongeza mtaji kulingana na maazimio ambayo yamekuwa yakizungumzwa huko nyuma. Pia hii Benki ya Maendeleo ya Kilimo ndiyo ambayo itasaidia mtaji kwa wakulima na tunajua asilimia 67 ya wananchi wanajishughulisha na kilimo, sasa malengo ya hii Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na juhudi miaka yote, tulikuwa na *CRDB*, haikufanya vizuri matokeo yake imekuwa benki ya kibiashara. Huko nyuma baada ya uhuru tulikuwa na *Agricultural Credit Agency* iliweza kutoa matrekta. Sasa leo hii benki hii ya kwetu na niliangalia kwenye *website* yao kwamba wanapata fedha kutoka *African Development Bank*, je, wamekwishapata hizo fedha? Kwa mfano, Jimboni kwangu nina wakulima wa tumbaku, wanatarajia wakope fedha kwa ajili ya shughuli zao katika riba ambayo itakuwa ni ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia kuhusu *Tanzania Investment Bank*, hii inamilikiwa na Serikali, ni kweli kuna benki kama *NMB* Serikali ina asilimia 31 ya hisa lakini je, taasisi nyingine za Serikali zinashawishiwa vipi kwenda kufungua akaunti huku *TIB* ili waongeze mzunguko wa fedha na ndiyo benki ambayo inasaidia hata mashirika yetu. Kwa mfano *TRL* wamekopeshwa fedha na *TIB* wameweza kuinua *operations* zao. Kwa hiyo, ni jinsi gani sasa pia taasisi nyingine za Serikali ziweke fedha zao *TIB* na pia na yenyewe iweze kukua kama ambavyo tunasisitiza upande wa *NMB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri pia atakapokuja, katika kitabu chake amezungumzia kuhusu mitaji inayozidi, nafikiri hizi ni taasisi mbalimbali za Serikali

ambazo sasa hivi zinapeleka fedha zake *BOT* baada ya kuondoa zile gharama sasa ni mitaji inayozidi. Mpaka Machi, wameweza kupeleka ziada shilingi bilioni 182 ambayo ni sawa na asilimia 24.1 lakini malengo ikiwa ni shilingi bilioni 756, tuna upungufu wa shilingi bilioni 574.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba hii mitaji inayozidi tumezungumza humu tunaomba tulenge kwenye maji. Tuweke kwenye upande wa maji ili Wizara ya Maji na Umwagiliaji ipate vyanzo vingine vya fedha yenye uhakika kwenye hii mitaji inayozidi, iende kwenye maji ambacho ndicho kigezo kikubwa ambacho wananchi wetu wanataka kukiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye madeni ya huduma mbalimbali pamoja na watumishi. Kumekuwa na malalamiko sana, wafanyabiasara wengi wanadai Wizara zetu miaka mitano, miaka minne, mpaka sasa hawajalipwa. Sasa Serikali kulipa haya madeni ya ndani tutaomba Waziri utuambie una mkakati gani juu ya kulipa madeni ya ndani? Kuna watu wamefanyakazi walikopa, wamekuwa-*charged* riba, kuna wengine wamepeleka mpaka kwenye Mahakama ya Kibiashara, Serikali ina-*charge interest*, sasa hizi gharama za Serikali kuendelea kuchajiwa riba kwenye haya madeni, Serikali ina mpango gani wa kulipa haya madeni ya ndani ili na mzunguko wa fedha katika nchi yetu uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali (*CAG*). *CAG* amefanya kazi nzuri sana na ameweza kutoa ripoti mbalimbali na vitabu tumeviona. Mimi tu nitoe ushauri kwa upande wa Ofisi wa *CAG*, kuna baadhi ya watendaji katika *auditing* yao nimewahi kuwauliza, nilikuwa kwenye Kamati ya *LAAC*, wakati wa *audit* tunajua *audit is all about analytical review*, kuna baadhi ya watendaji hawafanya *analytical review* na ndiyo *audit* inapo-*base* hapo. Unaweza kulinganisha, ukilinganisha tu mahesabu ya miaka miwili/mitatu na maongezeko, pale unaweza kujua kwamba hapa kuna upungufu kiasi gani au udhaifu kiasi gani, kwa hiyo niombe Ofisi ya *CAG* hili waweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Ofisi ya CAG teknolojia ya sasa hivi ime-*advance*, kampuni nyingi za *auditing* kama *KPMG, PWC, Deloitte & Touche* na wengine, wameweza ku-*advance* kwenye *technology* wana-*audit*, wanasambaza mafaili, sasa na hii Ofisi yetu ya NAO na yenyewe huku Serikali itoe fedha ya kutosha na kwa wakati ili wapate *training* na kuwekeza kwenye *technology*. Kwa hiyo, uwezeshaji upande wa Ofisi ya CAG uendelee kuwezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo pia kwa wakaguzi wetu, kwa mfano upande wa Halmashauri wanakagua miradi ya maendeleo, wanajua kusoma vizuri *BOQ (Bill of Quantities)*, wanajua kulinganisha? Kuna mahali unakuta kuna *variation* unakuta Ofisi ya CAG *know how* inakuwa haipo, tunaomba waweze kupata mafunzo kwenye hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *today I am too very faster*. Jambo lingine naomba nirudi upande wa TRA, huko nyuma mtu alikuwa akisimamisha biashara anaambiwa andika barua, lakini sasa hivi wanasema sheria ilikuwa haisemi vile, lakini ndani ya Taasisi hiyo ya TRA wanakwambia unatakiwa ulete *nil return*, halafu mtu anaku-*penalize* karibu shilingi milioni 15, shilingi milioni 20 na mtu hakufanyiabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba huku TRA kama mtu hakufanya biashara na mlimbwambia aandike barua, leo hii mnamwambia alitakiwa alete *nil return, how come* ofisi hiyo inatoa maelekezo mawili? Basi hawa watu wasamehewe, kama Waziri kwa mamlaka yako tutaomba utoe maagizo watu ambao hawakufanya biashara na leo hii wanakuwa *assessed* kodi pamoja na *interest* na ma-*penalty* waweze kusamehewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kidogo tu kwenye sehemu ndogo ya mapato pamoja na udhibiti wa matumizi ya pesa za umma. Kama alivyosema mwenyewe Waziri kwenye ripoti yake ukurasa wa 25 ya kwamba jukumu lake kubwa ni pamoja na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali, jukumu hili ni muhimu sana kwa sababu ukisimamia vizuri matumizi na kukawa na *cost saving*, nayo inakuwa ni sehemu ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uzoefu wangu kwenye Halmashauri zetu, nimeona upotevu mkubwa sana wa pesa kwenye matumizi ambayo sio yaliyolengwa. Waziri amezungumzia kuhusu kuimarisha ukaguzi wa ndani, ukaguzi wa ndani ni kitengo muhimu sana kwenye Halmashauri, lakini ukiangalia nafikiri Wizara ina wataalam wengi wa mambo ya uhasibu, itakuwaje Mkaguzi wa Ndani amkague Mkurugenzi halafu yeye aripoti kwa Mkurugenzi, unategemea hiyo ripoti ya Mkaguzi wa Ndani itakuwa na maana yoyote? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa *experience* tulizonazo huku kwenye Halmashauri zetu. Pesa nyingi zinazokwenda kwenye Halmashauri ambazo ni sehemu kubwa sana ya mapato zinapotea. Kwenye Halmashauri yangu tuna Mkaguzi mzuri sana, ameleta ripoti nzuri sana na bahati nzuri Madiwani wakazifanyia kazi, baada ya kuzifanyia kazi yule Mkaguzi wa Ndani akaonekana kuwa hakutenda jema kwa sababu aliweza kuwaambia Madiwani uovu ambao umekuwa ukifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi katika suala la usimamizi, hata yule aliyekuwa Mhasibu wa ile Halmashauri naye alipata matatizo, baada ya kuandika ripoti kuwa tuna matatizo ya matumizi ya pesa aliamishwa kupelekwa kijijini kutoka Halmashauri. Fikiria Serikali imemsomesha mtu kwa kiwango cha *CPA*, ndiye Mhasibu wa Halmashauri, kwa vile

tu ameandika ripoti ambayo inaeleza maovu kwenye Halmashauri anahamishwa ili waendelee kuficha yale maovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba hiyo Wizara yako kwa vile inasimamia matumizi bora ya hizi rasilimali, iweke hili kama chanzo kimoja wapo cha mapato ya Serikali kwa sababu tukikusanya pesa tena kwa shida kabisa zikaenda kutumika sehemu ambazo hazikulengwa, hayo mapato yote ambayo tunakusanya yanakuwa ni kazi bure. Naomba sana tuimarisha ukaguzi wa ndani. Vilevile, umezungumzia kuhusu Kamati za Ukaguzi kwenye Halmashauri zetu, hizi Kamati za Ukaguzi hatuzioni, ambazo nazo ni chombo muhimu sana cha kusimamia mapato na matumizi ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la vyombo vya fedha kusaidia katika kilimo, hasa hii Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Wabunge wengi hapa wamechangia kuhusu mtaji mdogo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo, kuna mchangiaji hapa kaongelea kuhusu shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Sasa nilichokuwa najaribu kuangalia, labda na kuishauri Wizara, kwa nini kama kuna hiki chombo ambacho ni kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kikapewa nafasi ya hizi pesa ambazo ni shilingi milioni 50 kwa ajili ya kila kijiji wakapewa, sio lazima iwe mtaji, ila wao wakawa ni wakala wa Serikali kwa sababu hizi pesa nazo ambazo zitakwenda huko ni kwa ajili ya kukopesha wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo, kwa hiyo zinahitaji usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo ni mahala pazuri na itapata nafasi hata ya kuweza kujitana kwenda mahali mbalimbali hapa Tanzania. Ningeomba hizi milioni hamsini hizo hata shilingi bilioni 60 ambazo sasa hivi zimezungumziwa kuwa zitatolewa mwaka huu pamoja na zile shilingi bilioni 52 ingepewa Benki ya Kilimo ili iweze kuanza kufanyia kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni masoko kwa ajili ya wakulima. Kuna chombo ambacho kilikuwa



kinazungumzwa kuwa kingeanzishwa (*commodity exchange*), sijaiona katika hii *report* labda kwa ajili yakuangalia haraka kama imezungumziwa, lakini kwa wakulima hiki ni chombo muhimu sana. Wakulima wetu wanalima sana na wakati wa mavuno bei zinakuwa chini, tungekuwa na chombo kama hiki kingetusaidia sana kuhakikisha kuwa bei za mazao yetu zinakuwa *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Msajili wa Hazina. Naomba sana tena sana Wizara ijaribu kuimarisha hiki kitengo cha Msajili wa Hazina vilevile wapewe bajeti ya kutosha. Kwa sababu kwa mchango wao mwaka huu wa shilingi bilioni 500 mpaka mwezi Machi, nina imani kuwa ingekuwa mara mbili au mara tatu zaidi kama wangepata nafasi ya kusimamia haya Mashirika yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda kumalizia ni suala la *deposits* zilizochukuliwa na Serikali kutoka kwenye mabanki kupelekwa Benki Kuu. Jana jioni nilikuwa namsikiliza Mkurugenzi wa Benki ya Mkombozi akielezea kuwa Benki zimepata matatizo baada ya Serikali kuondoa zile *deposits* kutoka kwenye Benki za Biashara na kuzipeleka Benki Kuu.

Sasa lile liliishtua kidogo kuwa inawezakana labda hayakuwa maksudi ya Serikali, lakini kwa kuondoa zile *deposits* zilipunguza ukwasi (*liquidity*) kwenye haya Mabanki. Labda nalo ningeliomba Serikali ijaribu kuangalia kwasababu nia na madhumuni ni namna gani tunaweza kuzisaidia hizi Benki ziweze kuwakopesha wakulima, ziweze kwenda vijijini, kuwe na *a real financial inclusion*. Kwa hiyo, naomba sana tena sana tuangalie kurudi nyuma wakati mwingine siyo vibaya kama tutafanya marekebisho ambayo yatasaidia kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza. Tunamkaribisha Mheshimiwa Shally Raymond na baadae Mheshimiwa Ali Hassan Omar ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mpango, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo kwa hakika naona hata hii siku moja mliyotupa haitoshi kabisa, ingefaa kila mtu hapa akapata muda wa kuchangia kwa sababu ni fupi na inaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye ukurasa ule wa 47 unaozungumzia huduma za kibenki, naanzia pale kwenye ukurasa wa 44 na nitakwenda moja kwa moja kwenye mikopo. Kuna riba inayotozwa kwa anayekopa lakini kuna riba anayopewa yule anayeweka. Wanakwenda kuwekeza kwenye *savings* au kwenye *FDR* na hizo hela zinakopeshwa sasa ile riba imetofautiana sana, anaekopeshwa analipa asilimia 17, huyu ambaye ameweka analipwa asilimia mbili mpaka tatu ndiyo inafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kuna haja gani mtu apeleke hela yake benki akaweke kama analipwa kidogo hivyo? Mbaya zaidi kuna yale makato ya *service charges*. Ukienda kwa mwaka kama mtu ameweka laki moja yake na hakuweza kuongezea unakuta yote imekatwa kwenye *service* na hakuna kitu anachopata, maana yake ni nini? Namuomba Waziri wetu aangalie jambo hili, akae na hizo benki husika ili waweze kuona tatizo hili kwamba limekuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile mikopo kuna ile mikopo ya wafanyabiashara na kuna mikopo ya wafanyakazi. Hii mikopo ya wafanyakazi haina matatizo kufuatilia, yeye anafanya kazi pale au hata kama ni Mbunge upo hapa mkopo wako utalipika tu na hata nikiondoka leo bado yale mapato yangu yatalipa ule mkopo. Kwa nini tunatozwa kiwango kinacholingana na wale wafanyabiashara? Mfanyakazi anatakiwa atozwe kidogo zaidi na isipishane zaidi na ile ya kuwekeza, ningomba kufahamu jambo hili siyo

haki kabisa. Mikopo hiyo ina bima, ufuatiliaji ni mdogo kwa kweli naona wakati sasa ufike, Waziri akae mezani na haya mabenki waone ni jinsi gani wanarekebisha jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo la mabenki, niende katika ukurasa wa 17 ule utaratibu au mikakati ya kupunguza umaskini. Napongeza hatua ya Wizara hii kutoa mafunzo kwa wataalam, lakini katika kutoa mafunzo kwa wataalam sikuona Wizara imejipanga kutoa mafunzo kwa wale ambao ndiyo wanaonufaika na elimu hii inakuaje? Mnatuelimishia wataalam, lakini hamkupanga fungu la kuelimisha wale ambao ni wanufaika, sioni kama hapo tutapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri sasa aangalie wataalam hao wakishaelimika pia aweke fungu ambalo wataelimishwa wajasiriamali wadogo wadogo, wale wa VICOBA, watu wote ambao wanataka kuingia kwenye biashara ili waweze kunufaika na hii elimu ambayo wamepatiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 34 naomba nizungumzie kidogo kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali. CAG anakwenda kwenye ukaguzi lakini tumeona kabisa na tumeelezwa hela ya kumuwezesha CAG ni kidogo japo kwa kipindi kilichotajwa ameweza kupatiwa, lakini tunaomba CAG afikiriwe, tumemuomba bajeti iliyopita na sasa tena tunamuomba kwa sababu tulienda tukaona kuwa hakuweza kutembelea maeneo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 35, kuhusu usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma. Naona hapa wameeleza vizuri usimamizi unavyokuwa lakini nauliza kwamba, Serikali ilikuwa na hisa kwenye mashirika mengi tu lakini hatukuorodheshewa hadi sasa imekidhi asilimia ngapi kwenye mashirika kadhaa na ufuatiliaji wake ukoje. Mashirika mengi yalikuwa mikononi mwa Serikali, mengine sasa yamekwenda *private*, mengine hayapo tena kabisa na Serikali. Je, Serikali imefuatilia hisa zake kwa yale mashirika

yote? Hapa tunapata wasiwasi. Mimi nipo kwenye Kamati ya PAC na tuliona kwamba kuna maeneo ambayo Serikali imesahau hata hisa zake. Nilikuwa naomba sana Wizara ifuatilie ili iweze kujua imewekeza wapi na inalipwa kwa jinsi gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika *currency* yetu, hela yetu hizi noti. *Coins* hazina tatizo japo zote zinaitwa noti na *coins*, naomba Wizara izungumze na Benki Kuu itoe elimu ya kufanya utunzaji wa noti. Kamati yangu ilipata nafasi ya kwenda kutembelea Benki Kuu tukaona jinsi ambavyo noti hizo sasa inafikia mahali wana-*thread*, wanaondoa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni gharama sana ku-*thread* ni bora tungekuwa na noti ambayo ingeweza kudumu, amezungumza mzungumzaji mmoja kabla yangu lakini mimi nataka niende mbali zaidi. Utunzaji wa noti unatakiwa uwe kwenye akili ya mtu *it is a mindset*. Mtu anaichukua noti yake vizuri, anaweka kwenye *wallet*, lakini Watanzania wengi anachukua noti yake anafunga kwenye kitambaa, anasokomeza anakosokomeza. Hiyo noti hata ingekuwa ya gharama namna gani lazima itachakaa. Naomba Serikali ione umuhimu wa kuelimisha watoto toka wakiwa wadogo namna ya kutunza hela, namna ya kuthamini noti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi za nje unakuta dola siku zote imenyoo shwa wanashangaa wakija Tanzania dola inakunjwa, wakija Tanzania *pound* inakunjwa, hela haikunjwi ndugu zangu, ukitunza hela inakutembelea. Weka notiyako kwenye *wallet*, hela ipendeze na hiyo hela itadumu na mfukoni itaenea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie umuhimu wa kuona kwamba imefikia wakati yeyote anayetaka kujaribu biashara kabla hajaingia kwenye biashara aingie katika elimu au ataelimishwa na wale wanaomhusu au atakwenda kupata mafunzo. Tuna vyuo vyetu vingi tu kimojawapo ninachokifahamu kwa undani sana ni Chuo cha Ushirika (Moshi Cooperative University).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna wakati wanafunga shule, wakifunga chuo nilikuwa naomba Waziri akiweza kutukutanisha akatupa semina kama Wabunge wake na tukianza kwenda kukutana na wale tunaowasimamia wapate elimu katika vyuo hivyo na sisi wenyewe pia tutachangia gharama za kuelimisha watu hawa. Tukielimika kutakuwa hamna tatizo, tutakuwa na Waziri wetu mzuri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri mzuri na wote tutazungumzia maendeleo, sioni kwamba saa zote tukikaa tulaumu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo yanatosha kutuambia tupongeze, naomba nichukue nafasi hii kupongeza sana Wizara hii kwa makusanyo yaliyopatikana na pia nipongeze Wizara hii kwa jinsi ambavyo imejitahidi kulipa deni la Serikali, hatuwezi kudaiwa kila siku, dawa ya deni ni kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Raymond. Tunamalizia na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia siku ya leo kuwa hai hapa na tukafika katika Bunge lako Tukufu na kuweza kujadili bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakushukuru wewe kuweza kunipa nafasi hii kuweza kujadili lakini kwanza kabla sijaanza kuchangia kitu ambacho nataka kukisema nina mambo kama nane, jambo moja tu ambalo ni muhimu sana kuzingatia.

Katika kitabu hiki cha rangi ya waridi ambacho walizungumza Kambi ya Upinzani wakasema kwamba wanawashukuru waliofanya utafiti mpaka wakaandika

kitabu hiki, lakini hiki kitabu kimeandika Bajeti Kuu, hakijaandika bajeti ya Wizara ya Fedha. Sasa pamoja na *research* hiyo halafu bado watu wako nje ya *beat*, watu wanaimba nje ya *key*, sasa sijui haya mambo yataendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linakuja kwa sababu ukiajiandaa sana kukosoa basi mwisho unakosolewa wewe, kwa hiyo ndilo nilitaka nitoe taarifa tu kwamba hiki kitabu kiko nje ya *beat* tena kiko nje ta *key* kinazungumzia Bajeti Kuu, ikifika siku hiyo ya Bajeti Kuu sijui kutaelezwa nini, ukikitafuta utakiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ninalotaka kuchangia la mwanzo, nataka kuchangia katika Fungu Namba 10 la Wizara ya Fedha. Fungu Namba 10 ni Tume ya Fedha ya Pamoja. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 40 na ukurasa wa 41 amezungumzia Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika Tume hiyo ya Pamoja ya Fedha amesema kwamba imefanya mapitio ya *study* tofauti za masuala ya kodi. Sasa na mimi nizungumze masuala hayo ya kodi ambayo labda mengine kwa kuwa mambo haya yanapita huko na haya yapite huko. Jambo lenyewe ni hili kama lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tumepitisha *Petroleum Act* pia tumepitisha *Oil and Gas Revenue Management Act, 2015* ambavyo vimelenga kuifanya kwamba Zanzibar kuwa inashughulika na mafuta na gesi ambayo wanachimba kule na Tanzania Bara watashughulika kwa upande wao, lakini kitu kimoja ambacho ninataka kikaangaliwe katika Tume hii ya Pamoja ya Fedha ni kwamba bado Sheria za Kodi ni za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni kwamba pato kubwa linalotokana na mafuta na gesi huwa linatokana na kodi, sasa hizi kodi bado ni za Muungano kwa kuwa hizi kodi bado ni za Muungano, Tume hii nayo basi ikakae na ikatazame kwa sababu watu wanazungumza wataalam zaidi ya asilimia 90 ya mapato ya mafuta na gesi ni kodi lakini kama zikiwa hazikuelezwa kodi hizo kama hazitokuwa

za Muungano ina maana kwamba bado patakuwa pana utata. Sasa zikaelezwe hizo kodi ambazo zitatokana na mafura na gesi nazo pia ziwe tofauti na Sheria za Kodi ambazo ni Sheria za Muungano, hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tume hii ipo kwa maslahi ya kuangalia *study* na kuangalia masuala ya kodi na kufanya mapitio kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 41 basi pia tukaangalie Tanzania Bara na Zanzibar ni sehemu ambazo hazijapakana kwa mipaka mikubwa, masafa ni madogo sana. Katika masuala ya bidhaa ambazo zinakwenda Zanzibar kuwekewa *zero rate* kwa masafa madogo inakuwa haiko vizuri ni bora tukatumia ile *compensation arrangement* kuliko tukatumia *zero based arrangement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala hili litakwenda litaafikiwa na litazungumzwa vizuri kwa sababu masafa yetu madogo, *zero based* mara nyingi watu wanatumia kwa masafa marefu na *zero based* ina gharama kubwa ina maana kwamba lazima uanze kuweka mambo ya *administration* katika *customs* zote, uanze kufanya masuala hayo, jingine ni magendo yanaweza yakaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nashauri katika Tume ya Pamoja ya Fedha ijaribu kuangalia hili kwa sababu mara nyingi inakwenda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 21 - Hazina; Wabunge wengi sana walisema kwamba fedha hawajaziona lakini ukienda katika Kitabu cha Maendeleo cha bajeti, Fungu 21- Hazina iko pale *village empowerment* na imewekewa fedha zake shilingi bilioni 60. Tukitazama katika vitabu hivyo tutaona. Sasa mimi nazungumzia katika kitu kimoja. Mwaka huu tumesema kwamba tutafanya *pilot study* lakini miezi tayari inataradadi nafikiri bado nafikiri bado tutakuwa hatujafanya *pilot study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sisi wengine wenye Majimbo na ambao tumechangamka haraka baada ya

kusikia fursa hii kwa wananchi, tulijaribu kwenda kuhamasisha, tulisajili vikundi, tulitoa elimu kwa vikundi tayari tulikwishajipanga. Jang'ombe tayari tulishajipanga. Kama hiyo *pilot study* inataka kufanyika ghafla basi tulateeni Jang'ombe kwa sababu tumeshatoa elimu na vikundi viko imara na vikundi vimehamasika na vinafanya kazi yake vizuri, kwa hiyo tutakapokwenda tukafanye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo moja, hili jambo tulisema kwamba kwa *pilot study* ndiyo shilingi bilioni 59.5 lakini iweje na mwaka unaofuata iwe bilioni 60? Na wakati vijiji vinajulikana au mitaa inajulikana idadi yake kwa fedha hizi ambazo tumezitenga kwa mwaka wa pili ni kidogo na fedha hizi mwaka wa mwanzo hazikutoka hatujui kama tumelishwa samaki wa kuchora au vipi! Kwa sabbau bado hazijatoka. Sasa Je, na hizi za mwaka wa pili zitatoka sambamba? Kwa hiyo, hapo namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuja kuangalia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu la Deni la Taifa, tunakubali Serikali ikope, nchi maskini ili iweze kuendelea ikope na tumefurahi kuona kwamba katika Deni la Taifa tunalipa, tunaishukuru na tunaipongeza sana Serikali yetu. Miradi ambayo inayofanyika tukikopa leo wanakuja kulipa wa kesho na kesho kutwa. Watakuja kulipa watu kwa miaka 20 au 25 mbele ambao hawajatumia, sasa miradi ambayo itakuwa inafanyika kwa kukopa fedha hizi basi *at least* iwe ina *record* nzuri, iwe inajulikana katika kila hatua kwa maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana umekopa umsomeshe mtu mpaka Chuo Kikuu, lakini kumbe yule mtu akamalizia *primary* lakini mkopo uliochukua ni wa Chuo Kikuu. Sasa tupate faida ile ya kusoma mtu Chuo Kikuu na huo mradi tunaosema ukubwa wake uwe vilevile ambavyo ulitarajiwa na usije ukawa ni mradi ambao ni mfupi ambao faida yake ni ndogo. Tutakuja kuwalipisha watu deni kubwa kuliko faida ya mradi ambao upo kwa sababu deni tutalipa mbele. (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Msajili wa Hazina Fungu Namba 7. Katika Fungu Namba 7 siku zote Serikali inahangaika kutafuta mapato lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa King muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kazi ambayo tumeifanya kutwa nzima ya leo Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu umefikia mwisho, tutakutana kesho. Naahirisha Bunge hadi kesho siku ya Jumatano Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*